Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Mbili - Tarehe 9 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 207

**Kiwanda cha Korosho - Lindi**

**MHE. BERNARD K. MEMBE (k.n.y. MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kiwanda cha Korosho cha Lindi ndicho kiwanda pekee kinachotegemewa kuwapatia ajira wananchi wa Lindi na kwa kuwa ilitolewa ahadi kwamba Serikali inatafuta wawekezaji ili kiwanda hicho kiweze kufanya kazi tena na hatimaye kutoa ajira:-

Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa katika kutafuta wawekezaji kwenye kiwanda hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kuwatafuta wawekezaji wa kufufua Viwanda vya Korosho nchini kupitia utaratibu wa kutangaza zaidi ya mara mbili katika kipindi cha mwaka 2003 bila mafanikio ya kuridhisha. Hata hivyo, mnamo mwezi Machi, 2004, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilitoa tangazo tena kuwataka wawekezaji kuwekeza katika Viwanda vya Korosho.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Mei, 2004, Tume ilipokea zabuni za ununuzi wa Viwanda vya Korosho ikiwemo zabuni kwa ajili ya ununuzi wa Kiwanda cha Lindi. Taarifa nilizozipata leo hii pamoja na ahadi ya Serikali viwanda nane tayari vimekwishapata wawekezaji, *TANITA I, TANITA II,* Kibaha, Masasi, Lindi, Newala, Likombe na Newala II. Viwanda ambavyo bado havijapata wawekezaji ni viwanda vya Nachingwea, Mtama na Tunduru.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa zoezi la kuwatafuta wawekezaji ni la muda wa miaka sita sasa na kwa kuwa Wilaya ya Lindi kwa viwanda vyake vya Lindi na Mtama ndivyo vinavyotegemewa kuleta ajira kwa wananchi wa Wilaya ile, ni kitu gani hasa kinachozuia upatikanaji wa wawekezaji katika viwanda viwili vile vya Mtama pamoja na Lindi Mjini?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na ushauri wangu kwamba wakati umefika sasa wa kutoa kipaumbele kwa viwanda viwili vile ili wananchi wa Lindi pamoja na Nachingwea wajisikie kwamba na wao sio wakulima tu lakini pia kuna sekta ya wafanyakazi ili kuleta maendeleo katika jamii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kiwanda cha Lindi tayari kimeshapata mwekezaji, kiwanda ambacho hakijapata mwekezaji ni Kiwanda cha Mtama na kile cha Nachingwea.

Kiwanda cha Mtama na Nachingwea ulitokea utaratibu kwamba kiwanda kile kimilikiwe na wakulima kupitia Halmashauri yao ya Wilaya. Sasa utaratibu ambao tunausubiri sasa hivi ni Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kuongea na uongozi wa Mkoa wa Lindi kuona ni jinsi gani Viwanda hivi vya Mtama na Nachingwea vinaweza kupewa wananchi wakaviendesha wao wenyewe ili vianze uzalishaji. Lakini bado tunatoa kipaumbele kwamba Kiwanda cha Mtama na Nachingwea viweze kupata wawekezaji ili vianze kuzalisha.

Na. 208

**Barabara ya Chubi-Itaswi-Kisaki**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa ahadi ya kusaidia kuikarabati barabara ya Chubi-Itaswi-Kisaki na kunyanyua tuta la barabara ili kujenga makalvati kuyawezesha maji ya mvua kupita na hatimaye magari kupita wakati wote na kwa kuwa mvua zikinyesha Vijiji vya Chubi, Itaswi, Kisaki, Iresi na Mauno vinakosa mawasiliano kabisa na Makao Makuu ya Kata, Tarafa na Wilaya:-

(a) Kwa nini *TANAPA* haitekelezi ahadi hiyo kwa faida ya pande zote?

(b) Je, ndiyo kusema kuwa *TANAPA* haitaki ushirikiano mwema baina ya Vijiji hivyo vinavyoshiriki kulinda wanyamapori?

(c) Je, ni lini kazi hiyo itatekelezwa ili wananchi waondokane na shida hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ujirani mwema ni mpango wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania unaolenga kushirikisha wananchi wanaozunguka hifadhi katika uhifadhi na kuhakikisha kuwa wananchi hao wananufaika na matunda yatokanayo na uhifadhi. Ili kutekeleza azma hiyo, wananchi hushirikishwa kwa kutumia njia ya elimu ya uhifadhi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii, hifadhi na uchumni kwa lengo la kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa ahadi ya kukarabati barabara ya Itaswi-Chubi-Kisaki kwa kuinua tuta na kuweka kalvati ili iweze kupitika kwa mwaka mzima na hivyo kuondokana na adha ya mawasiliano kwa wananchi wa Vijiji vya Chubi, Itaswi, Kisaki, Iresi na Mauno na Makao Makuu ya Kata, Tarafa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi iliyotolewa na Wizara, mnamo tarehe 10 Septemba, 2003, timu ya wataalam kutoka *TANAPA* ilitembelea eneo husika ili kukagua na kuona hali halisi ya barabara kabla ya kukutana na uongozi wa Wilaya ya Kondoa kwa majadiliano ya awali kuhusu utekelezaji wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Oktoba, 2003, uongozi wa Hifadhi ya Taifa Tarangire ulikutana na uongozi wa Wilaya ya Kondoa na kujadiliana juu ya ukarabati wa barabara hiyo. Baada ya majadiliano hayo kulikuwa na makubaliano kati ya *TANAPA* na Halmashauri ya Kondoa kwamba:-

(1) *TANAPA* itachangia shilingi milioni 10 endapo matokeo ya *EIA* yataonyesha kuwa hakuna athari yoyote katika mazingira kama Mradi huo utatekelezwa.

(2) Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa itatoa mtambo kwa ajili ya kazi hiyo.

(3) Halmashauri ya Wilaya iandae rasimu ya mradi ikionyesha gharama na maeneo mengine ambayo barabara hiyo inaweza kupita ili kuunganisha Vijiji hivyo na Makao Makuu ya Kata, Tarafa na Wilaya kisha kuiwasilisha *TANAPA*.

(4) Taarifa hiyo iwasilishwe *TANAPA* baada ya wiki moja kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa suala hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya *TANAPA* alitembelea eneo hilo tarehe 28 Oktoba, 2003 akiwa na viongozi wa Wilaya ya Kondoa na alishauri upembuzi yakinifu ufanyike na baadaye kuwe na kikao kati ya Halmashauri, *TANAPA* na *TANROADS* kujadili matokeo ya taarifa ya uchunguzi itakayotolewa na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna taarifa ya upembuzi yakinifu iliyoandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ili kuonyesha mahitaji halisi ya kazi, njia mbadala endapo kutakuwa na athari ya mazingira katika eneo hilo, athari ya mazingira katika eneo la Bwawa la Kisaki na Mto Tarangire kama walivyokubaliana na *TANAPA.*

Kwa mantiki hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge arudi Wilayani kwake ili wafanye upembuzi yakinifu na hatimaye taarifa hiyo ipelekwe *TANAPA* tayari kwa mkutano wa wadau wa barabara hiyo kama walivyopendekeza katika mkutano wao wa tarehe 2 Oktoba, 2003, pia kuungwa mkono na Mweyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya *TANAPA.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii bado ina nia ya kutekeleza ahadi yake kama ilivyoahidi. Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na kutamka kuwa *TANAPA* inaheshimu na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na wananchi wa Vijiji vya Chubi, Itaswi, Kisaki, Iresi na Mauno katika uhifadhi wa wanyamapori. Hivyo ni lengo la Wizara na *TANAPA* kuhakikisha kuwa uhusiano mzuri unaendelea kuwepo. Ni kwa msingi huo *TANAPA* imechangia jumla ya shilingi milioni 38 katika ujenzi wa bweni la wasichana linalojengwa na wananchi wa Tarafa ya Pahi katika shule ya sekondari ya Aman Abeid Karume. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu la msingi na namshukuru sana kwa kufuatilia sana suala hilo. Lakini pia kwa sababu upembuzi yakinifu umefanywa, nafikiri taarifa tu imechelewa kufikia, mimi nitaifuatilia. Je, ikifika haraka Waziri atasimamia ili kazi hiyo ifanywe safari hii kabla mvua za masika hazijanyesha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ndio tutafuatilia kama vile ambavyo tulikubaliana katika kikao hicho na kama vile ambavyo walikubaliana na Mwenyekiti wa *TANAPA* alivyokwenda huko.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba niulize kwamba, Wizara kwa kuishirikisha *TANAPA* imesaidiaje au imewaelimisha lini akinamama wa Vijiji hivyo vilivyotajwa ili na wao wahusike katika suala zima la kutunza hifadhi ya Tarangire ikiwa ni pamoja na

kusaidia shughuli za vikundi vya akinamama katika Vijiji hivyo? Naomba Serikali inipe jibu. Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni kwamba *TANAPA* inayo programu ya ujirani mwema na kwa maana hiyo imesaidia sana katika ujirani mwema lakini pamoja na hayo kuna programu maalum ambazo zinalenga pia moja kwa moja kwa akinamama.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano ya moja kwa moja ya jinsi gani akinamama wanashirikishwa katika kuuza vitu vyao pale ambapo watalii wanazungukia katika maeneo hayo. Lakini pia pamoja na hayo kuna programu za elimu za UKIMWI ambazo zinalenga moja kwa moja upande wa wanawake na upande wa jamii kwa ujumla wake. Lakini kama Mheshimiwa Mariam Mfaki anataka kujua hasa hasa katika maeneo hayo ni kitu gani hasa kimefanyika tupo tayari kumpa taarifa hiyo. *(Makofi)*

Na. 209

**Barabara Zinazozunguka Hifadhi ya Lukwika-Lumesule**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara zinazounganisha Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Lukwika-Lumesule ni mbaya sana kwa sababu imekosa matengenezo ya mara kwa mara na kwa kuwa barabara hizo ni muhimu sana kwa ulinzi wa hifadhi hiyo na kwa kuwa barabara hizo hutumika kwa kupitishia watalii wanaokuja kuwinda na kutembelea hifadhi hiyo na kwa kuwa barabara hizo ndiyo tegemeo pekee kwa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wananchi wa Vijiji husika:-

(a) Je, Serikali haijaona umuhimu wa barabara hizo kiuchumi na kijamii?

(b) Je, barabara hizo zitatengenezwa lini na kwa kiwango gani?

(c) Je, matengenezo ya barabara hizo yatajumuisha ujenzi wa madaraja kwenye Mto Lukwika kati ya Vijiji vya Chimika na Mpwahia na kwenye Mto Lukwamba kati ya Vijiji vya Mpombe na Mburusa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa hali ya barabara za Vijiji vinavyozunguka Pori la Akiba la Lukwika/Lumesule na Msanjesi sio nzuri. Barabara hizo ni pamoja na ile itokayo Mjini Masasi hadi Ndechelea kupitia Vijiji vya Mangaka, Michiga, Nakopi na Mpombe. Vile vile kuna barabara nyingine inayopitia Vijiji vya Mangaka, Chipuputa, Mpwahia na Mpombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizo kiuchumi na kijamii hasa ukizingatia kwamba barabara hizo huunganisha Vijiji hivyo na Pori la Akiba la Lukwika/Lumesule na Msanjesi. Aidha, barabara hizo zinaunganisha Wilaya za Masasi, Tunduru na Songea. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hizo katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara yangu kupitia uongozi wa Pori la Akiba la Lukwika/Lumesule na Msanjesi ilitengeneza barabara yenye urefu wa kilometa 54 kutoka Mpombe hadi Michiga kupitia Nakopi.

Vile vile kumekuwepo na mawasiliano ya karibu kati ya uongozi wa Pori la Akiba la Lukwika/Lumesule na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuhusu kuchangia gharama katika kufanya matengenezo ya daraja la Lukwamba linalounganisha Vijiji vya Mpombe na Ndechele na lile linalounganisha Vijiji vya Chimika na Mpwahia. Wizara yangu itaendelea kujitahidi kutengeneza barabara hizo. Ni matumaini yangu kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi pia itachangia gharama za matengenezo ya barabara hizo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Hifadhi ya Lukwika-Lumesule imekuwa inaingiza fedha kutokana na utalii na uwindaji. Je, ni kiasi gani cha fedha kimekuwa kinapatikana kila mwaka kuanzia mwaka 2000 hadi leo?

Mheshimiwa Spika, pili, je, kwa nini sehemu ya fedha hizi ambazo zinapatikana zisitumike katika ukarabati wa barabara hizi muhimu kwa biashara hii ya utalii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba katika eneo hili kuna Kampuni moja inayolinda katika kitalu hiki cha Lukwika-Lumesule na Msanjesi-Mnguwesu-Msacheli, nayo ni kampuni inayoitwa *Miombo Safari.* Sasa fedha ambazo zinapatikana ambazo zinachangiwa kwenye Halmashauri alitaka za mwaka 2002 na 2003, lakini nitampa toka mwaka 2000 mpaka 2003. Ni kwamba katika mwaka 2000 zilipatikana dola za Marekani 15,000 yaani kama shilingi milioni 15. Mwaka 2001 zilipatikana kama shilingi milioni 15. Mwaka 2002 zilipatikana kama shilingi milioni 14 na mwaka 2003 ni kama shilingi milioni 12.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukarabati kama nilivyoeleza hapo mwanzo ni kwamba ukarabati huu ulifanyika katika kilomita hizo 54. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Aridi Uledi, kwamba tutauagiza uongozi kwamba watengeneze zile sehemu ambazo ni korofi. Tunajua katika maeneo hayo kuna sehemu ambazo ni korofi, kwa hiyo, watatengeneza katika kipindi hiki cha fedha.

Na. 210

**Mtambo wa Simu Mji Mdogo wa Itigi**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

(a) Je, kuna mpango gani wa kuweka mtambo wa simu katika Mji Mdogo wa Itigi ili uwe na mawasiliano ya uhakika badala ya utaratibu wa sasa wa kutegemea njia mbili za simu toka mtambo wa Manyoni ambao nao huharibika mara kwa mara na njia zake kuwa na msongamano?

(b) Kwa kuwa utaratibu wa sasa wa kutumia njia mbili toka mtambo wa Manyoni unategemea nguzo na nyaya zilizotandikwa toka Manyoni hadi Itigi ambazo hukatika mara kwa mara kutokana na sababu mbalimbali na kusababisha kukosekana mawasiliano kwa muda mrefu, je, Serikali ina mpango gani wa kulipatia tatizo hili ufumbuzi wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika Mji Mdogo wa Itigi hivi sasa unahudumiwa na mtambo wa simu za kukoroga wenye uwezo wa kuunganisha jumla ya wateja 100 na umeunganishwa na Mji wa Manyoni kwa kutumia njia mbili za nguzo na nyaya. Hivi sasa mtambo wa Manyoni ni mpya na wa kisasa baada ya kubadilisha wa zamani na una uwezo wa kutosheleza mahitaji.

Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma za simu za kisasa Vijijini nchini kote, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ina mpango wa kuanzisha Mfuko Maalum ujulikanao kama *Rural Telecommunications Fund* kwa ajili hiyo. Wadau mbalimbali watahusishwa katika kuchangia Mfuko huo. Ni mategemeo yetu kuwa mara Mfuko huo utakapoanza kutumika tatizo la kukosekana kwa mawasiliano kutokana na kukatika nyaya hizo mara kwa mara litakwisha kwani mitambo itakayowekwa itakuwa ya kisasa ambayo haitumii waya.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, mwaka 2003 wakati wa kipindi cha Bajeti, Wizara ilikuwa imeahidi kwamba katika mwaka huu wa fedha Mji Mdogo wa Itigi ungepatiwa mtambo mpya wa kisasa lakini kwa majibu ya leo inaonekana inabidi tusubiri mpaka huo Mfuko wa kuchangiwa na wadau wengine utakapoanzishwa. Sasa, je, ile ahadi ya mwaka 2003 kwa nini ibadilike badala ya kutekelezwa kama walivyoahidi mwaka 2003?

Mheshimiwa Spika, pili, hivi karibuni Kampuni ya *Celtel* ilitoa vipeperushi ikionyesha maeneo ambayo huduma zao wamefikisha na miongoni mwa maeneo ambayo yaliyonyeshwa ni pamoja na Itigi, lakini mpaka sasa hivi hii huduma haijapatikana. Ukiwasha simu kweli unapata *signal* lakini hakuna mawasiliano. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutusaidia kutuulizia kwa watu wa Kampuni ya *Celtel,* tujue hii huduma itapatikana lini kwa sababu wameshaonyesha kuwa ipo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba mwaka 2003 tuliahidi kwamba tungepeleka simu, lakini nafikiri na yeye atakubaliana nami kwamba kutokana na mizozo tuliyokuwa nayo tumechelewa kupeleka simu kule Itigi, lakini nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge hatujabadilisha ahadi yetu ya kupeleka simu Itigi, ipo pale pale. Tunategemea watu wa *TTCL* wakimaliza Kiomboi ambako sasa hivi ndiyo wanafanyia shughuli, watahamia huko kushughulikia. Hiyo ndiyo *information* ya mwisho niliyoipata asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Celtel* ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba *signal* inawezekana wakapata kwa sababu Manyoni tayari wana *Celtel* lakini haiwezi kufika kule bila kuwa na mgongo wa *TTCL.* Kwa hiyo, mawasiliano ya *TTCL* yakifika kwa haraka na *Celtel* itafika Itigi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo wanalopata Itigi linafanana na ni sambamba kabisa na tatizo la Mji Mdogo wa Mtinko ambao upo karibu kabisa na Mji wa Itigi.

Je, Mheshimiwa Waziri atawaambia nini wananchi wa Mji Mdogo wa Mtinko ulioko Singida Kaskazini kupatikana kwa mtandao wa *Celtel* na mtandao wa *TTCL* ambao Serikali imeahidi na kila siku wanasubiri na wanamwuliza Mbunge wao? Naomba jibu. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii niwaombe wananchi wa Singida wajue umuhimu wa Mheshimiwa Mbunge anavyoshughulikia masuala ya simu katika Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwamba Mfuko huu kama nilivyosema hapo mapema utakapoanza mawasiliano ya simu katika Vijiji alivyovitaja navyo pia vitakuwa *considered.* Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, hivi sasa tupo kwake Kiomboi na tunategemea tutafika huko ambako yeye anataka twende.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea tu katika majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa taarifa tu kwamba sasa *Vodacom* inaongea Mafia na *Celtel* inaongea huko kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Jimboni kwake. Kwa hiyo, ni maendeleo makubwa. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 211

**Simu za Kisasa na za Mkononi Mji wa Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Kampuni ya Simu iliahidi kuupatia Mji wa Kondoa pamoja na Vitongoji vyake simu za kisasa lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea:-

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa kwa kuupatia Mji huo simu za kisasa?

(b) Je, ni lini Kijiji cha Soya kitapatiwa simu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuupatia Mji wa Kondoa huduma ya simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kondoa kwa hivi sasa unahudumiwa na mtambo wa kisasa wa *digital* wenye uwezo wa kuunganisha jumla ya wateja 1,000 na wateja wanaofaidika na huduma hizo hadi tarehe 16 Mei, 2004 ni 318. Mji huo umeunganishwa na Dodoma kupitia mtambo wa kisasa wa *digital* wenye njia 480. Mitambo hii ilianza kufanya kazi tarehe 29 Mei, 2004. Pia huduma za simu za mkononi za *Celtel* zinapatikana Mjini Kondoa.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Soya kitapatiwa huduma za simu baada ya Serikali kukamilisha mpango wa kuanzisha Mfuko Maalum ujulikanao kama *Rural Telecommunications Fund* na mpango huu una nia ya kupeleka simu Vijijini.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na kazi nzuri ambayo imefanywa ya kutupatia simu za kisasa, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa simu za mkononi za *Celtel* sasa hivi zinapatikana katika Mji wa Kondoa lakini hazifiki mbali kutoka Mjini. Je, kuna mpango gani wa kujenga minara katika njia za Dodoma hadi Kondoa na Kondoa hadi Kibaya na Kondoa hadi Babati ili tuweze kupata simu kwa wananchi wetu katika njia hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa simu za kisasa zipo Kondoa, je, kuna mpango gani wa kusambaza simu hizo katika Makao Makuu ya Tarafa katika Wilaya ya Kondoa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, mawazo yake nayachukua na nitawapa watu wa *Celtel* wayafanyie kazi. Nina hakika kwanza watahitaji kufanya utafiti wa kibiashara na kuona uwezekano wa kuweka huo mnara.

Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *infrastructure* ya simu ikifika Kondoa Kusini, Vijiji alivyovisema vitapata mawasiliano ya simu. Lakini napenda nichukue nafasi hii kuwaomba na kutoa nasaha zangu kwa wananchi wa Kondoa kwamba, kilio cha Mheshimiwa Mbunge wao kimesikika na mtambo wa simu wa *line* 1,000 umewekwa lakini hadi leo ni watu 217 tu ambao wanautumia mtambo huo. Kwa hiyo, zipo pesa pale zimelala, hazifanyiwi kazi ipasavyo. Nawaomba wananchi waone umuhimu wa mawasiliano katika kuendeleza huduma zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu Mji wa Kondoa, sasa wengine kama mna shida hiyo hiyo mlete maswali ya msingi. Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ushirika na Masoko.

Na. 112

**Benki ya Ushirika**

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA (k.n.y. MHE. ABU T. KIWANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kupitisha Muswada mpya wa Ushirika wa mwaka 2004, moja ya matarajio kwa wananchi ni uanzishwaji wa Benki ya Ushirika:-

(a) Je, ni lini benki hiyo itaanza ili kutoa huduma kwa wananchi?

(b) Je, taratibu za ukopeshaji kutoka kwenye benki hiyo zitakuwaje?

(c) Je, benki hiyo itashirikiana vipi au ina uhusiano upi na benki tarajiwa ya wakulima na wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuunda Benki ya Ushirika ya Kitaifa umekwishaanza. Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania *(Tanzania Federation of Cooperative)* inaratibu uanzishwaji wa benki hiyo. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha benki hiyo imekwishaanza kutekelezwa na washauri waelekezi, Kampuni ya *Ernst and Young* na imepangwa kumalizika mwezi Agosti, 2004. Utafiti huu, utakapokamilika utawasilishwa kwa wadau wakuu ambao ni Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali zikiwemo *SACCOs* pamoja na wadau wengine ili kuwapa nafasi ya kujadili na kutoa maamuzi kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yatakayokuwa yameainishwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu hayo ambayo yatakuwa ni pamoja na ukusanyaji wa hisa kutoka kwa wanachama waanzilishi ndio utakaowezesha kukidhi matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika na hatimaye usajili wa benki uweze kufanyika kwa kuzingatia sheria ya Benki na Asasi za Fedha *(Banking and Financial Institutions, Act)* ili kupata leseni ya biashara ya benki. Mara taratibu hizo za msingi zitakapokamilika benki hiyo itaanza kutoa huduma kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, taratibu za utoaji huduma ikiwa ni pamoja na ukopeshaji zitaainishwa kulingana na kanuni na masharti yatakayowekwa na Bodi ya Wakurugenzi watakaochaguliwa na wana hisa na Sheria ya Benki na Asasi za fedha *(Banking and Financial Institutions Act).* Lengo la msingi la benki hiyo ni kuwawezesha wananchi wenye mapato kidogo, kupata fursa ya kuweka akiba na kupata mikopo kupitia kwenye Vyama vyao vya Ushirika hususan *SACCOs.*

(c) Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu niliyoitaja katika sehemu (a) itaainisha masuala yote muhimu kuhusiana na uanzishaji na uendeshaji wa benki hiyo ikijumuisha uhai wa kiuchumi, muundo, uendeshaji wa benki na uhusiano na benki nyingine ikiwa ni pamoja na benki tarajiwa ya wakulima. Aidha, taratibu za utoaji huduma ikiwa ni pamoja na ukopeshaji zitaainishwa ili kukidhi haja ya kundwa kwa benki hiyo.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, inavyoonekana ni kwamba benki hii itaanzishwa mwaka huu, lakini mpaka hivi sasa wakulima wanapata shida sana wanapotaka kupata mikopo. Je, anaweza kuliambia Bunge kwamba benki hii ataisimamia na itakuwa tayari kabla ya msimu ujao?

La pili, ni kwamba kwa hivi sasa Serikali inapeleka fedha hizo kwenye benki moja ya *EXIM,* anaweza kuthibitisha kwamba tutakapoanzisha Benki hiyo fedha zote za Serikali zinazohusu pembejeo zitakwenda kwenye mfuko huo mpya?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kwamba mchakato wa uanzishwaji wa benki hiyo umeanza na sasa hivi utaratibu wa upembuzi yakinifu ndiyo unaendelea. Kwa hiyo, mpaka taratibu zote hizo zitakapokuwa zimekamilika tukawaita wadau wakapewa taarifa na hatimaye kuamua utaratibu wa kuiendesha hiyo benki ndipo hapo tunaweza tukasema kwamba sasa benki hiyo inaweza kuanza kufanya kazi. Kwa hiyo, si rahisi sasa hivi kusema kwamba benki hiyo itaanza kabla ya msimu huu, kwa sababu kazi ya uandaaji bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu fedha za pembejeo kutopitia *EXIM Bank* badala yake zipitie kwenye benki hiyo mpya. Hata hivi sasa fedha hizi za pembejeo licha ya kupitia huko *EXIM Bank* lakini bado kuna Taasisi nyingine ambazo zinatumia fedha hizi za pembejeo kama vile Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo kupitia

*SCCULT* pamoja na benki nyingine. Kwa hiyo, benki hii itakapoanzishwa itajiunga katika Asasi mbalimbali za fedha ambazo zinapitishiwa fedha hizo za pembejeo.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba utaratibu bado unaendelea na mikakati inaendelea na hii ni tabia ya Serikali kwamba mikakati inaendelea na utaratibu unaendelea. Lakini kwa bahati nzuri watu hao wa Kilombero wana *SACCOS* na benki zao kama pale Kidatu, Kiberege na Ifakara kwenyewe. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anakubaliana na mimi kwamba fedha hizo kama zipo azipeleke kwenye benki hizo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, labda nieleze tu hapa kwamba isije ikaeleweka kwamba uundaji wa benki hii ya Ushirika ya Taifa kuna fedha mahali ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuunda benki hii. Nimesema katika jibu la msingi hapa kwamba wadau wakuu ambao ni Vyama vya Ushirika pamoja na wadau wengine ndiyo watakaoiunda hii benki.

Kwa hiyo, fedha zitatokana na wadau hao siyo kwamba fedha ziko kwenye mikono ya Serikali tayari kwa kuunda hiyo benki ya Ushirika ya Taifa. Kwa hiyo, kama *SACCOS* hizo ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge kwamba zina fedha. Hizo sasa zitakuwa ndiyo *sources* za mwanzo za kuweza kuanzisha benki hiyo, kwa hiyo, tunawakaribisha wajiunge katika kuanzisha benki hii tutakapokuwa tumeitisha mkutano huo wa wadau.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sasa kwa kuwa ma-*giant* wa ushirika nchini hasa Kilimanjaro wana benki ya Ushirika na Kagera wana benki ya ushirika na kwa kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana kwamba Serikali ndiyo inataka kuwalazimisha watu waanzishe mabenki. Je, kule ambako kuna hayo mabenki makubwa kama Kagera na Kilimanjaro na yenyewe yatajifilisi ili yaingie kwenye hiyo kubwa au yatakuwa ndani ya mbili?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa ieleweke kwamba Serikali hailazimishi wananchi kuunda hiyo benki ya ushirika, tunachofanya hapa ni kuhamasisha wananchi waweze wakaianzisha hiyo benki. Ndiyo maana tumesema kwamba lazima tuanze na taratibu hizi za kuandaa mapendekezo na hatimaye wadau waitwe waweze wakakubaliana kuanzishwa kwa benki yao hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na benki hizi ambazo tayari zimeshaanzishwa *Kilimanjaro Cooperative Bank,* Kagera na nyinginezo pamoja na hizi *Community Banks* zote kwa pamoja nasema kwamba watakuwa ndiyo wadau wa kuanzia si suala la kuji-*affiliate* isipokuwa wanaweza kuwa na hisa. Kwa sababu tunachotarajia kuunda hapa tunaunda Benki ya Ushirika ya Taifa ambayo wanahisa wake watatokana na hizi benki nyingine ndogo ndogo *SACCOS* pamoja na hizo benki zingine ambazo zimeishaanzishwa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa yaelekea kwamba itachukua muda mrefu sana kuwatafuta wadau mpaka waanzishe Benki hiyo ya Ushirika na Benki ya Kilimo. Je, Serikali inafikiriaje kama ingeibadilisha Benki ya Posta ambayo ina mtandao katika nchi nzima ili ifanye kazi hiyo ya kuwa Benki ya Washirika na Benki ya Wakulima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaliweza swali hilo! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa wakati nikijibu moja ya maswali ya nyongeza kwamba benki hii itakuwa ni benki ambayo inatokana na wanachama wa Vyama vya Ushirika ama Vyama vya Ushirika si benki ambayo itakuwa ni benki ya Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anavyojaribu kupendekeza kwamba fedha zichukuliwe kutoka Benki ya Posta au Benki za aina nyingine za Serikali ili kuunda hii benki ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Benki hii ya Ushirika ni benki ya wanachama ambayo itakuwa inajitegemea yenyewe kwa ajili ya kuwahudumia wanachama wake. Ni tofauti na benki hizi nyingine kwa mfano, benki hii ambayo imependekezwa na Serikali itakayokuwa ni ya wakulima hiyo ndiyo inatokana na vyanzo vya fedha za Serikali na itakuwa na utaratibu ambao unafananafanana na anaousema Mheshimiwa Mbunge.

Na. 213

**Hali ya Ujambazi Jijini Mwanza**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa matukio ya ujambazi Jijini Mwanza yanatishia usalama na amani kwa wakazi wa Jiji hilo hasa pale wanaposhambuliwa kwa kukatwa mapanga, kutishiwa na silaha kali wakati majambazi hayo yanapokwenda kupora mali na kufanya wizi kwa nguvu:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani madhubuti za kurudisha hali ya usalama na amani kwenye maeneo husika Jijini Mwanza na kuhakikisha kwamba vurugu na ujambazi vinaondoshwa kabisa?

(b) Kwa kuwa wanaoshambuliwa na majambazi huumizwa sana na kwamba hulazwa hospitali kwa muda mrefu wakitibiwa majeraha makubwa waliyoyapata, je, kwa nini Serikali isigharamie matibabu hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Jiji la Mwanza mara kwa mara hutokea mtukio ya ujambazi wa kutumia silaha kama bunduki, mapanga, nondo na kadhalika. Katika kudhibiti hali hii ya uhalifu, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendesha misako ya mara kwa mara dhidi ya makundi ya wahalifu, kuimarisha doria Jijini Mwanza, kufuatilia kwa makini taarifa zinazohusu wahalifu na kuimarisha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na raia wema katika kupambana na uhalifu.

Kutokana na hatua hizo zilizochukuliwa na zitakazoendelea kuchukuliwa, kwa sasa hali ya utulivu imerejea katika Jiji la Mwanza. Hata hivyo kwa kuwa uhalifu ni matukio yanayoongezeka na kupungua mara kwa mara, mapambano dhidi ya uhalifu Jijini Mwanza pamoja na sehemu zingine nchini ni ya kudumu.

(b) Mheshimiwa Spika, watu wote wanaopata ajali mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanaoshambuliwa na majambazi na kujeruhiwa hutakiwa kuripoti kwenye Kituo cha Polisi ambako hujaziwa na kupewa Fomu ya Polisi Na. 3 ambayo hutambulishwa na Zahanati na hospitali za Serikali. Majeruhi hao wakiripoti kwenye hospitali zetu za Serikali wakiwa na fomu hiyo ya Polisi huhudumiwa bila malipo. Hata hivyo ndugu, jamaa na marafiki wanaruhusiwa kusaidia Serikali katika kumhudumia majeruhi kwa kugharamia gharama za ziada kwa mfano, dawa ambazo hazipatikani katika hospitali za Serikali.

Aidha, wananchi wote hapa nchini wanashauriwa wajiunge na mfuko wa Afya ya Jamii katika Wilaya zao, chini ya Mfuko huu mwananchi hutakiwa kuchangia kiasi kidogo cha fedha kwa mwaka ili awe mwanachama wa mfuko na hivyo kuweza kupata huduma za matibabu bila malipo kwa mwaka mzima katika hospitali za Serikali na za binafsi.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya kuridhisha kabisa yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia ningeomba nimpongeze Mkuu wetu wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza kwa kweli ameleta mabadiliko makubwa na sasa maeneo ya Nyamanolo na Igogo ujambazi umepungua. *(Makofi)*

(a) Kwa kuwa matukio ya ujambazi yanaachana na kwa kuwa wananchi wamejaribu sana mara nyingi kushirikiana na Polisi kusaidia matatizo haya. Sasa Mwanza kuna tukio kubwa la noti za bandia ambalo ni tatizo la kiujambazi kubwa na wananchi mpaka sasa hawajalifichua na kwa kuwa wananchi wanaweza kushirikiana na Askari wakaweza kufichua. Je, Serikali inaweza ikawalindaje hawa hasa Askari wadogo katika kusimamia kama watafichua tatizo la noti bandia?

(b) Katika mkesha wa mwaka mpya wa 2003 kuna wananchi walivamiwa katika hisia kwamba ni majambazi katika maeneo ya Bugarika na wengine walikufa na Serikali au Wizara ilikuwa inafuatilia jambo hili. Je, Serikali inaweza sasa kutueleza kwamba

wale waliohusika na hilo walikuwa ni majambazi au siyo na kwa vile wazazi wao bado wanafuatilia tatizo hili la vijana wao waliofariki katika mkesha huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza pongezi za *RPC* kwa kazi nzuri anayoifanya tumezipokea bila shaka na yeye aliko huko Mwanza anasikia na tunamwomba aendelee na kazi hiyo nzuri na ma-*RPC* wengine basi waige mfano wa *RPC* wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala la noti bandia kama nilivyosema awali Jiji la Mwanza kuna uhalifu wa aina mbalimbali na moja ya uhalifu huo ni huu wa utengenezaji wa noti bandia na mpaka sasa Jeshi la Polisi linapata ushirikiano mzuri sana wa raia na hata katika magazeti juzi tu kuna mtu ambaye alifichuliwa ana noti za bandia na akakamatwa. Kwa hiyo, wito tunaoutoa wa Serikali ni kwamba tunaomba wananchi wa Mwanza na Polisi wa Mwanza waendelee na kazi hii nzuri ya kufichua aina hii ya uhalifu na upo utaratibu siyo wa kuwalinda hao tu wanaotoa taarifa lakini vile vile kuwapa hata bahashishi. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia kwamba jinsi wanavyotusaidia tunao mfuko wa kutoa motisha kwa wale wote wanaotusaidia kufichua wahalifu na huu mfuko ni kwa ajili ya Watanzania wote nchi nzima mfuko wa motisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tukio la mwaka 2003 mwanzoni kwamba Serikali itoe tamko kuhusu wale vijana waliouawa na wazazi wao. Napenda nimweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi sina tamko lakini nataka kumuahidi kwamba baada ya muda si mrefu tutamfahamisha uchunguzi wa suala lile umefikia hatua gani. *(Makofi)*

**MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa hao majambazi wako miongoni mwetu katika Kata zetu na katika Wilaya zetu na kwenye Majimbo yetu na wanafahamika. Je, na sisi wote Wabunge humu ndani kila mmoja na Jimbo lake kwa nini tusiwe na kazi ya pamoja na tamko la pamoja kuwasaka majambazi hao popote walipo na kuwaua ili kuondoa tatizo hili ambalo kwa miaka minne nikiwa hapa Bungeni nimekuwa nalizungumza kuwasaka na kuwaua tunawafahamu. Kwa nini tusiende kuwasaka na kuwaua? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kwa wale wasiomfahamu Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, ndiyo Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ulinzi na Usalama. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Na ni mwanajeshi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba majambazi tunaishi nao, maana yake hawakai mahali pengine tunaishi nao katika jamii zetu, hili ni jambo la kweli kabisa na Serikali mara kwa mara tumekuwa tunatoa wito kwamba wananchi watusaidie kuwafichua na baadhi yao wanafanyakazi nzuri ya kuwafichua na kama nilivyosema tunawapa motisha.

Mheshimiwa Spik,a lakini sasa pendekezo kwamba tuwasake huko huko na tuwaue huko huko sasa hii ni sera ngumu sana siyo sera ya Chama cha Mapinduzi. Sera

ya Chama cha Mapinduzi ni kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda tena kutoa wito kwamba majambazi popote pale walipo kwamba ni vizuri wajisalimishe kwa sababu sasa hivi Watanzania wamechoka na hali ya ujambazi, wajue hivyo kwamba Watanzania wamechoka. Lakini vile vile tunawaomba Watanzania tudhibiti hasira zetu tunapowakamata majambazi tuwafikishe katika vyombo vya dola.

Na. 214

**Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Polisi**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Bahi wamejenga vituo vidogo vya Polisi Chipanga na Bahi lakini wameshindwa kukamilisha ujenzi huo kutokana na uwezo mdogo kifedha na wingi wa huduma za jamii wanazowajibika kuchangia:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia nguvu za wananchi hao ili waweze kukamilisha ujenzi huo, hasa ikitiliwa maanani kwamba, kutokana na ukosefu wa mvua za mwaka huu, itawalazimu wananchi kujishughulisha zaidi na utafutaji wa fedha kwa ajili ya kujinunulia chakula na hivyo kipaumbele zaidi kitaelekezwa kwenye eneo la kukabiliana na njaa kuliko maeneo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Jimbo la Bahi akiwemo Mheshimiwa Mbunge kwa kuwahamasisha wananchi wa vijiji vya Bahi na Chipanga katika ujenzi wa vituo vidogo vya Polisi kwa njia ya kujitolea. Serikali kwa upande wake inao utaratibu wa muda mrefu wa kuunga mkono nguvu za wananchi katika kufanikisha huduma za jamii. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awasilishe taarifa rasmi ya sehemu ya ujenzi iliyokamilika katika vituo hivyo na msaada gani ambao wananchi wanauhitaji. Serikali itaweza kutoa kauli baada ya kuyaona mahitaji hayo na kupima uwezo wake wa Bajeti.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nitatekeleza hilo alilonitaka nilifanye. Lakini swali langu ni kwamba kwa vile wananchi katika sehemu mbalimbali za nchi wanajenga vituo hivi vya Polisi ili kuimarisha ulinzi katika maeneo yao. Ni kwa nini Serikali haijihusishi moja kwa moja na jitihada hizi za wananchi ukizingatia kwamba ulinzi wa raia na mali zao ni

jukumu la msingi kabisa la Serikali. Kwa nini Wizara isitenge fedha katika Bajeti yake ili kuunga mkono jitihada za wananchi katika kujenga vituo vya Polisi badala ya kungojea maombi ya Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tungependa Wizara tuwe na fungu hilo moja kwa moja lakini hali ya Bajeti na nyie Waheshimiwa Wabunge huwa ni mashahidi. Kwanza karibu kwa miaka 10 Wizara hii ilikuwa haipewi hata senti moja kwa ajili ya maendeleo. Ni miaka miwili, mitatu tu ndiyo tumeanza kupata fungu la maendeleo na fungu hilo sasa linapambana na matatizo mengi kweli. Kwa mfano, tatizo la vitendea kazi katika majeshi yetu, magari ni machache, nyumba za askari hazitoshi na vifaa mbalimbali havitoshi. Kwa hiyo, kwa kweli tatizo ni la kibajeti siyo dhamira, dhamira tunayo ila Bajeti ndiyo inayotukwamisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa hizi fedha kidogo ambazo tunapata tumekuwa tunasaidia hapa na pale ambapo wananchi wameonyesha juhudi na kwa sababu Tanzania ni kubwa na miradi hii imesambaa katika maeneo mbalimbali Waheshimiwa Wabunge wanapoleta maombi kama haya ndiyo wanaotukumbusha kwamba mahali fulani wananchi wanafanya shughuli fulani tafadhali njooni muwaunge mkono. Mara nyingi tunawaunga mkono kwa kadri hali ya bajeti inavyoruhusu na hata huko Bahi na Chipanga *inshallah* tutafika kama Bajeti itaruhusu. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la Jimbo la Bahi linafanana sana na ujenzi wa vituo vya Polisi vya Makongorosi na Lupa Tingatinga katika Wilaya ya Chunya. Kwa kuwa wakati alipokuwepo Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alikuwa ametutia moyo kwamba wananchi wakianzisha basi Serikali inaweza ikawasaidia hata wakapata mabati lakini hayakuweza kupatikana na kwa kuwa Bajeti ya Serikali sasa ni nzuri katika Wizara hii.

Je, wako tayari sasa kusaidia kupatikana hata simenti kwa ajili ya vituo vya Polisi hivyo viwili kwa kuwa kituo cha Lupa tumeshaezeka sisi wenyewe na cha Makongorosi nimeshawapatia fedha za kununua mabati tunachohitaji sasa ni simenti. Je, tunaweza kupata hata mifuko 100 ya simenti kwa ajili ya vituo hivyo viwili kutoka kwenye Wizara hii?

**SPIKA:** Ilikuwa ni ahadi. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wana Makorongosi wana mradi wa kujenga kituo cha polisi na tunawapongeza kusema kweli kwa hatua hiyo. Ahadi ya Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, aliyoitoa wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi iko pale pale haijafutika kwa sababu Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, ameondoka na ahadi imeondoka hapana, bado iko pale pale.

Mheshimiwa Spika, tunasikitika hatujaitekeleza kwa sababu ya mambo ya Bajeti, lakini naomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Makorongosi wawe na subira kama Bajeti ya safari hii tutakayoipitisha kesho kutwa kama itaruhusu nataka nimhakikishie kwamba ahadi ya Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, itatekelezwa. *(Makofi)*

Na. 215

**Matengenezo ya Barabara ya Tabora**

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. SAID J. NKUMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Mkutano wake wa Bajeti 2003/2004 ilisema kwamba imetenga fedha za ndani na za *ADB* kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Tabora-Sikonge-Ipole-Koga na barabara ya Ipole -Rungwa:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika mpaka sasa kwa ajili ya kazi iliyopangwa?

(b) Je, baada ya matengenezo hayo kumalizika na fedha iliyotengwa kutumika kikamilifu, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Tarafa ya Kiwere kwa barabara ya Ipole - Rungwa kupitika kwa mwaka mzima?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Tabora katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 imefanya kazi zifuatazo kwenye barabara ya Tabora-Sikonge-Ipole-Koga sehemu ya Pangale yenye urefu wa kilometa 5 kwa kutumia fedha kutoka mfuko wa barabara kwa kunyanyua tuta, kuweka makalvati na kumwaga na kushindilia changarawe. Kazi zote hizi ziligharimu jumla ya shilingi 50,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwaka wa fedha 2003/2004 zimefanyika kazi kwenye sehemu ya Tabora-Tutuo yenye urefu wa kilometa 30 kwa kutumia fedha kutoka mfuko wa barabara kwa kuchonga barabara, kuchimba mifereji, kumwaga na kushindilia changarawe na kujenga makalvati mistari mwili. Kazi zote hizo zimekamilika na zimetumika shilingi 150,000,000/= kutoka mfuko wa barabara na barabara inapitika sasa.

Aidha, katika jitihada za Serikali za kurahisisha na kuboresha barabara husika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 zilitengwa shilingi 120,000,000/= kutoka mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Ipole-Rungwa sehemu

yenye urefu wa kilomita 10 kuanzia Ipole kuelekea Rungwa. Mkandarasi alianza kazi tangu mwezi Mei, 2004 na kazi zinategemewa kukamilika mwezi wa Julai, 2004.

Mheshimiwa Spika, pia barabara za Tabora-Sikonge-Ipole-Koga kilometa198 na Ipole- Rungwa kilomeata 172 zimejumuishwa katika mradi wa ukarabati wa barabara za kanda ya kati -Magharibi zilizoathirika na mvua za *El-Nino* zilizonyesha mwaka 1998. Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni matengenezo ya dharura *(spot improvements)* katika maeneo yaliyoharibiwa vibaya.

Mheshimiwa Spika, mradi huo wenye jumla ya kilometa 325 unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Serikali ya Tanzania kwa jumla ya shilingi bilioni 2,880 na kati ya hizo shilingi bilioni 2,592 ni za kigeni na shilingi milioni 288 ni za ndani. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 10 kuanzia mwezi Februari, 2004.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi wa kufanya matengenezo hayo aitwaye *M/S Badr East African Enterprises Ltd,* amesaini mkataba tarehe 8 Januari, 2004 na ameanza kazi sehemu ya Itigi-Rungwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Juni, 2004 fedha iliyotumika katika mradi huu wa Kanda ya Kati-Magharibi chini ya *El-Nino* ambao unajumuisha barabara ya Manyoni-Itigi-Rungwa kilometa 255, Rungwa-Ipole-Tabora kilometa 198 na Ipole-Koga-Mpanda kilometa 272 ni shilingi milioni 433.2 ambazo ni kwa ajili ya malipo ya awali *(Advance payment)* kwa Mkandarasi. Mkandarasi kwa sasa ameanza kazi katika barabara ya Itigi - Rungwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo wajibu Serikali ina jukumu la kuhakikisha inaimarisha miundombinu yake ikiwa ni pamoja na barabara ya Ipole-Rungwa. Nia na madhumuni hasa ni kuhakikisha wananchi wote wa maeneo husika ikiwa ni pamoja na wananchi wa tarafa ya Kiwere wanapata unafuu wa usafiri na usafirishaji wa mizigo na mazao yao kupitia barabara zetu nchini katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu bado inaendelea na mikakati ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kuwa barabara kuu zote nchini zinaimarishwa na kupitika katika kipindi chote cha mwaka kwa kuzijenga kufikia kiwango cha lami ifikapo mwaka 2012.

**SPIKA:** Mheshimiwa Said Juma Nkumba, huko aliko anasema ameridhika na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

Na. 216

**Mafundi wa Barabara**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* mafundi wengi wa barabara hawakuchukuliwa:-

(a) Je, ni mafundi wangapi *(Road Technician)* wameachwa nje ya shughuli za barabara?

(b) Je, Serikali imeandaa mipango gani ya kuweza kuwatumia wataalamu hao kwa manufaa kulingana na taaluma zao?

(c) Kwa kuwa Serikali za Mitaa kulingana na ikama ya watumishi wa fani hiyo katika Halmashauri za Wilaya kuna upungufu mkubwa sana wa mafundi hao na wale wa majengo, je, kwa nini mafundi hao wasihamishiwe huko badala ya kuwaacha kukaa maofisini tu bila ya kutumika ipasavyo na kuliletea Taifa letu maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utekelezaji na usimamizi wa karibu wa maendeleo na matengenezo ya barabara kote nchini ikiwa ni sera ya Serikali kujiondoa katika utekelezaji wa moja kwa moja wa miradi na pia kuongeza kasi katika uimarishaji wa miundombinu, mwaka 2001 Wizara ya Ujenzi ilianzisha Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kwa kuzigeuza Idara mbili za Barabara Vijijini na Barabara Kuu kuwa Wakala.

Aidha, Watumishi waliokuwa wakifanya kazi katika Idara hizi waliendelee na majukumu yao kwa kuazimwa na Wakala mpya kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini na uchambuzi wa mahitaji halisi ya watumishi *(Job evaluation), TANROADS* waliajiri upya wafanyakazi waliowahitaji. Katika zoezi hili mafundi sanifu 176 hawakuweza kuajiriwa na *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya mafundi sanifu hao, Wizara iliwapangia vituo vipya mafundi sanifu 88 ambao walienda TUMITAA, 17 walirejeshwa Serikali Kuu na waliobaki 71 walistaafishwa kazi kwa sababu ya umri mkubwa na viwango vidogo vya elimu yao na kisha kulipwa mafao yao. Hivyo hakuna Mafundi Sanifu wenye uwezo ambao wameachwa nje ya shughuli za barabara bila ya sababu.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mara baada ya kunyakua Uhuru wa Tanganyika tulitoka na sera ya *Africanisation* ambapo Taifa liliajiri Waafrika ili kutoa kidomodomo cha wale waliodhani kwamba Wanyamwezi, Wagogo, Wakimbu, hawawezi kushika kazi zilizokuwa zinashikwa na Wazungu. Sasa je, swali la kwanza hivi Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS* wa Taifa anatakiwa kuwa na sifa gani?

**SPIKA:** Uko mbali na *microphone,* hebu sogea. Eeeh, sawa.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS* wa Taifa anatakiwa kuwa na sifa gani?

Je, sifa hizo hakuna Mtanzania anayeziweza? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kazi ya *Chief Executive* wa *TANROADS* (Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS)* ni kazi ya kiutaalamu, ni kazi ya kusimamia wataalamu hawa na si kazi ya kusema lazima apate Mluguru, Mkutu ama Mnyamwezi. Ni kazi ambayo inatangazwa Kimataifa na kwa sifa ambayo inatakiwa Kimataifa na yule ambaye ana sifa hiyo ndiye anayeajiriwa. Bila kujali kama ni Mtanzania, Mkenya, Mzungu ama Mweusi. *(Kicheko)*

*(Hapa Wabunge walipiga kelele kuashiria kupinga kauli iliyokuwa ikitolewa Bungeni)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, najua mtasema hivyo, lakini ni ukweli pekee kwamba sifa mojawapo inatakiwa uwe umekwishasimamia Shirika la namna ile zaidi ya miaka 10. Yule ambaye yupo sasa ni Mghana, amekwishaendesha Shirika la namna ile kwa miaka 25. Hilo moja.

La pili, vijana wetu ambao wame-apply kwa kazi ile wametoka *TANROADS* ambayo imekuwepo kwa muda wa miaka 3 tu, wanataka kuendesha Shirika hilo. Ni kweli Wahandisi wetu wana digrii lakini kuwa na digrii sio una uwezo wa kuendesha chombo kikubwa kama kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba hakuna upendeleo tulichofanya sisi tumeteua Shirika la Kimataifa kufanya *interview* na kutuchagulia mtu bora anayefaa kwenye kazi hii. Walioomba kazi ni Waamerika, Waingereza, Watanzania, Wanigeria na watu wa Ghana. Aliyepata ni Mghana ana mkataba wa miaka mitatu tunafanya naye kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa. Sina matangazo ya leo na kwa sababu hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko ameniambia kwamba alikosea kidogo wakati akijibu swali hapa Bungeni leo. Sasa tunataka rekodi za Bunge ziwe sahihi kabisa, nampa nafasi aweze kurekebisha hayo makosa aliyoyafanya.

Ni Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko. Hapo hapo ulipo tu. Aha, ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ndiye aliyekosea. *(Kicheko)*

Ngoja niwasomee *note* niliyoipata.

"Mheshimiwa Spika, najuta na kukujulisha kuwa nimelidanganya Bunge kwa kusema Benki ya Ushirika itashirikisha Benki zote. Mathalani Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro ikijiunga na Benki ya Ushirika ya Kahama ambayo haina mtaji maana yake ni kwamba Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro itabidi iache kutoa mikopo kwa Ushirika huko Kilimanjaro, haitapata faida hivyo itakuwa imejiua yenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Sijui unanishauri nirekebishe vipi usemi wangu huo humu ndani ya Bunge?

Wako Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko."

**MBUNGE FULANI:** Huyo ni tapeli fulani tu.

**SPIKA:** Ni tapeli fulani. Basi nafuta ruhusa niliyotoa. Nafikiri kuna maelezo.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile maelezo yako hayo ni mazito na yataingia katika *Hansard,* unaonaje maandishi hayo yakitolewa kwa wataalamu wa maandishi ijulikane ni maandishi ya nani katika Bunge hili kama kweli Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko hakusema hivyo.

**SPIKA:** Sawa, nakubali ushauri huo, kwa hiyo, tuta-*check* nani aliandika hii na akijulikana atapelekwa kwenye Kamati ya Simpasa apate adhabu. *(Makofi/Kicheko)*

Sina matangazo mengine kwa hiyo, tunaendelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Elimu na Utamaduni

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kuu naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa sababu nilikwishawapa pole wale wote waliopatwa na mikasa na kuwapongeza wote ambao wamepata nafasi mbalimbali katika Bunge letu hili, niende moja kwa moja kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni

pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri ambayo kihistoria kwa kweli wote tunaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitakuwa sikufanya haki kama sitoutambua utendaji wa wafanyakazi katika Wizara hii ya Elimu na Utamaduni wakiongozwa na Katibu Mkuu, mama yetu shupavu, mcheshi Mwantumu Malale. Kwa mara ya kwanza Wizara inayoongozwa na mama imefanya kazi nzuri ya kuratibu shughuli za Wizara na kwa kweli inaonekana wazi kwamba wenzetu wana *vision* na wana mipango na mikakati ya kutekeleza *vision* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu wengi walivyosema katika Bunge hili Wizara imejitahidi sana kutengeneza mpango ambao kama ukitekelezeka kama tulivyoona katika MMEM na sasa hivi kuna mpango wa MMES mimi nitajielekeza katika maeneo matatu muhimu. Kwanza kueleza mafanikio ya MMEM na matatizo yaliyotokea kwenye MMEM yachukuliwe kama mafunzo ili mpango wa MMES ufanikiwe. Ninaamini yalikuwepo mapungufu mengi katika MMEM. Kama tukiyasahihisha katika MMES nina uhakika tutafanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, mapungufu machache ambayo yalitokana na MMEM na ambayo ni lazima yaangaliwe kwa undani sana kwenye mpango huu wa MMES ni utekelezaji ambao haukufikiwa viwango vinavyotakiwa. Utumiaji mbaya wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mpango wa MMEM. Tatu, udhibiti ambao kwa kweli haukutosheleza sana hatimaye kuna maeneo ambayo tumepwaya sana maana kuna maeneo mpaka leo mpango wa MMEM haujakamilika madarasa yalikwishatolewa fedha na nyumba za Walimu zilikwishatolewa zamani sana, lakini bado mpango haujakamilika. Kwa hiyo, mapungufu haya ni budi yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nikija katika mpango wa MMES. Kama alivyosifiwa Waziri na watendaji wake, mimi nauchukua mpango wa MMES kama ndege inayo-*take off* pamoja na hiyo MMEM. Ndege inapoondoka katika uwanja inapaa juu ikitegemea kwamba itatua katika uwanja unaokuwa na sura na hali kama ile ile katika uwanja ule iliyoondokea. Nasema mfano huu kwa sababu mimi nina woga sana. Mpango wa MMES na MMEM tumeupata kutokana na mikopo. Kama tumeupata kutokana na mikopo umepangwa vizuri kwa ufanisi mkubwa. Je, baada ya mwaka 2009 tutaweza kuubeba? Hili ndilo swali ambalo Serikali ni budi ijiulize. Baada ya miaka hii mitano tutakuwa tuna mpango wa kutosha wa kuweza kubeba mpango huu? Walimu watalipwa vizuri, madarasa tuliyonayo yataendelea kutunzwa. Maana uzoefu umeonyesha.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali hii inachukua jukumu la kuelimisha Watanzania kwa pamoja, wakati mpango wa UPE katika mpango wa kutaifisha shule za sekondari toka mashirika ya binafsi ulipofanyika pia nia ilikuwa ni hii hii ya kujenga *capacity* ya nchi hii katika elimu. Yaliyokuja kutokea baada ya miaka 10, 15 na 20 ni haya tuliyoona kuporomoka kwa elimu. Je, kuna mpango gani wa ku-*sustain?*

Sasa hili si la Waziri wa Elimu na Utamaduni peke yake, kwa kweli ni Serikali kwa ujumla. Hatuwezi kuendelea na mikopo hii tutakapofika huko mwishoni

tukashindwa kuilipa tukakwama tena na tukashindwa kuwalipa walimu ambao tumewaajiri. Sasa Serikali ni vizuri iwe na mpango unaoeleweka. Tutapata wapi mapato ya kulipa mikopo baada ya hiyo miaka 40 wakati huo huo tukiwa na uhakika kwamba tunaendeleza yale tuliyoanza leo. Maana bado walimu watahitajika kuongezeka, kulipwa vizuri na watahitajika kuwa na nyumba. Kwa hiyo, mpango huu ni lazima ujibu mambo yatakayotokea kwenye miaka 40 inayokuja ili tusiviweke vizazi vyetu katika hali ya utatanishi kama tulivyokuwa huko mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo sasa ningependa nilizungumze ni yanayohusu eneo langu la jimbo langu. Mimi ninalo tatizo katika sekondari ambazo ziko katika jimbo la Lushoto. Sekondari ya Magamba haina Walimu. Tumeanzisha kidato cha 5 na 6, lakini kwa kweli wanafunzi wanalalamika sana maana hakuna Walimu wa taaluma zinazotakiwa katika shule ile. Naomba sana Waziri atusaidie katika hili. Najua tatizo lipo kwa shule nyingi lakini naomba shule hii ina matatizo mengi kwanza iliunguliwa na jengo la bweni na Serikali nimeiomba ijibu swali langu bado halijajibiwa naamini litajibiwa na sijui nitajibiwa nini. Lakini wanafunzi wanakaa katika hali mbaya sana.

Kwa hiyo, shule ya Magamba iangaliwe na Waziri kwa kweli aipe *priority* kwa sababu imepata mkasa wa kuunguliwa na bweni. Kwa hiyo, wanafunzi wale wanaishi katika maisha magumu sana na hawana walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu, kuna shule ya Mlongwema ambayo pia imeanzishwa hivi karibuni. Shule ya Malibwi ambayo imeanzishwa hivi karibuni zote hazina Walimu. Tunaomba sana mpango wa MMES ufanikiwe, bila kuwa na msingi mzuri wa Walimu basi majengo hayatatusaidia. Maana lengo si majengo. Majengo ni kuongeza *capacity* ya kuwafundishia watoto katika maeneo mazuri. Lakini bila kuboresha upatikanaji wa Walimu na Walimu wazuri kwa kweli matarajio yetu hayatafanikiwa. Sasa namwomba Waziri sambamba na hizi ruzuku na nini zinazotolewa katika Majimbo kuwe na utaratibu wa kutosha sana kupata *quality teachers.* Lazima tupate Walimu wazuri wenye uwezo wa kusimamia mashule haya, wenye uwezo wa kuwa na *vision* na kuhakikisha kwamba yale yanayotarajiwa yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hili niliona nilizungumze kwa uchungu na naamini Waziri atakapokuja kutamka atanihakikishia kwamba shule hizi zinapata walimu. Iko shule ya Ubili nayo imeanzishwa hivi karibuni. Naomba sana tupate walimu hasa si kwa jimbo langu tu lakini shule nyingi ambazo zimeanza hivi karibuni zina uhaba mkubwa wa Walimu na vitendea kazi. Sasa naamini mpango wa MMES unaelekezwa huko. Kwanza kuimarisha hizi ambazo zipo zipate walimu, ziwe na maabara, *library* nzuri na ziweze kuimarika kuliko kuanzisha vipya ambavyo hivi vya nyuma havijatengemaa. Kwa hiyo, naliomba sana hili lieleweke hivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo mimi nitalizungumza kwa ufupi sana na kwa sababu kwa kweli hotuba ya Waziri ni nzuri sina sababu ya kuzungumza sana. Maana mtu akifanya kitu kizuri kumchokonoa chokonoa kwanza inampunguza imani na inamtia wasi wasi. Sasa napenda kumhakikishia Waziri kwamba kazi yake ni nzuri. Mimi haya

ninayozungumza ni kuboresha tu ambalo ningeomba nizungumzie hili suala la walimu. Wenzangu wengi walimelizungumza lakini ni vizuri kulisema tena.

Mheshimiwa Spika, mwalimu ni kama kuku anayetaga mayai. Kama hutampa mazingira mazuri huwezi ukapata mayai. Sasa kama walimu wataendelea kuishi katika hali ya wasi wasi, kukosa haki zao za msingi, kutokuwa na chombo cha kuwasimamia, kwa ukweli katika Wizara hili suala linakuwa na upeo wa kuhakikisha tatizo la mwalimu litatuliwe linapohitajika wapate mishahara yao kwa wakati, wanapohamishwa walipwe haki zao kwa wakati na wapate yale ambayo yanayowahusu kwa wakati. Mimi naamini nia yetu ya kujenga msingi wa kielimu katika nchi hii hatutafanikiwa maana hawa ndio wanaotaga hayo mayai. Matarajio yetu ni kupata watu walioelimika katika Taifa utapata wapi kama wale wanaofundisha watu hawa wako hawana moyo na saa zote wako katika wasi wasi.

Kwa hiyo, hili la walimu kulipwa haki zao, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa kutoa kauli lakini kutokana na kiasi ambacho walimu wenyewe wamesema chama chao na kiasi kilichotengwa tunaamini bado kiwango kilichotengwa ni kidogo. Kwa hiyo, Serikali itafute kila njia tatizo hili limalizike ili haya tunayoyaweka kwenye msingi yafanikiwe kinyume chake tunakuwa tunampelekea mtoto mtu akakulelee wakati hana imani na wewe, hatamlea mwanao vizuri. Atamlea vibaya matokeo yake hutafanikiwa kumpata mtoto mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nachukua nafasi hii na natangulia kusema sina sababu ya kuhoji sana. Namwomba Waziri anisaidie katika shule zile ambazo hazina walimu, ambazo tayari zimekwishaanzishwa, ziimarike na hasa shule katika jimbo langu kama nilivyozitaja. Lakini vile vile nimwombe azidi kuimarisha walimu wapate haki zao ili waweze kutoa mchango unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaachie wenzangu, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia moja kwa kazi nzuri ya Waziri na watendaji wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu mdogo kuhusu Bajeti iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakupa pole kwa tukio lililotokea hivi asubuhi, kwa kweli ni *embarrassment,* watu wazima kama sisi viongozi kutokea na lile suala ambalo limetokea. Pole sana.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Philip Marmo, kwa wazo alilokuwa ametoa ili kujielekeza katika hali ya utendaji na kuona kwamba yule aliyefanya tendo hilo labda atawajibishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache ningetoa pongezi nyingi sana, kama wenzangu wengi walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu wake, watendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa kazi kubwa

sana waliyokuwa wameifanya. Kwa kweli hotuba hii kama wenzangu waliotangulia kuzungumza kwamba tupo kuchangia kiasi cha kuchangia tu lakini imekamilika.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, ambayo mimi nikiwa ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati hiyo tuliokuwa tumesimama vyema na Waziri pamoja na watendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuifikisha hotuba hii hapa ilipo. Kwa hiyo, nadhani na sisi mngetufagilia vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza zaidi katika taasisi. Kama nilivyozungumza kwamba sisi ndio tuliokuwa tumo katika Kamati ya Huduma za Jamii na tulipitia Wizara hii na vitengo mbalimbali. Sasa mimi nizungumzie suala moja ambalo zaidi kushughulikia masuala haya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiw Spika, taasisi ya kwanza labda ningeizungumzia ni Baraza la Mitihani. Kuna mwenzangu jana, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, alizungumza lakini na sisi tunatilia mkazo kwamba Baraza la Mitihani ni chombo ambacho kilivyojengeka ni chombo cha Kitaifa na ni chombo ambacho kinategemewa na nchi nzima. Ufuatiliaji mzima wa Serikali inategemea utendaji wa chombo kile chenyewe kina matatizo. Matatizo yaliyokuwepo tulikuwa tunaomba Serikali na tunamwomba Waziri kama tulivyomwomba nyuma kwamba kitengo hiki kisaidiwe kupewa misaada na kupewa Bajeti iliyokuwa ya uhakika ili kuweza kuendeleza yale ambayo walitakiwa wayatekeleze.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kama kitavurugika nchi nzima itavurugika. Ni mfano wa hivi karibuni tumesikia masuala ya mitihani na si nchi nzima ni baadhi tu ya shule ambazo zilikuwa labda zina matatizo.

Kwa vile hayajatolewa kama ilivyokuwa imetegemewa na tumesikia magazetini malalamiko mbalimbali ambayo yamejitokeza kefu kama chombo hiki kishindwe kufanya wajibu wake kwa sababu ya ukata au ufinyu wa Bajeti au ufinyu wa taratibu za utendaji tutafika wapi. Kwa hiyo, mimi ningeomba chombo hiki kisaidiwe kama inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa kama ya mashine kongwe za kufanyia kazi na kuna utaalamu wa hali ya juu. Tulifika mahali pale tukakutana na Mkurugenzi tukamwuliza kuhusu maelezo tuliyokuwa tumepewa tukawa tunahofia kwamba kama atakufa huyu ambaye mliyekuwa mmemkabidhi kushughulikia masuala haya ya uwekaji wa rekodi wa utaalam wa *computer* mtampata mtu gani mwingine.

Mheshimiwa Spika, majibu tukaambiwa kwamba wako watu wawili, watatu, wako tayari na *inshallah* huyo aliyekuwepo Mungu atampa uhai mrefu. Sasa nazungumza kwamba, taasisi ipewe nyenzo, ili kiweze kufanya kazi zake barabara kimajengo, kivifaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pili, ningekuja nikazungumzia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Pale sisi tulipokwenda tumeona maajabu. Kama tungepata nafasi baadhi yetu Wabunge tukienda pale tungejiridhisha kwa hizi ni taasisi muhimu sana pale yenyewe tunavyoizungumza kama ni Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na tukaona kwamba watu wazima tu ndio wanaelekea kule, sivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kule ndani wanasomeshwa watu na kwa kweli ni *solution* au suluhu ya wale watu waliokosa kujiendeleza katika elimu ya juu na elimu nyinginezo. Pale tumewakuta vijana wa *Form Four* wanajitayarisha kwenye masomo ya *Form Five.* Tumewakuta vijana *Form Six* wanajitayarisha kwa ajili ya kufanya mitihani ya *Form Six* kuingia Chuo Kikuu na vile vile tumewakuta pale vijana ambao wanasomeshwa fani za sheria, polisi na watu wengine. Tofauti kabisa vile ambavyo tunavyokiona kwa mwelekeo wa nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nacho ningemwomba Mheshimiwa Waziri, yeye ametupeleka pale kwa kutusaidia sio kwamba kwa kuja kutoa shutuma au vipi. Lakini nasema namwomba Mheshimiwa Waziri kile chombo nacho akisaidie kina matatizo nacho yaani hata rekodi kuweka unakuta wanatumia mafaili na vikaratasi wanapachika hivi kama wanauza bidhaa. Samahani kusema kama wanauza bidhaa, nadhani hili lifahamike ndio natumia lugha hiyo. Kwa hiyo, tungeomba na pale napo paangaliwe wanavyotoa Elimu ya Posta na kuna haja ya kuangaliwa na kuona kwamba taasisi ile nayo inaelekezwa kule ambako itawaletea maendeleo baadaye.

Mheshimiwa Spika, ningekuja zaidi nikagota katika Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET).* Nafikiri sawa sawa ni *TET.* Tumeangalia hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri matokeo ya mtihani kidato cha 4. Katika mwelekeo wake wote tumejikuta kwamba kadri tunavyokwenda vijana wetu ndivyo wanavyofanya vizuri mwaka hata mwaka. *Statistics* wanazotupa Wizara ilikuwa hakuna haja ya kujiuliza wala haja ya kueleza kila kitu kiko wazi kabisa. Lakini hii ni nchi moja kwa maana ya Tanzania tuna tatizo kubwa sana la kupasisha watoto.

Mheshimiwa Spika, ningeomba hili tatizo likaonekana kwa mwelekeo wake. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyokuwa amei-*quote* jana Waziri wakati anawasilisha hapa hotuba yake, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja jina lake limenitoka kidogo lakini naye alizungumzia suala la umuhimu wa elimu kama sisi sote tunavyojua umuhimu wa elimu. Sasa kwenye kutoa elimu, kimoja katika vigezo kinachochukuliwa ukiacha suala la mtihani ni nini kinasomeshwa na nani wanasomesha.

Mheshimiwa Spika, tulichokigundua ni kwamba nimesema mwanzo nchi moja kwa maana ya Tanzania, ni kweli kwamba ni nchi moja. Tuna Serikali mbili lakini elimu haina Serikali. Elimu, afya haina Serikali. Sisi tulipofika kwamba kama tungeweka elimu Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Muungano nachelea tutafika mahali siku moja kule Visiwani tutazama kabla siku zetu za kufika kuzama na Mungu atatulinda *Inshallah. Amin.*

Mheshimiwa Spika, nataka kunukuu maelezo yaliyokuwa yametolewa hapa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kama ni ushauri kwa Wizara hii au kwa Serikali hizi. Wanasema: "Tunashauri kuwa ili kuwatendea haki watahiniwa, ni vizuri kuwepo makubaliano kati ya Serikali zote mbili kuhusu mitaala inayotumika nchini kote katika ngazi zilizotajwa hapo juu hasa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Elimu Zanzibar, Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani Tanzania na wadau wote wa Elimu kutoa tathmini."

Mheshimiwa Spika, kwa suala hili vile vile amezungumzia kwamba chombo hiki kingekuwa ni cha Muungano kwa sababu matokeo tuliyonayo hapa, matokeo ya kidato cha nne Zanzibar *division I, II, III* walio-*pass* wamepata *19.5 percent, Mainland 45.9 percent,* tatizo ni nini? Tatizo moja lililopo ni kwamba, mitaala inayotolewa katika *Primary School* Zanzibar na Bara ni tofauti na vile vile mitaala inayotolewa katika *Secondary School* Zanzibar na Bara ni tofauti. Wanasomeshwa mitaala tofauti, watafanya vipi mitihani sawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tumeliona, ukiacha suala la kuwa mazingira ya *Primary School* na mazingira ya *Secondary School* kuna mambo ya *Capitation Grants* ambayo sisi kule hatuna kabisa, lakini tunafukuzia huko huko, ikifika wakati tukae pamoja katika mtihani.

Mheshimiwa Spika, nina kigugumizi kidogo, utanisamehe.

Mheshimiwa Spika, ninachokizungumza ni kwamba, hii hoja iliyotolewa tunamwomba Mheshimiwa Waziri na tunaiomba Serikali kwamba hili suala la elimu lisiwe ni suala la Serikali ya Zanzibar wala Serikali ya Bara. Katika suala la kusomesha walimu wamepata *training* mbalimbali, kule wana *syllabus* yao na huku wana *syllabus* yao. Watafanyaje mitihani ya aina moja.Tunaomba hili nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, ukiacha suala la mazingira yalivyo, mfano sasa kuna suala hili la MMEM, lakini Zanzibar hatuna! Kuna suala la MMES, Zanzibar hatuna! Kama huu ni mkopo, kwa nini tusingekwenda pamoja bwana? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshazungumza na Waziri, suala hili si mara moja wala mbili, lakini hizi ndiyo *results* ambazo tunazo sasa hivi hatuwezi kwenda tutadanganyana. Ikiwa dunia nzima tunakwenda katika suala kama elimu, utandawazi au nini, hapa tutafika vipi kwamba tuna 1.8 *percent out of 9.9 percent? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kama wenzangu waliotangulia ningemuomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kuondoa zile kero ili sifa yake na sifa ya Wizara hii ibakie pale pale. Kero ndogo ndogo za masuala ya mishahara na masuala ya bakaa za pesa ambazo zilikuwa zilipwe, tunaomba Mheshimiwa Waziri isafishe hiyo. Ukisafisha hiyo umesafisha Wizara yako, umetusafishia na Kamati yetu vile vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri pamoja na safu nzima ya Watendaji wa Wizara hiyo. Ni wachapakazi hodari, naomba wote tuige mfano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, ni kati ya Mawaziri wachache waliofika Loliondo kwa gari na kurudi na kufanya ziara vijijini. Ninawapongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nakubali kabisa ni kweli tumepata mafanikio makubwa kwenye Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Msingi, MMEM. Mafanikio tumeyapata makubwa kabisa na kutokana na mafanikio hayo, kutokana na uzoefu huo, nina hakika kwamba zoezi hili la kuboresha Elimu ya Sekondari nalo tutafanikiwa kwa kiwango kikubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, ila kwenye Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Msingi, pamoja na mafanikio makubwa, naona tulikuwa na matatizo kadhaa ambayo yamezorotesha elimu nchini na haya matatizo ninayagawanya kwenye maeneo matatu.

Kwanza kabisa naona kulikuwa na Ujenzi wa Shule za Msingi ambao haukwenda sambamba na upatikanaji wa walimu katika shule hizo. Hili nalo kwa kiwango kikubwa limechangia kuzorotesha elimu nchini kwa sababu pamekuwepo na tofauti kati ya shule za vijijini na shule zilizoko mijini. Kwa shule zilizoko mijini wamekuwa na walimu wengi na walimu ambao ni bora, wakati ambapo shule za vijijini hawakuwa na walimu wa kutosha wala hawakuwa na walimu bora. Matokeo yake pamejengeka tofauti kati ya watoto wanaosoma shule za vijijini na wanaosoma shule za mijini. Naomba Mheshimiwa Waziri tukazane kuondoa tofauti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba, kumekuwa na ucheleweshwaji wa mishahara ya walimu. Ukifika kwenye Makao Makuu ya Wilaya wakati wa mwisho wa mwezi ukiona idadi ya walimu ambao wamekuja kufuata mishahara yao utafikiria kuna maandamano, kumbe siyo maandamano wamekuja kutafuta haki yao, haki ya kulipwa, haki ya kupata mishahara. Maana yake ni kwamba, kwa wiki nzima wanafunzi watakaa bila Walimu. Kosa siyo la walimu hao, kosa siyo la wanafunzi hao, ila wanaoadhibiwa ni wanafunzi. Nafikiri kosa lipo kwenye utaratibu wetu wa kutoa mishahara hiyo. Naomba nalo hili lirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukimtegemea mwalimu aliyeko Ngorongoro Kakesio aende mpaka Karatu zaidi ya kilometa 100 kufuata mshahara wake, itamchukua zaidi ya wiki moja. Mwalimu anayefundisha Shule ya Msingi Ngaresero atoke Ngaresero aende Loliondo kufuata mshahara wake kilometa 120, itamchukua zaidi ya wiki moja au mwalimu anayetoka Piyaya aende Loliondo, hakuna usafiri anaenda kwa mguu,

itamchukua zaidi ya wiki moja.  Kwa hiyo, kutokana na matatizo hayo tutaendelea kuzorotesha upatikanaji wa elimu nchini hususan kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo naliona ni tatizo lililopo kwenye maeneo ya wafugaji.  Kutokana na mazingira magumu wanamoishi wenzetu wafugaji, kutokana na utamaduni wao, mila na desturi zao mara nyingi idadi ile ya wanafunzi 40 kwa darasa haiwezi kukamilika na kwa mujibu wa taratibu na kanuni za Wizara ya Elimu na Utamaduni, wana *ratio* ya mwalimu mmoja kwa watoto arobaini (1:40).  Kwa maeneo ya wafugaji kutokana na matatizo ambayo nimeyasema, idadi hiyo inapungua na inapopungua wale wanafunzi wanakosa haki ya kuwa na mwalimu.  Binafsi naona hili ni tatizo kubwa, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa makini kwa sababu ni tatizo la kudumu *(perennial problem)* ukiendelea kufuata *ratio* hiyo.  Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aitazame tena upya sera hiyo au *ratio* hiyo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo, moja, naona tukiendelea na *ratio* hiyo itaendelea kuwakandamiza wafugaji na kuwanyima watoto wao haki ya kuwapata walimu.  Pili, tukiendelea na utaratibu huo, utaratibu huo unapingana na tamko na Dakar la mwaka 2000, tamko ambalo linataka kila mwanafunzi awe na haki na nafasi ya kupata Elimu ya Msingi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alivyokuwa akijibu swali langu namba 100 kwenye Bunge lako hili Tukufu alisema yafuatayo na naomba kunukuu: “Kimsingi Serikali ya Tanzania imekubaliana na Jumuiya ya Kimataifa na kuazimia kutoa Elimu ya Msingi kwa watoto wote kwa mujibu wa tamko la Dakar la mwaka 2000.”  Kwa tamko hilo, nafikiri tulizingatie, tuhakikishe kwamba watoto wanaotoka kwenye jamii za wafugaji na wao wanapata haki ya kuwapata walimu na kupata Elimu ya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya tatu ni kwamba, naona utaratibu huu wa *ratio* ya mwalimu mmoja kwa wanafunzi arobaini kwa maeneo ya wafugaji unapingana vile vile na maelekezo ya Katiba ya Nchi na nafurahi kwamba Waziri naye ametambua hilo, ame-*quote* hiyo Katiba na mimi nimeiangalia na naomba ku-*quote* kama na yeye alivyonukuu kwenye ukurasa wa 11 wa hotuba yake, anasema hivi: “Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo.”  Mwisho wa kunukuu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachojaribu kusema hapa ni kwamba, wanafunzi/watoto wanaotoka kwenye maeneo ya wafugaji wana haki ya kupata elimu kama Watanzania wengine.  Siyo kwamba tunaomba fadhila au wanaomba fadhila, hapana, ni haki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, niseme machache kuhusu utamaduni. Nakubali kabisa lugha ni sehemu kubwa ya utamaduni wa Taifa lolote lile.  Kwetu Tanzania Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wetu.   Lakini ni ukweli vile vile

usiopingika kwamba katika Taifa letu la Tanzania tunazo lugha nyingine zaidi ya Kiswahili ambazo ni sehemu ya urithi, ni sehemu ya utajiri wa utamaduni wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kidogo pamoja na uzuri wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ni kama ana shida kugusia ukweli huu. Tuna lugha mbalimbali sehemu ya utajiri wetu na mimi nafikiri lengo la kwetu kama Taifa ni kujaribu kuwa pamoja, kwa Kiingereza nitasema ni *unity in a diversity and not uniformity* na tutafikia hapo kwa kutambua mchango wa kila kabila, kwa kutambua mchango wa kila lugha katika kuchangia utamaduni wa Taifa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona mwenzangu Mheshimiwa Omar Chubi, leo hayuko hapa. Wakati mmoja alizungumza akasema: "Bwana, kuna watu hawavai vizuri wanaenda uchi." Mimi nadhani Utanzania siyo kuvaa suruali tu, Utanzania siyo kuvaa kofia na kanzu pamoja na koti tu, ni zaidi ya hayo. Utanzania siyo kuvaa *chew and lie,* hapana! Bali ni mchanganyiko wa mambo hayo yote na ndiyo ninaita *unity in a diversity and not uniformity.* Naomba Waziri tuliangalie hili nalo tutoe msisitizo unaostahili tutafute namna na mbinu za kukuza tamaduni hizo kwa ajili ya kuboresha utamaduni wa Tanzania kama Taifa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa ruksa yako nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara. Nawapongeza kutokana na utendaji wao mzuri. Mipango yao waliyoweka mwaka 2003/2004 imekamilika vizuri kama zaidi ya asilimia 80. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Pili, nawapongeza sana kutokana na mipango wanayotarajia kuifanya katika mwaka wa 2004/2005. Ni mpango mzuri, ni mpango unaoelekea pengine tutafika mahali Elimu ya Sekondari itatolewa bure. Hayo yote yanaonyesha katika mipango kama kupunguza ada na tunaelekea huko. Kwa hiyo, nawapongeza kwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee jambo moja zito sana na kubwa lililofanyika nalo ni mpango wa MMEM katika nchi hii. Sitaki kurudia mazuri na makubwa mengi yaliyotokea, hayo yanafahamika na mimi naungana na Mheshimiwa Henry Shekiffu. Niseme tu matatizo ya hapa na pale yaliyojitokeza katika MMEM. Hiyo itakuwa ni vizuri ili yasiweze kutokea kwa baadaye na katika mpango wa MMES tunaotegemea kuufanya.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni kwamba, katika mpango wa MMEM tulielezwa kuwa ili mwalimu mkuu, waweze kuendesha shule kwa mwaka mzima kwa

kila mtoto angepewa dola 10, lakini nini kilichotokea? Pesa zilizotolewa hazikufika dola 10 katika shule za Jimbo langu. Pesa zilizotolewa ni dola 2 badala ya dola 10! Sasa katika hali hiyo ilikuwa ni vigumu sana kwa walimu kuendesha shule. Wazazi wameambiwa ada hamna, wazazi wameambiwa hakuna mchango na mwalimu hana fedha za kuendesha shule. Kwa kweli ilikuwa ni tatizo kubwa na Mwalimu Mkuu aliendesha shule katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba tatizo hili katika kipindi kijacho lisitokee na napenda nifahamu katika kipindi kijacho katika Bajeti hii imezingatia nini. Je, Wizara itatoa dola 10 kwa kila mtoto ili mipango ya Wizara iliyowekwa kwa kuboresha Elimu ya Msingi iweze kufanikishwa? Kwa hiyo, ningeomba wakati Mheshimiwa Waziri akielezea katika mpango wa MMEM kipindi cha 2004/2005, aeleze kama dola 10 kwa mtoto zitatolewa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa MMEM ulikuwa na lengo zuri kuwa kila darasa liwe na watoto 45 ili mwalimu aweze kumudu kuwasomesha watoto vizuri, lakini hadi hii leo kuna shule nyingi tu zina watoto zaidi ya 100 kwa darasa moja. Sasa ningeomba shule hizo zote zenye watoto wengi kwa darasa zingeweza kuorodheshwa ili mipango maalum ikafanyika kufanikisha programu nzuri ya MMEM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni juu ya shule zilizoko pembezoni. Shule za pembezoni ziko mbali kabisa na Wilaya, Makao Makuu ya Mkoa na zina hali mbaya sana hasa kwa upande wa walimu na upande wa vifaa. Shule hizo watoto hawasomeshwi siku 194 zilizowekwa, walimu wanafuata mishahara Makao Makuu ya Wilaya wanatumia wiki nzima. Kwa hiyo, siku zilizopangwa ili walimu waweze kusomesha hizo siku 194 hazifiki. Kwa mwaka watoto wanasomeshwa siku chini ya 194, wanasomeshwa pengine siku 80 tu, lakini cha ajabu sasa mitihani wanapimwa kulingana na wale wenye sifa zote, wana walimu wengi, wana vifaa na walimu wanafundisha siku 194 kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, wote wanapimwa kwa pamoja wakati hawa wana hali mbaya sana. Hawana walimu, hawana vifaa, lakini mtihani ni mmoja!

Mheshimiwa Spika, katika hali hii shule za pembezoni zote nchi hii hatuwatendei haki. Ingefaa sana walimu wanaofanya kazi katika shule hizi za pembezoni wangepewa vivutio. Hali hii ikiendelea kwa kweli tutajenga matabaka makubwa sana. Tutajenga wananchi wanaozunguka Wilaya, wanaozunguka Mikoa, wanaozunguka Dar es Salaam ndiyo hao tu watakaokuwa na elimu na wale wote wanaokaa pembezoni watabaki bila elimu. Hivi wote tukae Dar es Salaam? Watu wote tukae tukizunguka Wilaya na Mikoa?

Mheshimiwa Spika, ningeiomba sana Wizara ifanye utafiti kwa hili, ni suala zito. Kama hatua makusudi hazitaweza kuchukuliwa za kutatua tatizo hili, kwa kweli Wananchi wa pembezoni watabaki bila elimu. Kuna shule nyingine miaka 10 hadi 15 hakuna hata mtoto mmoja anayechaguliwa kwenda sekondari! Tatizo siyo kusema watu wote wanoishi huko ni wapumbavu, hawana akili bali hawafundishwi. Mwalimu anatumia kwa kila mwezi wiki mbili kufuata mshahara. Kwa suala hilo, ningeomba Serikali iwape vivutio walimu. Waorodheshe shule zote za pembezoni, walimu wanaopelekwa huko wapewe vivutio maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule ni walimu, wanafunzi, vifaa na majengo. Mradi wa MMEM umeangalia upande mmoja. Mradi huu haukugusa matatizo ya walimu na walimu ni muhimu, bila walimu watoto hawawezi kupata elimu. Walimu wana madeni chungu nzima, walimu wanapandishwa vyeo, wanapata barua za *promotion* mara tatu, mara nne, hakuna mabadiliko ya mshahara. Walimu wanadai haki zao za uhamisho, walimu wanadai malipo yao ya likizo, katika hali hii nani anaweza kutoa elimu vizuri? Nani anaweza kufanya kazi vizuri kama haki zake za msingi hapewi? Barua za *promotion* wanapata walimu na hasa walimu wale wale wa pembezoni. Barua za *promotion* wanapelekewa, lakini mshahara hawabadilishi. Hivi kweli huyu mwalimu atafanya kazi? Walimu siku hizi wanapelekwa toka Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine, miezi sita hawapewi mshahara. Kwa hiyo, ningeomba matatizo haya Wizara na Serikali kwa jumla iyafanyie kazi watafute ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo juu ya Sekondari. Nina Sekondari mbili za Serikali katika Jimbo langu, Liuli na Lundo. Shule hizo nazo ziko pembezoni, zina matatizo kama haya niliyosema. Naishukuru Wizara inapeleka walimu, lakini walimu hawakai kule, wanaondoka kutokana na mazingira magumu. Tuna upungufu wa walimu hasa wa sayansi katika Shule za Lundo na Liuli.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nilipeleka maombi ya gari. Shule hizi ziko mbali sana na Wilaya, wanapata tabu sana juu ya usafiri. Kwa hiyo, niliomba gari kwa kila shule, kama haiwezekani walau hata gari moja iweze kutoa huduma kwa shule hizo mbili. Kwa hiyo, naikumbusha Wizara inifikirie kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sababu kengele ya kwanza imeshagonga ni juu ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Baraza hili linafanya kazi vizuri sana, lakini nashindwa kuelewa, waniweke sawa kwa hili. Iweje wakati shule imefanya vizuri sana Baraza linashangaa? Baraza halishangai wakati shule haitoi mtoto hata mmoja kwenda sekondari na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kwa shule kama hiyo. Hivi mitihani inayotungwa ili wanafunzi wetu waanguke? Wakianguka ndiyo sahihi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea shule ambayo watoto hawafaulu mwaka hadi mwaka, miaka 10 watoto hawafaulu, kama wamefaulu sana ni daraja la nne watoto wawili lakini hatua zingechukuliwa. Lakini hakuna Tume inayoundwa, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kwa shule hiyo kwa lengo la kuboresha hiyo shule. Lakini watoto wakifaulu sana Baraza linashtuka, Tume inaundwa, hivi mitihani inatayarishwa ili watoto wote waanguke? Kwa kweli ni jambo la kushangaza sana! Katika karne hii Baraza linashangaa watoto kufaulu sana na Tume inaundwa, lakini wakianguka wote hakuna Tume, hakuna kuchunguza wala hakuna hatua zozote zinazochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama kuna tatizo hivi kweli katika uhai wa binadamu unaweza ukacheleweshamiezi sita? Ni kwa nini ufumbuzi usitafutwe kwa haraka na uamuzi ukatolewa? Miezi sita uamuzi haujatolewa na chombo kizito, muhimu kwa wanajamii kama Baraza la Mitihani la Tanzania! Kwa kweli ni jambo ambalo halipendezi, linatisha. Mnatayarisha mitihani ili watoto wote waanguke, watoto

wasifaulu, wakifaulu ni ajabu! Sasa kwa nini zipo shule, kwa nini tunasomesha walimu ili wasomeshe watoto wetu waanguke na siyo wafaulu? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini Baraza halichukui hatua kwa shule zile ambazo mwaka hadi mwaka watoto wanaanguka? Miaka 10 watoto wanaanguka tu, wame-*pass* sana *division IV* na hakuna hatua yoyote, hakuna Tume, hakun uchunguzi na wala hakuna njia inayotafutwa ili shule ile iweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nashukuru kupata nafasi asubuhi hii ya leo kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Lakini na mimi nitoe pole zangu kwa mfiwa ambaye ameachwa na Marehemu Yete Mwalyego huko Mbeya Vijijini, Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mimi kama mwenzangu napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu ndugu Mwantumu Malale na wakurugenzi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Napongeza kwa sababu hotuba yao imeandikwa vizuri na imetuonyesha kwamba Wizara ya Elimu na Utamaduni inaweza kuchambua shughuli mbalimbali kwa kuweka takwimu ili tuweze kulinganisha maendeleo yetu ya elimu katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza sana Serikali kwa kuleta mapinduzi ya elimu hapa Tanzania. Haya ni mapinduzi makubwa sana. Labda nitakapokuwa naelezea hoja zangu tutaona kwamba ni vipi tamaa kubwa tuliyokuwa nayo kwa sisi Watanzania kuweza kunyanyua kiwango na ubora wa elimu katika nchi yetu. Naamini kwamba Serikali, pia baadaye itaandaa mipango kuhusu vyuo vya elimu ya juu ili kuweza kupokea haya mafanikio ambayo yatapatikana kutokana na mpango wa *secondary school* (MMES). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu siku zote kwenye pyramid ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, tunaonyesha kwamba wakati wa *O-Level* takwimu zinasema kwamba wanafunzi wanaume, 158,028 pia tuna wanafunzi 138,000 wanawake. Lakini tukija kwenye *A-Level* takwimu zinaanza kushuka tena sana, tunakuja kwenye 18,027 kwa wanaume na wanawake kutoka 138,000 tunashukua mpaka 8,752. Ukienda kwenye *University* inashuka zaidi 13,654 na kwa wanawake ni 4,767.

Sasa naomba hapa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwenye *pyramid* hii kila siku ndiyo hivi hivi labda kwa huu mpango wa MMES tunategemea itabadilika kwa sababu tumepata *O-Level* labda wanaandaliwa vizuri ili waweze kupata wengi kwenye *A-level* na *University.* Lakini hapa ningependa kusema kwamba wanafunzi wasichana wanashuka sana, labda Mheshimiwa Waziri na wataalam waangalie tatizo ni nini? Tunazungumza siku zote, kwamba tutasaidia, kuna upendeleo lakini bado takwimu iko chini sana.

Mheshimiwa Spika, sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri, labda ashirikiane na ndugu Besakoda, Mkuu wa Kitengo kule *University* ambaye anashughulikia Idara ya Jinsia *(gender)* na Maendeleo tuweze kushirikiane ili tuweze kuona kwa nini wasichana idadi inashuka kubwa sana. *(Makofi)*

Pia labda tuimarishe labda hosteli za wasichana ili wasichana wawe wengi kwenye hosteli labda wakipata walimu, wakipata nyenzo mbalimbali labda idadi itaongezeka. Mimi nilikuwa naomba hili, tumechoka kuona tena hii *pyramid* na hii *pyramid* iko ndogo halafu wasichana wako chini ambao ndiyo tunategemea kwenye maamuzi wanawake waamue sawa sawa na wanaume tutapata wapi kama huko hawajapata msukumo mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari tofauti kubwa hii imeonekana kwa hiyo, mimi nampongeza Waziri kwa mpango wa MMES. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa sababu umetuonyesha kwamba kutoka mwaka 2004 mpaka mwaka 2009 takwimu zinaonyesha kwamba idadi za wanafunzi wanaojiunga *secondary schools* zitaongezeka kidato cha tano, kidato cha sita, pia kupunguzwa mzigo wa elimu ya sekondari kwa familia kwa kupunguza ada kutoka 40,000 mpaka 20,000 tunakupongeza. Umetuambia ujenzi wa nyumba za walimu zitafika kwenye nyumba 8,000 ingawa sasa tayari kama nyumba 1,000 na zaidi. Umeeleza hapa vyumba vya madarasa vitakuwa na wanafunzi 40 kwa kila darasa. Kwa hiyo, hili tunapongeza maana walimu wote tunangoja ili tuone mafanikio yetu. *(Makofi)*

Lakini kuna suala moja ambalo Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa ana-*wind up* na mimi ningependa kufahamu zaidi wametuambia katika vitabu hapa kwamba kuna taarifa za utafiti zimefanywa za kufuatilia ubora wa elimu nchi 15 za Kusini mwa Afrika.

Mimi ningependa kujua taarifa hii inaeleza nini ili tuweze kujiona na sisi Tanzania tuko wapi au tunaelekea wapi. Kwa hiyo, ningeomba taarifa hii tupate na Waheshimiwa Wabunge wote tuelewe maendeleo haya na tujue katika nchi hizi 15 sisi tuko wapi. Pia katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba mfumo wa usimamiaji wa elimu utaboreshwa na mimi hilo nimefurahi zaidi kwa sababu bila mpango huu kusimamiwa itakuwa kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi mchango wangu kwa haya mazuri yote Mheshimiwa Waziri, aliyotueleza tuliyompongeza na tamaa tuliyopata nina swali moja kidogo linanitatiza, mwenzangu amesema hapa lakini mimi naona kwenye ukurasa wa 51 juu ya takwimu linanitatiza kuhusu Zanzibar. Linanitatiza kwa sababu katika matokeo ya mtihani ya kidato cha nne imeonekana hapa kwamba kwa Tanzania Bara daraja la kwanza ni 9.9% ukija darasa la kwanza Zanzibar kwa 1.8% lakini ukija daraja la nne sisi ndiyo tumeshika mkia, 72.3% wakati 44.3%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwamba hawa wanafunzi kwa nini waadhibike, sote hapa wenzangu wamesema tunakwenda kwenye mtihani mmoja, sasa inakuaje mitaala au maandalizi ya MMES iwe Tanzania Bara, Zanzibar usiweko?

Mimi sielewi kwa sababu hawa wanafunzi wote wanafanya mtihani mmoja. Mfano mimi nina timu ya Mlandege, katika Jimbo langu la Mlandege labda tuchukulie mfano timu ya Mpwapwa mimi timu yangu ina uzoefu, imecheza sana *first division* unakwenda kumshindanisha na Mpwapwa si tutamfunga magoli 10? Sasa na Zanzibar leo mimi nina *Vikokotoni Secondary School* na *Lumumba Secondary School,* hawana maabara, hawana vitabu, hamna *libraries,* hawana vitabu vya ziada, vya kiada mara nyingine yule pale Mheshimiwa Naibu Waziri Sakila, nakwenda nikimwomba ndiyo napeleka, *why?* Kwa nini? Ndiyo ni jimbo langu, ni kwetu lakini kwa nini na mpango huu wa upo MMES na mzuri na tunaandaa vijana wote watafanya mtihani mmoja. Hapa mimi sipendi kusikia mambo ya Katiba kwamba mpaka Katiba ibadilishe, Muungano hapa ni ushirikiano hatutaki mambo ya kuwa si Muungano mbona tunafanya elimu ya juu pamoja, mbona tuna mtihani pamoja, sasa kwa nini hii kidato cha nne tu kina tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri, tusiwaumize hawa vijana hii hali mbaya ya takwimu hapa imewekwa kabisa tunaona 1% halafu tutaandaliwa wenzetu watakwenda huko kwenye 50% sisi tunarudi 0% maana yake nini? Hawa vijana ni wetu sote, Tanzania ni yetu moja, kama mengi tulishaweza kuunganisha, mengine tunasema kwa ushirikiano. Namshukuru Mheshimiwa Joseph Mungai ameshirikiana sana na Waziri wa Elimu wetu kule wako pamoja kila mahali. Sasa hili hamulioni tatizo liko wapi? Wabunge wa Zanzibar wamelalamika kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niendelee lakini naomba hili lishughulikiwe kwa sababu ni haki ya kila mwanafunzi wa Tanzania apate elimu sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka mikoa iliyobaki nyuma kielimu. Mimi ni mtafiti na naamini Wizara ya Elimu wanao watafiti na humu ndani ya Bunge wako watafiti, Mheshimiwa Waziri, tuombe tukusaidie kwa nini mikoa hii mpaka leo, elimu iko nyuma? Hapa imetajwa Mikoa ya Kigoma, Lindi, Tabora, labda mazingira ya kijiografua ya *historical background* mambo mengi tu.

Kwa hiyo, naomba upendeleo maalum upelekwe kwenye Mikoa hii ili twende sambamba siyo wengine wanaendelea, wengine nyuma, sote ni Watanzania, tutakuja kujilaumu sisi wenyewe ambao tunawakilisha wenzetu. Kwa hiyo, hili nakuomba ulitafutie ufumbuzi. Halafu kule kwa mfano kule Kilwa nimeona hata kalo za shule wazazi hawana, watoto wanafaulu wanashindwa kulipiwa. Sasa ukisema ada shilingi 20,000, shilingi 40,000 hata hiyo, 20,000 hawana. Sasa hapa tuangalie hii Mikoa ambayo iko nyuma kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu walimu, mimi natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu tutaajiri kama walimu 10,000 na zaidi, lakini kubwa nasema na mishahara yao itengwe, tatizo la mishahara lisije tena likaleta matatizo hapa. Lakini Mheshimiwa Waziri, moja tu hapa wale walimu wabaya waliowatia mimba wanafunzi wa kike wachukuliwe hatua za kisheria, kwa sababu tunaandaa mipango mizuri kumbe kuna wengine wanatoa macho na udenda kwa watoto wa watu wasichana.

Mheshimiwa Waziri, hapa tuwachukulie hatua na tuwataje wajulikane ni nani hao ambao roho zao haziwezi kujihisi kwamba wao ni dhamana wa watoto wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa napenda kusema ni la elimu ya watu wazima. Mimi nilikuwa mkurugenzi kwa miaka mingi naelewa kwa hiyo, hapa naungana mkono na kamati ambayo ilipendekeza kwamba Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, iwe chombo cha Muungano, mimi napongeza sana na ninaunga mkono kwa sababu haya ni maendeleo, elimu ya watu wazima kwa kweli ni maendeleo na pia ni mambo ya siasa katika nchi yetu. Sasa kwa nini vitu viwe mbalimbali, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

Kwa hiyo, mimi ningeomba ifufuliwe na iende sambamba na Mheshimiwa Waziri, hii elimu ya watu wazima ukiifufua ndiyo itasaidia kuelimisha wananchi mambo ya MMEM na MMES, bila kuwaelimisha hawa wananchi itakuwa vigumu, kwa sababu baadhi yao mpaka leo ndiyo wanaowachukua watoto wao wanakwenda kuwapa ajira watoto wadogo. Wakati tunapita kuja Dodoma unawakuta ndiyo wanaouza korosho, wanauza maji na kadhalika.

Kwa hiyo, bado mtazamo wa baadhi ya wananchi kuhusu elimu bado uko nyuma. Kwa hiyo, mimi ningeomba elimu ya watu wazima ifufuliwe na ipewe jukumu hasa kufundisha umuhimu wa mpango wa MMEM na MMES. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba idara ya uchapaji ihamasishwe kwa sababu Wizara ya Elimu na Utamaduni, inahitaji sana majarida, magazeti hata Zanzibar tuliwahi kuwa na gazeti la Jipatie Maarifa kwa hii elimu ya watu wazima. Sasa hakuna tulipata msaada *UNESCO.* Sasa *UNESCO* nchi moja nafikiri tukipata Bara na Zanzibar pia tutapata. Wakati ule mbona mie niliomba nikipata mtambo safi wa kuchapisha magazeti na tulikuwa nayo elimu ya watu wazima. Kwa nini, haya mambo mazuri yaishe hivi hivi Mheshimiwa Waziri? Mimi ningeomba uangalie tena namna ya ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya utamaduni, mimi nina kikundi changu cha sanaa kinachoitwa *Gulioni Sanaa Group* ambacho kule Zanzibar tunawaburudisha watalii, kwa hiyo, kama humu ilivyozungumzwa, mnafanya mafunzo Bagamoyo, tungeomba basi msitusahau muwe mnatualiaka, hata kwa kulipia lakini sasa utalii kule Zanzibar, umekua na unahitaji vikundi hivi sana. Kwa hiyo, tunapenda viwe vya aina moja kama mlivyosema vazi la Kitaifa, basi na vikundi hivi vya kisanaa viwe vya aina moja, tunajua sote tunaimarisha na tuna-*promote* utaifa wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumaliza muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia sentensi yako.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja na naomba iwekwe *data base* na *website* ya Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Waziri ya Elimu na Utamaduni.

Kwanza ningeomba nitoe salaam za rambirambi kwa kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye nimefanya naye kazi takribani kwa miaka 18 na kwa hiyo, kifo hiki kimenigusa sana. Kimegusa sana vile vile hasa nikikumbuka kwamba moja ya kazi yake muhimu alizofanya katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ndiyo zinazaa matunda sasa mradi wa Gesi ya Songosongo. Hivi karibuni katika kipindi cha wiki hii tunatarajia kwamba Gesi ya Songosongo itafika Ubungo na *Wazo Hill* katika kipindi ambacho kwa bahati mbaya tunamkosa Mheshimiwa Yete Mwalyego. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Elimu na Utamaduni pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli wameifanya na inadhihirika kabisa mahali popote pale walipo.

Naomba pia nichukue nafasi hii basi kama nilivyowahi kuzungumza tena kwamba tunajisikia faraja sana tunapomwona Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, anapokuwepo hapa Bungeni. Kwa kweli siku zote tunamtakia afya njema amekuwa akifanya kazi nzuri sana na umma wa Tanzania unafahamu na unamlilia sana. Kila mtu pamoja na hali yake kuwa hivyo bado anaendelea kutafuta msaada wake. Mimi namkumbuka sana alivyonisaidia katika kuandikisha shule zangu za sekondari katika Wilaya ya Muheza, Shule ya Sekondari ya Songa, Shule ya Sekondari ya Goba, Lusanga na hivi karibuni Shule ya Sekondari ya Kerenge. Nawashukuru wote kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia kwa kuanzia upande huu wa elimu ya msingi ambayo kwa kweli Wizara hii imefanya kazi nzuri. Somo ambalo ni muhimu kwetu ni kujifunza mafanikio tuliyoyapata katika mpango huu wa MMEM na vile vile tuangalie ni matatizo gani ambayo yametusumbua ili tuweze kuyarekebisha na yatusaidie katika utekelezaji wa mpango wetu wa MMES. Mafanikio ni makubwa sana naweza nikazungumza machache katika jimbo langu, katika fedha ambazo baadhi ya shule wamepewa kujenga darasa moja kwa kushirikisha nguvu za wananchi kwa kutumia fedha hizo hizo wengine wamejenga madarasa mawili, wengine wamejenga darasa moja pamoja na ofisi na hii kwa kweli ni kazi nzuri ambayo imefanyika kule na nina amini imefanyika hivyo vizuri katika majimbo na Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yapo matatizo na pengine tatizo moja kubwa ambalo ni vizuri tukaliangalia na lisije likaleta matatizo katika mpango wetu wa MMES ni utaratibu wa utekelezaji katika matumizi ya fedha hizi na usimamizi wake. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni anapozungumza Bungeni anaeleza waziwazi taratibu na kanuni ambazo zitakuwa zinatumika na usimamizi wa fedha hizi. Lakini katika utekelezaji kwa sababu Halmashauri nyingi zipo chini ya TAMISEMI unapokwenda katika Halmashauri

zetu tunakuta vitu tofauti na vile alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, hapa Bungeni katika mpango mzima huu.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano, katika fedha za madaftari na vitabu fedha hizi kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri mwanzoni kabisa hapa Bungeni fedha hizi zilikuwa ziwe chini ya Kamati za Shule na Kamati za shule pamoja na shule yenyewe ndiyo waangalie mahitaji ya vitabu na madaftari. Lakini kinyume cha hapo Halmashauri zimekuwa zikihodhi fedha hizo na wao ndiyo waliokuwa wakinunua madaftari na kupeleka vitabu. Katika shule nyingi ambazo tumefika kufanya ukaguzi vitabu vilivyopelekwa siyo vitabu ambavyo kwa kweli vina upungufu pale na wakati mwingine ni vitabu ambavyo wala havihitajiki pale shuleni. Katika shule nyingine kwa zaidi ya miezi tisa shule hizi hazikupata daftari hata moja, lakini tuna uhakika fedha zimepelekwa. Sasa hayo ndiyo mapungufu makubwa na Wabunge wengi wamekuwa wakiyazungumzia hapa. Lakini je, ni hatua gani ambazo zimekuwa zikichukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pia naomba nizungumzie kasoro nyingine ambazo pia tumeziona. Waheshimiwa Wabunge, hapa Bungeni wamezungumza na hata mimi limetokea katika jimbo langu, kweli kwamba shule inajengwa inahitaji kupauliwa, taratibu zinaonyesha kwamba mabati yanayotumika pale ni *gauge 28,* lakini kwa uhakika bati lililoezeka shule ile pamoja na kwamba limenunuliwa bati kwa bei ya gharama ya *gauge 28* bati lililopo pale na lililotumika ni la *gauge 30* ambalo limenunuliwa kwa bei ya *gauge 28.* Sasa wananchi wamelalamika wameandika barua kwa Maafisa Elimu wa Wilaya, wameandika barua kwa Wakuu wa Wilaya hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa. Sasa maana yake nini tunalea tabia hizi? Tunalea ubadhilifu wa fedha za mpango wa MMEM basi tutaendelea kulea ubadhilifu katika mpango wa fedha hizi za MMES vile vile. Lazima hatua zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi tu, kuna shule moja ya msingi ya Enzi waliomba kununua vifaa vya bendi, fedha zikachukuliwa benki, vifaa vya bendi havikununuliwa, wananchi wamelalamika, habari zimefika mpaka kwa Mkuu wa Wilaya, alichofanya Afisa Elimu wa Wilaya ni kumhamisha aliyekuwa Kaimu Mwalimu wa Shule ile kumpeleka katika shule nyingine tena akawa Mwalimu Mkuu na fedha za bendi amekwenda nazo na hakuna hatua iliyochukuliwa, zaidi ya hiyo ya kumhamisha. Sasa hivi kweli ndizo taratibu tunazodhani zitasaidia kulinda fedha hizi za umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie mpango wa MMES mpango ambao ni mzuri sana. Kwa kweli unajieleza vizuri sana katika kielelezo hicho namba 18 ukurasa wa 27. Sasa yote ni mazuri lakini mimi nitazungumzia machache tu. Kwanza nitazungumzia kuhusu ujenzi wa madarasa katika shule 728 zilizopo jumla ya madarasa 1,456. Sasa ni vizuri basi kwetu sisi kama Wabunge, tukafahamu ni shule zipi hizi zinazozungumziwa 728? Je, katika Wilaya yangu ni zipi ili na mimi niweze kufahamu kwamba nitapata madarasa mangapi katika Wilaya yangu, katika jimbo langu. Hapa zimeandikwa tu na ndiyo hayo hayo ambayo yanaweza yakaonekana ni mazuri sana hapa katika utekelezaji hutapati darasa hata moja katika jimbo lako au katika Wilaya. Sasa ni vizuri basi tukafahamu ili tuwe na uhakika. *(Makofi)*

Sisi katika Wilaya ya Muheza ambayo kwa kweli tuna bahati mbaya sana, nimewahi kuzungumza hapa Bungeni na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, vile vile Mbunge mwenzangu amelizungumza tuna bahati mbaya kwamba katika Wilaya ya Muheza hatuna shule hata moja ya sekondari iliyojengwa na Serikali kwa miaka yote tangu tumepata uhuru mpaka leo. Tunazo shule chache ambazo kwa kweli Serikali inazihudumia na hizi ni shule walizojenga wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoona kuna mpango mwingine hapa unaozungumzia wa ujenzi wa shule basi tunaweka matarajio makubwa sana kwamba sasa Wizara ya Elimu na Utamaduni, italiona hilo kwamba sisi Wilaya ya Muheza pamoja na wenzetu wengine tunahitaji na sisi kupewa *priority* pamoja na kwamba wananchi wataendelea kujenga shule, lakini hakuna uwiano basi kama kuna Wilaya nyingine zenye shule zaidi ya 15 zilizojengwa na Serikali, wakati zipo Wilaya nyingine hazina shule hata moja iliyojengwa na Serikali. Sasa tuzitazame pamoja na Wilaya nyingine ambazo najua zipo nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba vile vile kwa sababu mpango huu ni mzuri basi tuendelee kuuboresha. Nimefurahishwa sana hapa katika kielelezo hicho hicho cha 18 ambapo sasa tunasema Serikali itatoa ruzuku ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia shule za Serikali na zisizo za Serikali. Kwa maana ni kwamba sasa tunatambua kwamba wanafunzi waliopo katika shule nyingine ambazo siyo za Serikali ni Watanzania na wanayo haki kama Watanzania wengine.

Kwa hiyo, tujitahidi tuwasaidie hawa na mimi hapa nilikuwa nazungumzia shule moja ya Muheza inaitwa *Muheza Muslim Secondary School* ni shule pekee ambayo imekuwa ikijitahidi kutoa watoto wa *division one.* Naomba shule hii kwa kweli isaidiwe. *(Makofi)*

Ningeomba pia nizungumzie mambo mengine. Katika mpango huu pia wa kusaidia watoto wanaosoma katika shule zetu za sekondari hebu tuwaangalie watoto yatima. Nafurahi kwamba tumekuwa tukiwaangalia na tumeandaa utaratibu mzuri wa kuwasaidia. Lakini hatukuwa tukiwaangalia watoto yatima ambao wako katika shule ambazo siyo za Serikali. Nasema tena nao ni Watanzania wanayo haki sawa na Watanzania wengine basi tuwaangalie. Kwa bahati mbaya inawezekana hawa wamepata uyatima huo wakiwa katika mwaka wao wa pili wa elimu au mwaka wa tatu wakiwa shuleni wakawa yatima. Sasa wanafika mahali nao wanashindwa kuendelea na masomo. Lakini ukitafuta msaada unasema shule hiyo siyo shule ya Serikali kwa hiyo, hatuwezi kuwasaidia watoto hawa. Basi tuwaangalie pia watoto yatima katika msingi huo katika shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu Mheshimiwa Waziri, utupe ufafanuzi hapa, umetoa punguzo la ada kweli na katika eneo lingine umeshaagiza bodi zilizopo kule kwamba zisitoze michango mingine. Sasa baadhi ya michango ilikuwa ni michango ya madawati, ilikuwa pia ni michango kwa ajili ya majengo ambayo kwa jumla ilikuwa inafikia kama shilingi 35,000/=. Sasa je, ndiyo haya tunayoyazungumza ili tuwe na uhakika wote tunapotoka hapa tunazungumza lugha moja kwamba sasa ada imebaki

shilingi 20,000 hakuna mchango wa majengo, hakuna mchango wa madawati, vinginevyo shule hizi zitakuwa zinatofautiana tu. Kwa hiyo, naomba utupe ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningeomba sasa kwamba shule nyingi za wananchi hazina utalaam wa usimamizi wa uendeshaji wa shule zenyewe. Wananchi kama ndiyo meneja wa shule zile hawana kabisa utalaam pamoja na kuwepo na bodi hizi bado hakuna kitu pale. Viongozi wengi wa bodi na wajumbe hawana utalaam. Kwa hiyo, fedha zinakusanywa kama ada pamoja na hizi za madawati, pamoja na hizi za majengo zinakwenda wapi? Ukienda shule hizo hakuna jengo jipya ambalo limejengwa, hakuna madawati ambayo yametengenezwa. Sasa matatizo ni kwamba hawana utalaam wa uongozi wa usimamizi wa shule hizi za sekondari. Tunaomba Serikali sasa iangalie shule hizi kwa sababu inalipa mishahara ya walimu, basi iangalie usimamizi wa shule hizi za wananchi na waweke wakaguzi watakaosaidia kusimamia mahesabu ya mapato na matumizi katika shule hizi za wananchi. Kuna matatizo makubwa sana na tusipowasaidia basi kwa kweli tutakuwa tunawafikisha mahali pabaya. *(Makofi)*

Mwisho, kwa kweli naomba kama wenzangu walivyosema, tuangalie tatizo hili la ulipaji wa mishahara ya walimu. Tatizo hili ni kero kubwa sana kwa walimu. Mishahara inachelewa na walimu wapya wanapelekwa katika vituo mbali na nyumbani walikozaliwa wanakwenda kukaa kule miezi minne bila kupata mishahara, hivi mnategemea wataishije hawa? Matokeo yake nini katika baadhi ya shule viongozi wanatumia fedha zile zinazoletwa kwa ajili ya uendeshaji angalau kuwapa posho walimu hawa wakiwa wanaendelea kusubiri mishahara yao, aibu! Miezi minne bila mishahara wewe unaweza kweli? Hatuwezi, sasa kwa nini wengine tuseme wanaweza na hatuwajali? Lakini tuangalie basi mfumo wetu nani wa kulaumiwa ni Wizara ya Fedha haijatoa fedha hizo au Wizara ya TAMISEMI haijapeleka fedha zile katika Halmashauri au Wizara yenyewe ya Elimu na Utamaduni, haijafuatilia ili kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa wakati na walimu wanalipwa kwa wakati au utumishi. Hebu ninyi Wizara nne mkae ili hili tatizo liishe haiwezekani mfanyakazi akafanyakazi bila mshahara kwa miezi minne na tukategemea kwamba atatoa tija tunayoitarajia kwamba atatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele ya kwanza imekwishalia naomba basi kwa leo niishie hapa nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa ili niweze kuchangia hoja hii muhimu hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Awali ya yote ningependa niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa msiba uliotupata wa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye majimbo yanapakana kule nyumbani. Salaam hizi nazitoa kwa niaba ya wananchi wote wa Rungwe na ningeomba ziwafikie vile vile wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Pia ningependa kukushukuru Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ulivyotuongoza siku ile tulipokuwa tunaaga mwili wa marehemu wakati unaandaliwa kwenda kwenye safari ya mwisho kule Utengule.

Ningependa kutoa pongezi nyingi sana kwa Waziri Joseph Mungai, kwa kazi nzuri na hotuba nzuri aliyotuletea hapa Bungeni. Pia nafurahi kuona kwamba wenzangu wote waliotangulia kuchangia wameunga mkono hoja hii na ningeshangaa wangefanya tofauti na hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba imeandaliwa vizuri na imetolewa vizuri ukiangalia kurasa hadi kurasa kuna *bar, graphs,* kuna majedwali ambayo kwa walimu wanajua kwamba zinatoa *visual impact* ambayo inatufanya tuelewe kwa urahisi. *(Makofi)*

Hongera sana Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mama Mwantumu Mtengeti Malale na *staff* nzima ya Watendaji, nawashukuru kwa kumsaidia Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wote wamesifu Mradi wa MMEM na mimi napenda niungane nao. Mradi huu umeonyesha mafanikio makubwa, sura za Shule zetu zimeboreshwa, ubora wa majengo na idadi za shule zimeongezeka. Mimi nilisoma Shule moja inaitwa Masoko ambayo ilikuwa inavutia sana Waandishi wa Habari na Wapiga picha. Mara nyingi nilikuwa naiona hiyo Shule iko kwenye magazeti na kwenye *TV* wanasema hapa ndio alisoma Mbunge wa Rungwe Magharibi. Lakini sasa imeboreshwa mpaka imekuwa kama Kituo cha Utalii watu wanakuja kuiona jinsi ilivyojengwa na shahidi yangu ni Mheshimiwa Mungai mwenyewe, amewahi kuiona hiyo Shule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kuboresha na kuongeza idadi ya majengo, muhimu zaidi ni kwamba taaluma vile vile iboreshwe. Miaka mitatu iliyopita ilikuwa tukikutana na wananchi tunaandamwa na maswali, wanatuuliza mbona watoto wetu wanamaliza Darasa la Saba lakini hawajui kusoma? Mbona watoto wetu hawafaulu? Mbona watoto wetu hawachaguliwi kwenda Sekondari? Lakini kutokana na juhudi za wananchi na sera thabiti za Serikali ya CCM na usimamizi mzuri wa viongozi tukiwemo sisi Wabunge, tunaiona taaluma imeboreka na takwimu kama alivyotuletea Mheshimiwa Mungai zinajieleza zenyewe. Kwa hiyo, kuna sababu ya kuipongeza Wizara na tujipongeze sisi wenyewe pamoja na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa niwapongeze wananchi wa Rungwe kwa sababu tukizungumzia taaluma na kufaulu, mwaka huu uliokwisha wa 2003 Rungwe ilishika namba moja kwa kufaulisha watoto Tanzania nzima. Hii haikuwa *accident* ni ishara ya uelewano na kujituma na kazi nzuri ambayo imefanywa. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mheshimiwa Spika, nawapongeza wananchi wa Rungwe kwa mwamko walionao katika ujenzi wa Sekondari. Ukurasa wa 16 wa kitabu cha Mheshimiwa Mungai, unaeleza kwamba mwaka huu wa 2004 zimefunguliwa Shule za Sekondari nane. Hizo shule labda kwa *record* naweza kuzitaja haraka haraka. Kuna Shule ya Sekondari ya Isongole, Ilundo, Ukukwe, Ilima, Isondela, Mwatisi, Selya na Mpuguso. *(Makofi)*

Vile vile ningependa niishukuru Wizara na Waziri kwa kuturuhusu kuzifungua Shule hizi. Ujenzi wa shule zaidi unaendelea katika Kata nyingine kwa sababu Halmashauri imeamua kila Kata iwe na Shule yake ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kujenga Sekondari sio lelemama, inahitaji gharama kubwa, moyo wa kujituma kutoka kwa wananchi, kujitolea na kuna michango mingi. Kwa maana hiyo basi, tulipoambiwa kuna mpango wa MMES wote tulifarijika na tunangojea huu mradi kwa hamu sana kwa sababu umekuja wakati muafaka. Niseme tu kwamba, nimetaja shule nyingi ambazo tunajenga lakini shule hizi hazijakwisha, majengo hayajakamilika. Kwa hiyo, tuna imani kwamba huu mradi utaangalia jinsi ya kutusaidia.

Niliposoma ukurasa wa 25 kuhusu mwaka wa kwanza wa MMES kipengele za 18(2) inazungumzia habari za kukamilisha ujenzi wa madarasa 458 katika Sekondari mpya katika maeneo yasiyo na Sekondari za kutosha. Sasa nina wasiwasi hapa kwamba zikionekana shule nane zimejengwa, Mheshimiwa Mungai asije akafikiri kwamba hizi pesa apeleke kwingine ambako hawajaanza kujenga, hizi shule hazijakwisha, tungeomba atukumbuke.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile tufanye masahihisho au ufafanuzi kidogo katika ukurasa wa 19. Ukurasa wa 19 wa hotuba ya Waziri, kipengele Na.19 mstari wa tano kutoka mwisho, katika huu Mradi wa MMES inazungumzia Shilingi bilioni 59 za maendeleo, lakini katika jedwali lililo mwisho kabisa kwenye cover tarakimu ni bilioni 56.6 tofauti ya bilioni 2.8. Naomba hizo ziangaliwe kwa sababu hizo ni hela nyingi sana, nina imani kutakuwa na maelezo au masahihisho mahali fulani.

Mheshimiwa Spika, haya mafanikio tuliyoyaona katika MMEM ni muunganiko wa nguvu za wananchi na miradi kama MMEM na *TASAF*. Tumeona madarasa yameongezeka, yameboreshwa, vile vile nyumba za walimu, vyoo vya kudumu, madawati, vitabu, lakini suala la Walimu kama wenzangu walivyozungumza halijapewa msukumo wa kutosha. Hizi Shule tulizozifungua sijui katika Wilaya nyingine, nyingi sasa zinaendeshwa na Waratibu wa Elimu ya Msingi (SAKATA), ndio wamekuwa viongozi wa Shule hizi. Katika hotuba ya Waziri Mungai ametueleza kwamba mwaka 2003 Walimu walioajiriwa ni 14,261 lakini Shule za Msingi zote ni 13,000. Kwa hesabu za haraka haraka, ina maana kwamba hawa Walimu wakigawanywa katika hizi Shule ambako tunajua kwamba kuna matatizo na upungufu mkubwa ni kwamba tuna uwezo wa kupeleka Mwalimu 1.054 kwa kila Shule. Hii haitoshi kabisa wakati Shule nyingi katika Wilaya yangu ina Walimu wawili tu. Lakini naipongeza Wizara kwa mikakati iliyojiwekea ku-*address* suala hili kama ilivyo katika ukurasa wa 28. Vile vile naipongeza Wizara kwa kukarabati Chuo cha Ualimu Mpuguso ambacho kipo katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, lakini nimefarijika kwa uamuzi wa kubadilisha Chuo cha Ualimu Chang'ombe na Chuo cha Ualimu Mkwawa ili viwe Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pendekezo ni kwamba tunahitaji Walimu wengi ambao wana Shahada kwa ajili ya Sekondari zetu. Nilitaka kupendekeza tu, kwa nini tusitazame uwezekano wa Vyuo Vikuu vingine vichukue Vyuo vilivyo jirani ili na vyenyewe viwe

Vyuo Vikuu Vishiriki? Kwa mfano Mzumbe tungewaomba wachukue Kigurunyembe na Tumaini wakachukua Chuo cha Marangu kwa kuanzia ili tuongeze idadi ya Walimu kwa ajili ya Vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, kuongeza idadi ni kitu kimoja, lakini nadhani tunasahau pia ubora wa Walimu wenyewe ambacho ni kitu muhimu sana. Tukumbuke kwamba mwaka 1977 kulikuwa na mpango wa *UPE* na tukatoa wanafunzi wengi na kwa sababu Walimu hawakuwa mahiri, nadhani hii ilichangia katika kuzorotesha elimu. Siri ya matokeo mazuri ya Kidato cha Nne nikitoa mfano tu ni kwamba watoto wanaoingia Shule fulani wanapitia mchujo mkali sana kuingia *Form One* na Shule nyingi ambazo zinatoa watoto wazuri mwishoni pale *Form Four* ni kwamba wanapitia huo mchujo. Kwa hiyo, sasa tukifanikiwa kuweka misingi imara ya elimu, Walimu ambao tutawapa dhamana ya kuendeleza huu msingi hadi vizazi vinavyokuja, ni lazima wenyewe wawe imara *academically.* Ni lazima tuanze na ngazi za usaili. Tunataka mtu ambaye yeye mwenyewe anafundishika na ana akili ambazo zina-*charge.* Ni mara nyingi tunasikia mtu anasema natafuta kazi, nimekosa, nimekwenda kila mahali, nanaulizwa, hata Ualimu? Sasa nadhani umefika muda wa kuliweka ngazi ya juu suala la Walimu, wawe ni watu ambao akili zao zina-*charge.* *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nilitaka kutoa wazo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba wafikirie kubuni mkakati wa kuwavutia vijana wenye alama nzuri ili wajiunge na Kozi za Ualimu na kuwavutia huko kuende sambamba na vivutio, maslahi, mishahara mizuri, mazingira ya kazi na waahidiwe nafasi za kusoma zaidi. Najua sio rahisi, lakini kupanga ni kuchagua. Mheshimiwa Waziri akileta hoja hii kwenye Bunge lijalo la Bajeti akaiombea pesa, hii hoja itapita bila kikwazo. Kuna Wabunge wengi humu ndani ambao ni wakereketwa wa elimu, najua tutakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kengele ya pili inigongee, naomba uniruhusu nikae nikiwa naiunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kama kuna kosa kweli la herufi au tarakimu, basi masahihisho yatafanywa wakati wa Kamati ya Matumizi. Namwita Mheshimiwa Philip Marmo na ndio wa mwisho katika waliokwishachangia mara moja. Sasa waliokwishachangia mara mbili wengi siwaoni Bungeni lakini wajiandae waliopo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Khalid Suru.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu wa mawazo katika hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nami pia natoa mkono wa rambirambi kwa kifo cha mwenzetu, Mheshimiwa Hayati Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, lakini pia natoa pole kwa Mheshimiwa jirani yangu ambaye tunaishi karibu hapa Dodoma, Mheshimiwa Lawrence Gama kwa kufiwa na mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mambo mawili. Kwanza, kwa kutambua jana Walimu Wakuu wa Shule kumi zilizofanya vizuri zaidi katika Wilaya yangu mwaka jana katika mtihani wa Darasa la Saba, lakini pia kwa kuitembelea Wilaya yangu siku za karibuni na kuona hali halisi ya elimu katika Wilaya hiyo. Ni muhimu niseme machache kuhusu haya mawili kwa sababu yana maana yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametambua wale Walimu kwa sababu Shule zao zilifanya vizuri sana katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na mpaka ngazi ya Taifa. Walimu wale wanaongoza Shule ambazo katika Mkoa wetu ndio za kwanza mpaka za tano nyingine na Kitaifa baadhi yao ni katika Shule 150 bora katika Shule zaidi ya 15,000 kama alivyosema Mheshimiwa Mwakyusa. Kwa hiyo walikuwa wanastahili kuja hapa kusikiliza hotuba ya Waziri wao. Lakini na Walimu wengine ambao walijitahidi pamoja nao tuliwapeleka kwenye Mbuga za Wanyama kule Serengeti na Ngorongoro ili kutambua jitihada zao sisi pale Wilayani.

Mheshimiwa Waziri alipotembelea Wilaya yetu hatukumpeleka kwenye Shule hizi ambazo zimetoa Walimu hawa aliowaona jana, tulimpeleka kwenye maeneo magumu. Kama ambavyo kuna tofauti kati ya Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa, pia kuna tofauti katika Wilaya zetu. Katika maeneo ambayo tulimpeleka Waziri kwa kweli asingeweza kuona Shule bora katika Wilaya au Shule ambayo inaweza kuwa na nafasi katika Taifa kwa sababu ni maeneo ya wafugaji na wawindaji ambapo kutoka shuleni pengine ni kilometa 100 mpaka anapotoka mwanafunzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba tulipofikia Kitongoji fulani tuliona ratiba inaingiliwa kwa ajili ya umbali wa Kijiji kile kwamba kutoka Kitongoji kimoja mpaka kingine ni kilometa zaidi ya 80. Kwa hiyo ilibidi tusiende Kitongoji kingine kwa sababu ingekuwa usiku na ni porini na isingekuwa vyema kumtembeza Waziri porini usiku.

Sasa hii ndio hali ilivyo katika nchi yetu na katika Wilaya zetu na hapa nafikiri ni mahali pake mimi sasa kutaja rasmi yale aliyowaahidi wananchi wale ambao ni wafugaji na wawindaji kuhusu wanatarajia nini katika hotuba yake ya mwaka huu wa fedha kwa maana ya MMEM na MMES ili sasa ionekane rasmi katika *Hansard* kwamba Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Joseph Mungai amewaelezea wawindaji na wafugaji wa Wilaya ya Mbulu kwamba kwa ajili ya mazingira yao magumu, sasa watakuwa na *PILOT Primary Schools* za Darasa la Kwanza mpaka la Pili katika maeneo yao ili wakimaliza pale waende kwenye Shule za Border ambayo itajengwa katika eneo lao na yeye mwenyewe ameona majengo yaliyoanza kujengwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Waziri alikwenda kule na alikiri kwa kumwambia pia Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba niliyoyasema hapa Bungeni wakati nikiuliza swali la nyongeza

kwamba iwapo Wizara inafahamu kwamba hakuna Mhadzabe hata mmoja toka dunia iundwe ambaye ameweza sio tu kupata Shahada au *Diploma* yoyote, lakini nina wasiwasi pia hakuna hata mmoja aliyefika Kidato cha Sita. Waziri alipofika Yede Chini ambako ndipo maeneo wanakaa wafugaji na wawindaji hawa na kuthibitisha kwamba ni kweli, mwenzangu Mheshimiwa Ole Timan amesema Elimu ni haki ya kikatiba kwa Watanzania wote. Hawa mimi ninaowataja pia ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya makusudi kutompeleka katika Shule zaidi ya 100 ambazo nadhani zilikuwa ni nzuri na ambazo walimu wao walifika hapa jana kwa makusudi kwamba katika Wilaya nyingine kuna maeneo magumu na kuna tofauti kubwa sana na tofauti hizi tusingependa ziendelee kwa sababu zikiendelea tunavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa ajili hiyo basi, ningeomba baadaye Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba matamshi yale sasa yatatafsiriwa katika hali halisi ya kwamba kutakuwa na wanafunzi ambao mwaka ujao wataingia Darasa la Kwanza katika zile Shule ambazo tunaita ni *PILOT* na hatimaye wataingia katika Shule za Bweni kwa ajili ya wawindaji na wafugaji waliopo katika Bonde la Eda ambalo ni bonde kubwa sana kwa kweli, mimi niliogopa kumtembeza Waziri kutoka Kaskazini mpaka Kusini kilometa 180. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme moja tu la takwimu. Mimi nadhani wamekosea katika kitabu hiki cha *Basic Statistics in Education 1995 to 2004* ukurasa wa 64 *table 3.12. - Distribution of Government and Non-Government Secondary Schools by level and region 2004.* Maana yake ni idadi ya Shule za Serikali za Sekondari kwa Mikoa na Mikoa ambayo haina Shule za Serikali kwa maana ya zile ambazo hazijajengwa pia na wananchi, ni Mkoa wa Arusha, Kigoma, Kilimanjaro na Lindi. Kwa hiyo, nafikiri hii sio kweli. Mkoa wa Kilimanjaro una Shule ya Sekondari ya Serikali, Mkoa wa Arusha una Shule ya Sekondari ya Serikali, labda Mikoa mingine kama Manyara nafikiri haina. Kwa hiyo, hapa kuna makosa. Takwimu hizi nafikiri sio sahihi, wazisahihishe.

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kuongelea kuhusu Mpango wa Elimu ya *Sekondary* MMES 2004/2005, lakini kabla sijasema lolote naomba nimkumbushe Waziri moja alilosemea mwaka jana au mwaka huu mwanzoni alipokuwa akiongea na Wakuu wa Shule za Sekondari wote nchini katika Mkutano wao wa Mwaka kule Arusha, kwamba Bodi zetu za Shule ya Sekondari kwa sasa zinaongozwa na Wenyeviti ambao ni wa kimila. Nafikiri alikuwa mstaarabu kusema wa kimila. Mimi na mwenzangu hapa Mheshimiwa Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini - Mashariki, tulimweleza kwamba baadhi ya Shule Wenyeviti wa Bodi ni wa kimila. Sasa haifai! Shule hizi zinataka Wenyeviti wa Bodi wawe ni watu ambao angalau wana elimu inayofanana na Taasisi wanazoziongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Waziri atuhakikishie kwa sababu nataka tuondoke hapa baadaye katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge utakapoahirishwa katika wiki ya pili ya Agosti, tukiwa na majina ya idadi ya Shule ambazo zitanufaika. Kwa mfano ruzuku ya maendeleo hii ya Shilingi milioni saba kwa kila darasa hasa kwa Shule ambazo zinaongeza mikondo miwili kwenda mikondo minne

kwa sababu hatimaye,watoto hao watajaza mwezi wa tisa mwaka huu *form* ambayo inaitwa *SS Form*. Kwa hiyo, Shule hizi ambazo zitakuwa na mikondo minne nataka tuzijue kwa majina tutakapoondoka hapa baadaye wiki ya kwanza ya Agosti.

Mheshimiwa Spika, pili, tunataka tuondoke na idadi ya haya madarasa 158 kwa *underserved areas* maeneo ambayo kwa kweli maendeleo yako nyuma sana, ni Wilaya gani na ni Shule zipi ambazo tumetenga Shilingi bilioni 3.2. Pia tunataka tufahamu kabla hatujaondoka hapa kwamba hizi Shilingi milioni tisa kwa ajili ya nyumba za Walimu 957 ambazo zimetengewa Shilingi bilioni nane ni shule zipi na ni Wilaya ipi? Lakini pia nataka pia tujue Shule za Sekondari 40 ambazo zinakarabatiwa kwa Shilingi bilioni 2.7. Pia tunataka kujua Maabara 90 hizi ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ni kwa vile tunaheshimiana sana na Waziri na ni mchapakazi na ni muungwana na ni muadilifu na Naibu wake na Katibu Mkuu, lakini suala la Maabara ni suala nyeti. *ADB* walitupa fedha nyingi sana kwa ajili ya Maabara na mimi ni mmojawapo ambaye siridhiki na jinsi ambavyo fedha hizi zimetumika. Kwa hiyo, wakati wa kutoa hoja angetuambia fedha za *ADB* zilizojenga Maabara ni Maabara ngapi, vigezo vipi vilivyotumika kujenga Maabara hizo na ziko wapi na kwa yale tuliyojifunza kutokana na utekelezaji mbovu huu, basi sasa MMES ijifunze sasa. Tufuate angalau maelezo na ushauri wa Wabunge kuhusu utekelezaji mbovu wa ujenzi wa Maabara kwa fedha ambazo tulipewa na *African Development Bank. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna moja hapa Waziri amelisahau, nalo ni ujenzi wa *hostel* za wasichana katika utaratibu huu wa MMES. Waziri akumbuke kwamba ameongea sana na wananchi karibu nchi nzima na wamemsikiliza kwamba katika MMES pia tutakuwa tukichangia ujenzi wa *hostel* za wasichana katika shule hii ambayo inajengwa na wananchi. Nina uhakika wasichana wengi tunawapoteza kabla hawajafika Kidato cha Nne kwa sababu wanaishi aidha katika nyumba za kupangisha au wanaishi kwa jamaa, au wanajijengea vibanda vidogo vidogo karibu na shule.

Hili ni muhimu, naomba litolewe tamko kwa sababu pia tunakiuka haki za binadamu tusipokuwa na watoto wa kike katika shule hizi ambazo sasa hivi tunazijenga na Waziri ametuambia kabisa kwamba katika MMES pia kutakuwa na ujenzi wa *hostel* kwa ajili ya wasichana na kama atatenga fedha, basi atuambie mgao wake utakuwaje kwa sababu tunapoongea juu ya shule za kutwa, watoto wanatembea kilometa 40 mpaka 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningesema mengi lakini kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa sababu nitaingia *speed* unafahamu, nianze kwa kuunga mkono hoja na pili, naomba msamaha kama sauti itapanda, itapanda kwa sababu ya msisitizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninayezungumza hapa *professionally* ni Mwalimu. Ninataka niseme haya nitakayoyasema kutokana na *profession* yangu. Haya mambo ya *Political Science na Public Administration* nilifanya juu huko lakini *basically* mimi ni Mwalimu. Ninataka nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mungai. Ninataka niseme kwamba kazi inayofanywa na Serikali kupitia Waziri huyu ni kazi nzuri, na kazi ambayo inaleta Mapinduzi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Samora Machel alikuwa anaeleza maana ya *revolution* akasema ni kitendo kinacholeta manufaa kwa watu kwa haraka. Kikichukua muda mrefu sana sio *revolution. Component* muhimu katika *revolution* ni uharaka. Yaani kikifanyika haraka utasema hapa yamefanyika Mapinduzi. Ndicho ninachokiona kinafanyika katika nchi yetu kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mungai aliniahidi atakuja katika Jimbo langu la Siha na akafanya hivyo. Katika mazingira magumu sana na ninataka nitoe ushuhuda hapa kwamba alikuwa anakwenda *Scotland,* amekwenda mpaka kule akaniahidi nitakaporudi nitashuka *KIA* kwenye *KLM.* Kweli huyu baba saa 4.00 usiku namwona anateremka na Wazungu Watalii wanakwenda Mlima Kilimanjaro, anashuka anakuja ananiambia nimekuja, kesho nakuja katika Jimbo lako. Nimetumwa na wananchi wa Jimbo langu la Siha kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa *commitment* ya hali ya juu ambayo ameionyesha katika Jimbo langu na katika nchi yetu. Mwanzoni tulipokuwa tuaanza haya mambo ya mgao wa Shule za Sekondari tulitaka kutofautiana, lakini nataka nikiri kwamba nimeiona *seriousness* ya Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu. Ninachoweza kusema hapa, nitatumia nafasi yangu kama Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha kuhakikisha kwamba ninam-*support* Waziri huyu ili haya mazuri anayoyazungumza hapa yaweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza habari ya *revolution*, kujenga madarasa mengi ya MMEM yamejengwa na sasa tunaambiwa kuhusu mpango wa MMES. Alipokuja kule alizungumza na wananchi wa Jimbo la Siha. Sasa hivi tumeanzisha Sekondari nyingine tatu mpya. Shule ya Sekondari ya Nuru, Shule ya Sekondari ya Magadini na Shule ya Sekondari ya Kambarage na yeye ndiye alitutia moyo. Wamenituma wakaniambia tunataka tuongeze, Jimbo hili ni Jimbo ambalo liko kwa wachungaji na wafugaji. Tunataka tujenge Shule ya Sekondari ya Dahani, Shule ya Sekondari ya Sumu na Shule ya Sekondari ya Pungo. Tunajua kwamba tunatakiwa tuingie mifukoni mwetu siku ya Jumapili, hivyo nitakuwa Siha kufanya harambee kubwa kuhamasisha wananchi wa Jimbo langu ili wajiandae mpango huu unapokuja tukutane nao. Hii yote inafuatia hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ni *component* ya *systems* zote mbili. Wajamaa na mapebari wanazungumza habari ya elimu. Katika ubepari *contradiction* kubwa unayoipata ni kati ya *labour na capital.* Katika Ujamaa una-*harmonize,* hakuna *contradiction* kwa sababu umefikia watu wote ni sawa, kila kitu ni sawa. Katika *developing countries, contradiction* kubwa uliyonayo ni kati ya *labour* na *the means of the productive forces.* Ni kati ya nguvukazi na kiwango cha vitendea kazi na kazi

inayofanyika katika nchi yetu sasa kupitia Wizara ya Elimu ni ku-*resolve* hiyo *contradiction,* kuhakikisha watu wetu wanapata elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unasema unataka kuleta mapinduzi katika *agriculture,* utatakiwa ulete *revolution* katika elimu. Unataka kuleta r*evolution* katika *science and technology* lazima ulete *revolution* katika elimu.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuwa-*empower* watu wako, wape *education* na ndicho kinachozungumzwa. Nataka niseme, Serikali ya Mheshimiwa Mkapa, ime-*demonstrate* kwa vitendo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na ninakiona kinafanyika. Na nataka niseme kazi hii ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuishii hapo, tunakwenda tunasema madarasa haya yatajengwa, tunasema tutahakikisha kwamba kunawepo na walimu. Lakini tunataka kuleta *revolution* hata katika kile kinachofundishwa kule darasani. Huwezi tu ukasema unajenga madarasa ya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushuhuda, waliokaa kule *Gallery* kuna mwalimu mmoja anaitwa Dr. Katunzi, alinifundisha kitu kinachoitwa *Curriculum Development and Evaluation* na napenda kumwambia Mwalimu wangu shikamoo na nampa heshima yake. Yuko kule, anayepunga mkono kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, alisema ukiingia darasani kuna *three domains* ambazo unaziangalia. Ni *the cognate of the main, the affective domain* na *the beside common domain,* alifundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *cognate of the main* inamsaidia mwanafunzi kuwa na *inquiry minded* kuuliza, si unajenga *study,* anauliza. Kwa nini hiki kinatokea? Bila *affective domain*, inaangalia maadili, inaangalia miiko, inaangalia mwenendo, *beside common domain,* inaangalia vitendo, *practice* namna ya kwenda kuvitekeleza. Vitu vitatu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwalimu usipoteze muda, mwanafunzi wako yuko hapa, mambo haya haya. Tunakwenda kuwafundisha nini watoto wetu kule darasani tunapoingia pale, ni *very important, revolution* itakuwa ni kuhakikisha kwamba matakwa ya kitaifa tulio nayo sisi yanaingia katika mpango huu. Elimu yake kazi yake ni kuleta *development* ya *mankind,* lazima ifanye hiyo. Tunapoingia pale unasema, ni lazima mitaala yetu iende na wakati. Lazima tufike katika *law* ya *demand and supply* nini *demand* ya sasa kwa wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anazungumza kengele haijalia hata moja, humu ndani humu umesema kwamba *agriculture* utaiondoa. Umesema na hivi vingine kama kwa mfano *commerce* vitaondolewa vitakwenda huko zinakofundishwa. *What is the assumption? Suppose,* anakwenda mpaka *Form Four* na ni mwisho wake anaishia hapa, hatakwenda *Form Five* na *Form Six* au hatakwenda kwenye vyuo.

Huyu ambaye hakwenda utampeleka wapi, utafanye na amekosa hiyo unamwondoa sasa. *Primary Education, education for self-reliance* ilikuwa inasema ni *complete education.* Anapomaliza darasa la saba kila kitu, anajua umeme, anajua *commerce,* anajua kilimo, anajua kila kitu. Ilikuwa *education for self-reliance* ni *totality* ya mambo yote anayojifunza mtoto pale shuleni. *What are saying* unaposema kwamba sasa utanyofoa *Agriculture,* havina kwa kwenda basi, ningeomba utufafanulie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huyu akishapita kwenye ile *corned week* akitoka hakupata hiyo *doze* ya kilimo sasa itakuwaje, kwa sababu *unless* unatuambia kwamba MMES ikija wote watakwenda *Form Five* na *Form Six* watakwenda vyuoni.

Lakini ukumbuke kwamba nia na shabaha ni kumpeleka mtoto katika *Primary Level na Secondary Level* ni kumwandaa ili aende akaishi kijijini aweze kujitegemea. Ukizuia hiyo sasa inakuwaje. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri unapoingia hapa utueleze unaposema kwamba utaziondoa hizi *imbalances* hizi pale unataka kusema nini ili tuweze kwenda wewe tujue kwamba sababu wote wote hawatakwenda *Secondary School,* watoto wote hawatakwenda katika hivi vyuo vinavyozungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na humu ndani inataka kutolewa. Unapofundisha watu wako unatakiwa uwafundishe vitu vyote. Huwezi ukasema hivi Mwalimu Nyerere aliwahi kuulizwa, pale Chuo Kikuu cha Da r es Salaam. Hivi tunapowafundisha, tuwafundishe ujamaa au tuwafundishe ubepari? Akauliza hivi hivi, walimu wakajibu na na-*quote* “Wafundisheni wanafunzi wetu kila kitu, wakipata elimu watachanganua wenyewe watajua kitu cha kufundisha. *(Makofi)*

Hapa sasa tutapelekwa na utandawazi, tutachukuliwa hapa kama dobi. Tutakwenda kule tukafundishe vitu vya ajabu ajabu hapa. Maadili yatamomonyoka. Halafu utafika mahali utasema utandawazi. Utandawazi gani Wamarekani wanawafundisha watoto wao *ethics* na *norms* za Marekani. Wachina wanawafundisha watu, *ethics* na *norms.* Watoto wetu watakaomaliza *Form Four* walio wengi watakwenda kwenye *market.* Ya kwanza hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!!

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Watakwenda kule, nimalizie. Watakwenda kwenye *market,* wakifika kule kwenye *market* kule, watatakiwa wajue mambo ya ufundi. Mpango huu unakuja kuunda, lazima sasa uanze kuonyesha namna tutakavyowachukua hawa watoto na kuwapeleka kwenye vyuo vya ufundi. Ndiko utakakowamwagia, utawapeleka wapi. Huwezi uka-*afford* elimu ya shule ya Chuo Kikuu ni ghali. Unasema nini katika hilo, lazima uwapeleke katika *technical schools,* uwapeleke katika *Commercial Schools* waende kule. Kwa hiyo, lazima tuwe na mpango huo kutoka sasa uanze kujitokeza. Vinginevyo tutasomesha watu hapa, kumbe unaandaa jeshi, la kusema hivi, mimi mmenisomesha mpaka hapa, sasa mmenifanyia nini? *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii ni vizuri ikajitokeza wazi wazi katika mipango yetu. Matumaini yangu ni kwamba tunakokwenda mbele, watakuja watatuambia pia kwamba tuna mpango kama huu kuhusu vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *language* linazungumzwa hapa, Kiswahili, Kiingereza. Na mimi nataka nitoe mchango wangu. Mheshimiwa Waziri huo msimamo unaokwenda nao nenda nao hivyo hivyo? Usikosee. Hapa tunakwenda katika mataifa makubwa makubwa hapa. Unafika mahali unabaki *Yes!, Yes!, Yes!, Yes you know, because you know, because.* Hakuna cha *you know, because you know because.* Unatakiwa unakwenda pale unakuwa *very accurate* katika Kizungu. Unazungumza watu wanasema *yes,* huyu ni Mtanzania anazungumza hapa. Wewe unatoka hapa unakwenda pale unabaki *yes.* Tanzanias *are stupid, yes.* Unaitikia *yes, yes, yes. Yes* nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna cha *yes,* fundisha watu Kiswahili, fundisha watu Kiingereza wajue. Kitu ambacho kina hatari ya kupotea ni Kiingereza. Ukikiacha hivyo namna hii, kitakwisha, itaondoka kabisa. Lakini mimi nikienda kwangu kule Siha, nikifika Siha nazungumza Kiswahili, sizungumzi Kiingereza. Nakuja kuzungumza Kiingereza nikija hapa Bungeni au nikienda katika Vyuo na maeneo mengine. Wewe leo unamwambia Waziri ondoa hiki Kiingereza tunataka watu wetu wajifunze. Wachina wanajifunza Kiingereza, Wajapan wanajifunza Kiingereza. Wewe ki-nchi kidogo *yes, yes, yes* hapa chenye *contradictions label* yake ya *productive process* ziko chini unasema hivi unajua sisi hapa tuko, wewe acha, achana na Kiingereza, halafu uniambie utakuwa *redundant* utakuta mahali utakuwa *irrelevant,* Kizungu tujifunze, Wabunge tujifunze Kizungu, unaona bwana, tujue Kiswahili, tujue Kiingereza, na-*insist* Kiingereza watu wajifunze kwa mazingira hayo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, huwezi ukaingia wewe katika utandawazi hapa unakwenda na Kiswahili unasema Mheshimiwa leo kimepata heshima kubwa kimeingia katika *AU.* Sawa, lakini tujifunze Kiingereza. Huko tunakokwenda kwenye utandawazi, watu wanaingia sasa hapa na matovuti, wanatuambia leo asubuhi tulikuwa tunajibiwa hapa, ametafutwa mtu wa kuongoza *TANROADS* katika nchi hii amekwenda kuchukuliwa Ghana huko. *What is that?* Ni haya haya mambo huwezi kufika kwenye mkutano una-*nod* unakaa kimya, *as if, if you keep quite* ndiyo *symbol* ya *wisdom, it is equivalent to zero.* Unataka kuwa *what you call you are, yes I am a Member of Parliament from Tanzania, I am representing my country,* unazungumza pale, watu wanasema *yes!* Pale kuna Mbunge pale. Ndiyo kitu tunachotaka kutengeneza hapa. Kiswahili kipewe *prominance* yake kifundishwe, kiwepo katika utaratibu kama tunavyokwenda na Kizungu kiwekwe hapa, Kizungu ni Kiswahili cha dunia au ni lugha ya dunia. Sasa mtu akitaka kunilaumu kwa nini umesema maneno hayo, hii ndiyo *position* yangu, mimi ndivyo ninavyoamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka nizungumzie tu kwamba Wizara ya Elimu na Utamaduni tunawashukuru sana, wakina Bureta, wakina Mwaimu, ahsanteni sana kwa kazi nzuri mnayofanya. *Bureaucracy* pale imeondoka. Lakini bado walimu wana-*complain* kwamba wakifika Wizarani pale kuna urasimu mwingi unajitokeza pale. Kuna suala la uhakiki wa haya madeni ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa amesema

yatalipwa. Tunaomba muyapitie, yaangaliwe haraka. TAMISEMI ndiyo wanatakiwa wafanye kazi hiyo. Haraka haraka kwa sababu mimi ninachoweza kuahidi hapa nikienda katika Jimbo langu la Siha, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, nitakaa pale nitapiga kikumbo pale kuhakikisha kwamba hizi hela za walimu hazikatishi *corner* ila zinakwenda kwa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hili zoezi linahitaji lifanyike haraka. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali pamoja na mawazo mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa tamko hapa, bado walimu wanalalamika kila siku kwamba hali yao ni mbaya. Hivi jamani tuwasaidie walimu wetu hao. Hizi hela kama zimeshatengwa tukienda kule tuhakikishe Wabunge wote tunakwenda kuchachamaa mle na sasa hivi mnajua ndiyo lala salama yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Siha naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante tumesikia. Au amekufilisi?

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Lakini kimsingi mimi sina kigugumizi chochote juu ya hoja yake, kwa maana naikubali kabisa mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza yale ambayo nimekusudia kuyachangia hapa, nawalisha shukrani na pongezi kwa wafuatao. Kwanza, Mheshimiwa Rais Mkapa kwa kuiongoza nchi yetu kimaendeleo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Rais huyu atakumbukwa sana. Nampongeza sana. Lakini pia namshukuru na kumpongeza Waziri Mungai kwa ujasiri wa kufanya kazi yake katika Wizara yake. Na kazi inaonekana, lakini pia namshukuru sana tena sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Sakila. Amefanya kazi vizuri sana. Amemsaidia Waziri wake vizuri sana. Lakini pia namshukuru sana Mama Malale, Katibu Mkuu kwa juhudi zake na anachapa kazi bila kuchoka. Ufanisi huu tunaouona wa kitaalam ni matokeo yake pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana na kumpongeza Afisa Elimu Kiongozi, kwa kuongoza Ofisi yake vizuri na kufanikisha hoja hii ikawa inasifiwa. Lakini pia nawashukuru Wakurugenzi na Wasaidizi wote wanaofanya kazi katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa shughuli mbalimbali za kumsaidia Mheshimiwa Waziri na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa nchi kwa sababu Wizara hizi zote ni za Mheshimiwa Rais Mkapa. Tunamshukuru sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na pongezi hizo kwa wananchi wa Jimbo na hasa wa Wilaya ya Kondoa nishukuru kwa mambo fulani fulani hivi yaliyofanywa vizuri. Niliyokuwa nayapigia kelele. Lakini Wizara na Serikali ikatekeleza. Nashukuru sana

kwa kukarabatiwa Chuo cha Ualimu cha Bustani. Sasa kinaonekana vizuri kabisa kwamba ni Chuo cha kisasa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunashukuru kwa kushughulikia maji katika Chuo hicho cha Ualimu Bustani. Maji yanapatikana, lakini bado kidogo. Mheshimiwa Waziri anatakiwa aongeze fedha ili tutatue tatizo zaidi la maji pale katika Chuo cha Ualimu Bustani. Namwomba Mheshimiwa Waziri aandike hilo, asije akasahau. Lakini akisahau nitamkumbusha kwenye vifungu huku. Pia ununuzi wa gari STK 1. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine niishukuru na kumpongeza kwa kujitahidi kutatua tatizo la maji katika Sekondari ya Wasichana kule Kondoa. Ametoa zaidi ya milioni 10 ambazo zitasaidia kuondoa kabisa tatizo katika Sekondari ile ya Wasichana. Namshukuru sana, anachapa kazi. Huyu ni yule askari aliyetua anafanya kazi sasa ardhini. Tunashukuru sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile namshukuru kwa kukubaliwa kuanzisha Kidato cha tano mpaka cha sita katika Sekondari ya Wasichana kule Kondoa. Nina uhakakika maandalizi yatafanywa kipindi kinachokuja vijana wataanza kuletwa pale. Tunamshukuru sana. Ndiyo kazi nzuri hizo, ndiyo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Kwa hiyo, tunamshukuru sana katika hilo. Lakini vile vile Mheshimiwa Waziri nampongeza na kumshukuru hata kabla hajafika lakini ipo ahadi ya kwenda kule, lakini tumpigie makofi najua atafika. Alisema atafika kabla Bunge halijaahirishwa kule Kondoa kuonana na viongozi kule na hasa wa Taasisi za Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo au maendeleo huwa yanazaa matatizo na pia unapotatua matatizo vile vile yanazaa maendeleo na hivyo ni vitu ambavyo vina mzunguko. Huwezi kumaliza kabisa. Haya yanakwenda pamoja. Kwa hiyo, sasa naomba nibaini baadhi ya matatizo ambayo nayaona ili yaweze kushughulikiwa na Serikali. Tatizo la kwanza ni hili la upungufu wa walimu katika shule za Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nitajikita katika Wilaya yangu. Wilaya yangu inahitaji walimu 2,408 waliopo ni 1,824. Pungufu ni 584, upungufu ni asilimia 24. Kwa hiyo, naomba mara tu tutakapoanza kuajiri walimu nipate walimu wa kutosha ili kazi ya kuimarisha MMEM na tuendelee tuimarishe MMES kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili ni upungufu wa walimu wa Sekondari nchi nzima. Lakini mimi nataka nieleze upungufu katika shule zangu za sekondari Kondoa, ambako nafanya kazi karibu nazo. Shule zifuatazo zina upungufu mkubwa wa walimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitazitaja ili Mheshimiwa Waziri aweze kuzikariri na azishughulikie zipate walimu mara moja. Kwanza Sekondari ya Kwapakacha, Sekondari ya Mondo, Sekondari ya Bereko, Sekondari ya Pahi, Sekondari ya Amani Karume pia ndiyo hiyo ya Pahi, Sekondari ya Intela, Soya na Kondoa Wasichana. Sekondari hizi

zote zina upungufu mkubwa wa walimu. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri azingatie na kwa sababu na Wasaidizi wake wanasikia nafikiri watamsaidia kufanya hiyo kazi kabla ya Mheshimiwa Waziri hajafika kuwauliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la tatu ni upungufu wa shule za sekondari Wilayani Kondoa. Katika ile mikoa yenye matatizo ya elimu ni pamoja na Mkoa wa Dodoma na Kondoa ipo katika Mkoa wa Dodoma. Kufaulu kwa wanafunzi katika Wilaya ya Kondoa nataka kuzungumzia Wilaya ya Kondoa. Waliofaulu darasa la saba kwa mwaka 2003 ni asilimia 36. Waliofanya mtihani ni 9,407. Waliofaulu mtihani ni 3,368, waliopata nafasi ya kwenda sekondari, au waliopata shule ni 1,008. Waliorudi nyumbani kwa sababu ya kukosa nafasi ni 2,360 sawa na asilimia 70. Ni kiama kabisa ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuliona hilo, wananchi wa Wilaya ya Kondoa, Jimbo la Kondoa Kaskazini na Kondoa Kusini tukaanza kuhangaika katika hii sera ya kujenga shule katika Makao Makuu ya Kata. Sasa hivi shule zifuatazo kama 16 zimefika katika hatua mbalimbali. Kwa hiyo, nataka nizitaje hapa na Mheshimiwa Waziri azijue tutakapokuwa tunaomba kibali asipate kigugumizi na hasa akizingatia kutupa nafasi kwa ile Mikoa ambayo iko nyuma sana kielimu na Kondoa ikiwa ni moja katika Mkoa wa Dodoma. Shule hizo ambazo tunahangaika nazo tumejenga ni Bukulu, Mnenia, Kikore, Ula, Farkwa, Mrijo, Kingale, Paranga, Busi, Kisese, Bumbuta, Masange, Ovada, Jangalo, Goima na Kalamba. Zingine nimeacha. Hizi hasa ndizo zimeonyesha sura nzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, hizi usisahau hebu zikariri, tutakapokuja kuhitaji kibali utusaidie. Tatizo lingine ni upungufu wa Wakaguzi wa Elimu. Mahitaji ya Shule za Msingi katika Wilaya yetu ya Kondoa, shule za msingi ziko 202. Tungehitaji Wakaguzi angalau 10. Lakini waliopo 7. Pungufu ni Wakaguzi watatu. Tunaomba basi angalau tuongezewe wawili tu. Tafuta mahali popote. Kwanza wapo walimu wengi tu wana sifa hizo. Toa kibali tu waajiriwe ili waweze kusaidia. Shule 202 ni nyingi. Kwa hiyo, hilo ni ombi nalitoa kwako.

Mheshimiwa Spika, tatizo la tano ambalo pia ni tatizo la mwisho katika yale ambayo nilipanga. Ni walimu wananung'unika kutokurudishwa kwa posho ya kufundisha *Teaching Allowance,* ambayo ilikuwepo zamani lakini imeondolewa kiujanja ujanja hivi. Halafu inaelezwa ipo katika mshahara. Hii ina sababu zake. Na ina faida zake, ni muhimu sana. Faida ya posho hii kwanza itapunguza sana habari hii ya *tuition, tuition,* walimu wanatafuta ziada ya pesa. Ni ziada inatafutwa. Sasa hii ziada tuwape *Teaching Allowance* watatulia, watatufanyia kazi vizuri na wala hakuna hasara. Katika hizi hizi fedha za MMEM mega tupeleke pale ni sehemu ya MMEM vile vile tunataka kuimarisha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili ni la msingi sana pamoja na mambo mengine yote walimu umesikia, lakini hili la *Teaching Allowance* kwa nini limepotezwa? Tunaomba sana hili lifanyiwe umuhimu. Sasa kama nilivyoeleza ziko faida nyingi za hii *Teaching Allowance,* nyingine ni kwamba walimu watakuwa makini sana, unajua kazi ya ualimu, mimi bahati nzuri vile vile nimefanya kazi hii ya kufundisha. Maana mwalimu kwanza

lazima awe na kitu kinaitwa *syllubas,* mitaala na ili mwalimu avutike zaidi lazima awe na kishawishi fulani cha kutafsiri huu mtaala kwenda katika kitu kinaitwa Maazimio *scheme of work na scheme* hiyo nayo itafsiriwe iende katika maandalio na maandalio nayo yatafsiriwe yaende katika kufundisha na baada ya pale sasa ndiyo watoto wanalishwa kwa kufundishwa vizuri. Sasa hawa tusipofanya hivyo, wanakata tamaa ndiyo maana wanafundisha haraka haraka time ikiisha wanakwenda kwenye *tuition.*

Mheshimiwa Spika, lakini haitoshi hiyo, ndiyo maana tunasema walimu wanafanya kazi wakati wote, bado wakasahihishe madaftari, bado wakati wote wapo kazini wanasahihisha kule nyumbani, wanaandaa. Yaani hawapumziki. Mimi mke wangu ni mwalimu. Halali, siku zote analala wakati mimi nimeshalala. *(Kicheko)*

Lakini vile vile walimu hao ndiyo walezi na vile vile tunawatumia katika mambo mengi. Tunawatumia hata katika sensa ya Taifa, tunawatumia hata katika uchaguzi. Hawa lazima tuwape vitu vya kuwapa motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuunga hoja mkono na nimemaliza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kuniruhusu nichangie. Na kabla sijaendelea, ananitania hapa Mheshimiwa Semindu Pawa ama ananikumbusha kwa sababu kabla hatujatoka kunywa chai kuna memo ulikuwa nayo hapo. Sasa ilipotajwa wote wakasema Mutungirehi, nadhani walijua nilikuwa nakutania. Sasa ninaomba radhi kwa hilo na ndiyo maana...

**SPIKA:** Ni vizuri umejisalimisha. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Lakini kabla sijaendelea, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni pamoja na timu yake. Ninakumbushwa kwamba ni mara ya kwanza. Lakini siyo mara ya kwanza na wanaofanya vizuri huwa nawapongeza na nampongeza Waziri kwa sababu kuna mambo mengine katika mtindo wa kiungwana kama Mheshimiwa Spika, unakuta mtu amenunua sabuni ana karai, ameweka nguo zake, ameanza kuzifua, halafu wewe unamwambi nguo zako chafu. Kwa kweli unakuwa una matatizo. Unachoweza kubishanana naye ni namna ya kutumia sabuni au aina ya sabuni anayoitumia kana kwamba inaweza kumchubua mikono na kama amemaliza kufua unaweza ukamwelekeza jinsi atakavyonyosha, lakini siyo kumwambia afue nguo zake wakati ameshaanza.

Mheshimiwa Spika, sasa hivyo kwa sababu gani? Kila mmoja, kila Mbunge, kila mtu humu ndani alikuwa akijaribu kusema tupunguze karo za shule za sekondari, tufanye mpango wa shule za sekondari kama tulivyofanya shule za msingi. Sasa ni bahati nzuri kwamba hotuba ya Waziri imeyafuatia hayo yote na wamefanya kama tulivyokuwa tukishauri hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua ni Serikali mzima imefanya. Lakini Serikali mzima imefanya inategemea vile vile na msimamizi wa Idara ile au wa Wizara ile anafanya nini. Anavyoweza kujenga hoja, anavyoweza kuwa *courageous* kuzitetea ndani ya Baraza la Mawaziri na hata anavyoweza kuwa nje akaweza kubuni utaratibu ambao utafanikisha zoezi hilo. Kwa hiyo, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyosema ya kwamba kama unakuta anafua, lakini unadhani kuna sabuni nyingine, ile inaweza ikamchubua mkono unapomwelekeza. Kwa hiyo, nitakayoyasema mengine ni katika kuboresha kwamba kile wanachokifanya ni kizuri lakini wayaangalie na haya.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa hapa kuhusu matatizo ya walimu na kwamba Wizara ya TAMISEMI wameunda Kamati kwa ajili ya kuhakiki madai ya walimu hasa wale walimu wa shule za msingi ambao wanahusika na Wizara ile.

Lakini ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba kwa walimu wa Shule za Sekondari, Vyuo na Wanavyuo wengine ambao wanasoma ambao wako chini ya Wizara yake na wana madai hakutuelezwa kana kwamba na yeye sasa ameunda Kamati ya Kuhakiki madeni yao na kuchunguza yale mambo ambayo tuliyataja kwamba yalikuwepo.

Kwa hiyo, ningekuomba kwamba Mheshimiwa Waziri atujibu wakati ana-wind up kama na yeye ameunda Tume au Kamati ya Kuhakiki madeni ya walimu wa Shule za Sekondari pamoja na Vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa kuendeleza elimu ya shule ya sekondari, ningeomba kuikumbusha Wizara pamoja na Wajumbe wengine pamoja na Wabunge wengine wamesema, kuangalia hela tumekwishazipata, lakini tuendelee kuangalia bila ya kujali kama tumekwishakupitia nchi mzima na kuangalia ni sehemu gani ambazo ziko nyuma katika ujenzi wa shule za sekondari. Kwa sababu za kihistoria, kwa sababu za kijiografia na kwa sababu za kimazingira.

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaposema watajenga madarasa, watajenga pengine *hostel,* kwa sababu hosteli ni za muhimu, ukizingatia sera ya Wizara katika shule ambazo ni za wananchi lakini zinasaidiwa na Serikali, wanapozungumzia *catchment area* wanazungumzia eneo lile lile kama kilomita 6, lakini ukikuta shule moja iko pale Mabira kwangu na hamna shule nyingine katika jimbo, utakuta watu wanatoka umbali wa kilometa 20 kuja kwenye shule ile.

Sasa lazima utafute wanafunzi wa kujaza mle, hii inakuwa ni kero kubwa sana. Kwa hiyo, suala la *hostel* tungedhani kwamba ni kitu cha muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichotaka kusisitiza ni kwamba pamoja na hilo watu wa Dar es Salaam ambako shule zote kuna umeme au pale Bukoba Mjini, mimi nimesoma Kahororo pale, Ihungo, Nyakato kuna umeme na kuna maktaba.

Sasa wale wa vijijini ambao hawana umeme, hawana mwanga wakati wa kusoma jioni kama watakuwa na hosteli kwa kweli kunakuwa na usumbufu.

Kwa hiyo, tungependa *component* moja iingizwe kwamba kwa sababu Serikali imesema hela zile ambazo wanalipa karo zitabaki shuleni, zile sh. 20,000/= na Serikali imeongeza ruzuku nyingine, suala la wao kununua *generator* kila shule iliyoko huko kijijini ni la msingi sana, ili wanafunzi wale waweze kufanya *evening studies* itawasaidia sana katika kujiendeleza kwa sababu umeme hauwezi kupatikana kwa mara moja katika shule zote za vijijini kama ilivyo katika shule za mjini. Na hii pengine ndiyo inayosababisha kuwa na tofauti za *performance* kati ya wale walioko shule za mjini na wale walio katika shule za vijijini.

Kwa hiyo, lazima hilo tulione kuweza kuondoa ili lengo letu la kuwapeleka hawa wote waweze kumaliza wakiwa na elimu ambayo ni bora na ambayo kwa kweli itakidhi viwango vya kitaifa na vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika hilo limezungumzwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi hapa, suala la watoto yatima, sasa kwa kuwa serikali itajenga karibu kila Kata shule, kwa kusaidiana na wazazi.

Tungeomba suala la watoto yatima kwa kweli lipewe umuhimu kwa sababu hawa na ndiyo wangefikiriwa au wangetengewa hata hela nyingi sana. Kwa sababu wazazi wake walishakufa, kila kitu kilishaharibika. Na hela zote zilitumika wakati wanaumwa au wakati wa mambo mengine.

Kwa hiyo, hawa wanahitaji na nitampa mfano Mheshimiwa Waziri alipotoa maelekezo kwamba jinsi ya kupata watoto yatima kutokana na mapendekezo ya mwalimu mkuu, Kamati za Shule pamoja na Serikali za Vijiji. Kwangu Karagwe waliorodheshwa kwa utaratibu huo na bahati nzuri wakashinda.

Lakini ni asilimia 40 ya wale ambao walikuwa wamependekezwa na kwa kweli wakashinda kwa utaratibu ambao Wizara ilikuwa imeruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wale wengine asilimia 60 wakabaki. Kwa hiyo, tungependa Wizara ilichukue hilo kwamba watoto wale yatima kama wamependekezwa kwa utaratibu ambao Wizara imekwishaanzisha, na wameshinda Wizara ihakikishe kwamba hata mtoto mmoja asibaki kwa utaratibu ambao wanaweza kuu-design ili uweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la shule ya Siti Mwinyi, *St. Mathew,* Masjid Kuba, za Dar es Salaam na *Southern Highlands* zilikuwa na matatizo ya kwamba mitihani iliibiwa, ikavuja na imechukua muda mrefu, wameunda Tume.

Sasa tunaangalia kwenye vyombo vya Habari na mambo mengine, tungelipenda labda Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* anaweza kuwaambia nini Bunge hili na Watanzania kwamba hawa watu hizo Tume, Kamati zimemaliza kuchunguza?

Mheshimiwa Spika, kama ni kweli wameiba mitihani basi ijulikane, basi ijulikane na kama haikuibwa basi tujue kwanza ili wenye shule waweze nao kupata sifa yao mzuri, waweze kupelekewa wanafunzi na wale ambao wanahusika waweze kwenda katika shule nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie ambalo alikuwa anazungumzia Mheshimiwa Mwanri, sitaki kurudia rudia lakini ni la msingi, nalo ni kuhusu matumizi ya Kiswahili. Ninavyoelewa mimi si kazi ya Bunge kulazimisha mambo ya *academic* au kutunga mitaala, ni kazi ya wataalam, Wabunge wanaweza wakasema ama wakachangia katika dira ama katika mawazo, lakini yapo mambo mengine ya kiutaalam zaidi, yanafanyika katika Vyuo Vikuu au katika shule au katika taasisi ambazo zimepewa jukumu hilo kisheria la kutayarisha mitaala. Lakini matumizi ya Kiswahili kwamba sasa Kiingereza tufute, tutumie Kiswahili *as a medium of instruction in all schools* kwa kweli mimi sikubaliani na hilo. Mimi nimechukua *KLF (Kiswahili, Literature in English and French)* wakati nasoma *Milambo High School* na nimesoma Kiingereza na Kiswahili na *Literature* nikiwa *University of Dar es Salaam* pamoja na masomo mengine. Lakini nadhani tukubaliane kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Mwanri, kwamba kama tulidhani tulikuwa tunasoma Kiswahili kwa ajili ya umoja wa Tanzania, ni muhimu kusoma sasa Kiingereza kwa juhudi zote katika masomo hayo kwa ajili ya umoja wa dunia, kwa sababu tupende tusipende hatuwezi kuukataa ukweli huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilikuwa na Profesa Masenge wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, jana nilimwona sijui kama yupo hapa. Nakumbuka kulikuwa na mgomo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa wanafunzi ambao wamegoma wameandikiwa barua aeleze ni kwa nini hakwenda darasani. Nakumbuka mmoja alikuwa anasoma *Faculty of Engineering* akasema, aah, *I did not attend classes because I intimidated the whole group.* Sasa badala ya kusema *I was intimidated by the whole group* akasema *I intimidated the whole group* na kwa kweli walimwondoa mwaka mzima. Sasa kwa kushindwa *structure* ile akaondokana na nadhani Mheshimiwa Mwanri ndilo analosema.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunapokuwa katika utandawazi, wewe unakwenda pale na Kiswahili Swahili chako watu hawakusikilizi kwa sababu kuna *hard concept* na katika mambo haya *science probably and technology will become a system of the world,* itakuwa ni *system* ya dunia. Sasa na ndiko tunakotaka kwamba dunia ya sasa hivi sio kusema kwamba tuna dhahabu nyingi, sijui tuna madini, tunataka sayansi na teknolojia na hayo hatuwezi kuyapata kutoka kwa wenzetu, ni lazima tujue ile lugha ambayo kwa kweli ni ya dunia. Nilikuwa naangalia Mkataba wa *TTCL* na nadhani tulipata tabu kwa sababu ya watu ambao tuliwapeleka ku-*negotiate, they were very inferior some how, somewhere.* Sasa mtu umemwambia kwamba huyu *strategic investor* apate *bank guarantee.* Yeye anakwenda anafuta pale anaandika *a pledge,* ame-*pledge* sasa *pledge* akikataa kulipa unamfanyaje unampiga na ndiyo maana niliwahi kuliambia Bunge

kwamba hamwezi kupata. Sasa mambo kama haya tunayaona ni madogo lakini yanatu-*cost.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Mwanri ni kweli kwamba wanafunzi waende pale wasome Kiswahili na wajifunze wale waliokwenda juu Kiingereza na masomo yote kwa Kiingereza na kama zipo lugha nyingine za Kimataifa kwa ajili hiyo waweze kuzichukua kwa sababu hatuwezi kulikwepa hilo. Wale wanaodhani huu ni utani, maana yake wakati tunasoma sisi sekondari miaka ya 1987, wanasema kama hukushinda Kiswahili unapata F kama ulipata *division one* wanaku-*penalize* unakwenda *division three* kama sikosei. Siasa hukushinda umepata mahesabu yote, tena umepata hata hesabu A au *Physics,* wanaku-*penalize* wanakupeleka *division three* na mambo haya kwa kweli yametuathiri sana. Tunaweza tukasema sana katika Afrika Mashariki tukasema kwingine kote, lakini inapokuja kwenye mambo ya ujasirimali *(entrepreneurship)* na mambo mengine *the poorest.* Sasa tusije kurudi huko na cheti cha Kiswahili na Siasa sijui kama siasa wanaitaje, tukarudi huko kwa kweli nadhani itakuwa inatuchelewesha sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naomba sasa Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara nyingine waanze kufanya tathmini ya athari chanya na athari hasi za ni nini kitakachotokea tunapopeleka mpango huo mkubwa wa kuboresha elimu ya msingi na elimu ya sekondari kwa sababu lazima tujiandae. Sasa kama umepeleka watoto wengi sekondari, sio wote watakaokwenda high school wala sio wote watakaokwenda Vyuo Vikuu kuna wengine watapaswa kwenda kwenye Vyuo vya Ufundi na Vyuo vingine. Kwa hiyo, mpango huu lazima uanze sasa kuanza kutathmini tunajiandaa vipi kukabiliana na wimbi hilo kubwa. Vinginevyo tutaelimisha watu wengi kama hakuna jinsi ya kuwa-*incorporate* katika mzunguko wa uchumi na shughuli za kijamii tutakuwa na jeshi litakalotupinga kwa sababu watakuwa wanaelewa. Mtu atamaliza *High School,* atamaliza Chuo Kikuu, kazi haipo, halafu ukaja kumwambia unajua, unajua, tutagombana na hilo jua lako halafu unapata shida.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GWASA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, niruhusu kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango kuhusu hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Naomba kabisa nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Afisa Elimu Kiongozi na timu nzima katika Makao Makuu ya Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Ni hotuba ya kutia moyo na kama alivyosema yeye mwenyewe wakati anawasilisha hoja hii hapa, ni hotuba ambayo haijawahi kutokea katika historia ya elimu katika nchi yetu. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya ni mazuri lakini mojawapo ambalo nalifahamu Mheshimiwa Mungai ni kwamba wakati wote yeye ni mwanafunzi na hupenda kushauriwa na hupenda kusikiliza na kutokea hapo akaenda kutenda. Kwa bahati nzuri niseme kwamba Wilaya ya Ngara Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu na naomba Mungu amrudishie afya yake kwa haraka sana. Mheshimiwa Katibu Mkuu alikuwa Ngara si muda mrefu kuanzia leo, baadhi ya Wakurugenzi katika vitengo mbalimbali

wametembelea Ngara na Serikali inajua matatizo ya Wilaya ya Ngara kwa muda mrefu. Kwa hiyo, natangulia kusema kwamba shida za Ngara leo kielimu namwomba Mheshimiwa Waziri atege masikio niziseme kwa niaba ya wananchi wa Ngara ili aweze kutusaidia kulingana na mpango mzuri na mrefu ambao ameuandaa kwa mwaka ujao wa fedha. Naomba kusema kwamba mwaka 1995, Mheshimiwa Rais alipokuwa yupo kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu Wilaya ya Ngara, aliahidi kuipa sekondari. Ni kwa sababu Wilaya ya Ngara haina sekondari, ina upungufu mkubwa sana wa sekondari, nitaeleza baadaye. Sekondari hiyo mpaka leo haijajengwa. Kwa bahati nzuri watu wawili niliowasema Mheshimiwa Naibu Waziri na mama yangu Malale wamefika pale wameona shule hiyo. Alipewa mkandarasi kujenga sekondari hiyo, Wilaya ya Ngara haimfahamu huyu, akaishia Wizarani, pesa anapewa kazi haifanyiki. Sekondari hii mwaka huu ndiyo inafanya mtihani wa kidato cha nne. Hakuna maabara katika sekondari hii, hakuna nyumba za walimu, kuna nyumba ya Mwalimu Mkuu tu nayo haijakamilika, hakuna Maktaba, hakuna mabweni na tunapoteza watoto wa kike karibu sita mpaka kumi kila mwaka kwa sababu ni sekondari inayohudumia Tarafa mbili za Murusagamba na Lurenge zenye Vijiji ishirini na tisa. Pia hakuna maji, umeme, wala usafiri na sekondari hii ipo kilomita sabini kutoka Makao Makuu ya Wilaya, ipo porini kabisa, je, wananchi wa Ngara warudi kwa Mheshimiwa Rais, kumlilia?

Viongozi niliowasema wameiona na ipo katika njia kuu ya wakimbizi kutoka Burundi wanapokuwa wakikimbia kwao kuja Wilayani na kila wakati kuna matatizo katika njia ile. Shule hii haina walimu, kwa uchache, licha ya kusema kwamba haina samani, haina vyoo, ni ahadi ya Rais kwamba hii shule itajengwa lakini mpaka inafikia kwamba Mheshimiwa Rais anamaliza vipindi vyake viwili vya Urais shule hii haijaonekana kwamba inaweza kuwasaidia wananchi wa Ngara. Katika mpango uliopo wa ukarabati, wa kufikiria kupanua shule, namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri kwanza kabisa naye afike pale akashuhudie kama wasaidizi wake walivyofanya, lakini pia awasaidie wananchi wa Ngara kumaliza sekondari hiyo. Inatutia uchungu sana tangu mwanzo mpaka leo karibu wanaoijenga ni wananchi wa Ngara ambao hawana kipato na wapo katika matatizo ya wakimbizi. Inauma sana, namwomba mama yangu Malale arudi Ngara pengine atusaidie, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje, najua kwamba Naibu Waziri afya yake haimruhusu kwa wakati huu lakini ninaposema hivi najua kwamba wananchi wa Ngara wametega masikio wananisikiliza, ninasema nini kuhusu shule hii. Ni shule ambayo inatupa matatizo, ni shule moja tu katika Tarafa hizo mbili naomba sana tufikiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili linahusu shule moja ambayo ndiyo shule ya kwanza katika Wilaya ya Ngara, nayo ni shule ya Kabanga ambayo imejengwa mwaka 1991. Shule hii kwa bahati nzuri mwaka juzi Mheshimiwa Sakila alikuja kusimamia mahafali ya kumi na moja. Haya haya niliyoyasema kwa shule hii yapo pale pale, shule haina nyumba za walimu, haina usafiri, haina maji wala umeme. Ni kitu cha kutisha kwamba Wilaya ya pembeni kama hiyo, Wilaya ambayo ina matatizo mengi, miundombinu yake inasumbuliwa na watu wanaoingia bila kuwategemea na Serikali inafanya kama inaipuuza, mimi nasema kwa kweli Wizara hii kwa uwezo na nguvu ilizonazo naomba sana watusaidie. Hii ndiyo shule ya Sekondari mama Wilayani. Tunaomba usafiri baada ya ule wa mpaka 1994 kupotea.

Mheshimiwa Spika, pia kuna sekondari zingine mbili ndiyo zimefunguliwa mwaka huu, sekondari ya Mgoma ndiyo imepata Mkuu wa Shule miezi miwili iliyopita na sekondari ya Kibogora haina Mkuu wa shule mpaka sasa hivi, haina Mkuu wa shule. Walimu hakuna na imefunguliwa mwezi Machi, mwaka huu. Kwa jumla ni kwamba tuna visekondari vitano hivyo, Wilaya iliyo na Tarafa nne, Kata 17 na Vijiji 73 inahudumiwa na sekondari tatu ambazo zinaonekana zipo katika hali ya unafuu nafuu. Sasa niombe Mheshimiwa Waziri akisaidiana na Katibu Mkuu watazame Wilaya hii ya pembeni inaweza kusaidiwa vipi ili kuinua elimu ya wananchi. Nazungumzia upungufu wa sekondari katika Mkoa wa Kagera. Wilaya ya Ngara kwa miaka yote inahemea elimu kutoka Mikoa ya nje kwa sababu ya wananchi wake. Pamoja na yote hayo najua kwamba Mheshimiwa Waziri atapongeza mwamko uliopo katika Wilaya hiyo. Mwaka 2003, Wilaya ya Ngara ilikuwa ni ya kwanza katika Mkoa wa Kagera wenye Wilaya sita. Ilikuwa ni ya kwanza katika Kanda nzima ya Ziwa, katika Mikoa minne na ilikuwa ni ya nne Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana walioingia kwenye mtihani walikuwa 2,656, walioshinda walikuwa 1,868, waliochaguliwa 633 peke yake. Sasa yawezekana Mheshimiwa Waziri atakapokuja tutalazimika kukinga kinga gari lake lisitupiwe mawe kama gari la Mbunge wa Wilaya ya Ngara. Watoto hawa wote wapo Vijijini wanahangaika. Hawa 633 ni kwamba wamesambazwa katika sehemu zote ambako tuna *quarter* katika nchi nzima. Lakini bado watoto 1,235 wapo Wilayani wakiwa na alama kuanzia 150 mpaka 180. Naomba Mheshimiwa Waziri alie pamoja na mimi. Naomba Mheshimiwa Katibu Mkuu alie na mimi, atazame kwa kweli hali ilivyo katika Wilaya hiyo inafananaje. Wilaya inaomba ipewe sekondari moja kwa kila Kata kwa maana ni Kata kubwa na yenye shule za msingi nyingi. Katika kuongeza sekondari, katika ku-*rehabilitate* sekondari, katika kuongeza mikondo, Wilaya hii inahitaji msaada wa Wizara hii kwani pamoja na matatizo yote nguvu tunayo, nia tunayo na kwa wakati huu tunaandaa shule nane kama nilivyozungumza wakati wa swali langu namba 183. Shule hizo zinazoandaliwa ni Nyamiaga, Kanazi, Kasulo, Kirusha, Murusagamba, Mabawe, Nyakisasa na Kibimba. Ni katika kujaribu kuondoa tatizo hili ambalo limewakabili wananchi wetu. Naomba Wizara hii kama kweli ni kugawa elimu kwa usawa basi iisaidie Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie nyumba za walimu. Hii ni kwa shule za msingi au kwa elimu ya msingi na sekondari. Nina shule ambazo naweza kuzitaja ambazo walimu wake wanatembea kati ya kilomita kumi na kumi na tano kutoka wanakoishi kwenda shuleni. Nina shule za Kigina, Nyakariba, Magereza Lusumo, Lusengo, Mubwilinde, shule hizi na nyingine nyingi hakuna nyumba wa walimu. Wananchi wanachopigana nacho zaidi katika kujikomboa kujitoa katika ujinga ni kujenga madarasa na vyoo, lakini kwa sehemu nyingine wanaacha na hii ipo kila mahali katika nchi hii. Naomba ijulikane kwamba kwa kweli walimu wetu wanaishi katika hali mbaya na kwa jumla sehemu kubwa inayorudisha nyuma elimu yetu ni kwa sababu ya mazingira mabaya wanamoishi walimu wetu. Walimu hao wanafanya kazi nzuri, nyingi na katika mazingira magumu, lakini bado nchi hii inaendelea kwa uwezo wa walimu na wote hapa

tumepita mikononi mwa walimu. Lazima tuiheshimu kazi ya walimu na tuwape maisha mazuri kwa kutazama mazingira wanamoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka vile vile nizungumzie Chuo cha Ualimu. Wilaya ya Ngara, Karagwe, Kibondo, Biharamulo, Geita, Bukombe ni Wilaya ambazo zinapakana. Ukubwa wa Wilaya hizi unajulikana, wingi wa shule zilizopo sasa za msingi na sekondari unajulikana. Naomba Wizara ifikirie kujenga Chuo cha Ualimu katika eneo hili. Naomba sana. Juzi tarehe tisa Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa Ngara kilio cha wazee alipokutana nao cha kwanza ilikuwa ni kumwomba eneo hilo lipewe Chuo cha Ualimu. Naomba Mheshimiwa Waziri alione hilo na afikirie kufanya kitu hicho. Inasikitisha, Jimbo Katoliki la Lurenge liliomba kujenga Chuo cha Ualimu lakini sasa ni miaka mitatu Jimbo hilo linazungushwa, Chuo hicho kilikuwa kijengwe Mjini Biharamulo lakini mpaka leo imekuwa ni shida. Wakati huo naye Baba Askofu alikuwepo wakati wananchi wanamwomba Makamu wa Rais kupewa chombo hiki ambacho ni muhimu kuongeza wingi wa walimu na kupunguza adha ya ujinga. Naomba Mheshimiwa Waziri hili alifikirie na kujenga Chuo cha Ualimu Wilayani Ngara.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kuhusu mishahara ya walimu. Walimu wa Ngara wanalazimika kwenda Bukoba kilomita 350 kufuata mishahara. Wakati mwingine inafika mpaka majuma matatu hawajapata mishahara yao na ni lazima mwalimu atoke shuleni kufuata mishahara hiyo. Kwa sababu hivi vishule ni vichache na vipo mbalimbali pengine hata mawasiliano yanakuwa ni kidogo kuweza kupangana ni shule ipi ifuate mishahara yao kutoka Bukoba kila inapofika wakati wa kupokea mishahara. Hii isiwe kwa Wilaya ya Ngara, kama kuna mahali pengine kuna matatizo kama hayo, mimi naomba kabisa mishahara ya walimu iwe inakwenda na kupokelewa kwenye ngazi za Wilaya. Kwa nini Mkurugenzi Mtendaji asipokee mishahara ya walimu kutoka Wizarani? Kwa nini mishahara hii isipelekwe benki kwa sababu bado tuna hiyo benki ya *NMB* katika kila Wilaya? Inawanyima nafasi ya kufanya kazi vizuri, inapoteza masomo ya wanafunzi, inachukua gharama zaidi kuongezea kwa hizo wanazotegemea kuzipata. Mimi nafikiri kwamba si kitu kizuri na kusema kweli kama tunafanya mapinduzi katika maendeleo ya nchi yetu, naomba sana Wizara ifikirie kufanya mapinduzi katika kupeleka mishahara kwa walengwa ili kusudi wawape nafasi ya kufanya kazi zao vizuri. Naomba nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri ajue kwamba Wilaya hii ipo pembezoni na kwa miaka yote imekuwa ikihemea elimu. Kwa hiyo, ifike wakati atusaidie.

Kwa hayo, machache niliyoyasema, naunga mkono hoja hii na nasema tutakusaidia katika kuendeleza shughuli hizi. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, anafanya kazi nzuri sana hasa kuwa karibu na matatizo na maendeleo ya Wizara yake. Nampongeza mno Ndugu yangu Bujiku Sakila. *Comrade* Bujiku Sakila, yupo karibu sana na sisi Wabunge. Nampongeza Katibu Mkuu na wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo katika Jimbo langu linalohusu shule ya sekondari ya Mwaya ambayo iko kilomita 30 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Tatizo lolote likitokea Mwalimu Mkuu analazimika kutembea kwa miguu, hakuna usafiri wowote wa gari. Nilikwenda mimi mwenyewe kumwona Katibu Mkuu wa Wizara, kuomba wafikiriwe kupewa usafiri. Aliahidi atalitazama. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie gari la aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wakuu wa Vitengo katika Wizara hiyo wanatusikiliza sana sisi Wabunge tunapofika katika ofisi zao. Tunaomba waendelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu pamoja na maafisa wote wa Wizara hii kwa kutayarisha hotuba hii vizuri sana.

Mchango wangu nauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

(a) Watoto waliokosa nafasi ya kuingia darasa la kwanza;

(b) Mafunzo ya ufundi kwa wanafunzi;

(c) Elimu ya watu wazima; na

(d) Madawati.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka wanafunzi wa darasa la kwanza wanaoandikishwa ni wachache sana. Hivyo, husababisha watoto wengi kukosa nafasi ya kuingia darasa la kwanza. Naiomba Serikali iwe na mpango maalum wa kuwapatia elimu watoto ambao walikosa nafasi ya kuingia darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la kuwapatia wanafunzi mafunzo ya ufundi ili wanapomaliza masomo yao endapo hawataajiriwa na Serikali waweze kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaomba Wizara ya elimu isimamie elimu ya watu wazima ili wazazi wawe na uwezo wa kusimamia masomo ya watoto wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za walimu, Wizara iwe na mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa nyumba za walimu zinajengwa kila penye shule, ujenzi huu wa nyumba za walimu wahamasishwe na wazazi wa wanafunzi ili nao washiriki ujenzi wa nyumba hizo. Kwa hiyo, basi Wizara hii na Wizara zingine zilizo na uhusiano na Wizara hii washirikiane katika suala hili la ujenzi wa nyumba za walimu badala ya Wizara kuchukua jukumu peke yake.

Mheshimiwa Spika, uwepo mpango maalum wa kutafuta madawati kila shule, wananchi na wenye uwezo wahamasishwe kuhusu suala hili la madawati. Hii iwe ni kampeni ya kudumu.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Nianzie pale nilipoachia juu ya maslahi ya walimu. Walimu wakiachwa bila malipo muda mrefu inaleta manung'uniko na kuwafanya walimu wasifanye kazi kwa moyo. Katika hali hii watoto watapata elimu inayotakiwa? Naomba Serikali sasa ipunguze urasimu wake wa kulipa mishahara ya walimu kwa sababu walimu wanapoajiriwa mishahara yao inakuwa katika bajeti. Serikali inapoacha kuwalipa kwa zaidi ya mwaka, fedha zilizotengwa katika Bajeti ile zinakwenda wapi? Serikali haioni hapa kuwa kuna kasoro kubwa?

Namshukuru Waziri Mkuu kwa maagizo yake ya kutaka madeni ya walimu yalipwe. Pamoja na kutekeleza agizo hili, nashauri kuanzia sasa walimu walipwe mishahara, *arrears* zao na marupurupu yao mengine kwa wakati. Uzembe huu usiachiwe kuendelea na Serikali sikivu ya CCM nina hakika italifuatilia hili na kulitekeleza kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushauri katika mahitaji ya walimu. Walimu wa shule za msingi hawana nyumba nadhifu zenye kumpa hadhi mwalimu. Mpango wa MMEM uangalie utaratibu wa kuwajengea nyumba walimu wetu. Walimu wasipokuwa na yumba za uhakika hawataweza kuandaa *lesson notes,* kusahihisha wala kujifunza. Vitu hivi ni muhimu sana kwa kutoa elimu ya uhakika na itakuwa motisha kwa walimu kukubali kufundisha hata Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezungumzia sana elimu ya awali, lakini hotuba ya Waziri haielezi chochote juu ya walimu wa elimu ya awali. Walimu hawa ni muhimu katika kujenga msingi wa elimu ya mtoto. Hivi sasa hakuna chuo chochote cha Serikali kinachoandaa walimu hawa. Baya zaidi hakuna muundo wa kada hii ya walimu. Kwa msingi huo, elimu ya awali haitiliwi mkazo Vijijini. Mijini kuna shule nyingi za binafsi za awali tofauti na Vijijni, hivyo watoto wa Mijini wanapata msingi wa kuanza tangu darasa la kwanza. Nashauri Serikali ilitafakari suala hili kwa makini, sababu wananchi wengi wako Vijijini na sio Mijini. Kama lengo ni kuboresha elimu basi hata Vijijni wanastahili huduma zilizo bora.

Mheshiimwa Spika, napongeza uamuzi wa Serikali wa kupunguza ada ya sekondari ya kutwa, angalau itasaidia. Lakini bado naunga mkono ushauri wa Kamati wa kufuta kabisa ada hii. Iwapo ada itafutwa, utasaidia sana wananchi wa Vijijini ambako umaskini umekithiri. Mzazi abaki na jukumu la kutafuta sare za shule. Naomba Serikali iliangalie hili kwa uzito wa pekee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Mungai Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Sakila, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya. Wizara hii imefanya kazi nzuri sana tangu 2001 hadi leo. Inatoa fedha bila upendeleo wowote nchi nzima. Hongera sana na hongera sana Mheshimiwa Mungai. Naomba Mola akubariki na akupe afya njema na hekima katika kuiongoza Wizara hii. Vile vile napenda kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujenga hoja ninayo machache ya kusema kuhusu hotuba hii. Tunashukuru kuwa MMES imepata fedha nyingi na madarasa na nyumba za walimu zitajengwa. Tunaomba Wizara iweke watu wa kufuatilia na kuhakikisha kuwa fedha zinatumiwa vizuri na pale itakapogundulika kuwa fedha zimetumiwa vibaya hatua kali zichukuliwe. Mfano mbaya wa matumizi wa fedha za MMEM umekuwa unatokea sehemu kadhaa ikiwemo Wilaya ya Serengeti lakini Wizara imekuwa haichukui hatua zinazopasa wakati Wabunge wanaleta taarifa kwa wahusika. Tunaomba sasa Wizara iwe macho na ichukue hatua mara tu ikisikia fedha zinatumiwa vibaya.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Serengeti imejenga shule nyingi za sekondari. Kila Kata sasa ina shule ya sekondari. Lakini hizi shule hazina walimu wa kutosha, vifaa vya kufundishia ni kidogo sana na hazina nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba hizi shule zitupiwe macho ili ziweze kupata walimu wa kutosha na nyumba za kutosha. Vile vile zipatiwe vifaa vya kutosha ama sivyo tunawakatisha tamaa wananchi wanaojitolea kuzijenga na kukuta watoto wao wanaanguka mitihani ya kidato cha nne. Vile vile tunaomba Waziri wa Elimu atembelee shule hizi. Inakuwaje tangu 2001 hadi leo hajafika Serengeti? Serengeti tutakupokea kwa shangwe, kwani kazi yako ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ikazanie masomo ya hisabati na Kiingereza. Watoto wengi wanafeli haya masomo. Haya masomo ni muhimu sana na mtu yeyote asiyefanya vizuri katika masomo haya, ni dalili ya kutosha kuwa hawezi kuendelea na masomo ya juu.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, namshukru na kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba yake nzuri na yenye kina kirefu. Pia nachukua nafasi kuwashukuru wataalam wote kwa jitihada zao na ufanisi mkubwa waliopata kwa kuendesha Wizara hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ada za sekondari za kutwa za Serikali kutoka shilingi 40,000/= na kuwa sh. 20,000/=. Suala hili linahitaji pongezi kubwa sana. Tatizo langu ni juu ya shule za sekondari za Serikali za bweni. Shule hizo pia hupokea watoto wa maskini, lakini bado ada zao ni sh. 70,000/=. Nashauri kuwa kiwango hicho hicho cha sh. 20,000/= kiwe kwa sekondari zote za kutwa na za bweni ili wazazi wote waweze kupata nafuu kwa mfano watoto wote wa kifugaji ambao wote wanalazimika kwenda shule za bweni watalazimika kulipa shs. 70,000/=. Naomba ufafanuzi zaidi kama shule zenye hosteli zimewekwa katika fungu lipi.

Mheshimiwa Spika, kuongeza maradufu ruzuku ya elimu ya sekondari kwa watoto wa familia maskini ili watakaonufaika waongezeke kutoka 6,000 kwa mwaka kuwa 12,000 ni kuzuri. Ombi langu ni kuhusu watoto wa kike kutoka makabila ya kifugaji katika Wilaya ya Kiteto ambao tunawapeleka kwa nguvu, tupewe ruzuku kwani tumezidiwa.

Mheshimiwa Spika, nazidi kutoa ombi langu juu ya watoto katika shule za msingi wapatiwe maziwa. Nimesikitika sana kuhusu afya ya watoto wetu. *WFP* wanatoa chakula lakini hawatoi maziwa kwa watoto. Tunaomba itolewe ruzuku kwa ajili ya lishe bora kwa watoto wetu katika shule za msingi.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuwapongeza kwa kazi nzuri na hasa MMEM. Bado nina ushauri na kuomba ufafanuzi. Walimu wanaofundisha mpango wa MEMKWA, wanaosumbuliwa mapato kwa kazi wanayofanya, posho zao hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa MMES utasaidia zile shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, miaka ya nyuma na kukabidhiwa Serikali majengo kama bwalo na hosteli.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya mashindano ya Taifa ya mavazi Serikali imetumia shilingi ngapi. Vazi la Taifa halihitaji kutafutwa hujitokeza lenyewe tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasaidia kusomesha watoto wa wazazi wasiokuwa na uwezo wa ada. Je, si vema wakalipiwa na ada ya mitihani? Naipongeza Serikali kwa kupunguza ada ya shule za sekondari. Kwa kuwa shule za binafsi zinapandisha kwa sababu ya matumizi makubwa ya mishahara, maabara, uendeshaji na kadhalika.

Je, Serikali haioni ni vema kutoa ruzuku kwa shule za sekondari za binafsi kwa mtindo kama unaofanywa kwa Wizara ya Afya kwenye hospitali za binafsi?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana mtoa hoja Mheshimiwa Joseph Mungai. Aidha, nampongeza kwa jitihada za kuboresha elimu kwa kumwangalia kwa karibu mtoto wa Tanzania na kujali hali halisi ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kipekee pia Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri japo afya yake bado si nzuri, lakini anajitahidi kuona elimu inasonga mbele. Hii imethibitishwa na Waziri wake jinsi alivyomsifu, ninamtakia afya njema na Mungu amsaidie.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ujinga limekuwepo tangu tulipopata uhuru mwaka 1961. Ni tatizo kuu miongoni mwa maadui watatu wakubwa waliotajwa kukwamisha maendeleo ya nchi, yaani umaskini, magonjwa na ujinga. Kwa wakati wote kila Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kuboresha hali halisi ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga Kidato cha Kwanza na kuhitimu Kidato cha Nne ifikapo 2010. Aidha, lengo lake la kuongeza idadi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze jitihada ya kuondoa tatizo la walimu, kwa staili ya kutekeleza malengo yanayopimika. Ningeshauri katika kunijibu hoja hii, Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge baada ya ongezeko la wanafunzi katika shule tunazotarajia, tutakuwa na mahitaji ya walimu wangapi? Pengo litakuwa ni kiasi gani? Kwa kuzingatia kustaafu kwa walimu, kuacha kazi, vifo na mengineyo pamoja na uanzishwaji wa Vyuo Vishiriki viwili kama mipango yetu ikisimamiwa inaweza kulichukua Taifa miaka mingapi kuziba pengo la walimu. Ninajua tatizo haliwezi kwisha kabisa, lakini angalau kuhakikisha kila shule ya sekondari inapata walimu wasiopungua asilimia sitini ya mahitaji. Malengo haya yataonyesha mwelekeo wa wazi na kila mmoja wetu ataelewa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kutoa punguzo la ada kwa wanafunzi wote nchini katika sekondari zetu. Ni nafuu kubwa na faraja ya kipekee kwa Watanzania kuona kila mtoto aliyeko sekondari atanufaika na mpango wa punguzo la ada na uboreshaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kwa mwaka ujao ione uwezekano wa kutoa ruzuku ya mishahara kwa walimu katika shule binafsi. Kwa sababu watoto wote ni wa Taifa na hii imefanyika na Wizara ya Afya, imetenga baadhi ya vitanda katika hospitali binafsi na inatoa ruzuku kwa hospitali hizo kwa kuwa zimesaidia wananchi wa Tanzania. Nashauri hivyo ili kuondoa tatizo la kuajiri walimu wasio na sifa katika shule za binafsi kwa sababu ya uwezo mdogo wa kuwalipa mishahara mizuri.

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Serikali ione uwezekano wa Wizara hii kubwa sana kuipatia Manaibu Waziri wawili. Wizara hii inashughulikia masuala yote ya shule za msingi, sekondari, Vyuo vya Elimu na Walimu na utamduni pia. Ni vizuri Manaibu kuwa wawili. Ushauri wangu umezingatia ukweli kwamba elimu ndiyo ukombozi wa Mtanzania. Masuala ya elimu yaongezewe nguvu kwa kupata Naibu Waziri wa ziada.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara na Serikali kulitazama upya suala la utamaduni. Hapa nasemea michezo mashuleni irejeshwe na iwe sehemu ya mitaala ya shule za msingi na sekondari kama zamani.

Mheshimiwa Spika, kucheza ni haki ya mtoto. Tumeitaka Serikali kutenga maeneo ya watoto kuchezea. Je, ni michezo gani? Tunataka kuboresha michezo ya watoto chini ya miaka 18, je, tunawapata wapi hao? Suala la michezo mashuleni lirejeshwe na liangaliwe kwa makini lisivunje ubora wa ufundishaji. Liwepo na lipewe uzito sawa na masomo mengine.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii, afya na uzima Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote katika Wizara husika. Aidha, Mwenyezi Mungu awatie nguvu ya kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza hotuba imeandikwa kwa mtiririko mzuri na imegusia kila idara. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa maamuzi yenye manufaa kwa jamii katika kuinua kiwango cha elimu hasa elimu ya sekondari kwa lengo la kufikia asilimia hamsini na kwa kupunguza mzigo wa elimu ya sekondari kwa familia kwa kupunguza ada na michango. Nampa hongera sana kwa mtazamo huo wa kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Waziri atatambua kuwa alifanya ziara Wilayani Babati hususan maeneo ya wafugaji kwenye Jimbo la Babati Mashariki na kuijionea matatizo ya jamii ya wafugaji. Napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mungai kwa uamuzi wake wa kukubali kujengwa kwa shule tatu za bweni za msingi katika Wilaya ya Babati kwa awamu na kwa kuanzia na shule ya msingi ya OLTUKAI iliyoko Kijiji cha Minjingu.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kuwa ujenzi wa shule hiyo umeanza kwa kukusanya nguvu za wadau wote.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika ziara yake Mheshimiwa Mungai pia alipata nafasi ya kuzungumza na viongozo wa elimu Wilayani Babati na Mkoani Manyara. Katika mazungumzo na viongozi wa Wilaya ya Babati kuhusu matatizo makubwa hasa kwenye Idara ya Ukaguzi, Mheshimiwa Waziri alionyesha nia nzuri ya kutaka kusaidia tatizo la usafiri kwa Wakaguzi hasa kwa kuzingatia ukubwa wa Wilaya yenye maeneo ya ufugaji yaliyotawanyika Wilaya nzima na pia ukweli kwa sasa Babati imekuwa Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara na zaidi imepata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji.

Hivyo basi, kwa heshima na kwa niaba ya wananchi wa Babati naomba Mheshimiwa Waziri akubali ombi hili kwa kukamilisha nia yake kwa kutupatia gari moja jipya kati ya magari yakayonunuliwa na Wizara, hotuba ya Mheshimwa Waziri, Ukurasa wa 31, kifungu cha 21(b), magari 13.

Mheshimiwa Spika, ni ombi maalum la kuongeza fedha za MMEM kukamilisha madarasa mengi yaliyojengwa kukidhi haja ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wa darasa la kwanza wanapata mahali pa kusomea, ni madarasa ambayo yanahitaji kupauliwa.

Nimepokea ombi la aliyekuwa mwanafunzi wangu ambaye sasa ni mwalimu Ilonga *TTC,* baada ya kumaliza Shahada ya Ualimu kuwa hajalipwa mishahara yake ya nyuma ya miezi nane baada ya ajira pamoja na kukumbushia sana hiyo haki yake. Naomba asaidiwe. Maelezo yake mafupi ni kama ifuatavyo: Mwalimu Adela E. Mudale, *Ilonga TTC, EDPF 33188 C. 9729847. Date of employment, February, 2002.*

Mheshimiwa Spika, mwisho, namtakia kazi njema Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yake.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, chini ya Mpango wa Elimu za Sekondari *SEDP* naomba shule zifuatazo zikarabatiwe.

(i) *Bwiru Girls (*Bwalo la chakula - *Mess*).

(ii) *Ngaza Girls* (Bwalo la Michezo na *Mess* pamoja na bwalo la kulala lilikuwa *condemned* na halitumiki)

(iii) Kitangiri sekondari- Bwalo ya wasichana na michezo pamoja na madarasa mapya.

(iv) *Bwiru Boys* - *New Multi-purpose hall.*

(v) *Nsumba Boys* - Ukarabati wa *Hostels.*

Mheshimiwa Spika, kumalizia ujenzi wa shule mpya (Sekondari za Kata za Pasiansi, Ilemela, Bugogwa, Buswelu, Igoma, Buhongwa, Mkolani, Butimba, Sangabuye na Nyakato. Maeneo haya yana shule za msingi ambazo wanafunzi wanaopata nafasi sekondari ni wale tu wenye *pass mark* zaidi ya asilimia themanini. Hii ina maana shule za sekondari hazitoshi kabisa. Kwa kusaidia kumalizika shule za Kata husika itasaidia kupandisha idadi ya wanaoingia shule za sekondari.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Utamaduni inastahili pongezi za dhati kwa kazi nzuri sana inayofanya katika nchi yetu. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Kamishna wa Elimu na wafanyakazi wote wa Wizara wanafanya kazi kwa juhudi, ufanisi na maarifa. Wananchi wa Wilaya yangu ya Kyela ambao mimi ndio Mbunge wao wamefurahishwa sana na kazi nzuri ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Kyela tatizo kubwa la elimu liko katika eneo la elimu ya sekondari. Hivi sasa tunazo shule za msingi mia moja ambazo hali yake kimajengo na ikama ya walimu, kutokana na mpango wa MMEM ni ya kuridhisha kwa kiwango kikubwa. Tunazo shule za sekondari za Serikali sita (kutoka moja mwaka 1995) ambazo mwaka huu wa 2004 zimechukua wanafunzi 866 kidato cha kwanza kutoka wanfunzi 1,800 waliofaulu mtihani wa darasa la saba na kupata sifa za kujiunga na kidato cha kwanza. Watoto 934 waliofaulu wanakosa nafasi ya kuingia kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kupanua na kuboresha elimu ya sekondari na MMES ni mapinduzi makubwa ya elimu katika nchi yetu na kama utafanikiwa nchi itakuwa imepiga hatua kubwa sana katika vita dhidi ya ujinga.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa MMES wananchi wa Wilaya ya Kyela wangependa mambo yafuatayo yakamilike:-

(i) Kuongeza mkondo wa nne. Katika shule za sekondari za Serikali za Itope (sasa hivi kuna mikondo mitatu), Ipinda sekondari (sasa hivi ina mikondo mitatu) na *Matema Beach* ambayo sasa hivi ina mikono mitatu)

(ii) Kuongeza mikondo miwili katika shule za sekondari za Serikali za Ikolo (sasa ina mikondo miwili) na *Kiwira Coal Mine* (sasa na mikondo miwili).

(iii) Wananchi wa Kata ya Ipande wameanza kujenga sekondari katika Kijiji cha Njugilo. Madarasa manne na nyumba ya utawala zimekamilika. Tungependa mpango wa MMES usaidie kujenga nyumba tatu za walimu na vyoo ili shule hii ianze mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza ada ya shule toka sh. 40,000/= hadi sh. 20,000/= kwa mwaka. Hofu yangu ni kwamba katika miaka mitano iliyopita Tanzania imeshuhudia mapanuzi makubwa ya matumizi katika karibu nyanja zote; maji, elimu ya msingi, afya na barabara. Uwekezaji katika sekta hizi unatokana na mikopo na misaada kutoka nje. Sasa tunaingia mpango wa MMES ambao nao utatumia mabilioni ya fedha. Hofu yangu kubwa ni kwamba tunapanua wigo wa matumizi *(which is good development, thought)* nje kabisa ya uwiano na pato la Taifa. Hapo baadaye Serikali lazima ihakikishe kuwa pato la Taifa linakuwa na kuongezeka ili ku-*sustain and service this huge expenditure in basic services.* Tusifute michango ya wananchi kijazba na kiholela. Wenye uwezo wachangie na maskini wasaidiwe. Hii miundombinu tunayoijenga hivi sasa lazima tujenge uwezo wa kuihudumia. Tukishindwa kuihudumia na kuiendeleza hapo baadaye itazeeka na Taifa litaingia katika umaskini mkubwa na matatizo makubwa ya kisiasa yanaweza kuibuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa hongera kwa kazi nzuri na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Elimu kwa juhudi zake za kuboresha elimu katika nchi yetu. Nawapongeza na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia ubadhirifu wa fedha za karo ni vizuri fedha zote zikalipiwa benki na mwanafunzi akaenda shule na *pay-in-slip* badala ya fedha taslim.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa udanganyifu wa vyeti vya sekondari wakati wa kujiunga na Vyuo vya Ualimu ni vema ukawepo mtihani wa kujiunga na vyuo. Wale wasio na uwezo wasijiunge. Ni aibu mtu wa *Division II a*sijue kuandika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweze kuwadhamini wale ambao wana ujuzi wa kutengeneza vifaa vya maabara ili waweze kuwa na viwanda nchini kuliko kuagiza nje.

Namfahamu kijana mwenye uwezo na ujuzi. Amewahi kufungua kiwanda huko Kenya kwa kusaidiwa na Serikali ya Kenya.

Kwa kuwa kiwanda hicho hakikuwa chake binafsi ameamua kurudi nchini. Ni imani yangu kwamba atatoa mchango mkubwa sana hasa wakati huu ambapo tutajenga shule nyingi za sekondari hasa katika vifaa kama *test tube, bakers* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake Wizarani kwa juhudi kubwa wanazofanya kuhakikisha Taifa hili linaondokana na ujinga hasa katika yafuatayo:-

Elimu ya msingi - mradi wa MMEM, juhudi ya kupata walimu wa shule hizo, mipango sawia ya maboresho na mradi mpya sasa wa MMES.
Lakini nina ushauri na maombi muhimu kuhusu masuala hasa ya MMEM.

Mheshimiwa Spika, sidhani kwamba ni haki kuwa na gharama sawa za kujenga shule. Aidha, iwe ya MMEM au MMES kati ya Dar es Salaam na Urambo kwa sababu vifaa vitakavyojenga shule hizo ni ghali zaidi Urambo kuliko Dar es Salaam na kwa hiyo fedha zitakuwa chache zaidi Urambo kuliko Dar es Salaam. Kutatua hili ni lazima vifaa vya kujenga shule hizi *(inputs)* visiwe na kodi na usafiri ufidiwe ili kuwe na *level playing field.*

Mheshimiwa Spika, hatma ya Maabara na Maktaba katika kila shule ya sekondari itakuwaje? Nani atasimamia je, ni Serikali Kuu? Kwa sababu elimu ya teknolojia inategemea sana uimara wa sehemu hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, mipango maalum ya kuwa na *core* ya walimu wa kutosha kuweza kusimamia *quality* ya elimu ya kila shule, ili kuepuka matatizo ya elimu kwa shule za MMEM.

Mheshimiwa Spika, maombi muhimu. Shule zangu za Urambo Sekondari na Azimio sekondari ni chakavu na za zamani sana kwa kweli zinahitaji ukarabati, kama nilivyoandika mwaka jana ni muhimu sana hili likatiliwa maanani na hasa mabweni ya wasichana ya shule hizo ambayo yakikarabatiwa tutaongeza wasichana wengi zaidi wa kiwango cha sekondari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa uliyonipa ili nichangie hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa J. J. Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri kuliko hotuba zote nilizowahi kusikia tangu nizaliwe kutoka kwa Mawaziri wa Elimu waliopita. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja. Pesa zote ulizoomba umepewa na zikiisha kabla ya wakati wake njoo Bungeni omba *Extra Budget* tutakupa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa matumizi mazuri ya fedha za wahisani na za hapa nchini. Shule za msingi zimejengwa vizuri, sekondari zinazojengwa na wananchi na kukabidhiwa Serikalini zinaendelea vizuri. Watoto wetu wanasoma na kufaulu vizuri kwa manufaa yao wenyewe na kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Waziri atakapotoa majumuisho akemee tabia mbaya ya wanafunzi kudokoa au kuiba vitabu rejea na vya kiada toka shule nyingine au kutoka shule hiyo hiyo anayosoma mwanafunzi. Vitabu vingi vimezagaa mitaani vinauzwa na Wamachinga na hata maduka binafsi na vingine vina hata mihuri ya shule husika. Aidha, Walimu Wakuu wadhibiti uingiaji na utoaji wa vitabu hivyo. Wapige mhuri wa shule kila baada ya karatasi tano.

Mheshimiwa Spika, Waziri anaombwa atoapo vitabu na vifaa vya shule nakala ya utoaji apewe Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu. Mkaguzi wa Elimu afanye ukaguzi wa shule kila siku za kazi kwa vile ni kazi yake na akague vifaa na vitabu ya madarasa yote. Akigundua upotevu wa aina yoyote ile Mwalimu Mkuu awajibike haraka na apewe onyo la maandihsi na siku chache sana za kurudisha vitabu au vifaa hivyo. Ikilazimu mshahara wake ununune vitabu au vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu amjalie Mheshimiwa J. J. Mungai.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilipata fursa ya kuchangia kwa kusema lakini bado naomba nisisitize kwa kuandika baadhi ya maeneo ambayo ningependa kuiomba Wizara ituangalie wakazi wa Bagamoyo kwa namna ya pekee katika mkakati wa Bajeti wa utekelezaji wa MMES 2004-2009. Bagamoyo pamoja na kuwa karibu mno na Dar es Salaam kilomita 66 Dar/Bagamyo Mjini; kilomita 70 Dar/Ruvu Darajani, bado ni mojawapo miongoni mwa maeneo ambayo naweza kusema ni *most underserved area* nchini.

Mheshimiwa Spika, Bagamoyo ni moja ya Wilaya zilizosimamia kwa ufanisi sana mpango wa MMEM, hivyo nina imani Mheshimiwa Waziri pindi Serikali ikitutengea

fedha za kutosba katika mpango huu wa MMES naamini tutasimamia kwa umahiri mkubwa na kuhakikisha mpango huu nao unafanikiwa katika Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, tunayo majengo mazuri sana yaliyokuwa yakitumika kama Kambi ya Wapigania uhuru wa *PAC* wa Afrika ya Kusini. Naamini majengo hayo yanaweza kuwa mwanzo mzuri kwa ukamilishaji wa mpango wa MMES katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika eneo la Makurunge kwa lililokuwa shamba la mifugo la Zanzibar (RAZABA) pale tunayo shule ya msingi yenye madarasa kadhaa mazuri lakini idadi ya wanafunzi kwa madarasa yote saba hawafiki mia moja. Karibu na shule hii pia kuna majengo kadhaa yaliyokuwa kambi ya Watumishi wa RAZABA.

Kwa kutilia maanani upugufu mkubwa sana wa shule za sekondari Wilayani napenda kuishauri Wizara iangalie uwezekano wa kutumia majengo hayo kwa kujenga sekondari na wale wanafunzi wachahce sana waosoma katika shule hii wahamishiwe shule ya karibu ya Kijiji cha Bigilo ambayo iko karibu na pia haina msongamano wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mfanikio makubwa sana yaliyofikiwa katika mpango wa MMEM bado Wilaya inakabiliwa na upungufu iliokithiri wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa jengo lililoungua la Chuo cha Sanaa. Nakumbuka baadhi ya nchi rafiki na wahisani ziliwahi kuonyesha nia ya kutusaidia katika kulijenga upya jengo lililoteketezwa na moto.

Mheshimiwa Spika, pengine ni wakati muafaka sasa kuliweka wazi jambo hili la msaada wa nchi rafiki umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kikamilifu.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyo Mezani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri kwa kipindi kilichopita cha Mwaka 2003/2004, hususan mafanikio ya MMEM.

Pia ningependa kuipongeza Wizara kwa kupiga hatua nyingine nzuri ya kuendeleza mpango wa maendeleo ya elimu kwa sekondari -MMES.

Ningeomba Mheshimiwa Waziri wakati anafunga mjadala azungumzie kuhusu mioto inayoikumba shule, hususan shule zilizo Mkoa wa Kilimanjaro. Nini maelezo ya mioto hiyo na Wizara inafanya nini kuhakikisha kuwa shule ni salama na watoto wana utulivu na amani ili waweze kusoma sawa sawa. Je, Wizara ina mpango gani kuhakikisha shule zetu zina *fence.* Ninafahamu hii ni gharama kubwa ukilinganisha na idadi ya shule tulizo nazo, lakini gharama hiyo haiwezi kulinganishwa na uhai wa watoto wetu. Labda kazi hii ingefanywa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba pia Mheshimiwa Waziri aangalie shule zilizo katika maeneo kwa mfano ya sehemu za hifadhi kwa mfano msitu wa Tarakea Rombo. Wananchi hawa hawaruhusiwi kuanzisha shule bila ya kibali cha Wizara ya Mali Asili na kadhalika. Ni sawa, ni lazima kuwe na *control,* lakini wananchi wanatoka na kufanya kazi katika sehemu hizi wanazo familia zao na zinahitaji elimu.

Shule ziko chache mno kiasi cha kumfanya mtoto kutembea kilomita nyingi kwenda na kurudi shule. Wakati mwingine watoto wanashindwa kurudi nyumbani kutokana na umbali. Ninaomba Waziri aangalie suala hili kwa karibu ili wananchi wa Tarakea, Rongai, Rombo waweze kupata shule zaidi, hasa Shule za sekondari.

Mwisho Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara wakati inazama katika MMES, isisahau kuendelea kuboresha MMEM, kwa sababu kuna shule nyingine hazijakamilisha kazi kwa mfano kazi ya kuongeza matundu ya vyoo, nyumba za walimu na kadhalika.

Ninapenda kuipongeza tena Wizara Elimu na Utamaduni, kwa kazi nzuri na ninaunga hoja mkono.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutamka wazi kuwa naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa moyo mkunjufu sana na kwa furaha. Wizara hii nyeti ya Elimu na Utamaduni, sasa inafanya kazi kikweli na nasema kuwa *this is a very pleasant surprise and we are all proud of this spec tactatar and historical phenomenon.* Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza kwa moyo na kwa haki kaka yetu Mheshimiwa Joseph Mungai - Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kuwa ni kionambali katika masuala ya elimu na pia kuwa ujasiri ya nguvu tele za utekelezaji wa yale anayoyaamini na kuyafanyia maamuzi. Vile vile nawapongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara na Wasaidizi wake kwa kuendesha shughuli za elimu kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa elimu ya sekondari MMES ni mpango ambao unapaswa kuungwa mkono na watu wote walio na *structured minds.* Yatupasa sote tuunge mkono mpango huu kwa vitendo na kwa mwendo wa kasi. Katika jimbo langu la Kalenga tumekwisha jenga shule tatu za sekondari - moja kwa kila Tarafa na moja kwa Kata moja - jumla shule nne. Naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Elimu na Utamaduni na Wizara nzima kwa kuzichukua shule zote kuwa za serikali, yaani shule za sekondari za Kalenga, Isimila, Kiponzelo na Wasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mpango huu wa MMES wananchi wa jimbo la Kalenga wameamua kujenga shule za sekondari kwa kila Kata. Matofali mengi sana

yamekwisha fyatuliwa, mawe mengi yamekusanywa, na ardhi ya kutosha kabisa imetengwa kwa kila shule ya Kata.

Kwa wakati huu wameanza kujenga misingi ya shule hizo. Kata ambazo zimekwisha anza ujenzi ni za Magulirwa, Mgama, Mseke, Ifunda, Lumuli, Kalenga, Kiwere na Nzihi. Hivyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba fedha hizo za MMES zitolewe kwa Kata hizo nilizozitaja. Ni muhimu kusiwe na urasimu unaoweza kuchelewesha ujenzi wa haraka. Lakini kuwe na utaratibu mzuri wa udhibiti wa fedha ili zitumike ipasavyo bila wajanja kuingilia kati na kunufaika wao.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kwa mpango huu wa MMES tunaomba shule tulizozijenga na kuchukuliwa na Serikali zikamilishwe. Shule ya sekondari ya Kalenga imeongezewa mikondo mitano *Form I.* Hivyo imekuwa ni shule kubwa yenye wanafunzi wengi. Kwa fedha za MMES itawasaidia kukamilisha na kujenga majengo mengine muhimu. Naomba wapewe fedha hizi mapema ili waendelee na ujenzi kwa kasi kabla ya masika kuanza. Shule hii ya Kalenga inahitaji umeme. *TANESCO* imekwisha fikisha nyaya za umeme shuleni na watafunga *transformer* siku za karibuni. Tunaomba Wizara itoe fedha umeme uingizwe shuleni. Vile vile shule hii inahitaji gari la shule. Wanafunzi wengi wanaishi kwenye mabweni ya shule. Wakiugua usiku gari linahitajika. Lakini gari la shule linahitajika sana kwa shughuli nyingi za huduma shuleni.

Mheshimiwa Spika, shule nyingine za Isimila, Kiponzelo na Wasa zote zimeongezewa mikondo *Form I.* Tunahitaji sana fedha za MMES kuongeza madarasa, nyumba za walimu na majengo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, shule zote nne za sekondari zinahitaji sana fedha za MMES ili kujenga majengo ya maabara, maktaba na mabweni. Ni muhimu sana kuwa tunachukua nafasi ya mpango huu wa MMES kukamilisha shule hizi ziwe shule kweli za sekondari zenye viwango bora vifaavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mafanikio ya MMES ni muhimu sana Wizara ibuni mpango wa elimu ya ufundi. Kwa maendeleo ya kweli vijijini lazima vijana wetu wanaomaliza darasa la saba na hawakuingia katika shule za sekondari wengi wapate nafasi ya elimu ya ufundi. Hali hii itawafanya wajiajiri wenyewe vijijini. Wnapomaliza shule wapewe pia vyombo vya ufundi ambavyo ni ghali sana. Shule hizo ziruhusu hata wale waliomaliza *Form IV* waingie shule hizo hizo na kujifunza ufundi kama wanapenda.

Mheshimiwa Spika, tukijenga shule nyingi za sekondari katika Kata wanafunzi wengi watashindwa kupata nafasi za *Form V.*

Hivyo nimeishauri Bodi ya Shule ya Kalenga sekondari iombe ruhusa yako Mheshimiwa Waziri wapewe fedha za ziada za MMES ili wajenge na wafungue *High School* ndani ya Kalenga Sekondari yaani *Form V-VI.* Naomba Mheshimiwa Waziri ulikubali ombi hili muhimu. Hapo baadaye tutaomba pia shule za Isimila na Kiponzelo wafungue *Forms V-VI.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii nzuri.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia l00. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Naipongeza serikali kwa kupjnguza ada ya shule za sekondari za kutwa kutoka sh.40,000/= hadi sh. 20,000. Naishauri Serikali ifikirie pia kupunguza ada ya shule za sekondari za Bweni ili watoto wengi waweze kupata eliu ya sekondari na kuwapunguzia wazazi mzigo.

Shule ya sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School)* ina *Form I-VI* lakini shule hiyo haina *computer* hata moja. Je, ni lini shule hiyo itapatiwa *computer* na vifaa vya kisasa vya wanafunzi wasioona. Je, ni lini shule ya sekondari ya Mpwapwa itapatiwa gari jipya, gari lililopo ni bovu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kutoa kibali cha kuanzisha shule mpya ya sekondari inayoitwa Ilolo, Shule ya sekondari - Mpwapwa na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Joseph Mungai alitembelea shule hiyo mwezi Februari, 2004. Shule hiyo inajengwa kwa nguvu za wananchi wa Kata za Vinghawe, Mazae na Mpwapwa Mjini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kusaidia ujenzi wa shule hiyo ambayo ina upungufu wa vyumba vya madarasa na maabara.? Je, ni lini shule hiyo ya sekondari ya Ilolo itapatiwa gari, *computers* na vifaa vingine vya muhimu?

Je, ni utaratibu gani unaotumika sasa wa kuchagua vijana wanaojiunga na vyuo vya Ualimu ili Wizara au vyuo vyenyewe Daraja la Ualimu IIIA na *Diploma*? Mwisho narudia tena kuipongeza Serikali kwa mpango mzuri wa MMEM hivi sasa watoto wetu wanasomea madarasani sio chini ya miti tena kama ilivyokuwa zamani kutokana na ufinyu wa Bajeti. Nashauri mpango wa MMES uboreshe majengo ya shule zetu za Sekondari na pia ujenzi wa nyumba za walimu uende sambamba na ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Walimu wanaishi katika mazingira magumu sana. Suala la upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari lipewe umuhimu ili kuboresha taaluma katika hizo.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja .

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa kuweza kujadili hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Ninayo maeneo machache ambayo nafikiri yanaweza kuboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, yapo madai ya msingi ya malimbikizo ya madai ya walimu ambayo ni ya msingi ya wilaya ya Chunya. Ingawa inasemekana majibu ya Serikali ni kwamba fedha zipo zitapelekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumfahamisha Waziri kuwa, shule ya sekondari ya Kanga, tunaomba kusaidiwa kujenga *Laboratory/*Maabara suala hili nilishalileta Ofisi ya Wizara bado sijapata majibu. Naomba kupitia hotuba hii nipewe msaada wa kujenga maabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu inajitahidi sana lakini yapo mambo ambayo sasa Wizara lazima iyafanye:-

Kila shule ya msingi iwe na *Nursery School.*

Kila shule ya *Primary School* ianze kufundisha - Kiingereza/Kifaransa na Kiswahili iwe ni *compulsory.*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri kwa kuwa mstari wa mbele kurekebisha matatizo ya msingi ya Wizara na kuleta marekebisho mengi mazuri. Pongezi kwa yeye mwenyewe na Naibu wake pamoja na wafanyakazi wengine wote wa Wizara, akiwemo Katibu Mkuu.

Na niliyoyaeleza naomba yatiliwe maanani kwa sababu najua yapo ndani ya uwezo wako. Naunga mkono.

**MHE. ALHAJ SHAWEZI ABDALAH:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Isipokuwa maelezo yaliyokuwemo katika ukarasa 26 yanayohusu kuacha kufundisha michepuo ya *technical studies, agriculture and Commerce.*

Mheshimiwa Spika, napendekeza michepuo hiyo ibakie kwa hoja zifuatazo:-

Tayari katika secondari michepuo ya *technical studies, agriculture and commerce* imekuwemo na kujengeka katika katika mfuo wa mitaala yetu. Haitoshi kufikiria masomo ya *agriculture* yatatolewa katika vyuo vya Wizara ya Kilimo kwa sababu Wizara haina *capacity* ya *training.* Nielewavyo *capacity* ya vyuo vya kilimo ni 1,200 lakini uwezo wa Serikali ni 200 tu. Kufuta mtaala wa *agriculture* utadhoofisha taadhima ya kilimo katika nchi yetu.

Shule kama *Ifunda Technical School* ina walimu wahitimu *Ph.D* na *Masters* hawa utawapeleka wapi. Pia pale na *investment* kubwa hakuna sehemu nyingine yeyote Tanzania. Ipo mitambo mingi ambayo haipatikani kokote kule. Mitambo hii Wizara itaipeleka wapi.

Kuhusu mchepuo wa *Commerce.* Nafikiri Wizara naishauri ikubali utandawazi ili tufanikiwe taaluma ya *Commerce* ni muhimu sana. Kuacha mtaala huu uendeshwe na vyuo vya Wizara ya Viwanda na Biashara utapunguza kasi ya kupata wataalamu wa taaluma ya *commerce.*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hii nashauri Wizara ya Elimu na Utamaduni iwasiliane na Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Viwanda na Biashara ili

kuweza kujua *capacity* ya Wizara hizo katika kufundisha mitaala hiyo. Kwa maoni yangu masomo haya yaendelee kubaki ila yawe *optional* lakini shule kama Ifunda au *Moshi Technical* si vizuri mitaala hiyo kufutwa.

Hoja ya kusema *Agriculture* ni *Science,* ni ya Wizara ya Kilimo haitoshi kwa sababu hata *Biology* ni ya Wizara ya Afya mbona mtaala huu umeachwa uendelee.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi kwa kazi ya Wizara hii kutokana na kazi inayofanyika. MMEM imekuwa na mafanikio makubwa sana. Ila upande wa matumizi ya pesa za MMEM kumekuwa na matumizi mabaya kwa sababu uthibiti kutoka serikali ya Mitaa ni hafifu. Imekuwa kama wamepelekewa pesa kwa matumizi yao binafsi.

Naomba sana tena sana pesa za MMES zisipelekwe kwenye Wilaya kupitia kwa Wizra ya TAMISEMI. Kama utazipitisha huko basi kuwe na watu wako wa kufuatilia kwa karibu.

Naomba walimu wapya ambao wanapelekwa kazini kwa minajiri ya mazoezi ya kufundisha kwa mwaka mmoja. Ufuatiliaji na malipo yao viwe na maandalizi toka vyuoni kwani wanateseka sana na kuichukukia kazi ya ualimu. Halmashauri haziwajali kimaslahi na kimalezi.

Nakupongeza kwa kuanzisha mpango wa MMES Geita wananchi wamekwisha anza kuunga mkono serikali. Tunakuomba wewe binafsi uje Geita uangalie juhudi zao. Tuna imani neno lako ni dawa katika kuhamasisha.

Kwa upande wa MMEM wananchi hivi sasa wanayo maboma 800. Tunaomba uje uone kazi inayofanyika ili kutupa moyo. Aidha, Geita tunaomba uwezo ili tuweze kukamilisha ujenzi wa maboma hayo.

Mwisho, nashauri tatizo na kusimamia maslahi ya walimu ikiwezekana walimu wote wawe chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwani huko waliko kuna gap ya kiutendaji. Wamekaa kama yatima. Lawama zote zinatupiwa Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Tunaomba maeneo ya Biharamulo, Kahama, Geita, Sengerema, Ngara, kujengwe Chuo cha Ualimu kwani tunapata upungufu wa walimu kwa sababu ya kutokuwa na chuo cha ualimu kilicho karibu katika maeneo hayo.

Tunaomba chuo kijengwe Katoro kwani ni katikati ya Wilaya zote hizo. Ardhi tutaitoa bure. Wananchi wako tayari kusaidia kwa linalowezekana kujenga chuo hicho kikubwa. Wilaya zinazozizunguka maeneo hayo yana wanafunzi wengi sana ukilinganisha na maneno mengine nchini. Ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wewe binafsi, Naibu Waziri,

Katibu Mkuu, na viongozi na Wataalam wote wa Wizara yako. Mnafanya kazi nzuri sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa Waziri mimi nina maombi machache sana katika Wizara hii ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, hii ni taarifa kamba katika jimbo la Morogoro Kusini kuna makabila mawili ambayo ni Waluguru na Wakutu. Waluguru wamesoma lakini hili kabila la Wakutu ni la wawindaji na wavuvi. Hata hivyo, kwa sasa wametulia.
Watu hawa sasa wamezuka na jitihada kubwa ya kujenga shule. Wamejenga sekondari ya Selembala.

Ninaomba walimu wapelekwe kwenye sekondari hii mpya. Hadi sasa kuna walimu wawili tu.

Ninaomba pia kibali cha kujenga majengo ya *Form V and DVI katika* shule hii. Hii ni kwa sababu Wilaya nzima ya Morogoro Vijijini hakuna *High Chool.* Sekondari ya Selembala ina eneo kubwa sana siyo tu ya kujenga *High School* bali hata *TTC. High School* itakuwa na soko kubwa la sekondari za Morogoro Vijijini.

Ninashukuru sana *average number* ya walimu katika shule za msingi jimboni inafikia 3. Lakini upungufu wa walimu sasa ni tatizo kubwa sana Hao walimu wachache waliofika waliondoka baada ya kukosa mishahara kwa muda mrefu mno. Naunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mungai kwa hiotuba nzuri inayoonyesha mipango na mikakati ya wazi itakayolikomboa Taifa letu kutokana na ujinga ambao ni chanzo kikubwa cha umaskini. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri kwa namna anavyojitahidi kushiriki katika shughuli mbalimbali pamoja na hali yake ya afya. Nawapongeza sana watendaji wa Wizara wakiongozwa na bibi Mwantumu Malale, kwa kazi kubwa, ngumu na nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mpango wa elimu MMEM/PEDP ya msingi MMEM umekuwa wa mafanikio makubwa nchini kote lakiin yapo matatizo madogo madogo hasa udokozi wa fedha, viwango vya ujenzi kutokukidhi haja na kadhalika ambavyo vinahitaji usimamizi wa karibu.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wizara kwa kuliiona tatizo la uhaba wa walimu na hivyo kulipunguza kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo walimu hawa wanastahili kutimiziwa haki zao za mishahara na haki zao nyingine za kiutumishi ili wawe na moyo wa kufanya kazi yao ya kufundisha watoto wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa elimu ya sekondari ulioelezwa kwa kina katika bajeti ya 2004/2005 umekuja kwa wakati wake ili watoto wote wanaofaulu darasa la saba waweze kuendelea kidato cha kwanza. Ili kuhakikisha watoto

wa kike wanaendelea na masomo ya sekondari ni jambo muhimu sana mabweni yakajengwa ili kuwaepusha na ajali zinazowakumba njiani wakati wa kwenda shule na kurudi lakini pia kuwaongezea umakini katika masomo.

Mheshimiwa Spika, suala la maktaba nililizungumzia wakati nikichangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, lakini kutokana na umuhimu wake nakuomba Mhehsimiwa Waziri ulitupie macho maktaba ya Mkoa wa Kagera. Jengo lile ni bovu sana, vioo vya madirisha vyote viliishatoka sakafu imebhomoka, ni finyu sana na yaelekea vitabu na maandiko mengi muhimu havipo. Watu wengi wanapenda kujiendeleza kielimu na hata wale wanaosoma chuo kikuu huria, maktaba ingekuwa msaada mkubwa kwao kupata rejea mbalimbali. Ni lini maktaba ya Bukoba itafanyiwa ukarabati kama si ukarabati au kujengwa upya.

Namaliza kwa kuzidi kumwombea Mheshimiwa Sakila apone ili aendelee kukusaidia katika majukumu mazito uliyo nayo. Naunga mkono hoja.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara yako lakini naomba maelezo yafuatayo:-

Chuo cha Ualimu Mkoa wa Shinyanga ambacho aliahidi Mheshimiwa Rais alipotembelea Shinyanga mwezi Februari, 2004 alipokuja kufungua ujenzi wa barabara ya Ilula - Nzega. Je, kitaanza kujengwa lini?

Shule za *Private* hasa za *Mission* nazo zipate fungu toka Wizara/Serikali kuu ili kukarabati na kubhoresha mazingira ya shule hizi. Hizi shule zinatoa huduma kwa Watanzania kama zilivyo za Serikali.
Kila shule ya Msingi lazima iwe na shule ya awali. Hili liwe ni agizo na litekelezwe na hizi nazo watoto wasome bure.

Watanzania wahamasishwe kujenga na kuendesha vyuo vya ualimu na watakaofuzu watambuyliwe na Serikali na kuajiriwa. Vyuo hivi vya Serikali havitoshelezi mahitaji makubwa ya waalimu. Mpango wa waalimu kukaa chuoni mwaka mmoja tunapata walimu *half cooked.* Chakula cha mchana kwa shule za msingi ni muhimu na iwe kwenye Bajeti na wazazi wanaweza kuchangia. Maeneo ya njaa watoto hawaendi shule na hili ni tatizo kubwa.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya 2003/2004 katika kuboresha elimu hapa nchini na hasa kwa kusimamia vema mradi wa MMEM. Aidha, ninapenda lkuwashukuru kwa kushirikiana vizuri na uongozi wa Mkoa wa Kigoma mpaka kuuwezesha Mkoa huu kufungua shuole za sekondari 9 (tisa) katika mwaka mmoja (2004). Kati ya hizo, sekondari mbili ziko katika jimbo la Kasulu Mashariki. Ninawatakiwa kheri zaidi mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja moja kwa moja. Ninapenda kuipongeza Wizara kwa hatua nyingi ambazo itachukua mwaka huu wa fedha kuboresha elimu ya msingi na ya sekondari. Ninaipongeza zaidi kwa kupunguza ada ya sekondari

ya kutwa kutoka sh.40,000/= hadi 20,000/= kwa mwaka. Hakika Wizara inazingatia hali hali ya wananchi wetu. Hongera sana, Mheshimiwa Mungai na wote ufanyao nao kazi. Pamoja na kuunga mkono ninayo yafuatayo:-

(i) Walimu kupandishwa vyeo kwa muda. Walimu wengi wanakaa muda mrefu sana bila kupandishwa vyeo na hivyo morale ya kazi yao kupungua. Ni vyema wakawa wanapandishwa au kushushwa vyeo katika muda uliowekwa kiutaratibu na kikanuni. Aidha, madai yao halali yawe yanashughulikiwa haraka.

(ii) Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikopo kwa walimu, ninaiomba Serikali iongalie uwezekano wa kuwapa walimu nchini kote mikopo ya masharti nafuu ya kuwawezesha hasa wale wa vijijini kununua vyombo vya usafiri kama vile pikipiki na baiskeli. Aidha, wakipata mikopo ya kujijengea nyumba watafanya kazi kwa moyo mkunjufu na kwa bidii.

(iii) Upungufu wa walimu wa sekondari. Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ichukue hatua za makusudi kusomesha vijana wengi zaidi kwenye vyuo vya ualimu ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa sekondari na hasa wale wa masomo ya sayansi na hisabati. Sambamba na hilo, Wizara isimamie kuhakikisha kuwa shule zote zinakuwa na maktaba zenye vitabu vya kutosha na maabara zenye vifdaa vitakiwavyo. Ninaunga mkono hoja na kuitakia Wizara ya Elimu na Utamaduni kila la keri katika mwaka 2004/2005.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukupongeza sana wewe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hoituba yako nzuri sana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wa Idara mbalimbali na wote walioshirii kwa namna moja au nyingine katika kuandaa Bajeti hii nzuri. Nasema hongera, hongera sana. Nampa pole sana Naibu Waziri wa Elimu kwa kuugua muda mrefu, iko siku tu atapata afya njema, Mungu yupo.

Naipongeza sana Serikali kwa kupunguza karo kwa wanafunzi wa sekondari hadi kufikia/kubakia sh.20,000/= tu. Hapo nawapongeza sana. Wanafunzi wengi wanaotoka katika familia duni wataweza kuendelea na masomo yao ya sekondari. Hongera sana.

Tatizo lingine ni hili la masomo ya *tuition.* Naishauri serikali masomo ya *tuition* ni tatizo la kitaifa. Wato wengi hawapati masomo yao kama ilivyo kwa kukosa hela ya masomo ya tuition. Walimu wengi hupenda kufundisha masomo hayo kwa kuongezea kipato chao. Kumbe basi, wanaacha nafasi ya kufundisha madarasani kwa kukimbilia masomo hayo ya sekondari.

Wanafunzi wasiokuwa na fedha wanapunjika/wanaathirika sana na mpango kabambe. Naishauri Serikali kuwa na utafiti wa somo/masomo ya *tuition* kitaifa ili kuwa na mkakati mahususi wa kuendelea na masomo hayo ya *tuition* au la. Utaratibu huu wa masomo ya *tuition* yanawanyima raha na kuwakatisha tamaa wanafunzi baadhi wasio kuwa na uwezo wazazi wao.

Masomo ya *tuition* bado Serikali haijayaweka sawasawa katika mpango wake wa kuboresha elimu nchini. Masomo haya yanatia dosari kubwa katika *syllabus* ya masomo ya serikali hasa kwa masomo ya sekondari.

Mkoa wa Shinyanga kupitia chombo chake cha *ALAT* Mkoa, kimeomba kuruhusiwa kujenga chuo cha Ualimu cha daraja la A au daraja la stashahada. Arua ya kuomba ruhusa alipewa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph James Mungai mwezi Aprili 2004 hadi sasa Mkoa haujapata jibu la ombi hilo muhimu. Naomba kupata jibu la barua hiyo wakati wa majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wabunge. Hii ni kutokana kwamba mkoa poekee wa Shinyanga hauna chuo hata kimoja.

Ombi la gari, Idara ya Ukaguzi Wilayanhi Meatu. Ombi hili ni la muda mrefu, tangu 1998 - 2004 hatujapata. Wilaya ya Meatu ni kubwa na lina majimbo mawili, Kisesa na Meatu na mazingira yake ni magumu sana hasa kwa shule zile za jamii ya wafugaji kama vile, Wataturu, Wamaasai, Wandorobo na Kabila la Wahadzabe ambao ni warina asali. Huwinda wanyamapori na kutumia mizizi kama chakula chao.

Kwa hiyo, kwa kuwa jamii hiyo niliyoitaja hapo juu ni watu wa kukaa porini na ambako kuna shule za msingi idara ya Ukaguzi inawawia vigumu kuzifikia shule hizo na kuzifanyia ukaguzi. Shule hizi ni Lukale shule ya Msingi, Mwabagimu, Wifa Mhilya, Mbushi, Jinamo, Usiulize, Makao, Shushuni, Iramba Ndogo, Sungu, Mwangudo, Sapa, Mwanzagamba, Nzanza, Busia na Butuli ambazo ni shule 16. Pia maeneo hayo yana mbung’o wengi kiasi kwamba huwezi kuendesha baiskeli wala pikipiki. Sioni sababu kwa nini Idara hii ya ukaguzi isipewe gari hata Samurai ili kuleta ufanisi zaidi wa kuzifikia shule hizo.

Mheshimiwa Spika, ombi - mradi wa lishe shuleni. Naiomba serikali iuingize na mkoa wa Shinyanga katika mpango wa mradi wa Lishe shuleni katika bajeti ijayo 2005/2006. Hii ni kutokana na Wilaya ya Meatu kuwa na watoto wa jamii zinazohama hama kwa ajili ya ufugaji, uwindaij, kula matunda na urinaji asali, kama vile Wamasai, Wataturu, Ndorobo na Wahadzabe. Mpango huu wa *(WFP)* ni muhimu sana Wilaya ya Meatu.

Aidha, naiomba Serikali kujenga shule za bweni Wilayani Meatu kwa maeneo ya:-

(a) Mwabagimu ambako kuna jamii ya Wataturu
(b) Makao ambako kuna kuna jamii ya Wamaasai
(c) Sungu ambako kuna jamii ya Wahadzabe.

Jamii hii itakuwa imefaidika sana na mpango mzima wa kuboresha elimu nchini na kuleta mabadiliko makubwa ya kielimu kama shule hizo za bweni zitajengw wilayani Meatu.

Kwa kutimiza hili, Serikali itakuwa imetekeleza wajibu wake wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu 11 (3) kinachosema: "Kuwawezesha watu wote kupata fursa ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi kwa ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo. Naomba haya yazingatiwe. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, nato apongezi za dhati kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu mkuu, Mama Mwantumu Malale, viongozi wengine na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa jitihada wanazofasnya kuendeleza na kuboresha elimu nchini. Mafanikio ya juhudi zao yanaonekana dhahiri. Katika utendaji wa taasisi za Serikali, Wizara ya Elimu na Utamaduni zinaonekana dhahiri kuwa na mojawapo wa visiwa vya mafanikio makubwa *a centre of excelence.* Ni mojawapo wa taasisi za Serikali zinazotekeleza kukamilisha Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Ni Taasisi inayoleta matumaini kwa Watanzania. Hongera sana!

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kuhusu makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2004/2005 ni mahsusi *a landmark speech* kwa mambo yafuatayo:-

Kupunguza kwa asilimia 50 ya ada ya shule za kutwa za sekondari

Kutoa ruzuku za uendeshaji wa shule za sekondari za serikali na binafsi zisizo za kibiashara.

Kukarabati shule za sekondari zilizopo.
Kujenga shule mpya za sekondari.
Kujenga nyumba za walimu.

Kujenga hostel kwenye shule za kutwa Kuimarisha mitaala ya elimu ya sekondari. Haya mambo ni makubwa sana katika hatua hii ya maendeleo ya elimu nchini ni asusa na chachandu murua kwa CCM inapojielekeza katika uchaguzi mkuu wa 2005!

Pamoja na kutoa pongezi hizo kwa Waziri Mungai na Watebdahu wa Wizara yake, ningependa kuzungumzia changamoto kadhaa ambazo zinaikabili Wizara hii.

Kwanza, ni haja ya kutoa elimu inayoambatana na teknolojia ya mawasiliano - *information technology.* Elimu bora katika karne hii ya Sayansi ya teknolojia, inaambatana na matumizi ya kompyuta kuanzia shule za msingi. Lakini petu Tanzania matumizi ya kompyuta mashuleni bado ni finyu, yanakomea zaidi mijini kuliko na umeme. Kwa kuwa shule nyingi ziko vijijini ambako umeme hauko, ina mahanisha vijana wengi zaidi wanasoma katika shule za vijijini hawabahatiki kutumia kompyuta katika masomo yao.

Hivyo, kuwafanya wawe na elimu yenye bora wa chini ikilinganikshwa kwa wenzao wa mijini wanaotumia kompyuta. Kwa misingi hii, ninapendekeza kwamba

kama sehemu ya kuendeleza na kuboresha elimu nchini, Serikali kupitia Wizara ya elimu na Utamaduni, iandae programu maalum ya kusambaza/kuweka umeme katika shule zote ili matumizi ya kompyuta yawe kwa shule zote. Vinginevyo, itakuwa kukiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu 11(3) kama alivyonukuu Mheshimiwa Mungai, katika ukurasa wa 11 wa kitabu cha hotuba yake, ambapoo na mimi ninakinukuu.

Serikali ifanye jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo (Msisitizo wangu).

Pili, umuhimu na kuhuisha usimamizi wa maendeleo ya elimu nchini - *institutional rationalization and synchronisation.* Mpaka sasa kuna taasisi huu tatu zinazosimamia maendeleo ya elimu nchini:-

(a) Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa elimu ya msingi, ya sekondari na ya ualimu.'

(b) TAMISEMI kwa utekelezaji wa miradi ya elimu hiyo huko vijijini na mijini; na

(c) Wizara ya Sayansi, Teknolojia, na Elimu ya Juu. Taasisi hizi zote zina majukumu ambayo, japo yanafanana, yaani kuendeleza na kuboresha elimu nchini, lakini zina mtazamo na misukumo tofauti kuhusu elimu kwa mfano, pamoja na kuwa na ambitions programme ya kuboresha elimu ya msingi (MMEM) na elimu ya sekondari (MMES) lakini sina hakika kama Wizara ya Elimu na Utamaduji wakati mwingine haipati *frustratio*n kuona changamoto hii ama haichanganuwi ipasavyo vijijini (mpano kwa ujenzi wa nyumba za walimu, usimamizi kukamilisha ubora wa majengo na kulipa kwa wakati mafao ya walimu - masuala ambayo, kwa ujumla, yanasimamiwa na TAMISEMI) au kasi ya kufundisha walimu wa shule za sekondari (wengi wao wakiwa wa shahada za vyuo vikuu, vinavyosimamiwa na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia) haiendi sambamba na matarajio ya kupanua elimu ya sekondari.

Japo Mheshimiwa Waziri Mungai amezungumzia programu tano ili kuongeza vijana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu elimu ya sekondari wakiwa na matokeo mazuri ya kujifunza, programu ambazo ni pamoja na kufanya mageuzi ya kutoa madaraka, na kuboresha mfumo wa usimamizi wa elimu. Lakini matatizo ya *institutional synchronisation and rationalisation* yataendelea kuwa kikwazo kwa jitihada hizo. Hii ni kwa sababu taasisi hizi zina majukumu tofauti na haziwezi kuchukulia umuhimu wa elimu ya ngazi tofauti kwa uzito sawia.

Labda ni pamoja na tatizo la kutokuwepo *institutional rationalisation* kuhusu masuala ya elimu ndio maana sasa hivi hatuna mkakati bayana wa kuandaa rasilimali watu a herent human *resource development strategy.* Ili tuweze kuhimili changamoto za utandawazi ambapo soko la ajira linakuwa la ushindani zaidi, kwa kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni ninaishauri Serikali iwe na mipango mbadhubuti ya kuendeleza rasilimali watu. Suala moja muhimu katika azma hii ni kutoa elimu yenye ubora wa

kmataifa. Suala la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia ni Serikali kufikiria kwa makini kuwa na *USE - Universal Secondary Education Scheme* Hoja hii inazingatia masuala yafuatayo:-

(a) Tanzania kwa ujumla, tuko nyuma kielimu ikilinganisha na nchi jirani za Kenya na Uganda ambazo tunazo ushiriiano wa kikanda. Ili tuweze ku-*catch-up* na wenzetu budi tuwe na *an accelerated education programme;*

(b) Kuamrisha *USE* nchini Tanzania na ku-*complement* mpango wa MMEM ambao hauna mfano hapa Afrika. Sijapata kusikia nchi nyingine iliyoanzisha programu ya kupanua elimu ya msingi kama mpango wa MMEM mpango ambao kuanzia mwaka 2004/2005 unadakwa MMES. Hivyo, inaleta mantiki kwamba kundi la vijana wanaomaliza elimu ya msingi kwa kiwango cha asilimia 100, wapatao fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari; na

(c) Mazingira ya kuwa na *USE* nchini Tanzania tayari yameandaliwa na Serikali kama ambavyo Waziri wa Elimu na Utamaduji ametangaza katika hotuba yake kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005. Mazingira hayo ni pamoja na kupunguza ada ya wanafunzi wa elimu ya sekondari kutwa kuwa sh.20,000 tu na kuongeza sana ruzuku za kuendesha elimu ya sekondari nchini.

Ninaunga mkono hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kuhusu makadrio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Kutokana na uamuzi wa Wizara wa kugeuza shule ya Mkwawa kuwa chuo cha Walimu na ili kutopunguza idadi ya wanafunzi wa *forms V* na *forms VI* nchini napendekeza kuwa:-

Wizara ikubali kuongeza majengo (shule nyingine) katika eneo la shule ya Bweni ya serikali *Njombe Secondary School* ili kupokea wanafunzi 2,000 wa *form V* na VII tu kwa sasa shule hii ina uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 800 *(Form I - 6).*

Eneo la wazi chiin ya shle ni zaidi ya ekari 300. Kwa sasa eneo hili liko katika hatari ya kuvamiwa na wakazi wa mji wa Njombe. Zaidi ya ekari 40 tayari limevamiwa. Lengo kuu ni kwamba *Njombe Secondary School* iwe *Njombe High School* ingawa ingefaa hata jina libadilishwe kwa vile tutakuwa na *several high schools even within Njombe town. Ulembwe Folk Development College* ichukuliwe na Wizara hii na kuwa *Teachers College or Girls School.* Kwa vile majengo yake hayatumiki vizuri kikamilifu.

Eneo ni zuri na kubwa kwa upanuzi. *Note,* tayari Njombe tuna *FDC* mjini Njombe hivyo hakuna madhara kwa kuamua kutumia Ulembwe kwa njia hii. Napendekeza na kuiomba Wizara ichukue *Manyunyu Girls Secondary School* iliyoko chini ya *NDDT* kwa sasa. Pili, *Manyunyu Girls* iwe *Girls High School.* Iko mahali pazuri na ina eneo kubwa na zuri kwa upanuzi.

Shule ya Lupembe haina walimu. Walimu wawili waliopelekwa Lupembe hawajafika mwaka mzima. Naomba walimu wa Sayansi Maabara, Maktaba na Ukumbi kwa shule hii.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Makuu na Watendani wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri ya kuboresha sekta ya elimu na utamaduni nchini. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema Mheshimiwa Naibu Waziri na nampongeza kwa moyo wake wa kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhehismiwa Waziri Mungai kwa ziara yake hivi karibuni Wilayanhi Ileje. Tunamshukuru kwa misaada na maamuzi yote aliyofanya ya kuboresha elimu katika ngazi ya msingi na sekondari. Kama alivyojionea mwenyewe, Wilaya ya Ileje, kwa sababu za kihistoria, iko nyuma katika idadi ya shule za Sekondari. Lakini matokeo ya mitihani ya darasa la saba ni ya kutia moyo.

Wanafunzi wanafaulu vizuri, lakini wanakosa nafasi za elimu ya sekondari kwa sababu shule za sekondari ni chache. Kwa kuzingatia hali hiyo, na kutokana na taarifa nzuri ya mpango mpya wa kuboresha elimu ya sekondari, naomba Wizara itoe kipaumbele kwa wilaya ambazo ziko nyuma kielimu, ziko pembezoni mwa nchi yetu, zina mazingira magumu ki-jiografia, na kadhalika. Wilaya yangu ya Ileje imo katika kundi hili.

Mheshimiwa Spika, badhi ya matatizo yaliyopo kwa shule zilizopo ni upungufu wa walimu, kukosekana kwa vyombo vya usafiri katika shule za sekondari, upungufu wa majengo kutokana na nguvu ndogo ya wananchi na kadhalika. Natumaini mapango huu mpya utasaidia kutatua matatizo haya.

Aidha, naomba Wizara isaidie kutoa mwongozo kwa mashirika ya dini yanayoshirikiana na wananchi kujenga shule za sekondari na kisha kutoza ada kubwa, ambazo wananchi hawazimudu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu mfano wa Ileje. Tusaidie.

Namalizia kwa kuipongeza tena Wizara kwa mafanikio mazuri ambayo yanaonekana kila pembe ya nchi yetu. Nawatakia utekelezaji mwema kwa Bajeti ya 2004/2005. Naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kazi

nzuri anayoifanya kuleta mabadiliko ya elimu hapa nchini. Vile vile naomba nimpongeze kwa hotuba nzuri aliyoitoa hapa Bungeni.

Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia ifuatavyo:-

(a) Elimu ya Awali: Utaratibu unaoendelea hivi sasa wa kuwa na madarasa ya awali ni mzuri kwani hayo ni maandalizi mazuri ya mtoto kuingia katika Elimu ya Msingi. Ni vizuri Elimu ya Awali iwekewe mpango maalum kwa kuzishirikisha Shule za Msingi zote ikiwa ni pamoja na kuwaandaa Walimu kwa madhumuni hayo. Zipo Shule za Msingi zenye madarasa ya awali, Shule nyingine hazina madarasa hayo. Hali hiyo italeta tofauti ya ubora wa Elimu miaka ijayo.

(b) Mpango wa MEMKWA:Mpango huu ambao unaendelea katika baadhi ya Wilaya hapa nchini ni mzuri, Wizara ina mpango wa kuusambaza mpango huu katika Wilaya zote. Nashauri ieleweka ni lini mpango huu utasambazwa Wilaya zote. Je, wahitimu wa wanafunzi wa mpango huu wanapata utambulisho gani ili wawezeshwe kuingia katika mafunzo mengine au katika ajira mbalimbali.

Katika Wilaya ambazo mpango wa MEMKWA haujaanzishwa rasmi, shule au Wilaya zenyewe zinaendesha, Walimu wanaofundisha madarasa hayo wengi hawalipwi na hawana marupurupu yoyote. Mpango huu unafaa kusimamiwa vizuri.

( c) Malengo ya MMES: (i) Ili kuleta usawa katika utoaji wa Elimu ya Sekondari, nakubaliana na malengo ya kuongeza idadi ya wasichana mashuleni na wanabaki. Ili kufanikiwa vizuri, ni vema kipaumbele kitolewe kwa ujenzi wa Hosteli za Wasichana katika Shule za Kutwa za Sekondari. Uzoefu unaonyesha kuwa wasichana wengi wanaojiunga katika shule hizi za Kutwa wanashindwa kumaliza *Form IV* kwa sababu ya umbali, na kupata vikwazo vya mimba na kadhalika. Kwa kutembea kwenda na kurudi au kuishi kwenye majumba ya kupanga au kuishi kwa majirani.

(ii) Katika ujenzi wa shule mpya, nashauri upendeleo utolewe kwenye maeneo yenye ufukara mwingi, hakuna shule nyingine jirani na zilizo mbali sana na barabara na kutoka Makao Mkuu ya Wilaya. Maeneo hayo ni kama maeneo ya Mwambao mwa Ziwa Nyasa Mkoa wa Iringa, Wilaya za Ileje Mkoa wa Mbeya, Kyela, Mbarali zote za Mkoa wa Mbeya. Wilaya hizo zina maeneo magumu ambayo hayafikiki kwa urahisi. Wizara ifanye uchunguzi wa kina katika utekelezaji. Kama hilo halitaangaliwa matokeo yake ni kujaza shule na mikondo katika maeneo machache.

Mwisho, naunga mkono hotuba ya Waziri asilimia mia.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Pongezi nyingi kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya kutekeleza Ilani ya CCM ya 2000.

Maombi: (1) Naomba msaada wa haraka ili ahadi ya kuwasaidia wananchi wa Chigoli-Mtera-Iringa kukamilisha nyumba 15 za Walimu ambazo maboma

yameshajengwa tayari na wananchi. Tangu shule hii ianze kuchukua wanafunzi mwanzoni mwa 2005.

(2) Shule ya Sekondari ya Ismani haina bweni hata moja, haina maabara, haina Walimu wa kutosha. Wanayo *Generator* lakini hawana fedha za kufanyia wireling. Aidha, madarasa yamechakaa na nyumba za Walimu iko moja tu. Shule hii inahudumia Kata 3 zenye idadi ya watu 38,000. Naomba msaada.

(3) Idadi ya Sekondari haina Maabara na nyumba za Walimu. Aidha, madarasa ni machache sana. Naomba msaada.

Nawatakiwa kila la kheri Viongozi na watendaji wote wa Wizara. Pongezi kwa kazi nzuri sana sana!!

Naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Joseph Mungai (Mb.), Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri inayofanywa ambayo sisi sote ni mashahidi. Pongezi pia kwa wasaidizi wake wote.

Ningependa kushauri yafuatayo: Idara ya Ukaguzi wa Elimu ya Msingi Wilayani Kongwa ina gari moja bovu, *Toyota Stout Pick Up*, la zamani sana na siyo *roadworthy.* Tunaomba sana yakipatikana magari basi na Idara yetu hiyo isaidiwe.

Mpango wa MEMKWA bado utekelezaji wake haujawa sawa kwa sababu Walimu wanaojitolea kufundisha madarasa haya hawalipwi chochote. Wizara ilitoa ahadi ya kuwa kuanzia Januari 2004 wangekuwa wakipata japo kaposho ka kujikimu. Nashauri walipwe.

Shule za Sekondari za Zoissa, Kongwa na Mlali Wilayani Kongwa bado zina uhaba wa Walimu na zaidi ya yote Walimu wa Sayansi hakuna. Hasa masomo ya *Mathematics, Chemistry, Physics and Biology.*

Walimu wa Shule za Msingi Wilayani Kongwa wanadai zaidi ya Shilingi million 86. Tafadhali walipwe. Najue TAMISEMI ndio wahusika zaidi lakini Wizara hii ndiyo Wizara Mama ya masuala yote ya Walimu.

Kongwa, tumeanza ujenzi wa Sekondari kote hata Saba *Population* yetu ni 250,000 wakazi - tuna Sekondari tatu tu. Kwa hiyo, tunaomba sana *support* ya *Mess* kwa Sekondari hizo saba na hivi sasa michango yetu ya wananchi inaendelea kwa maeneo yote husika. Tumechelewa sana, tunaomba tukimbie pamoja. Naunga mkono hoja.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Joseph Mungai (Mb.), Naibu Waziri

Mheshimiwa Bujiku Sakila (Mb.), Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi yao nzuri na moyo wao wa kuwatumikia wananchi jambo linaloendelea kudhihirisha kuwa wanao wito wa kuwatumikia watu.

Kimsingi naomba kuchangia katika maeneo machache yafuatayo:-

I. Mahitaji ya Walimu wa Sekondari: Naomba Wizara inipangie Walimu wa Sekondari katika shule mpya ya Iselamagazi ambayo imeanza mwezi wa Aprili mwaka huu. Aidha, kuongezea Walimu katika Shule za Sekondari Zunzuli na Samuye.

II. Ahadi ya Waziri: Katika ziara yake ya kazi Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Joseph Mungai (Mb.) alipotembelea Shule ya Sekondari ya Samuye aliahidi kunipatia umeme kupitia Mfuko wa Serikali, ili mradi apelekewe gharama halisi; jambo ambalo lilifanywa na *TANESCO* na makisio hayo yalitumwa kwa Wizara tangu mwaka jana 2003 mwanzoni.

Nashauri Wizara itekeleze ahadi hiyo ya Kiongozi ambapo itasaidia sana shule hii kwani umeme umepitia eneo hilo la shule lakini haujaunganishwa katika nyumba/madarasa yao.

III. Malipo ya Walimu: Kama ujulikanavyo kuwa Walimu ni wito ni vyema watu wanaoonesha kuifanya kazi hiiwasikatishwe tamaa. Nashauri Serikali kuhakikisha kuwa inawalipa Walimu malipo yao halali ya malipo ya likizo, mishahara yao (Walimu wapya), *subsistence allowance* na kadhalika.

Hii itachochea moyo wa watumishi hawa kuipenda kazi yao na kujiona kuwa Serikali inathamini mchango wao.

IV. Mpango wa kuwawezesha Walimu wapate vifaa/nyenzo za usafiri. Naishauri Wizara kuanzisha utaratibu ambao utawawezesha Walimu wakakopeshwa pikipiki na baiskeli ili kuwasaidia wakarahisisha kusafiri hasa maeneo yenye tatizo la usafiri nchini kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, Napenda kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye kina. Nitachangia katika sehemu chache tu kwa maana ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara ya Walimu kuwa duni na la siku nyingi na kwa kweli Serikali inabidi ipange mpango wa muda mrefu, wa kati na muda mfupi katika ufumbuzi wa suala hili. Vinginevyo Walimu wetu watabaki na mishahara midogo.

Naipongeza Serikali kwa mpango mzuri wa MMEM, ambao umeleta ufanisi mkubwa katika ujenzi wa madarasa. Nashauri sasa mkazo uwe katika kujenga nyumba za Walimu, hususan Vijijini, ili kuwaondolea kero Walimu. Zikijengwa nyumba Vijijini suala la upungufu wa Walimu Vijijini litakuwa limetatuliwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta mpango wa Bima ya Afya kwa wafanyakazi wake. Hata hivyo zoezi hili lina matatizo ya kucheleweshwa kupewa kadi wahusika, hasa Walimu. Kwa mfano, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tabora, iliyoko jimboni kwangu, wafanyakazi wafuatao bado hawajapata kadi zao:-

- Mwange Malilo;
- Agatha Daudi Mashwa;
- Mwaka Lintu;
- Israel Ndyamkana; na kadhalika.

Naomba Wizara ifuatilie suala hili.

Kero nyingine kwa Walimu ni ucheleweshaji wa marekebisho ya mishahara ya Walimu baada ya kupandishwa vyeo na kuanza kwa miundo mipya ya mishahara.

Katika Sekondari ya Wasichana ya Tabora, kuna Walimu wengi ambao mpaka hivi sasa hawajafanyiwa marekebisho ya mishahara baada ya kupandishwa vyeo na kuanzishwa kwa miundo mipya ya mishahara; kwa mfano Mwalimu Eliezer S. Ukwai, Ndugu Margareth Z. Kissiwa, na kadhalika

Naiomba Serikali sasa ifanye marekebisho hayo haraka ili Walimu wapate mafao yao.

Kero nyingine kwa Walimu ni ucheleweshaji wa malipo ya mirathi ya Walimu wanaotangulia baada ya kuitwa na Mola na kuitikia. Naomba Wizara ya Elimu isaidie ili Wahanga wapate mafao yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kutoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Joseph Mungai kwa kuwasilisha hotuba nzuri yenye dira ya maendeleo ya mbele kwa elimu ya watoto wetu nchini.

Hali kadhalika nampongeza Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri Elimu na Utamaduni na Katibu Mkuu Mama Mwantumu J. Malale kwa kazi bora wanazozifanya hadi kumwezesha Waziri kutenda kazi zake kwa makini na leo anaweza kuwasilisha hotuba yake Bungeni kifua mbele kwa jinsi ilivyoandaliwa kwa makini, kwa umakini wa hotuba hii nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Kuna mambo machache ya kuboreshwa. Kwanza haki za walimu kulipwa posho za uhamisho likizo, matatibu, marekebisho ya mishahara baada ya *promotion* wale wanaofundisha MEMKWA. Halmashauri za Wilaya nyingi haziwalipi walimu ipasavyo ingawa ruzuku toka Serikalini inapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya utatuzi wa hili iwe kama ifuatavyo:-

(i) Waziri awe anatoa orodha ya fedha ambazo zinatumwa kwenye Halmashauri za Wilaya au Manispaa ili kuhakiki ukweli wa malipo hayo kwa walimu.

(ii) Walimu Wakuu wanaowakemea walimu wao wa chini na kuwaadhibu kwa kudai na kusema wazi manyanyaso wanapotembelewa na viongozi wa juu waadhibiwe kwa tabia zao mbaya.

(iii) Walimu waruhusiwe kutuma nakala za barua zao juu ya madai yao halisi kwa sababu wanazotuma Kiwilaya au kwa Walimu Wakuu, kuna mtindo wa kukata madai ya Walimu wao na kuwapunja haki zao kwa sababu za ubinafsi tu. Hali kadhalika maafisa waliopo Wizarani waongezwe kazi ya kuhakiki madai ya Walimu kwa kila Mkoa kwa sababu maafisa hao Wizarani ni wengi kiasi kwamba wanatosha kwa Mikoa yote 21 au 26 pamoja na Zanzibar.

(iv) Mishahara ya Walimu lazima yapitie kwenye *computer* hazina Dar es Salaam ndipo waweze kulipwa mishahara yao, kurekebishwa mishahara na kadhalika.

Lakini huko Hazina kuna umangimeza/ucheleweshwaji wa kazi hizo na kuleta malalamiko kwa Walimu na dhana inakwenda Wizara ya Elimu badala ya Waziri wa Fedha.

Kwa hiyo, Waziri wa Elimu na Utamaduni awapange maafisa wake waliopo Wizarani kufuatia Hazina utekelezaji wa haraka wa marekebisho ya mishahara ya Walimu nchini.

Pili, mapunguzo ya ada ya sekondari toka shs. 40,000/= hadi 20,000/=. Wananchi na hasa wazazi tunashukuuru sana kwa mpango huu wa mapunguzo ya ada na kwamba nina hakika wasichana sasa watasoma kwa wingi na akina mama wajane watapunguziwa mzigo wa ada, kwani watoto wengi nchini wanasomeshwa na mama zao kutokana na wanaume kuhama miji yao na kwenda machimboni kwenye biashara mbalimbali na wengine kufariki.

Kwa hiyo, nasema ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mungai Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa mpango huu.

Lakini kuna baadhi ya wazazi wana kasumba ya kuacha makusudi kuwaelimisha wasichana na kuwalazimisha kuolewa ili wapate ng'ombe au fedha za mitaji ya biashara na mengineyo basi namuomba Waziri wa Elimu na Utamaduni kuleta Muswada wa Sheria Bungeni kwa wazazi wa aina hiyo kufungwa miaka 10 jela bila kutozwa faini ya fedha. Kwa sababu wenye uwezo wanalipa faini na kuendelea kuhujumu elimu kwa wasichana.

Tatu, mafunzo ya Walimu vyuoni. Wananchi wamezoea utaratibu uliopo wa kuomba nafasi ya kusomea kazi hiyo ya ualimu na mwaka huu tunasikia utaratibu ni kuchukua mashuleni na tutauzoea vile vile lakini tunaomba walioomba kipindi hiki nje ya shule wachukuliwe hadi mwisho wa maombi yaliyopo na wakati huo huo wananchi watazoea utaratibu mpya.

Nne, kulipia utoaji wa vyeti vya sekondari kidato cha nne na cha sita. Naomba malipo yafutwe wakati wa wanafunzi kuhitaji vyeti vyao toka Baraza la Mitihani ya Taifa. Hii ni kero kwa wazazi na wanafunzi wengi hadi sasa hawajachukua vyeti vyao kwa kukosa fedha za kuchukulia vyeti.

Tano, ombi la ruzuku kwa wanafunzi wa *Private Secondary School* 2005/2006. Tumefurahi kwa Serikali kutoa punguzo la ada kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari kuanzia 2005 na kuendelea. Lakini wananchi wanazungumzia sana wanafunzi waliofaulu kwenda Elimu ya Sekondari. Lakini nafasi za Sekondari za Serikali Kuu ni chache na hivyo wazazi kulazimika kuwasomesha watoto wao shule binafsi kwa ada kubwa na hivyo baadhi ya watoto na hasa wasichana kukosa elimu kwa ubaguzi wa kijinsia. Je, Wizara ya Elimu na Utamaduni inaweza katika bajeti ya 2005/2006 kutenga ruzuku ya fedha kwa ajili ya kuwakopesha wazazi waliokosa watoto wao kuteuliwa nafasi za Shule za Serikali ingawa walifaulu mitihani ya kwenda sekondari?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache narudia kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wengine wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na pia taasisi na asasi za Wizara hii kwa hotuba nzuri sana pamoja na viambatanisho vingi ambavyo vimeelezea kwa uwazi na ufasaha mkubwa kazi nzuri iliyofanyika kwa mafanikio makubwa. Ningependa pia kuwapongeza kwa mipango mizuri yenye mwelekeo mzuri unaoleta matumaini makubwa kwa wananchi. Naunga mkono hoja na kuitakia wizara hii utekelezaji na mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoahidi Mheshimwia Waziri Mungai akijibu suala langu mapema mwaka huu, wananchi wa jimbo la Mkinga wamehamasika sana kuhusu hatua thabiti za kuendeleza Elimu ya Msingi chini ya mpango wa MMEM. Wananchi wa Jimbo la Mkinga wamehamasika zaidi kuhusu MMES na tayari kila Kata iko katika hatua mbalimbali za kuendeleza Shule za Sekondari zilizopo na kuanzisha mpya. Wananchi wamepata hamasa kubwa kutokana na sera nzuri lakini hususan kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwamba Wizara itajitahidi kuziunga mkono jitihada za wananchi katika kuboresha na kuendeleza elimu. Kwa misingi hii ni matumaini yangu makubwa kwamba Wizara itatoa kipaumbele cha kwanza katika kuziendeleza Shule za Sekondari za Lanzoni, Maramba na Zinzibari ziwe na maabara, mabweni, nyumba zinazofarajiwa. Vile vile ni matumaini yangu kwamba Serikali itasaidia shule hizo kuwa na madarasa ya kutosha pamoja na vitabu, vifaa na vitendea kazi vinavyostahili kwa shule hizo kuwa na kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kueleza kwamba zaidi ya jitihada za kuwa na angalau shule moja ya sekondari kwa kila kata bado wananchi wa jimbo la Mkinga wanaendelea na jitihada za kuendeleza Elimu ya Msingi kwa kuongeza vyumba vya madarasa, madawati, vitabu na vifaa vingine. Kwa haya, bado tunategemea ushirikiano wa karibu wa Serikali katika kuzikabili kero hizo.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Mkinga yapo malalamiko mengi ya Walimu kuhusu malimbikizo ya madeni, ugumu wa kupata mishahara, marekebisho ya mshahara, ukosefu wa makazi, upungufu wa Walimu, upungufu wa vitabu vya kiada ziada na rejea, idadi kubwa zaidi ya wanafunzi kwa darasa kuliko inavyostahili na ucheleweshaji wa kufikisha fedha za maboresho. Hivyo ushirikiano wa Wizara katika kuzipatia ufumbuzi kero hizi kwa wakati ufaao ni muhimu ili maboresho yawe na tija na mafanikio makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa tena kuipongeza kwa dhati Wizara na kuiombea mafanikio makubwa zaidi katika jitihada za kutekeleza mipango hii inayotekeleza sera za CCM kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Joseph Mungai (Mbunge); Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku K. P. Sakila (Mbunge), Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni; Bibi Mwantumu J. Malale, Viongozi na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga hoja mkono, nina yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Elimu ya Msingi. Elimu katika maeneo ya wafugaji ni duni na wananchi hao bado wanahitaji mpango maalum. Mpango maalum ni pamoja na kuongeza Shule za Msingi za Bweni kila Kata kuwa na Shule moja ya Bweni. Hizi Shule za Bweni husaidia watoto kusoma wakati wazazi wao wakihama kutafuta mahitaji ya mifugo yao.

Mpango mwingine ni kuwapatia Walimu kulingana na mikondo na siyo uwiano wa wanafunzi kwa Walimu kwani shule moja yenye darasa la I - VII yenye wanafunzi 180 uwiano wa Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45, shule hiyo inastahili kuwa na Walimu wanne (4). Je, Walimu wanne wanaweza kwa usahihi kufundisha wanafunzi wa darasa la I - VII? Kwa uandikishaji unaoendelea sasa huenda uwiano huo ukafanya kazi lakini siyo kwa hivi sasa. Simanjiro tuna upungufu wa Walimu takriban 300 na wanafunzi kufika shuleni kucheza na kurudi nyumbani wazazi wanakata tamaa na kushawishika kwamba bora watoto wangebaki kuchunga mifugo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni Elimu ya Sekondari. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipofanya ziara Wilaya ya Monduli, Simanjiro na Kiteto alitamka kwamba Serikali itajenga Sekondari za Bweni katika Wilaya za Wafugaji. Mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri wa Elimu akijibu swali kuhusu hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa uliahidi kwamba zitajengwa hizo Sekondari pindi ukianza mpango wa MMES. Je, katika bajeti hii 2004/2005 unaniahidi kwamba utatimiza hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais Wilaya ya Simanjiro?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule hasa sekondari ni suala geni kwa wananchi wa Simanjiro. Kabla ya kipindi cha ubunge wangu hapakuwepo na sekondari hata moja na wanafunzi waliokuwa wanakwenda kidato cha kwanza kabla ya 1995 walikuwa (15) kumi na tano. Sasa baada ya kufungua Sekondari mbili (2) sasa wanafunzi wanaokwenda kidato cha kwanza ni 200 , japo Sekondari hizo wanafunzi wamefikia kidato cha nne kuna mapungufu. Naiomba Serikali mwaka huu wa fedha 2004/2005 ikamilishe mapungufu hayo. Aidha, naiomba Serikali ishiriki katika ujenzi wa sekondari mpya inayojengwa kwa nguvu za wananchi ili sekondari hiyo ianze Januari 2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kwamba alama ya chini kwenda kidato cha kwanza ni 60%. kwa Wilaya ya Simanjiro alama ya chini kwenda kidato cha kwanza ni alama 85% hii ni kutokana na uhaba wa nafasi za sekondari. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa mpango huu wa MMES tupatiwe mpango maalum. Sekondari mbili tulizonazo zina uhaba au upungufu mkubwa wa Walimu, tunakuomba utupatie Walimu.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa idhini ya kuchangia hoja hii. Kabla sijaanza kutoa ushauri nilionao, kwanza naunga mkono hoja ya Elimu na Utamaduni. Kwa maana hii ninaipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara hii. Mapinduzi yaliyofanywa katika miaka mine hii ni hatua kubwa katika kutokomeza umaskini uliokithiri katika jamii ya Watanzania kutokana na ujinga. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, sasa natoa ushauri kwa Wizara. Kuhusu MMES, Serikali na Wizara ya Elimu na Utamaduni itoe upendeleo wa makusudi kwa Wilaya zisizo na sekondari za kutosha. Wilaya ya Ngara ni mfano mzuri. Sekondari ya kwanza ilijengwa mwaka 1991 Katani Kabanga kwa kuhudumia Kata mbili tu za Kabanga na Mabawe. Miaka yote ya nyuma Wilaya hii ilitegemea kupata elimu kutoka Bukoba na Mwanza kilometa 350 na 455 bila usafiri wa kutumainiwa na hivyo ikabaki nyuma kielimu. Wanafunzi walishinda lakini hawakupata nafasi kwa kukosa uwakilishi/utetezi wakati wa uchaguzi.

Sekondari ya pili Wilayani Ngara ilijengwa mwaka 2001 na ya tatu mwaka 2002. Leo Ngara ina sekondari tano tu na zinajengwa na wananchi wenye matatizo makubwa ya wakimbizi wengi tangu 1993 hadi leo. Sekondari mbili kati ya tano zimefunguliwa mwaka huu 2004, hazina Walimu wala samani na vitabu vya kufundishia. Hazina majengo muhimu kama maabara, maktaba na nyumba za Walimu. Wananchi wa Ngara wanaomba sekondari hizi zikamilishwe katika mpango wa MMES.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anaifahamu Serikali ya Muyanzi iliyojengwa kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 1995. Ni sikitiko kubwa kwa wazazi, wanafunzi na Walimu kwamba licha ya kuendelea kuijenga na wananchi baada ya Wizara kutoitilia maanani vya kutosha, shule hii haina maabara, nyumba za walimu, vyoo, mabweni, maji, umeme na kadhalika. Waheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mhandisi wa Wizara na Wakurugenzi kadhaa wanaifahamu, lakini nasema wameipuuza. Shule iko kijijini kusiko na nyumba za kupanga. Kila mwaka tunapoteza wasichana kwa kubeba mimba kwa kulala ovyo ovyo pasipoaminika na uchovu wa masafa marefu. Tafadhali tunaomba sasa shule hii ikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 - (18.1 - 18.4 na 18.6), Ngara ijengewe sekondari zaidi. Wilaya ina Kata 17 na Vijiji 72 vinavyohudumiwa na Sekondari zisizo na uwezo 5. kama shule hizi zingejengwa kikata, bado Kata 12 zingekuwa hazina Sekondari kila moja. Upungufu huu ni mkubwa sana.

Mwaka 2003 Ngara kwa mtihani wa darasa la VII kitaifa ilikuwa ya kwanza kimkoa, ya kwanza kikanda na ya nne kitaifa kwa kushindisha wanafunzi 1868 kwa alama za juu kati ya watahiniwa 2656. Kwa ukosefu wa sekondari ni wanafunzi 633 tu waliochaguliwa kujiunga Wilayani, Mkoani Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Arusha, Moshi, Kigoma na kadhalika. Waliokosa Elimu ya Sekondari kwa alama tangu 150 - 180 ni 1235 ambao wanatutupia mawe njiani na lawama kubwa za wazazi na Walimu. Pia, wananchi wanaothamini elimu.

Kwa kuwa wakazi wa Ngara wanaandaa Sekondari nane (8) katikati ya umaskini na usumbufu wa Wakimbizi, Serikali inaombwa sana na wakazi wa Ngara na mimi Mbunge wao nakuomba Mheshimiwa Waziri kwanza atembelee Ngara. Naamini atapata wazo halisi la kuimarisha elimu kwa kutujengea Sekondari zaidi kwa mpango huu wa MMES. Itakuwa hatua ya kutulinganisha na Wilaya nyingine za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 - (18.11), naipongeza Serikali kuona umuhimu wa kuunga mkono Sekondari Binafsi kwa upande wa Elimu ya Sekondari, Shule Zisizo za Serikali Sh.10,000/= kwa mwanafunzi. Msaada huu ni mzuri unaowaongeza ari wahusika, lakini hautoshi.

Watu binafsi na Mashirika mbalimbali yako tayari kujenga Sekondari lakini wanaogopa kwanza kuwa wakazi hawataleta watoto kwa sababu ya gharama kubwa na pili kwamba Serikali haitaruhusu kupandisha karo. Kwa sababu sekta hii ya elimu inaipunguzia mzigo Serikali na hivyo kuisaidia kutekeleza malengo yake ya maendeleo, ni vyema wakafikiriwa zaidi ili kuwaondolea mawazo ya kuendesha shule kibiashara na kutumia Walimu walio na uwezo/ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 - (18.8) inahusu wanafunzi toka familia maskini. Naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwamba itafutwe njia nzuri ya kuwalipia watoto badala ya utaratibu uliopo sasa. Ruzuku hii haiwafikii baadhi ya walengwa. Wanafunzi kadhaa, baadhi wakiwa waliosamehewa tangu 2002 wanahangaika mashuleni bila msaada huo.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano wa mwanafunzi Emmanuel Vedatus asomaye Sekondari ya Nsumba, Mwanza, ambaye tangu mwaka wa 2002 aliposamehewa hajapata ruzuku hiyo. Wakati wa likizo ya muhula wa kwanza 2004, Mbunge wa Ngara alipaswa kulipa gharama zote aende likizo kilometa 450 hivi Ngara, badala ya kubaki shuleni sijui angebaki kwa nani na kupewa msaada wa kuishi na nani! Wizara iweke kitengo kidogo cha kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ruzuku zinazotolewa kusudi zifanikishe malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Walimu, Ibara ya 18, sababu kubwa za elimu nchini kudorora ni nyingi. Mojawapo kubwa ni mazingira mabaya wanayoishi Walimu wetu. Napenda kusema kuwa mafanikio ya MMEM ni makubwa sana, lakini hayagusi ujenzi wa nyumba za Walimu vya kutosha. Naiomba Wizara kwa utaratibu mzuri sasa ijenge nyumba za Walimu ngazi zote za chini.

Walimu wengi sana wanafundisha vijijini ambako hakuna nyumba za kupanga. Hakika wananchi wanakazana kujenga madarasa na vyoo kwa elimu ya watoto kwa kuona kuwa huo ndiyo umuhimu wa kwanza. Iwe ni kwa elimu ya msingi au ya sekondari nyumba hazipo. Shule nyingi hazina nyumba hata moja, labda ni Ngara tu?

Lakini nafahamu ni nchi nzima. Walimu husafiri masafa marefu hadi kilometa 15 kwa mfano wa Shule za Rugariba, Kigina, Magereza Rusumo, Rusengo na kadhalika.

Walimu Ngara wana shida kubwa. Naiomba Wizara iunde timu kuzunguka nchi ikifika kila Wilaya kuona hali ya elimu ilivyo kabla ya MMES kuanza kutekelezwa kwa muda mrefu ili kuwe na usawa katika kuboresha elimu nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Nampongeza Waziri na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulea na kuelimisha watoto na vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri na ina taarifa nyingi muhimu. Hata hivyo, natoa ushauri ufuatao:-

(i) Cheo cha *REO* kibaki na Ofisi ya *REO* iimarishwe kifedha na kiutumishi, kuwe na Wasaidizi wa Elimu ya Msingi, Sekondari, Walimu na kadhalika.

(ii) Somo la Hesabu liwe somo la lazima kutoka *Form I* hadi *Form IV.*

(iii) Ikama ya shule zote izingatiwe. Shule hazina Walimu wa kutodha kiidadi na kitaaluma.

(iv) *REO* asimamie elimu ngazi zote, isipokuwa Elimu ya *University.*

(v) Wanafunzi wa Ualimu watokane na wanafunzi waliofaulu vizuri mitihani ya *FormIV* na *Form VI.*

(vi) Wizara iunde Tume ya kuangali a mfumo wa elimu nchini. Miaka zaidi ya 20 imepita tangu lifanyike zoezi kama hilo (1981).

(vii) Nini msimamo wa Wizara kuhusu lugha ya Kiingereza na Kiswahili?

(viii) Nashauri mfumo wa kuwa na *Special Schools* kama Mzumbe na Ilboru uendelee badala ya kufuta, ila kila mkoa uwe na *Special School* (au kila Kanda).

(ix) Somo la Hesabu linakufa. Tafuta Walimu kote duniani na kuwapeleka katika Vyuo vya Ualimu (Wahindi) ili kufufua somo hilo. Pia mkakati uandaliwe kwa madhumuni hayo.

(x) Kuna mafanikio makubwa sana katika uboreshaji wa mazingira. Hatua ya pili iwe katika uboreshaji wa Mitaala, ubora wa Elimu na *relevance* ya Elimu katika dunia ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, pongezi sana Mbelembo!

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki, naunga mkono hoja ya Waziri Joseph Mungai kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri imewasilishwa Bungeni kwa ufasaha wa hali ya juu. Kwa matayarisho yaliyomwezesha Waziri kutoa hotuba ya kihistoria katika maendeleo ya elimu nchini, nawapongeza Wasaidizi wake - Mheshimiwa Bujiku Sakila (Mb.), yeye nampa pole na kuendelea kumtakia afya njema; Katibu Mkuu - Mama Mwantumu Malale, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya. Lakini Mashujaa Wakuu wa Wizara hii ni Wakuu vya Vyuo na Shule, na hasa hasa Walimu. Tunawashukuru.

Mheshimiwa Spika, leo mchango wangu utakuwa mfupi. Nao ni kuonyesha jinsi gani wananchi wa Rungwe Mashariki watasaidia kufanikisha mpango wa MMES. Tayari Shule za Jumuiya, za Sekondari zimeongezeka toka 1 Januari, 2000 kufikia 8 Machi, 2004. Hii imetokana na mshikamano baina ya Wananchi, Uongozi wa Wilaya, Uongozi wa Elimu Mkoa, na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Shule tatu zaidi zimeanza kujengwa na wananchi. Wamedhamiria kukamilisha hizo shule za Sekondari za Lupatu, Kisegese na nyingine moja ifikapo Januari, 2005. Tunaomba ushirikiano wa Wizara hii ili kufanikisha azma hiyo, kwani ni katika utekelezaji wa azma ya mpango wa MMES.

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika kuendeleza elimu, ni ufunguaji au uanzishaji wa kasi wa Shule zenye Kidato cha 5 na cha 6. Katika hili, wananchi wa Rungwe Mashariki wamedhamiria kuwa na shule moja zaidi ya Kidato cha 5. Shule hiyo ni Shule ya Sekondari ya Lufilyo. *(Lufilyo Secondary School)*. Wananchi tayari wamejenga vyumba vya Kidato cha 5 na cha 6. Katika kipindi cha wiki 2, tayari ujenzi utakuwa umekamilika. Sasa madawati yanatengenezwa. Hosteli ya wasichana ipo, na hosteli ya wavulana ipo kwa kutumia jengo lililokuwa likitumiwa na wasichana kabla ya kuingia jengo jipya. Umeme upo, maji safi yapo, nyumba za kisasa zipo - ambazo kwa muda tutakodisha kwa matumizi ya Walimu na wanafunzi wa ziada.

Mheshimiwa Spika, ombi hili lilikubaliwa kimsingi na Waziri wa Elimu na Utamaduni alipotembelea shule mwaka 2002, mwezi Juni. Tunamhakikishia kuwa tunafanya kila liwezekanalo ili azma hii ifanikiwe. Tunasaidiana pia na Taasisi ya FAWE - ambao wameiteua shule kuwa *Centre of Excellence.*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la kukubali ombi la wananchi kuhusu Kidato cha 5 Lufilyo ili tusaidiene kutekeleza MMES. Akifanya hivyo, anapofanya majumuisho ya kufunga hoja yake, tutamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Rungwe Mashariki tunatarajia mpango wa MMES utakuwa endelevu baada ya wafadhili kujiondoa, na kwamba hautapunguza ari ya wananchi kujitolea wakitegemea msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kurudia tena kumpongeza sana Waziri Mungai, Naibu Waziri Sakila, Katibu Mkuu Mwantumu Malale na Uongozi wote wa Wizara. Nawapongeza sana mashujaa wa Wizara hii - Walimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Wake - Mheshimiwa Bujiku Sakila (Mb.), Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kuelimisha watoto wetu na kudumisha utamaduni wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni dhahiri kama yalivyowekwa bayana katika hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Nawashukuru sana. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, kwa kuboresha elimu katika Wilaya ya Muleba na ushirikiano ambao wananchi wanaupata kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni katika kupanua Elimu ya Sekondari na kuimarisha Elimu ya Msingi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwahakikishia ushirikiano wa Ofisi ya Mbunge na Wananchi kwa ujumla katika kutekeleza malengo mazuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni ameyaeleza katika hotuba yake ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULO N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, maombi kwa Wizara ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupatiwa Walimu wa Somo la Sayansi kwa *Shinyanga Secondary School.*

(ii) Kupatiwa Walimu kwa shule zilizojengwa na wananchi (Serikali) kwa shule za *Mkunze Secondary School* na *Mipa Secondary School.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu - Mheshimiwa Joseph Mungai, Nasibu wake, Katibu Mkuu, Afisaelimu Kiongozi na Wataalam wengine wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, maelezo mazuri na mafanikio makubwa yanayoelezwa katika kitabu cha hotuba ya Waziri Mungai, pamoja na vitabu vingine vilivyoambatishwa na hotuba hiyo, ni kielelezo cha wazi cha utendaji bora - kiasi cha kustahili pongezi nyingi sana sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya kupunguza ada ya wanafunzi wa Shule za Sekondari, uwezekano uangaliwe wa kuondoa kabisa ada hiyo kwa jinsi mapato ya Serikali yanavyoendelea kuboreka.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Waziri ifufuliwe kwa sababu kwa kweli elimu hiyo katika maeneo mengi ya nchi yetu imekufa. Jitihada za kuifufua, ziwe endelevu, vinginevyo sehemu kubwa ya Watanzania isije ikarudi katika ujinga.

Mheshimiwa Spika, mpango mpya wa kuendeleza Elimu ya Sekondari (MMES) pamoja na mpango unaoendelea wa MMEM, ni mipango inayostahili kupongezwa; na kwa kweli kusimamiwa kwa uhodari unaostahili ili kuendeleza mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mafanikio zaidi ya mipango hii yanategemea upatikanaji wa Walimu. Naomba mpango wa haraka *(crash programme)* ili kuwapata Walimu wengi kwa Shule za Msingi na za Sekondari kwa mipango hii.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili kama lugha yetu, kipewe kipaumbele. Hongera Serikali kwa lugha ya Kiswahili kuanza kutumika katika Mkutano wa Umoja wa Afrika kule Addis Ababa. Kwa kuwa Tanzania ndipo nyumbani kwa lugha ya Kiswahili, naomba Kiswahili kipewe uzito na umuhimu mkubnwa kinavyostahili sana.

Mheshimiwa Spika, mafanikio kwa Wizara hii ni makubwa sana. Wasiwasi wangu ni namna gani Serikali kwa ujumla wake, itakavyoweza kuyalinda mafanikio haya makubwa. Najua pia kwamba misaada mingi tunayoipata kutoka kwa wahisani, inategemea jitihada zetu wenyewe za kuelekea kujitegemea. Naomba jitihada za kujitegemea ziendelee.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya mapato yaendelee kuboreshwa, jitihada za kuzalisha mali zisimamiwe kwa umakini mkubwa, hasa katika maeneo ya Kilimo na Viwanda. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote kwa bajeti nzuri ambayo Waziri ameitoa.

Mhjeshimiwa Spika, mipango ambayo Wizara imepanga kwa ajili ya elimu katika nchi yetu, ni mizuri ili nchi yetu iweze kujitoa kwenye ujinga. Kubwa ambalo Wizara inatakiwa kufanya katika mipango yake hii ni usimamizi wa fedha zilizotengwa. Kwa kweli kama usimamizi hautakuwepo, basi yale yote yaliyopangwa hayatatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wachache ambao siyo waaminifu. Hutumia pesa zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya elimu, kwa mambo mengine ya binafsi. Hivyo, tunaomba wale wote watakaobainika katika hili, wachukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa wale watakaobaki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina jambo moja ambalo naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo au mwongozo katika jambo hilo, nalo ni kuhusu Shule na Vyuo ambavyo havijasajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo hili kwa wanafunzi na wazazi katika jambo hili, na haata sasa kuna baadhi ya wanafunzi wamekwenda Mahakamani. Ningeomba Wizara wangeweka utaratibu wa kutangaza Shule na Vyuo ambavyo vimeshasajiliwa wazi ili kuondoa tatizo hili ambalo ni mzigo mkubwa kwa wazazi, ukizingatia wanakuwa wameshalipa karo za watoto wao.

Mheshimiwa Spika, langu ni hilo tu. Namwomba Waziri na Wataalam wake waweze kufanikiwa katika haya yote waliyoyapanga na tutawapa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuelezea machache niliyo nayo katika kuchangia hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni - Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa hotuba yake nzuri sana yenye kuonyesha dira sahihi katika kulitoa Taifa katika Ujinga, Umaskini na hata Maradhi. Lakini wakati huo huo natoa pole nyingi sana kwa Naibu Waziri - Mheshimiwa Bujibu Sakila, kwa maradhi yaliyodhoofisha sana hali ya afya yake na uwezo wake wa kufanya kazi. Naomba kwa Mungu aendelee kumsaidia azidi kupona na kumwondolea kabisa ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Elimu, yanaonekana wazi na yanastahili sifa kemkem kutoka kwa wananchi. Utaratibu shirikishi wa uandaaji wa mipango ya elimu, utekelezaji wake na tathmini ya utekelezaji, ni mfano wa kuigwa na sekta nyingine zenye kuhudumia jamii. Si hivyo tu, Wizara ya Elimu imetupa fundisho la utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado matatizo yapo, bado lipo tatizo la autoaji wa elimu kwa uwiano sahihi kwa maeneo na makundi mbalimbali ya Watanzania. Mikoa inapishana na Wilaya zinapishana katika maendeleo ya elimu. Iko mikoa iliyo mbele sana na wilaya zilizo mbele sana, na mikoa iliyo nyuma na wilaya zilizo nyuma. Ingefaa mwaka hadi mwaka, Taarifa kamili ionyeshe tofauti hizo ili mikoa iliyo nyuma na wilaya zilizo nyumba, zibainishwe na kutangazwa - ijulikane nchi nzima ili taarifa hizo ziwe changamoto kwa mikoa na wilaya zilizo nyuma ziongeze juhudimaradufu kukimbia badala ya kutambaa kuzikaribia wilaya na mikoa iliyotangulia.

Mheshimiwa Spika, suala la Elimu ya Wasichana katika ngazi zote, liwekewe mkakati maalum, na ikiwezekana wasichana wapatiwe muda wa ziada wa kufundishwa masomo muhimu ya Hisabati, Lugha - kwa maana ya Kiingereza, Kiswahili na Sayansi. Kama tunavyoelewa, Hisabati ndilo somo maalum linalomfundisha mwanafunzi kufikiri na kurahisisha au kuwezesha ujasiliamali. Lugha ndiyo ufunguo wa elimu nyingine, na inahitajika katika kujifunzia masomo mengine yote. Na Sayansi ndiyo msingi wa teknolojia. Ili binadamu aweze kutawala mazingira yake na kufanya kazi kwa ufanisi, anahitaji ufundi wa kisayansi na ujuzi wa kufanya kazi zenye kumletea maendeleo. Sheria ya *The Primary School (Compulsory Enrolment and Attendance) Rules 2002,* iwabane vilivyo wasichana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Kilosa bado tuko nyuma kielimu. Kwa sensa ya mwaka 2002, Wilaya ya Kilosa ina wakazi 489,513; Tarafa 9, Kata 37, Vijiji 161 na Vitongoji zaidi ya 500. Lakini tuna Shule za Sekondari 12 tu. Kati ya hizo, 10 ni za Serikali, moja ya Jumuiya ya Wazazi na moja ya Shirika la Dini. Ziko Tarafa mbili - ya Nongwe na Kidete, hazina sekondari hata moja. Tuna Shule za Msingi 182. Wizara itupie macho Wilaya ya Kilosa, na tunaomba Waziri atutembelee.

Mheshimiwa Spika, nina ombi maalum kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa ajili ya Shule ya Sekondari Nongwe, tunayoijenga kwa nguvu za wananchi. Tayari tumekwisha kujenga madarasa manne, nyumba za Walimu 4 na tunakamilisha hosteli kwa ajili ya wanafunzi wasichana. Tunaomba sana Wizara itupe kibali cha kuifungua Sekondari ya Nongwe (mwaka huu wa 2004) ili iweze kuwachukua wanafunzi watakaofaulu mtihani wa Darasa la 7 mwaka huu. Bado wananchi wa Tarafa ya Nongwe wana ari ya kuendelea kujenga majengo zaidi. Na jengo la Maabara nalo limo katika kukamilishwa. Tatizo kubwa ni kupata vifaa vya maabara. Naiomba Wizara itusaidie kupata vifaa vya maabara.

Mheshikiwa Spika, tatizo lingine kubwa ni Walimu kukwepa kwenda kufanya kazi kwenye shule vijijini. Inafaa Wizara itoe tamko rasmi la kuwachukulia hatua kali kama si kuwafukuza Walimu wanaokataa kwenda kufundisha vijijini.

Mheshimiwa Spika, juhudi kubwa na mafanikio makubwa katika elimu, yanagubika suala la utamaduni na kufanya suala la utamaduni lisipewe uzito unaostahili. Utamaduni wetu ndio unaotutofautisha na mataifa mengine. Utamaduni unategemea sana kiwango cha ufundi wa kisayansi na ujuzi uliofikiwa na jamii. Utamaduni wetu ndio pia

msingi wa kufanya kazi na jinsi ya kufanya kazi yenyewe na kutuwezesha kutawala mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wetu wa mambo na taratibu zetu za kuendesha maisha, ndiyo utamaduni wenyewe. Hivyo basi, iko haja kubwa kutambulisha waziwazi kwa jamii, mila, desturi, lugha, sana, burudani na itikadi zinazomtambulisha Mtanzania kutoka kwa mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuendesha Tamasha la Vazi la Taifa kama sehemu ya utamaduni wetu. Malezi toka utoto hadi uzeeni katika maadili ya jamii, lazima yasimamiwe kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati tulio nao, mila na desturi potofu zinachangia sana katika kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI. Mila na desturi potofu, na mila na desturizilizopitwa na wakati na zinazokwamisha maendeleo, lazima zipigwe vita na kutokomezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia kumpongeza Waziri na Wasaidizi wake wote katika Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED ABDULY ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu mradi wa MMEM. Nakubali kwamba umekuwa ukitoa maelezo mengi kuhusu fedha MMEM upande wa Zanzibar. Na sisi Kamati sote tunafaidika. Lakini walio wengi hawafaidiki. Je, Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana kwa heshima na taadhima, naomba utoe maelezo ili wananchi wote waelewe na masikitiko kuwa Zanzibar hawafaidiki.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mpango wa MMES. Je, Zanzibar watafaidika vipi na mpango huo? Nategemea ufafanuzi wako.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwana kabisa napenda kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii kwa uvumilivu wao mkubwa wa matatizo ambayo yamewakumba muda mrefu. Waswahili wanasema "Mvumilifu Hula Mbivu". Haya ndiyo matunda ya kuvumilia hali mbaya waliyokuwa nayo kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Mawaziri wote wa Elimu kwa kubuni mbinu na mikakati ya kuendeleza elimu katika Taifa letu. Nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu, Geita imedhamiria kuongeza elimu kwa kuwasomesha vijana wake wote waliofikia umri wa kwenda shule, wamepata elimu hiyo. Pia kwa kuona kuwa tatizo kubwa ni kutokuwa na vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu pamoja na Shule za Sekondari. Wananchi wameamua kwa moyo mmoja na wa kujitolea nguvu na mali zao, kujenga Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Geita mpaka sasa ina maboma ya madarasa na nyumba za Walimu, yapatayo 800 tiu. Haya yote yemejengwa kwa nguvu za wananchi. Pia Wilaya ya Geita imeamua kujenga sekondari. Mwaka huu tu tumefungua Shule 7 za Sekondari, na mwakani yapo maboma yanatosheleza Shule za Sekondari 21. Majengo yote yako tayari kwa kiwango renta.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba Wilaya ya Geita ipewe kipaumbele cha kupewa fedha za MMEM na MMES. Kwa kuwa kutowapatia kutawavunja moyo wananchi hawa ambao kwa kweli wamejitolea vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kiasi cha Shs. 4.4 bn./= kwa ajili ya mpango wa MMEM. Kwa upande wa MMES, walikuwa bado hawajapata maelekezo ya gharama za majengo. Hivyo, naomba Shule za Sekondari 21 zinazoendelea kujengwa na wananchi, basi zipewe fedha ili ifikapo mwakani 2005 zifunguliwe.

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natoa shukrani zangu za dhati kwa jinsi ya hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni - Mheshimiwa Joseph Mungai (Mb.), kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kutamka wazi na kuwashukuru Watendaji wa Wizara hiyo wanaoongozwa na Bi Mwantumu Malale - Katibu Mkuu mahiri, ambaye amesaidiana na Waziri, kuleta maendeleo ya Elimu katika awamu hii na kuweza kutekeleza kwa dhati Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2000 - 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hiyo, naomba kutoa maoni yangu kwa upande wa Wizara hii kama ifuatavyo. Kuna haja Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia Idara ya Utamaduni, kuangalia mambo. Kama inavyoeleweka kwamba utamaduni ni kielelezo cha utashi wa maisha ya kila sikun ya mwanadamu, hivyo basi Idara ya Utamaduni inapopaswa kuangalia jinsi ya utamaduni wa Mtanzania ukiwa hatarini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoeleweka kwamba Tanzania inavyo vombo vya habari vingi sana vya Serikali na vinginevyo vya watu binafsi. Vipindi vingi ambavyo vinaonyeshwa katika *TV* za Taifa na za Watu Binafsi, havilingani na utamaduni halisi wa Mtanzania, na havitoi mafunzo kwa vijana wetu. Vyombo hivyo vimeelemea utamaduni wa kigeni, aidha utamaduni wa Mashariki au Magharibi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ngoma zetu za asili wakati zikionyeshwa katika vyombo vya *TV* za hapa nchini, hazina uasili wake. Badala yake utasikia zimeboreshwa au kutoholewa na kushtukia zinabadilika sana maana yake. Pia vivazi ambavyo vinatumiwa siyo yale mavazi ya asili.

Mheshimiwa Spika, filamu zote ambazo zinaoneshwa katika *TV* zote, sijui kwamba zinaangaliwa na Bodi ya Filamu na kuruhusiwa kuonyeshwa ndani ya vyombo hivyo. Kama haifanyiki hivyo, naomba juhudi zichukuliwe ili zikaguliwe na kupewa kibali, ili kulinda maadili ya Taifa letu.

Kuhusu Makumbusho ya Taifa. Kwa muda mrefu sasa Tanzania imekuwa na Kumbusho Kuu la Taifa, ambalo lipo Dar es Salaam. Na pale Arusha, tuna Kumbusho la Azimio la Arusha. Nahisi ipo haja ya kufikiria kuwa na Makumbusho kwa kuazima takwimu na Makumbusho Kikanda. Kwa mfano, Kanda ya Kati - ikiwemo Dodoma, Kanda ya Kusini - likawepo Mtwara, Kanda ya Kaskazini - likakuzwa lile la Arusha.

Mheshimiwa Spika, kuhifadhiwa barabara iliyokuwa ikitumiwa kwa Biashara ya Utumwa na kuwekewa kitambulisho chake maalum ili iwe inajulikana barabara hiyo inatoka kuanzia Bagamoyo, Singida, Tabora hadi Kigoma. Kuhifadhi barabara hii, tutawapa vijana wetu kuelewa historia ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Makumbusho itoe taaluma kwa wananchi, namna ya kuhifadhi maandishi au maandiko ya zamani. Maandishi ambayo yamo majumbani kwa muda mrefu sana, pengine maandishi hayo mengine yameweza kufikia miaka 80 - 100.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mungai - Wasiri wa Elimu, na Naibu wake - Mheshimiwa Sakila, pamoja na Katibu Mkuu - Ndugu Malale, kwa kazi nzuri wanayoifanya kiasi kwamba ni miongoni mwa Wizara chache ambazo kazi zake zinaonekana. Siyo lazima uambiwe tazama.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mungani kwa kuanzisha mpango wa MMES kwa shabaha ya kuimarisha Elimu ya Sekondari. Mpango huu utasaidia kuleta uwiano mzuri wa wananchi wanaomaliza Elimu ya Msingi, kupata nafasi ya kuendelea na Elimu ya Sekondari. Vinginevyo, kuendelea na mpango wa MMEM, dira ya mpango wa MMES ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu, hasa ikizingatiwa kuwa wanaomaliza Elimu ya Msingi wana umri wa miaka 14 au 15. Hawana uwezo wa kufanya lolote.

Mheshimiwa Spika, ni vema mpango huu usimamiwe vizuri na kuimarishwa, ili vijana wengi wapate Elimu ya Sekondari. Pamoja na hali hii, bado upo umuhimu wa kuangalia upya ili Elimu ya Msingi imalizie *Form II* au *Form III,* kuwawezesha vijana watakaomaliza darasa hilo watakuwa na umri wa miaka 17, na hivyo kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida na hasa Wilaya ya Singida, ipo nyuma sana kielimu. Mwaka jana, Mkoa ulikuwa wa 20 kwa matokeo ya wanafunzi waliomaliza Darasa la 7 - aibu. Tunajiuliza, pamoja na hatua nzuri za kuwa na mpango wa MMEM, lakini tunakuwa mkoa wa 20 - kulikoni!!!

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba uongozi wa Serikali wa Mkoa na wa Wilaya, wametakiwa kufanya tathmini ili kujua tatizo liko wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ifanye tathmini ya kitaalam, kwani ni kwa miaka mitatu sasa, Mkoa wa Singida unakuwa wa mwisho, ili baadaye Wizara itusaidie kutujulisha tatizo ni nini na kasha kurekebisha tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tathimi yangu ni kwamba tatizo kubwa ni uhaba mkubwa wa Walimu katika shule zetu. Kwa mfano, Shule za Msingi za Matare, Nkhoiree, Mahambe, Ikuwa, Mnanga na Sepuka, zina upungufu mkubwa wa Walimu. Vipi Mwalimu Mkuu atawapanga Walimu 8 (Maatare) kati ya Walimu 21 wanaohitajika, au atawapanga vipi Walimu 7 kati ya Walimu 16 wanaohitajika, na ukategemea shule hiyo ikatoa watoto kwenda Sekondari? Haiwezekani asilani.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa wazazi watakata tamaa ya kuwasomesha watoto wao hapo shuleni kwa vile shule kadhaa hakuna hata mtoto mmoja anayechaguliwa kwenda Sekondari mwaka hadi mwaka. Hivi Mheshimiwa Waziri una mpango gani na shule kama hizo ambazo miaka mitatu hadi mine hachaguliwi hata mwanafunzi mmoja kwenda Sekondari. Lile agizo lako la kuwatahini Walimu husika kwa mtihani wa Darasa la 4 limefika wapi?

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, ya kuanzisha mpango wa MMES na shabaha zake, ni nzuri. Lakini tatizo litajitokeza katika kugawa wapi shule mpya zijengwe, kwani kule kwenye shule nyingi au mikoa na wilaya zenye shule nyingi za Sekondari, zitaongezewa zaidi na kuachwa Wilaya ya Singida ambayo ina shule chache sana za Sekondari za Serikali, pamoja na za wananchi - kwa maana ya kufuata usemi wa Kitabu Kitukufu cha Biblia kuwa mwenye nacho ataendelea kuongezewa, na yule asiye nacho atanyang'anywa ha kuongezewa yule mwenye nacho.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Wazairi Mungai atekeleze kwa dhati yale aliyoyaeleza katika ukurasa wa 20, kifungu (a) na vile vile ukurasa wa 21, kifungu (a) na (b). Namwomba sana Mheshimiwa Waziri na wenzake, watusaidie sisi wa Singida hasa Singida Kusini katika Kata za Isuna, Ntuntu, Ngungira na Misughaa, zipatiwe mgao wa kujengewa Shule mpya za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa Walimu wa Sekondari nao ni tatizo, hasa Walimu wa Sayansi. Pamoja na kufika Wizarani na kuonana na Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari kuhusu ombi la Walimu hasa wa Sayansi kwa Shule ya Sekondari ya Sepuka, lakini hadi leo hii hakuna lolote. Kulikoni Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Mungai unafanya kazi nzuri sana katika Wizara hii. Nakupongeza sana, naomba haya niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Joachim Chissano wa Msumbiji - Mwenyekiti wa *AU* anayemaliza Uenyekiti wake, kwa kutoa hotuba nzuri kwa lugha ya Kiswahili huko Addis Ababa, licha ya kwamba Kiswahili siyo lugha yake ya kuzaliwa nayo. Mwenyekiti huyo wa AU ametoa changamoto kubwa kwa Afrika na hasa Tanzania ambako Kiswahili kilizaliwa na kukua. Nashauri Serikali ichukulie Kiswahili kama bidhaa ya kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waende kueneza Kiswahili kama vile Wazungu na Waarabu walivyoeneza dini ya Kikristo na Uislamu. Tusisubiri hadi Wanigeria waje kufundisha Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Zipo tetesi kuwa Rais wa sasa wa *AU* - Mheshimiwa Obasanjo wa Nigeria, ameanza kuzungumza Kiswahili. Kwa ushauri, ni vizuri masomo ya *Arts* kama vile ya Historia, Jiografia na Uraia, yangeanza kufundishwa ngazi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, napenda niunge mkono hoja hii kwa sababu Wizara imetekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2000 kwa vitendo. Wilaya ya Mbinge ni moja kati ya wilaya ambazo zimebadilisha kabisa sura za majengo ya Shule za Msingi kwa mpango wa MMEM.

Mheshimiwa Spika, gharama za kununua vitabu vya ziada na kiada, zinakuwa kubwa zaidi kadri unavyoenda mbali na Dar es Salaam. Kwa hiyo, ili uwiano wa vitabu kwa wanafunzi uwe sawa kwa nchi nzima, ni budi suala la usafirishaji wa vitabu likazingatiwa. Vinginevyo, shule zilizopo pembezoni zitanunua vitabu pungufu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, imeangalia maeneo mengi, isipokuwa elneo la Elimu ya Awali. Elimu ya Awali ni kitangulizi muhimu. Kwa kuwa hakuna mtoto anayeweza kutembea ama kukimbia kabla ya kutambaa. Nashauri uboreshwaji wa Elimu ya Msingi uanzie na Elimu ya Awali, na hili jukumu lisiachwe hivi hivi - kila mtu na mtazamo wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wasiri atatuambia kama upo mtaala wa Elimu ya Awali, na kama kweli unafuatwa. Je, upo ukaguzi katika shule hizo? Baadhi ya Walimu niliwahoji wanasema wanatumia uzoefu. Watoto wanafundishwa alfabeti, wanafundishwa kuandika majina yao, kuhesabu na kucheza. Wengine wanatumia muhtasari wa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Shule za awali ni chache kuliko Shule za Msingi; na nyingi ziko mijini. Kwa ujumla Walimu wenye ujuzi ni wachache sana. Kwa hali ilivyo, piramidi ya elimu inaweza isiboreke kama Elimu ya Awali haitapata msukumo wa MMEM na MMES.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango wa MMES. Lakini ili mpango huo ulete matunda yanayokusudiwa, sharti tuangalie mapungufu ya Elimu ya Sekondari hasa kwenye shule za wananchi - *Community Secondary Schools* ambazo ni nyingi. Shule hizo zimejengwa kama shule za kutwa, lakini *catchment area* hasa katika maeneo ya mashambani kwa mfano Wilaya ya Mbinga, wanafunzi hutumia zaidi ya masaa matatu kwenda. Kwa hivyo, huchelewa masomo na kufanya vibaya kwenye masomo yao. Nakubali utaratibu wa kujenga hosteli, lakini utaratibu mzuri ungekuwa ni kuwa na shule za bweni kwenye maeneo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Wilaya ya Mbinga kabla ya kumalizika kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nasema tena kuwa naunga mkono hoja hii.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, ninataka kwanza nitamke kuwa naunga mkono hoja asilimia 100%.

Mheshimiwa Spika, nina mambo yafuyatayo ya kuchangia. Kwanza, Wilaya yangu ya Geita ina watu wengi zaidi ya laki saba, kwa sensa ya mwaka 2002. Tuna watoto wengi ambao wako Shule za Msingi. Tunahitaji Walimu wengi sana. Wizara inatupangia Walimu, lakini wengine hawaripoti kazini.

Mheshimiwa Spika, kwa kujua hilo, sisi Wabunge wa Geita (Busanda, Nyanghwale na Geita), tumeishaleta majina ya vijana Wizarani waliomaliza *Form IV* ili wapangiwe Vyuo vya Ualimu; na kwamba wakishafuzu waje wafundishe huko kwenye mazingira yao, kitu ambacho wako tayari. Tulipeleka majina hayo kwa Mkurugenzi wa Mafunzo ya Ualima (Mama Masenga) kupitia kwa Msaidizi wake Ndugu Binde mnamo mwezi Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, awali tulikuwa tumepewa ushauri huo Wizarani hapo kuwa ni vema tukapata vijana wa maeneo yetu ambao wako tayari kufundisha huko baada ya Walimu wahitimu kutopenda kufanya kazi huko. Kwa hiyo, tulihamasisha vijana hao na wazazi wao. Tunaomba Wizara iwapatie mafunzo vijana hao ambao tayari sisi tumeji-commit, ambnapo pia kwetu ni dosari kisiasa endapo hawa hawatafikiriwa kupata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, tunajua utaratibu wa kupata Wanavyuo umebadilika, na kwamba sasa Wanavyuo wanachukuliwa moja kwa moja kutoka shuleni. Pamoja na hayo, utarawtibu huu ulikuja nyuma, sisi tukiwa majimboni tukitafuta hayo majina tuliyowaletea. Tunaomba sana vijana hao wafikiriwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa MMEM. Tumehamasisha wananchi wetu, wameitikia na wametutuma tuiombe Wizara itupatie jumla ya Shs. 4.4bn./= kwa ajili ya maboma ya ya madarasa 620 na nyumba za Walimu 230. Wananchi wetu watavunjika nguvu sana iwapo maboma haya hayatakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa MMES. Tuna maboma katika Sekondari 21, ambayo ni pamoja na madarasa, nyumba za Walimu, Maabara, majengo ya Utawala na vyoo. Hili nalo tuliwapa moyo kuwa kuna mpango wa MMES, wakajituma.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wana-Geita, Waziri wa Elimu atuangalie sana kwa maombi/masuala haya matatu. Ninaomba kuwasilisha.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Ninaiunga mkono asilimia 100%.

Wizara hii ya Elimu na Utamaduni ndiyo msingi wa mwanzo muhimu wa Taifa letu la Tanzania na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama wanavyosema Wataalam mbalimbali duniani kuwa msingi mkuu wa maendeleo na uchumi wa nchi yoyote ile hapa duniani, ni elimu. Bila ya kuwa na elimu, huwezi kufikia maendeleo ya kweli katika maisha na maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Wizara hii zinaonekana katika nchi yetu, hasa katika mipango ya shule za Msingi, ambapo mradi wa MMEM. Matumaini yangu ni kuwa na mpango wa Shule za Sekondari nchini (MMES) utasimamiwa na kuimarishwa kama ulivyobuniwa kwa faida na maslahi ya nchi yetu na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 42 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unaelezea sehemu ya Elimu dhidi ya UKIMWI. Kwa kweli Wizara ninaiomba iendelee kutoa semina na hata miongozo sehihi kwa Walimu na wanafunzi wote nchini juu ya tatizo hili la janga la UKIMWI. Walimu ni sehemu muhimu sana kwa Taifa letu. Kwa hivyo, ni vizuri kuwa na hadhari sana na majanga kama haya yenye kuhatarisha maisha ya Watanzania na hatimaye kuangamiza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 56 wa hotuba, unaelezea Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Napenda kulipongeza sana Baraza letu hili muhimu kwa usimamizi wa majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa nchini petu Tanzania. Na kwa bahati nzuri hivi karibuni, Umoja wa Afrika *(AU)* umeamua kutumika Lugha ya Kiswahili katika kikao chake ambacho hivi sasa kinaendelea huko Addis Ababa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio haya makubwa ambayo lugha yetu hivi sasa imefikia, ni mpango gani ambao Serikali yetu imeuandaa juu ya lugha hii ya Kiswahili hasa baada ya miezi ya hivi karibuni, palikuwepo mvutano wa vipi lugha ya Kiswahili inaweza kutumika katika masomo ya Sekondari na Vyuo vyetu nchini?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hivi sasa imefika wakati wa kuona na kuithamini lugha yetu ya Kiswahili, hasa baada ya mafanikio haya makubwa ambayo Umoja wa Afrika umeamua kuiweka lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi katika Umoja huo.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya hivi sasa wanafundisha lugha ya Kiswahili katika Vyuo vyao Vikuu. Kenya wanayo sera ya kufundisha Kiswahili katika shule zao za Msingi, na wamesema kuwa hivi sasa Kenya hawana tatizo la Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwa kweli, lugha ya Kiswahili imeleta umoja katika nchi yetu ya Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa ujumla. Lugha ya Kiswahili inazungumzwa nchi nzima hapa nchini petu Tanzania, na kwa kweli imefanikisha kujenga umoja wa kitaifa na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nataka muungane na wasomi nchini kufuatia mapendekezo yao waliyoyatoa katika kongamano lao lililofanyika hivi karibuni kuhusu lugha za Tanzania kuwa Kiswahili kitumike katika kusaini mikataba ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mbali ya wasomi hawa, mbali ya Umoja wa Afrika kuamua kutumia Kiswahili katika Kikao chao cha Addis Ababa na pia mbali ya Kenya hivi sasa kuwa na sera ya kufundisha lugha ya Kiswahili katika Shule zao za Msingi, pia kwa mujibu wa vyombo vya habari (magazeti) vinasema kuwa mtandao wa kompyuta kuwa wa Kiswahili Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu vyombo hivyo vya habari, vinasema kuwa Kampuni ya *Microsoft* inatarajia kuingiza lugha ya Kiswahili katika programu zake za kompyuta, ikiwa ni harakati za kampuni hiyo kuongeza idadi ya wateja wake. Pia imeelezwa kuwa watafanya tafsiri ya programu hiyo katika lugha ya Kiswahili, kumelenga kuongeza watumiaji wa programu hiyo kwa nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, kupitia vyombo hivyo vya habari, tumeelezwa kuwa Kiswahili kinatarajiwa kutumika kwenye programu mbalimbali za kompyuta, ikiwa ni sehemu ya mpango wa dunia katika kuongeza matumizi ya kompyuta duniani. Katika kulifanikisha hili, tunaona kuwa kompyuta ya *Software Giant* imekubali kutafsiri maneno yake yaliyoko kwenye *Office Software* kwa lugha ya Kiswahili ili yasambazwe kwa ajili ya kuongeza idadi ya watumiaji wa kompyuta Afrika.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwa kiasi gani wenzetu ndani ya Afrika wanavyojiandaa kutaka kutumia lugha ya Kiswahili katika suala zima la kimaendeleo, ambapo msingi wake ni Umoja.

Mheshimiwa Spika, nina imani kuwa Serikali yetu itaona umuhimu huu nambao sisi wenyewe tulikuwa tunaonyesha kuudharau.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii, na pia naipongeza kwa dhati Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika katika kuendeleza elimu hasa kupitia mpango wa MMEM, na sasa unakuna mpango wa MMES.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo maoni yafuatayo yenye lengo la kuboresha zaidi Elimu yetu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi kiimarishwe (Manyoni). Wilaya ya Manyoni tunazo Sekondari za Serikali 6 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Moja ya tatizo kubwa sana linalozikabili Sekondari hizo ni upungufu mkubwa wa Walimu wa Masomo ya Hisabati, Fizikia, Kemia na *Biology.* Sekondari za Sanza, Chikuyu na Kilimatinde, baadhi ya masomo hayo hayafundishwi kabisa kutokana na kukosekana kwa Walimu wa masomo hayo. Kupitia mpango wa MMES, tumeelezwa kuwa unalenga kuongeza idadi ya Walimu. Hizi ni habari nzuri. Hivyo, Wizara itakapoanza kusambaza Walimu wapya, kipaumbele kiwe Wilaya ya Manyoni, kiwe ni Walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la Sekondari za *O'Level* na *A'Level* (Manyoni). Kama nilivyoeleza awali, tunazo Sekondari 6 (moja kwa kila Tarafa); hazitoshi, na baadhi ya wanaofaulu Darasa la 7 wanakosa nafasi. Hivyo, chini ya MMES, tunaomba maeneo *under-served* kama Manyoni tupewe kipaumbele. Wananchi wapo tayari kushiriki katika ujenzi. Wilayani pia hatua Sekondari inayotoa masomo ya *A'Level (Form V and VI).* Chini ya MMES, tunaomba Wizara iruhusu tuanzishe mikondo ya *A'Level* katika shule moja au mbili Wilayani.

Mheshimiwa Spika, narudia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Nashukuru sana kwa Mheshimiwa Waziri kutuunga mkono watu wa Manyoni wakati wa Harambee ya kuchangia ujenzi wa *Hostel* za Wasichana tarehe 5/6/2004. Tunaheshimu msaada wa Wizara wa kutujengea moja Sanza Sekondari,mahali ambako *drop rate* ya msichana ni kubwa mno na inasikitisha mno. Ujenzi wa *hostel* hiyo itarekebisha dosari hii. Mungu awe nanyi.

**MHE. BALOZI GEORGE C. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai (Mb.) kama Kiongozi wa Wizara, na Wasaidizi wake.

Mheshimia Spika, kama yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri alivyotamka katika hotuba yake kwamba mpango mkubwa kama huu wa maendeleo ya elimu katika Tanzania haujawahi kutokea tangu tupate uhuru, ni kweli kabisa. Mimi nauona kama ni Mapinduzi makubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunataka Mapinduzi haya muhimu yafanikiwe, napenda nitue ushauri mdogo ufuatao. Wizara ianzishe *Management Unit* katika

Wizara ya kuongeza *efficient management* ya mpango huu *in every aspect (financial technical and quality output).*

Mheshimiwa Spika, *Inspection Directorate* za Wilayani ziendeshwe na Wataalam wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha na ikiwezekana wataalam hao wapewe mafunzo *(crash programme)* ya menejimenti kabla ya kuanza kazi, na tathmini ya kazi zao ifanywe mara kwa mara, kusudi wale ambao watabainika kwamba hwana uwezo wabadilishwe. Hii *Management Cadre* ilipwe *special salaries,* kusudi wasishawishike na rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika yote haya, jambo la kusisitiza liwe ni *quality* ya *output* bila kusahau kuandika na kuongea lugha ya Kiingereza kwa ufasaha. Natazamia lazima wakumbushwe kwamba sasa tunaishi katika dunia ya ushindani, siyo katika *EAC* na *SADC.* Lakini duniani kote kwenye mazingira ya *survival of the fittest.*

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia kwa mia. Zaidi ya hayo, nina maoni mawili ya pekee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shule ya Sekondari ya Sasawala - Wilayani Namtumbo. Hii ni shule ya Sekondari pekee ya Tarafa ya Sasawala, iliyoko Kijijini Lusewa - karibu na mpaka wa Tanzania/Msumbiji. Nimeomba shule hii ikaguliwe, na wamepeleka Wakufunzi kuikagua. Shule in *Form I* hadi *Form IV* ina watoto wanaosoma katika shule hii ya wazazi. Wengi wa wazazi hao ni fukara sana. Hivyo, ile ada wanayowalipia watoto wao - inayozidi Shs. 100,000/= kwa mwaka kwa kila mtoto, inawashinda sana.

Mheshimiwa Spika, tayari nimepata msaada toka Japani - wa Shs. 23m./=, wa kujengea bweni la wasichana. Bweni la vijana wanaume lipo. Hata hivyo, naomba shule ichukuliwe na Serikali Kuu ili vijana hawa wafaidi kupunguziwa ada katika Shule za Serikali. Pia naomba Walimu wapewe mafunzo ya Ualimu *Pedagogy* ili kuwawezesha kuinua ubora wao wa kufundisha. Tafadhali shule ya Sekondari ya Sasawala ichukuliwe na Serikali mwaka huu wa 2004. Sehemu hii wanaishi wananchi walio katika eneo lililo mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya na Mkoa. Aidha, hali ya uchumi katika eneo hili ni duni, hali ambayo inasababisha watoto kuwa *disadvanged.* Nyumba za Walimu chache zipo, na tunaendelea kujenga kwa *self-help.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shule ya Sekondari ya Namabengo - Wilayani Namtumbo. Hii ni Shule ya Sekondari ya Serikali, ina madarasa F*orm 1 - Form IV.* Nyumba na Ofisi za Walimu zipo. Mabweni ya vijana wanaume na wanawake, yanakamilika Agosti, 2004. Tunayo maabara na vyumba vya ziada za *Form V* na *Form VI.* Tayari nimepata fedha za kukamilisha ujenzi wa Hall ya kufanyia mitihani na mikutano.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba shule hii isajiliwe pia *Form V and Form VI* ili hapo mwakani 2005, tuanze masomo ya *High School* ya Wilaya mpya ya Namtumbo.

Hadi sasa Wilaya ya Namtumbo haina *High School.* Tutashukuru sana iwapo Namabengo itapata hadhi hii ya *High School* kwa kuanza na *Form V* hapo 2005. Shughuli na majenzi yanayohusika, zinakamilika kiangazi hiki cha 2004.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mmheshimiwa Spika, kwanza niunge mkono hoja hii kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba yake nzuri. Hotuba hii ya bajeti ni ya kuondoa kabisa moja ya maradhi yaliyokuwa yanatukabili Watanzania, yaani adui Ujinga.

Mheshimiwa Spika, kama tujuavyo kwamba ili Taifa hili liendelee , Elimu ndiyo ufunguo na Elimu ni usukani. Hivyo, ninaendelea kumpongeza sana kwa kupunguza karo ya Sekondari kutoka Shs. 40,000/= na kubakia Shs. 20,000/=. Kwa kufanya hivyo, tutafanya kila mzazi amudu kabisa kumlipia mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote hayo mazuri ambayo Wizara imeyafanya, lakini lipo tatizo kubwa la kuwakatisha tamaa baadhi ya Watoto, Wazazi na Shule za Sekondari husika hasa pale Serikali inapositisha/kufuta matokeo ya mitihani. Kwa mfano, zipo shule kadhaa za Sekondari zilifutiwa/kusitishwa matokeo aidha kutokana na zababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala hili limechukua muda mrefu hasa katika Shule ya Sekondari ya *St. Methew* iliyoko Kongowe - Mkulanga. Tume imeundwa ichunguze, lakini imechukua muda mrefu mno kutoa matokeo. Hii inawafanya wanafunzi husika kuathirika ki- saikolojia, kwani hawaelewi uchunguzi utasemaje. Lakini si hivyo tu, wazazi wa watoto hawa nao hawaelewi nini cha kufanya kwa watoto wao.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up*, atoe tamko nini hatima ya wanafunzi hao, kwani kipindi cha kuanza Kidato the 5 kimeanza sasa. Na hii leo wazazi na wanafunzi wa *St. Mathew* wanatarajia lolote kutoka kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Wasiri pamoja na Naibu Waziri wa uongozi bora ambao wanaendelea kutoa katika sekta hii ya elimu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu - Ndugu M. Malale, kwa kazi nzuri wanayofanya katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, alipokuwa anawasilisha hoja ya Waziri, Mheshimiwa Joseph Mungai alieleza kwa ufasaha juu ya kudorora kwa uandikishaji watoto waliofikia umri wa kwenda shule katika mikoa mitano, Lindi ukiwa ni mmoja wa mikoa hiyo. Mikoa

hiyo imeshindwa kufikia asilimia 100% ya idadi ya watoto wa rika lengwa *(Gross Enrolment Ratio - GER).*

Mheshimiwa Spika, wakati naipongeza mikoa ambayo imepita asilimia 100% ya uandikishaji, nina wasiwasi na takwimu kama zilivyotolewa katika kielelezo 7.2. Hapa imeonyesha idadi ya watoto wenye umri wa miaka 7 - 13, na idadi ya wanafunzi wa Darasa la I - VII. Takwimu hizi zina utata. Itakuwaje idadi ya wanafunzi wa Darasa la I - VII inakuwa kubwa kuliko idadi ya watoto wa miaka 7 - 13? Watoto hawa ziada wametoka wapi? Pengine inawezekana takwimu ambazo Wizara inazo zinapishana na takwimu zilizotolewa na *population census* ya mwaka 2002. Ni vyema pawe na *consistence* katika takwimu ili wahusika waweze kulenga sawasawa mikakati ya kusahihisha udhaifu uliojitokeza katika kufikia malengo ya *enrolment* ili kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule, wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi mbalimbali ambayo Mheshimiwa Waziri ameionyesha katika hotuba yake, ni ya kupongezwa kwa vile yhote hiyo imelenga katika kuboresha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari kwa Watanzania wote. Hongera sana kwa hili. Rai yangu ni kwamba katika kutoa fursa sawa kwa mikoa na wilaya zote na kuhakikisha kuwa hakuna wilaya zinaachwa nyuma katika haki ya kupata elimu kama Katiba ilivyobaini, miradi hii isambazwe nchi nzima. Isionekane kuwa mikoa fulani inapendelewa kwa vile mtandao wa miradi hiyo hulengwa kwenye mikoa/wilaya zile zile karibu mara zote!

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuipongeza Kamati ya Huduma za Jamii kwa mchanganuo wao wa hotuba hii, hususan katika masuala ya nidhamu kwa Walimu, ambayo imekuwa kero sugu. Mathalan, Walimu wanaowatia mimba watoto wa shule, ni lazima waadhibiwe mara moja kwa kufukuzwa kazi. Hali ya sasa kuleana kwa kutokuchukua hatua zozote dhidi yao, zinazidi kuendeleza tatizo hili sugu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, mia kwa mia na kumhakikisha ushirikiano wangu katika kutekeleza majukumu yake.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kuanzia, kutoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni (Mnyalukolo) pamoja na timu yake kwa kazi nzuri inayoifanya, husuan chini ya mradi wa MMEM na MMES.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuiomba Serikali iangalie kwa umaskini wa pekee, kuondokana na Elimu ya Msingi ya miaka saba, na hapo kuwa ni mwisho wa vijana wengi kuendelea kusoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa ihakikishe kuwa Shule za Msingi zinapanuliwa na kuendelea mpaka Darasa la 12 (kumi na mbili) kama nchi nyingine za *SADC* zinavyofanya. Elimu ya Msingi ni finyu sana na mtoto anayemaliza Darasa la 7 ni bado mtoto sana (ni wa miaka 11 tu).

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi ni sawa na Viwanda vinavyotoa vijana wanaojua kusona na kuandika tu. Matokeo yake ni kwamba hawa watoto wadogo wanakuwa ni mzigo tu kwa jamii. Hivi hawa vijana wa kundi hili wanategemewa wafanye nini? Wazurure au wawe Machinga?

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa iangalie uwezekano sasa wa kubadili mitaala yake katika Shule za Msingi. Wanafunzi wa madarasa ya kwanza na pili wamerundikiwa masomo ambayo ni vigumu kwa mtoto wa darasa la kwanza kuelewa.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji *quality education*, na siyo kujaza madarasa yenye Walimu ambao wao wenyewe hawana elimu ya kutosha. Walimu wanahitaji kupatiwa elimu za kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, naishauri tena Serikali kupitia Wizara hii kuwa Shule za Msingi zifundishe lugha ya Kiingereza. Umuhimu wa Kiingereza hauwezi kubishiwa, kwani Serikali yetu inatumia lugha hiyo. Tanzania haiwezi kuingia katika utandawazi ikitumia lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, leo hii vijana wanaomaliza *Form IV* hawawezi kuelewa na kuzungumza lugha ya Kiingereza. Hawa ndiyo wengi na hawataweza kupambana na makali ya *globalization* na Kiswahili. Hivi sasa tumejenga matabaka ya Watanzania wanaoelewa Kiingereza na wasioelewa chochote, pamoja na kwamba wote wana elimu zinazofanana.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja ya Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, ambayo ni ya aina yake - safi sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Mhjeshimiwa Waziri anazungumzia dhamira ya Serikali kujenga Shule za Sekondari 1,500 mwaka huu wa fedha 2004/2005. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi na ombi pia. Kwa kuwa Majimbo ya Uchaguzi kama vile Kinondoni na Ilala ya Mkoa wa Dar es Salaam, hayana maeneo ya kujenga shule. Je, Serikali itakuwa tayari kununua maeneo ambayo yatafaa kwa kujenga Shule za Sekondari kwa maana ya kufidia wenye nyumba hizo na kuwapa viwanja vingine?

Vinginevyo, Mheshimiwa Spika, majimbo hayo kwa mfano Kinondoni yenye wakazi zaidi ya 450,000 na Shule za Msingi zaidi ya 25, hawataweza kujenga Shule za Sekondari kwenye maeneo/majimbo hayo. Naomba Serikali iwe na mtazamo wa upendeleo wa kupata maeneo hayo ya ama *squatter* au yale yanayopendekezwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni kuwa-*buy out* wananchi wa maeneo hayo ili Shule za Sekondari ziweze kujengwa Jimboni Kinondoni - Jimbo lenye Kata 10. Sasa hivi Kinondoni ina shule moja tu ya Sekondari ya Kambangwa.

Pili, Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Kambangwa ni ya Serikali. Tunaomba sasa shule hii ijengewe *Science Laboratory* na vifaa vyake na *computer room*. Wananchi tayari wamechangia matofali na *cement* kwa ajili ya ujenzi huo. Naomba Serikali itujengee hiyo *Science Laboratory,* vifaa vyake pamoja na *computer room* kwa mwaka huu 2004/2005 kutokana na hizo fedha za kujenga Sekondari 1,500, hasa baada ya kueleza uhaba wa maeneo ya kujenga Sekondari Jimboni Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sana Waheshimiwa Wabunge tumeilalamikia Serikali kwa ucheleweshaji wa malipo ya mishahara ya Walimu. Mheshimiwa Waziri ameliona hili katika hotuba yake. Mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba na kusisitiza tena chonde chonde, mwaka huu wa fedha 2004/2005. Tatizo hili, Serikali ilimalize, tulonge ya baadaye. Walimu wamenyanyaswa sana kwa miaka mingi. Tuwapunguzie adha hiyo ili wa-*concentrate* kusomesha Taifa letu, kuondokana na Umaskini, Ujinga na Maradhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naipongeza sana Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mipango yake mizuri hasa kwa kuliona suala la kupanua nafasi za watoto wetu kujiunga na Shule za Sekondari kwa asilimia 50% kutoka asilimia 8% -12% - 21% ya sasa kuanzia mwaka 2007 - 2009.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia 100%. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanazofanya za kupambana na umaskini kwa njia ya kuielimisha jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imetekeleza kazi yake kwa kiwango cha hali ya juu. Na pia katika bajeti hii, kiasi cha Shs. 159,411,932,000/= kimeombwa ili kuweza kutekeleza mipango yake ya mwaka 2004/2005. Nakubaliana na ombi hilo kwamba wapewe. Pamoja na hayo, ningependa tu yatazamwe maeneo yafuatayo. Katika maeneo ambayo hayakuwa na Shule za Sekondari, kama vile Wilaya ya Misungwi, Shule tano za Sekondari zimeanza kwa miaka tofauti na bado zina mapungufu:-

(i) Misungwi Sekondari;

(ii) Paul Bomani Sekondari;

(iii) Misasi Sekondari;

(iv) Busongo Sekondari; na

(v) Koromije Sekondari.

Mheshimiwa Spika, shule hizi zimejengwa kwa nguvu za wananchi, bado zina mapungufu mengi. Hazina nyumba za Walimu, Maabara, Maktaba na Vyumba vya Madarasa. Hivyo, Serikali izione kwa ukaribu zaidi. Lakini pia ipo Shule ya Sekondari ya Mbarika - ambayo tayari, lakini haijapokea watoto. Ni kwa nini? Naomba jibu katika majumuisho. Ombi lingine ni kwamba Sekondari hizo zifikiriwe angalau magari mawili. Kila Tarafa mbili zipate gari moja ili kusaidia katika kazi zake.

Mheshimiwa Spika, niishauri pia Serikali au Wizara iimarishe ukaguzi wa Shule za Msingi kwa kuwapatia vitendea kazi kama vile magari, na pia maslahi yao yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na kauli ya Waziri Mkuu kuhusu madai mbalimbali ya Walimu, ambayo pia Waziri ameahidi kuyalipa; ni vyema nikaiomba Wizara ifuatilie kwa karibu kuwa malipo hayo yanawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia 100% kwa kukubali ombi la TShs. 158,411,932,000/= zipitishwe bila mabadiliko. Ahsante sana.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya Walimu. Je, zile Tume za Mikoa zimeundwa, zimeshapewa hadidu za rejea? Nani atasimamia Tume hiyo - *SEMITEMI, PMO* au *WEL?*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa Umaskini kwa Walimu. Walimu wengi wamekopa katika vyombo vya fedha nchini. Wizara inasemaje - hivi unaweza kuondoa umaskini kwa kukopa? Mikopo harusi, kulipa matanga. Wizara inasemaje? Kuhusu vyombo vya usafiri Sekondari. Vyombo vya usafiri katika Shule za Sekondari ni muhimu sana. Wizara ina mpango gani kwa shule za Jimboni kwangu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Kiswahili. Wizara inasemaje kuhusu maneno ya kihuni yanayojipenyeza kwenye lugha hii? Mfano:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Kuchabanga | ) | |
| (ii) | Kubugiza | ) | magoli. |
| (iii) | Kuichapa | ) | |

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za maendeleo. Vigezo vinavyotumika kusaidia maabara hizo za Serikali.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kifupi sana juu ya mambo mawili makubwa kuhusu mishahara ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo linaloeleweka kwamba mishahara ya Walimu wanaotumikia Serikali ya Tanzania ni midogo sana, ukilinganisha na mishahara ya

Walimu wanaofundisha private. Itakumbukwa kwamba tarehe 1/4/2003, nilihoji hapa Bungeni kuhusu utofauti huo wa mishahara baina ya Walimu hao ambao wana sifa moja, lakini wakiajiriwa Serikali, mishahara midogo - na wakiajiriwa private, mishara ni zaidi ya mara mbili. Waziri wa Elimu na Utamaduni alijibu kwamba Wizara yake imeshawasilisha mapendekezo ya mishahara mipya katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, leo nimemsikiliza Waziri wakati wa hotuba yake, na sikusikia lolote juu ya mabadiliko niliyotarajia. Pamoja na hali ngumu ya uchumi wa nchi, tungefikiria walau kidogo - ukizingatia ile ahadi ya Waziri juu ya kurekebisha mishahara ya Walimu. Tunaomba maelezo juu ya kilichotokea baada ya kuwasilisha mapendekezo hayo kama nilivyokwisha taja hapo juu. Jambo la pili ni kuhusu Sekondari za Wananchi za Kata. Katika Jimbo langu nimejitahidi kuhamasisha na ni pamoja na kutoa michango yangu mwenyewe na kufanikiwa kupata Sekondari 8 ambazo tayari zimepata usajili katika Kata nane ni kama ifuatavyo.

(i) Kindi Sekondari - Kata ya Kindi, nilichangia Shilingi 400,000/= na pia nilichangia *cement* mifuko kumi. Tayari imesajiliwa na inasomesha sasa.

(ii) Somsom Sekondari - Kata ya Kibosho Magharibi, ambayo nilihamasisha na kuchangia Shs. 200,000/= pamoja na kuomba msaada *KINAPA* na kupatiwa Shs. 16,500,000/= kupitia Halmashauri yangu ya Wilaya ya Moshi Vijijini. Shule imesajiliwa na inasomesha wanafunzi sasa.

(iii) Sungu Secondari - iliyopo Kata ya Kibosho Mashariki. Hapa nilihamasisha na kuchangia kutoka mfukoni mwangu Shs. 200,000/= na kudhamini mkopo usio na riba Shs. 3.3m./=. Hivyo shule imekamilika na imesajiliwa na watoto wanasoma sasa.

(iv) Mabogini Sekondari - Kata ya Mabogini, ambayo nimehamasisha na kuchangia mifuko 20 ya *cement.* Shule imesajiliwa na inasomesha watoto wetu sasa.

(v) Sahoni Sekondari - Kata ya Mbokomu. Nimdhamasisha na kuchangia Shs. 200,000/= taslimu, na shule imesajiliwa na inasomesha watoto wetu sasa.

(vi) Kisarika Sekondari - Kata ya Uru Kaskazini. Nimehamasisha, na shule imeandikishwa na watoto wetu wanasoma sasa.

(vii) Okaoni Sekondari - Kata ya Okaoni. Nimehamasisha na kuchangia Shs. 100,000/=, na shule imeandikishwa na inasomesha watoto wetu sasa.

(viii) Shimbwe Sekondari - Kata ya Uru Mashariki. Shule hii imesajiliwa na watoto wanasoma.

Mheshimiwa Spika, shule zote hizi ni juhudi za wananchi, na naipongeza Wizara kwa juhudi na ushirikiano uliosababisha shule hizo kupata usajili, na wala hilo siyo

jambo la mchezo na si rahisi. Bado zipo shule zingine katika Kata zingine zinazoendelea kujengwa katika Kata nne:-

(i) Kirima Sekondari - Kata ya Kirima;
(ii) Meli Sekondari - *Old Moshi* Mashariki;
(iii) *Old Moshi* Magharibi; na
(iv) Kata ya Kibosho Kati.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayosababisha kutokuanza kwa shule hizi ni kwamba kuna tatizo la ardhi. Ardhi eka moja Moshi - eneo la mlimani, ni zaidi ya Shs. 5m./=. Hivyo, siyo jambo rahisi. Kama hivi sasa kuna tatizo ambalo ningeomba busara itumike ili Shule ya *Old Moshi* Mashariki - iitwayo Meli Sekondari, iweze kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vine (4), yaani Kijiji cha Kikarara ambako ndiko alikozaliwa *First Lady* (Mama Anna Mkapa), Kijiji cha Dhuduni, Kijiji cha Mahoma na Kijiji cha Kidia; wamefika leo hapa kumwomba Waziri wa Elimu na Utamaduni kupitia kwa Mbunge wao ambaye ni mimi Ngawaiya kwamba:-

(i) Shule imejengwa na ina vyumba vitatu.

(ii) Kwamba kulikuwa na maamuzi ya Serikali ya Kijiji, ya kugawa shamba ekari 40 kwamba ekari 30 zibakie kwenye shule yao wenyewe Kidia Sekondari na ekari 10 tu ziwe kwa ajili ya Shule yao ya Kata - ambayo wameshajenga, nami nimechangia mifuko 40 ya *cement* pamoja na rangi Shs. 50,000/=.

(iii) Kwamba wanafunzi waliofaulu na kukosa nafasi ni 100,020. Ndipo walipokuja na jani la Kichagga liitwalo *isale* - likiwa na maana kuwa *isale* lilitumika kuomba Machifu wetu wa zamani kitu fulani na lilitumika kwa jambo kubwa tu. Ninalo hapa hapa ninasubiri kumkabidhi Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kutaka kujua juu ya Tume ya kufuatilia zile shule zilizoiba mitihani *St. Mathew S. Highland* Mkuranga na kadhalika. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DANIEL N. YONA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya Walimu. Tafadhalini chunguzeni ubadhilifu (wizi) wa fedha katika Halmashauri za Wilaya. Kwa mfano, Mwalimu wa Shule ya Sekondari moja aliniambia kuwa aliambiwa mshahara wake ni Shs. *"X"* ambazo ni zaidi ya *scale* yake. Kila mwezi anapewa mshahara wake halali + kiasi kidogo. Zinazobaki, wanachukua Wahasibu na kadhalika. Kwa mfano, anaambiwa mshahara wako ni Shs. 100,000/= - *scale* yake ni Shs. 70,000/=. Kwa hiyo, hizo Shs. 30,000/= anapewa Shs. 10,000/=, na wakubwa wanachukua Shs. 20,000/=

Mheshimiwa Spika, kuhusu Lishe ya Watoto Shuleni. Tafadhali anzisheni mpango wa kuwapa watoto katika kila shule maziwa kila siku. Kwa mfano, 1/4 au 1/2 au lita nzima kwa kila mtoto kila siku bure. Hili litawapa watoto wote afya nzuri na

litasaidia kukuza ufugaji wa ng'ombe na biashara ya maziwa nchini. Nchi itakapunguza kuagiza maziwa toka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *sustainability.* Mipango ya MMEM na MMES ni mizuri kama tutaiwezesha kuwa endelevu. Tumeianzisha kwa mikopo ya wafadhili. Je, Bajeti zetu zitaweza kuiendeleza kikamilifu miaka ijayo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi zangu nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Wataalam wote kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kupongeza mpango wa MMEM. Kwa kweli mpango huu ni mzuri sana, ambao umelenga katika kumkomboa Mtanzania. Pamoja na kazi nzuri ambayo tayari imefanyika, lakini ningependa nitoe ushauri wangu kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri kuhusu Ikama ya Walimu ambao Mheshimiwa Waziri ameelezea, ningeomba kabisa litiliwe mkazo mkubwa. Kwani kujenga nyumba (madarasa mazuri), itakuwa kazi bure endapo hatutakuwa na Walimu wa kutosha. Hii itakuwa sawa na kupamba vizuri jeneza wakati ndani kuna maiti. Kwa hiyo, suala la Walimu liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuamua kuchukua vijana wengi wanaomaliza shule na kuwepo kwenye crash programme, lazima tuwe makini kwa hao vijana watakaochaguliwa. Kwani kwa sababu mpango huu ni mpya, hivyo tutegemee matatizo. Sasa ningeshauri tujiandae kwa kupokea matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara ya Walimu, lazima liangaliwe upya. Kwani Walimu (shule) ndiyo msingi wa maisha, hivyo tusiwape majukumu kwa kuchanga Idara hii na Idara au Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza madarasa mawili ya Ufundi/Biashara, ni muhimu sana. Liangaliwe, kwani watoto wanamaliza shule wakiwa na umri mdogo sana, na ambao hawawezi kuanza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, nipongeze mpango mpya wa MMES, ambao utaanza kutumika siyo muda mrefu. Kwa yale mapungufu yaliyojitokeza kwenye mpango wa MMEM, ndiyo tuyatumie kujifunza zaidi ili tufanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, maswali ambayo inabidi tujiulize ni haya yafuatayo:-

(i) Je, tumejitayarishaje kushindana na wenzetu wa Kenya/ Uganda?

(ii) Je, tumejitayarishaje kwenye utandawazi?

(iii) Je, tumetembelea kwenye nchi za wenzetu wa Kenya/ Uganda?

(iv) Je, tumewatayarishaji Wataalam (Walimu)?

Maswali haya ni muhimu sana kujiuliza endapo tunataka kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Chissano kwa kuamua kutumia Kiswahili kwenye mikutano uliofanyika na nchi za Kusini mwa Afrika. Kwa kuwa umuhimu wa Kiswahili umeanza kuonekana, hivyo ningependa kuomba Wizara hii itilie mkazo. Kwa sababu nchi zote zinategemea kujifunza kutoka kwetu. Sasa sisi tuoonyesha jitihada hizo za kuendeleza na kufundisha Kiswahili, umuhimu wa Kiswahili kutumika kwenye *computer.*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kabisa Wizara ya Elimu na Utamaduni ishirikiane na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ili tuanze kuona um,uhimu wa kutafsili Miswada ili ieleweke kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara hii iangaliwe uwezekano wa kujenga Shule Maalum ya wenye vipaji vya michezo. Michezo tusipoipa kipaumbele sasa, tusitegemee kama tunaweza kufanya vizuri hapo baadaye. Kwani bila msingi mzuri kwenye jambo lolote, usitegemee matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Wizara hiiitoe waraka wa kuzuia Walimu kutojiingiza kwenye mambo ya Siasa za Vyama. Kwani Walimu ni kioo, hivyo ni vizuri wakawa mfano mzuri. Baadhi ya sehemu, Walimu wameacha shughuli zao za Ualimu na kujikita kwenye siasa. Ni vyema Wizara ikaliangalia hilo mapema na kutoa tamko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msaada mkubwa unaotolewa kwenye Shule zetu za Sekondari, Wizara hii ione umuhimu wa kutoa nguvu kidogo kwa Shule za Taasisi za Dini. Kwani lengo letu ni kuwasaidia vijana wa Kitanzania ambao ndio watakaojenga nchi hii (ambao husoma Shule za Serikali/Taasisi). Mfano, kule kwenye Wilaya ya Kilolo, kuna Shule za *Lutheran Church* zimejengwa. Ni vyema zikawekewa utaratibu wa kuzipa ruzuku ili nazo zipunguze ada zake ziwe katika standard ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Waziri na Naibu pamoja na Wataalam wote, kwamba waelewe wao ndio waliobeba nchi hii na tunawategemea. Pia wale Watendaji na Wataalam/Walimu watakaofanya vizuri, wapewe motisha nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%. Mungu ibariki Wizara ya Elimu na Utamaduni.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa hoja hii, nashawishika kuendeleza yale ambayo nilianza kuchangia kwa maandishi pia, jana tarehe 8 Julai, 2004.

Mheshimiwa Spika, namalizia mchango wangu katika maeneo mawili. La kwanza linahusu Utamaduni. Wananchi wa Rungwe wameamua, takriban miaka miwili iliyopita, kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu au cha Makumbusho ya Historia, Utamaduni, Mila na Desturi za Unyakyusa. Pamoja na mambo mengine, kituo hiki kitasaidia watafiti, wanafunzi na wakufunzi katika fani zinazohusika, ikiwa ni pamoja na mchango wa jamii hizo katika Taifa na katika lugha na utamaduni. hicho kitakuwa Ikama-Lwangwa. Jengo linaendelea kujengwa kwa ushirikiano kati ya wananchi na mfuko wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia Kurugenzi ya Utamaduni, isaidie katika azma hii. Miaka miwili iliyopita, nilileta katika mchango wa maandishi, ombi kama hili. Zoezi hili pamoja na kuwa na nyumba, ni la kitaalam. Mkurugenzi wa Utamaduni anaalikwa atembelee eneo la mradi, yeye na Wataalam wake ili waone jinsi ya kusaidia.

Mheshimiwa Spika, la pili na la mwisho katika mchango wangu, ni ombi la Wizara kusaidia wananchi katika kuendeleza maabara. Shule zote nane za Sekondari za wananchi, zina majengo ya maabara. Ujenzi huu ulikuwa ni sharti mojawapo katika shule kufikiriwa kuandikishwa. Lakini kuziwekea vifaa, madawa *(chemicals)* na vielelezo vya maabara; hakika ni nje ya uwezo wa wananchi. Kwa hiyo, kinachofanyika ni ama kuziacha maabara kama zilivyo tupu au kuzitumia kama madarasa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mradi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* uliosaidia ujenzi wa maabara. Kwa bahati mbaya haukufika Rungwe. Ni matumaini yetu kwamba MMES itatoa kipaumbele kikubwa au cha juu katika kukamilisha na kuendeleza maabara. Vinginevyo, sayansi na teknolojia itabakia ni wimbo tu.

Mheshimiwa Spika, namalizia kama nilivyoanza, kwa kumpongeza tena Waziri Mungai, kuwapongeza Naibu Waziri Sakila, Katibu Mkuu Malale, Afisa Elimu Kiongozi - Ndugu Ricky Mpama na Watendaji wote katika sekta hii muhimu, Elimu.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Ninawapongeza pia Wasaidizi wake wote waliotumia muda wao usiku na mchana katika kumshauri na kusaidia katika uandaaji wa hotuba yake hii. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa ujasili wake wa kujaribu na kuthubutu kuyafanya yale kwa, wengi yanaonekana hayawezekani. Kama ni moyo, bila shaka ana moyo na robo ya Mkwawa. Bila ujasiri huu, mambo mengi yanayojitokeza katika mabadiliko yanayoonekana sasa, ingelikuwa vigumu kuyaona. Naomba Waheshimiwa Wabunge tumwunge mkono ili aendeleze elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kwimba wamefurahi sana kusikia mpango wa MMES, kwa vile mpango huu umewakuta wakati wakishughulika na ujenzi

wa Shule za Sekondari za kila Kata. MMES wanaiona kama mkombozi wao. Kila kitakachowezekana watafurahi kupokea.

Mheshimiwa Spkka, mipango hii ya MMEM na MMES ni mipango ambayo imetegemea sana ufadhili kutoka nje ya nchi. Ni vizuri muda muafaka utakapofika, Waheshimiwa Wabunge kila mmoja katika eneo lake, akaendelea kuwakumbusha na kuwaelimisha wananchi ya kuwa maendeleo yao yataendelea kutegemea wao wenyewe. Tusijilegeze, tusibweteke, nguvu zetu ndiyo mtaji weti.

Hivyo, tusitupe mbachao kwa msala upitao, na tusidharau dafu (uwezo wetu), kwani embe (misaada na mikopo) ni tunda la msimu; ilimradi sasa misaada na mikopo hii inapatikana kutokana na nchi yetu kukubalika chini ya uongozi wa Serikali, yaani tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu - Mama Malale, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wote na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni Makao Makuu, Mikoani na Wilayani, kwa ushirikiano walionipa na wanaoendelea kunipa muda wote wa kuugua kwangu. Ukaribu wao kwangu na familia yangu, kumenipatia faraja kubwa na kunipatia nafuu. Naomba waendelee kuniombea ili afya yangu iendelee kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia 100%. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na Wataalam kwa maandalizi yao ya hotuba nzuri inayotoa kila msaada wa majibu kwa Mbunge Jimboni kwake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimechangia kwa kusema Bungeni, kuna machache ambayo panenda yatolewe majibu na Mheshimiwa Wasiri atakapokuwa anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukaguzi Wilayani. Ili Afisa Ukaguzi Wilaya afanye kazi ya ukaguzi kwa ufanisi, anatakiwa apewe gari na ofisi yake ifanyiwe ukarabati wa hali ya juu sana na iwekewe samani. Gari la Mkaguzi ni muhimu sana kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira na jiografia ya Wilaya ya Biharamulo ilivyo na mapori mengi, na ni eneo la ujambazi - ikizingatiwa kuwa ni eneo lililokaliwa na wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ninavyomfahamu Afisa Ukaguzi wa Wilaya - Mwalimu Flora Kagaruki, alivyo mchapa kazi, mwadilifu, mwaminifu, anayejituma na ambaye yuko tayari kuhatarisha maisha yake katika kulitumikia Taifa lake, kwani sifa hizi zinaonekana kutokana na matunda au matokeo nya kazi yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi la Walimu. Shule ya Sekondari ya Nyakahura ina Walimu wawili (2( tu, na ina wanafunzi 102 na mikondo minne (4) na ni mwaka wa

pili, yaani *Form I - IV*. Hivyo, ina upungufu wa Walimu 10. Naomba nipewe, ni muhimu sana.

Biharamulo Sekondari yenye wanafunzi 368 na mikondo 8, Form I - III, ina upungufu wa Walimu 15. Kagango Sekondari, umuhimu wake nimeueleza katika hotuba niliyoitoa Bungeni kwa kusema. Ina *Form I - IV,* ina jumla ya wanafunzi 267, mikondo 8, na ina upungufu wa Walimu wanne (4). Walio na umuhimu kwa sasa ni Walimu wa somo la Hesabu (Maths) na Mwalimu wa Biology kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha nikitegemea kupata majibu toka kwa Mheshimiwa Wasziri atakapokuwa anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, na Wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri iliyo fasaha na yenye maelezo ya kina. Naiunga mkono hoja hii moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa njia ya Waziri wa Wizara hii, kwa jitihada za kuboresha Elimu ya Sekondari - mpango wa MMES. Mpango wa MMES ni mpango wa kihistoria na ni mpango mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba lengo la mpango huu liwe hatimaye kuifanya elimu ya Sekondari kuwa ya kawaida, na ya wote. Stadi zingine zifuatie baada ya O'Level. Mpango mkubwa kama huu utahitaji Walimu, na ni lazima kuwa na mkakati wa kutosheleza Walimu.

Mheshimiwa Spika, para ya 11.9 (d) ya hotuba ya Waziri, inaonyesha sehemu ya jitihada hizo za kupata Walimu wa kutosha. Tunaweza kuwa na Walimu wengi nje ya ajaira ya Serikali - ambao wana taaluma kubwa na uzoefu mkubwa, hususan upande wa masomo ya sayansi, lakini ajira yao inakuwa ngumu. Hii itatokana na masharti yanayohusiana na Kanuni za Kudumu za Utumishi - Toleo la 1994, Kifungu D.33, ya kwamba miaka 40 ndiyo kikomo cha Mtaalam kuajiriwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri kipaumbele hiki kirekebishwe ili umri huo ufikie miaka 45, kwa kuwa hata umri wa kustaafu Serikali umepanda kutoka miaka 55 hadi 60. Ninao mfano wa Mwalimu mmoja mwenye utaalam na uzoefu mkubwa katika *Physics* na *Chemistry.* Pamoja na kujitolea kufundisha kwa kujitolea, hufundisha *Physics/Chemistry* katika Shule ya Serikali (ya kutwa) kwa miaka miwili, akitokea *Private Secondary School,* anazuiwa ajira yake kwa sababu tu umri wake ulikuwa umezidi kwa miezi mitatu (3) tu juu ya umri wa miaka 40; na sasa shule ina upungufu wa Mwalimu wa *Chemistry/Physics,* naye anaomba aendelee kufundisha kwa kujitolewa ili kusaidia wanafunzi.

Hivyo, Mheshimiwa Spika, naomba/nashauri tusikose Walimu wengi. Tukiwazuia kwa umri wa miaka mitano tu. Sheria husika ije Bungeni kwa marekebisho ikibidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MMEM Jimboni kwangu, kuna Walimu waliokuwa wanafundisha MEMKWA, hawajalipwa bado. Naomba wasaidiwe. Pia kuna tatizo la Walimu waliohitimu Daraja B la Ualimu, hawana ajira ingawa walisomeshwa na Serikali. Ningeomba kuwepo utaratibu wa kuwa na *upgrading* yao kwa kuruhusiwa kujinga na Vyuo vya Ualimu *Grade IIIA.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri J.J. Mungai, binafsi kwa kuvalia njuga ya kupandisha hadi Wizara ya Elimu na Utamaduni mwaka hadi mwaka. Juhudi zake sasa zimeanza kuzaa matunda. Aidha, Mheshimiwa Spika, nawapongesa Naibu Waziri - Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kufanya kazi walizokabidhiwa na Taifa letu, kwa ufanisi mkubwa. Naunga mkono hotuba ya Waziri kwa asilimia mia moja. Kwa kuwa hotuba hiyo imejaribu kutatua matatizo mengi ya msingi ambayo yalikwamisha kasi ya maendeleo ya Elimu, mchango wangu ni katika maeneo haya: Licha ya hotuba ya Waziri kusisitiza umuhimu wa ukaguzi kwenye Shule za Msingi, bado tatizo litakuwa jinsi ya kuwawezesha Wakaguzi kuzifikia shule hizo. Tatizo la usafiri, kwa mfano Wilayua ya Ludewa, haina usafiri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusaidia katika ujenzi wa Sekondari. Aidha, naiomba Serikali kuweka nguvu zao katika ujenzi wa *High Schools,* sambamba na shule nyingine za Sekondari. Kwani ingawa wananchi wana ari kubwa ya kujenga *High Schools,* ujenzi wake unahitaji nguvu kubwa sana. Hasa baadhi ya majengo ni ya gharama kubwa, na vifaa vya bei kubwa. Hivyo, naiomba Serikali kuunga mkono juhudi za wananchi wa Ludswa na mfadhili wa Kanisa la *Roman Catholic* Ludewa katika juhudi zao za kujenga *High School* Wilayani Ludewa, na hadi sasa majengo kadhaa yamekamilika, bado msaada wa Serikali unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Elimu na Utamaduni.

**MHE.MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naipongeza Wizara kwa kazi nzuri. Hapana shaka kuwa kupishana kwa mwamko wa kupenda elimu baina ya wananchi kati ya mkoa na mkoa, kunatokana na sababu za kihistoria.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi kwa mfano, unazo jumla ya Shule za Sekondari 19 tu. Kabla na baada ya uhuru, Wamisionari hawakuona sababu ya kuwekeza katika elimu, hususan ya Sekondari. Hata baada ya uhuru, Serikali pia haikuona sababu ya kujenga hata shule moja tu ya Sekondari. Katika mazingira haya, halipatikani hata jambo moja la kumhamasisha mzazi kushiriki kujenga Shule za Sekondari au kumsomesha mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi nzito na endelevu, wananchi pamoja kasi ndogo, wameanza kutambua kuwa hakuna wa kuwajengea shule hizo zaidi nguvu zao wenyewe. Katika Jimbo langu la Mchinga, tumeamua kujenga shule moja ya Sekondari kwa kila Kata, ili kukidhi mahitaji ya elimu hiyo. Hivyo, Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuamua kusaidia nguvu za wananchi kwa kujenga darasa na maabara kwa kila shule. Naiomba Wizara ituongezee Walimu na vifaa vya kufundishia katika Shule ya Sekondari ya Mchinga, ambayo mwaka huu ina Kidato cha III na mikondo miwili. Kutekelezwa kwa ombi hili kutatuletea matarajio yetu kuwa ufanisi na kubwa zaidi, kutowapa morari wananchi katika kuchangamkia suala zima la elimu.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Mchinga, ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi, tayari inayo madarasa sita, jengo la Utawala, vyoo na nyumba mbili za Walimu. Msingi wa maabara na nguzo zake, vimeanzwa. Tunatarajia msaada wa Serikali utatufikia mapema. Shule ya Sekondari ya Milola, inatarajiwa kufunguliwa Januari, 2005. Shule hii pia imejengwa kwa nguvu za wananchi. Tunaomba Walimu na vifaa vya kufundishia pindi muda ukifika.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukupongeza Mheshimiwa Waasisi na timu yako imara, kwa kuwa na mipango mizuri inayotekelezeka. Nakuahidi kukupa ushirikiano wangu katika Jimbo la Uchaguzi Mchinga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri - Mheshimiwa Mungai, Naibu Waziri - Mheshimiwa Sakila, Katibu Mkuu - Bibi M. J. Malale na Wataalam walioandaa hotuba hii nzuri ambayo ninaiunga mkono *100%.*

Ninaipongeza sana Serikali ya awamu hii ya tatu kwa juhudi zake za kuboresha elimu kupitia Wizara hii ya Elimu na Utamaduni. Ninaishauri Wizara ifanye mikakati kabambe kupata Walimu wengi wenye sifa na uwezo wa kufundisha vizuri Shule za Msingi hadi Sekondari. Vinginevyo, Mheshimiwa Spika, kuboresha vifaa, maabara na manengo peke yake, haitasaidia kuinua elimu nchini.

Pia Walimu kama wafanyakazi wengine, waboreshwe maslahi yao popote walipo na wapate mikopo ya Benki bila kubaguliwa. Baadhi ya Walimu hawajapata mikopo ya Benki au mikopo imesitishwa na Benki kwa madai kwamba Wizara ya Elimu na Utamaduni haipeleki marejesho ya mikopo mapema kwenye Benki walizotoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii kuwa nzuri, haielezei kila mkoa hadi wilaya zake zitanufaika vipi na Bajeti hii ya Elimu na Utamaduni. Kwani ingesaidia Wabunge kufuatilia kwa karibu zaidi na kubaini makosa kama yapo, ili yarekebishwe kabla ya utekelezaji wa miradi husika. Ninaipongeza Wizara kwa kupunguza ada kwa Sekondari za kutwa, lakini pia ifikirie kwa Sekondari za *boarding.*

Ninachukua fursa hii kuishauri Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Taifa, kuharakisha mawasiliano yanayohusu malipo ya ada ya mitihani hasa kwa wazazi wanaochelewa kulipa. Baadhi ya wananchi hushindwa kulipa *fees* za mitihani mapema na kusababisha wanafunzi waliofanya mitihani kukosa au kuchelewa kupata matokeo yao kwa madai kwamba hawajalipa fees hizo. La kushangaza ni kwamba hata baada ya kulipa, inachukua muda mrefu kupata matokeo, hali ambayo inawafanya wazazi washukuru kwamba fedha zao zimeliwa na Walimu Wakuu wa shule hizo. Hivyo, ni vizuri mawasiliano yaharakishwe ili Wakuu wa Shule waondokane na tuhuma hizo. Matatizo ya namna hiyo yametokea Jimboni kwangu Liwale katika Shule ya Sekondari ya Kutwa.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara Mkoani Lindi, hususan Wilaya ya Liwale ambako elimu ni duni. Matokeo ya Shule ya Msingi na Sekondari siyo mazuri hata kidogo. Sababu kubwa ni ukosefu wa Walimu wa kutosha kwa masomo mbalimbali. Ingekuwa vyema kwa Mheshimiwa Waziri kufanya ziara katika maeneo yaliyokuwa nyuma kielimu na matokeo mabaya, ili kujionea yeye mwenyewe mazingira ya maeneo hayo kama ilivyo Liwale. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, Liwale ina Sekondari moja tu ya Kutwa. Hivi sasa kuna mipango kabambe inayosimamiwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Banduka, ya kujenga Sekondari mpya 10. Sekondari ya Barikiwa imeanza kujengwa mpaka sasa madarasa mawili (2), nyumba ya Mwalimu, jengo la Utawala linajengwa na kazi zingine za ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa ushirikiano mzuri ninaopata kila ninapofika Wizarani kufuatilia mahitaji/masuala mbalimbali ya Jimboni kwangu Liwale. Nilifanikiwa kupata Walimu wa Sekondari ya Liwale zaidi ya 10. Kwa bahati mbaya, wachache baada ya kuripoti waliihama shule hiyo kwa visingizio mbalimbali, hali ambayo imechangia kiasi kikubwa kutofaulisha wanafunzi Kidato cha IV. Naomba Wizara ifanye utafiti kujua kwa nini Walimu wanahama au hawataki kwenda Liwale ambako hatuna tatizo kama hilo katika sekta zingine zilizopo Liwale?

Mheshimiwa Spika, ninaamini Wizara inaweza kutafiti na kujua. Kama tatizo ni kwamba Liwale ipo pembezoni, Walimu hawana motisha wakiwa Liwale au sababu za kiutawala; hayo yote, Wizara inaweza kuyatatua bila shida. Ninaomba Wizara ifanye hivyo haraka ili kuokoa hali hiyo ya matokeo mabaya katika shule hiyo. Baadhi ya wazazi wanawahamisha watoto wao na kuwapeleka Shule za Sekondari nje ya Wilaya na siyo wananchi wote wanye uwezo huo.

Kutokana na kero ya upungufu wa Walimu wa Sekondari ya Liwale na Walimu wa Shule za Msingi, wakati huu ninaochangia hoja hii, ujumbe wa viongozi watatu (3) wa Wilaya ya Liwale, Mwenyekiti wa Halmashauri - Ndugu Abbas Matulilo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya - Ndugu Kitula, ukiongozwa na *DC* wa Liwale - Ndugu David Holela, wamefika Wizarani kuonana na wahusika kufuatilia kero za upungufu wa Walimu na masuala mengine ya kuboresha elimu Liwale.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itoe kipaumbele kuikwamua Wilaya hii kielimu. Pia naomba Mheshimiwa Waziri, maeneo kama Liwale ambayo haijawahi kuwa na Shule ya Sekondari iliyojengwa na Serikali, Wizara ina mikakati ya kujenga Shule ya Sekondari moja tu kama mfano, iwe changamoto kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninarudia kusema ninauanga mkono tena hoja 100%, na kuwatakia kheri Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam wote Wizarani. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwingine. Lakini nichukue nafasi hii kuelezea utaratibu tuliouweka kwamba, kwa Wizara zenye siku moja moja tulikubaliana na Serikali kwamba mjadala uendelee mpaka saa kumi na mbili, halafu ndiyo hatua zinazofuata zianzie hapo.

Lakini kwa Wizara zenye siku mbili mbili kama hii ya Elimu na Utamaduni, tulikubaliana kwamba mjadala uishie saa saba mchana ili watoa hoja wapate nafasi nzuri na ya kutosha ya kushauriana na wataalam wao ili watoe majibu ya uhakika zaidi kwa sababu mjadala unapokwisha na Waziri anatakiwa kujibu hapo hapo mara nyingi yale yanayosemwa mwisho mwisho anakuwa hajapata kujadiliana vizuri na wenzake.

Kwa hiyo, utaratibu ndio huo, kwa hiyo kwa leo kwa kuwa hii Wizara ina siku mbili sawa na Wizara zitakazoanza Jumatatu tarehe 12 Julai, 2004 - wiki ijayo basi tutakuwa tunamaliza saa saba mjadala wa jumla ili kusudi watoa hoja wajiandae kujibu kipindi cha mchana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri jiandae utakuwa wa kwanza kipindi cha jioni. Najua Naibu wako hali yake hairuhusu kushiriki, kwa hiyo utaitwa wewe moja kwa moja.

La pili, asubuhi nilighafirika sikutoa tangazo kuhusu kesho. Jumamosi ni siku ya Semina lakini tulikuwa tumepanga kwa Jumamosi ya kesho Semina ya *TANESCO* na Wizara yake ili watueleze mikakati na mipango iliyopo ya kupeleka Umeme Vijijini, ule mradi wa umeme Vijijini.

Waheshimiwa Wabunge, tulishakubaliana hivyo, lakini dakika za mwisho wame-*postpone,* wameahirisha kwa naelezo kwamba hiyo semina waifanye Mkutano ujao wa Bunge. Bado tutakuwa na semina, lakini kwa kuwa wamejiondoa katika ratiba ya kesho basi kesho tena hatuna semina, utakuwa ni utawala binafsi tu. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii vile vile kwa kuwa hatuonani tena mpaka Jumatatu nieleze ratiba ya Jumatatu. Nilishawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Jumatatu tuna

mgeni maarufu, Mheshimiwa Sam Nujoma, Rais wa Jamhuri ya Namibia, anakuja Dodoma kuhutubia Bunge letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ratiba tutakayowagawia inasema kwamba, tutaanza Bunge saa tatu kama kawaida. Tutaendelea mpaka kipindi cha maswali kitamalizika, Mheshimiwa Waziri mtoa hoja atapewa nafasi ya kuwasilisha hoja yake. Msemaji wa Kamati atasema na Msemaji wa Upinzani atatoa maoni ya Upinzani. Hiyo kwa kawaida huwa inatufikisha kwenye saa tano na nusu hivi.

Basi ikifikia hatua hiyo tutasitisha shughuli za Bunge, ili tukampokee mgeni wetu. Amepangiwa aingie kwenye viwanja vya Bunge saa 5.45 ili kusudi taratibu za kawaida za kumpokea Mkuu wa nchi zikamilike, halafu hotuba yake itaanza saa sita kamili.

Lakini akimaliza hotuba akiondoka jioni tutaendelea na shughuli zetu za Bunge kama kawaida na Wizara inayoanza Jumatatu ni Mambo ya Ndani ya Nchi, imepewa siku mbili. Kwa hiyo, nadhani hiyo disturbance ndogo ya ujio wa Rais haitakuwa imetuvurugia ratiba yetu.

Mwisho namshukuru Mheshimiwa Mutungirehi kwa kujisalimisha kwamba ndiye aliyesababisha vurugu za asubuhi. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Marmo mambo haya yameshaingia kwenye *Hansard.* Bungeni utani unakubalika, lakini utani unaovuka mipaka mpaka ukafikia kum-*embarrass* Waziri wa Serikali, nadhani unastahili kuwekewa msimamo na Spika alishasema asubuhi kwamba atakapopatikana huyu atapelekwa Kamati ya Simpasa. Sasa amepatikana, ametupunguzia tu kazi ya kumtafuta.

Kwa hiyo, bado nitaiomba Kamati ya Simpasa ijadili jambo hili kwamba linaingilia maadili ya Bunge, halafu Kamati itatushauri tufanye nini kwa utani unaovuka mipaka kama huu. Mwisho wa maelezo.

Waheshimiwa Wabunge sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.54 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja zilizochangiwa katika mjadala wa hoja ya bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuipokea vizuri tangu nilipokuwa naiwasilisha na kwa kuchangia katika hoja hii. Tumepata wachangiaji kwa kuzungumza humu Bungeni 33 na wachangiaji kwa

maandishi 58, kwa hiyo, jumla ni 91 na michango yote ni mizuri sana, imetuonyesha baadhi ya maeneo tunayohitaji kuyapa mkazo, tunayohitaji kuyatazama upya na tunayohitaji kuyatolea ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwataje waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni, nao ni: Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma ya Jamii, akafuatia Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mbunge wa Mgogoni, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nawashukuru wote waliofungua mjadala vizuri tu sikuona hata neno moja la kuchukiza ila yanahitaji ufafanuzi, nawashukuru sana. Hata wenzetu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine waliochangia ni Mheshimiwa Margerath Mkanga, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mathew Taki Ole -Timan, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Gwassa Sebabili. Hao ndiyo waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata michango vizuri sana kwa maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa George Kahama, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud na Mheshimiwa Lucas Selelii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Philip Alfred Magani, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Prof Mark Mwandosya, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Njelu Kasaka,

Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Frank Mussati na Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Parseko V. Kone, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, alitupa nyongeza, Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa George Francis Mlawa. Wote nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wangu na mimi mwenyewe tumerekodi mawazo mengi ambayo tumeyapata na nilipoandaliwa ya kuja kutolea maelezo basi ni makablasha yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda tulionao si rahisi niyapitie yote haya. Lakini napenda niwashukuru kwamba, hii ni rekodi ambayo tutakwenda kuifanyia kazi na nitajaribu kugusia yale ambayo naona wengi wametaka yafanyiwe ufafanuzi. Yale ya kutusaidia kufanyia kazi tutakwenda kuyafanyia kazi. Tuliyachukua kwa Idara na mengi ambayo nitayagusia yamelenga elimu kwa ujumla, kwa hiyo, yanatokana na majibu ambayo yameandaliwa na Wakuu na Idara na hasa haya yamesimamiwa na Afisa Elimu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika nikianza na Mheshimiwa Sophia Simba katika mchango wake alitaka tuweke mkazo kufundisha somo la Kiingereza katika shule za msingi. Napenda nimhakikishie kwamba, somo hili linafundishwa katika shule za msingi tangu darasa la kwanza. Lakini napenda kukiri kwamba, hivi sasa halifundishwi vizuri sana, kwa sababu hatuna walimu maalumu ambao wameandaliwa na baadhi ya walimu wanaofundisha somo hili wao wenyewe hawakufundishwa Kiingereza vizuri. Lakini katika mipango tuliyonayo, walimu tunaowaongeza sasa ukiondoa wale tuliokuwa tumechukua kwa utaratibu wa *UPE,* moja ya masomo tunayoyaangalia tunapowachagua kwenda katika Vyuo vya Ualimu ni kufaulu kwao kwa somo la Kiingereza na kufaulu kwa somo la Hisabati katika ngazi ya *form four.* Kwa hiyo, hii inaanza kutubadilishia kidogo kuweka nguvu mpya ya kufundisha somo la Kiingereza katika ngazi ya shule zetu za msingi. Lakini tunaiona haja ya kufanya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, mtupe muda tutajitahidi kuboresha ufundishaji wa somo la Kiingereza. Kwa sababu wataalamu wanasema ukianza kulifundisha vibaya ndiyo unaharibu kabisa, afadhali usiliguse ovyo ovyo ni afadhali ulifanye vizuri. Kwa hiyo, tunajiandaa kuweza kulifanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitambue kwamba, katika orodha niliyotaja kwa haraka haraka nimeruka kumtaja Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, naye alichangia katika hoja hii. Nakushukuru sana. Samahani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo moja nilitaka kusema kuhusu Kiingereza.

Kuna Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, alizungumzia suala la kanuni ya uandikishaji na uhudhuriaji wa lazima wa watoto katika shule zetu za msingi na akasema inatakiwa tuweke juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba, wasichana wana mahudhurio mazuri na hawaharibikiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge kwamba, katika kanuni hiyo ikisomwa kwa makini, wajibu wa kusimamia uandikishaji na uhudhuriaji wa shule tumeuweka sasa kwa watawala wa ngazi ya kijiji na ngazi ya Kata. Kwa hiyo, wenye wajibu ni Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji na mle ndani tumeweka adhabu kwa yule ambaye hamwandikishi mtoto kuanza darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka saba na kwa mtoto ambaye hahudhurii. Walimu watakachokuwa wanafanya sasa ni kutaarifu kwa Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji kuhusu watoto ambao hawaji shuleni ili wazazi wao na watoto wenyewe waweze kuwajibishwa na adhabu zimetamkwa katika kanuni ile. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata watambue kwamba suala la mahudhurio ya lazima shuleni na suala la lazima la kumwandikisha mtoto wa miaka saba asome elimu ya msingi tumesema ni ya bure lakini ni ya lazima. Mwenye kutilia mkazo ulazima huu ni Mtawala wa pale Kijijini ahakikishe elimu hii inawafikia watoto wake wote. Kwa hiyo, naomba sana tusaidiane katika kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitambue kwamba, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', pamoja na kuchangia hapa alituletea mchango mwingine kwa maandishi. Naomba aingizwe katika orodha. *(Makofi)*

Sasa jambo la pili, ambalo ningependa kulifafanua kwa sababu limegusiwa na wengi hususan amelitamka kwa nguvu sana Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah katika mchango wake wa maandishi na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kuhusu suala la michepuo ya ufundi. Kwamba, je, tunatoaje elimu ya msingi ama elimu ya sekondari halafu tunaondoa michepuo ya ufundi. Nitamke wazi kwamba, ni uamuzi wa Serikali kuondoa masomo ya michepuo kutoka katika ngazi ya sekondari. Kwa lengo la kupunguza masomo yetu katika ngazi ya sekondari, sasa yanayofundishwa ni 13 tunapunguza yawe manane. Wataalamu wa Elimu wanasema masomo 13 ni *overload* na ndiyo inawafanya watoto wetu wasielewe vizuri. Kwa sababu unapanga vipindi vingi mno bila ku-*focus* kwenye masomo ambayo ni *core subjects for secondary education* na wataalam wanasema masomo yaliyo muhimu katika elimu ya sekondari ambayo mtoto asiyakose ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hapa kwa sababu naelewa katika Bunge hili kuna walimu wengi ni vizuri wajue kwa undani tunachofanya. *Mathematics, English*, Kiswahili, *Biology, Physics with Chemistry, Geography, History* na *Civics,* masomo haya ni *core* kwa Elimu ya Sekondari. Mtu akisema nina Elimu ya Sekondari au nina Elimu ya Msingi hajui hisabati kwa kweli hana Elimu ya Msingi. Hili ni somo linalosaidia mtu aelewe masomo mengine. Halafu huwa tunasema elimu ni ufunguo wa maisha, lugha ni ufunguo wa Elimu kwa sababu unahitaji lugha fulani ili uweze kupata elimu. Kwa hiyo,

ni muhimu sana watoto wajifunze lugha na wataalam wa elimu wanasema kujua lugha moja haitoshi kabisa, *infact* nchi zingine zimefikia wanatumia lugha tatu. Lakini sisi tunasema lugha hizi mbili ni lazima *English* na Kiswahili hakuna ruksa mwanafunzi yeyote kuacha masomo haya ya *English,* Kiswahili na Hisabati mpaka afike Kidato cha Nne, hayo hayaruhusiwi kuachwa. *(Makofi)*

Sasa tunaachaje haya ya michepuo, mchepuo biashara, mchepuo wa ufundi, mchepuo wa kilimo, nimesema katika hotuba yangu masomo haya yana Wizara nyingine ambazo zinafundisha masomo haya. Kwa mfano, *Agricultural* kuna Waziri mwenzangu Mheshimiwa Charles Keenja, masomo ya Biashara hata hapa Dodoma pana Chuo cha Biashara na Dar es Salaam kuna Chuo cha Biashara, masomo ya ufundi kuna mlolongo mzima wa *VETA,* kinachohitajika ni kupanua hizi *VETA* zienee katika kila Mkoa.

Sasa kama mkisoma vizuri katika hotuba yangu ya bajeti, niseme *simultaneously* unafanya *Curriculum Review* ya kuondoa haya masomo lakini unayaingiza ndani ya masomo haya Elimu ya Kujitegemea, tunayaingiza ndani ya masomo haya *Core Subjects,* Elimu ya Kujitegemea *(Education for Self Reliance),* pamoja na Stadi za Kazi *(Life Skills),* unaingiza kwenye *Curriculum* na nitatoa mfano wa somo wa hisabati. Somo la hisabati unaweza ukaingiza ndani yake *Life Skills* na Elimu ya Kujitegemea, kwa kufundisha katika Hisabati, hesabu za Biashara, kuna hesabu zinajulikana kabisa kwamba, ni *Commercial Arithmetic,* kwa hiyo, unahakikisha kwenye somo lako la hesabu kuna *Commercial Arithmetic* ya kutosha ili huyu kijana akimaliza *form four* anaweza kufungua na kuendesha biashara ndogo ndogo hata kabla hajaenda kupata mafunzo ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuhakikisha katika hisabati kuna *geometry* ya kutosha badala ya kuchukua muda mrefu kumfundisha kijana kwenye sekondari kupiga randa na kutengeneza kiti, wewe unamfundisha *geometry* ya kutosha atoke pale anajua kuchora mlango, kuchora dirisha hii haendi kufundishwa tena, akienda *VETA* anaanza kufundishwa namna ya kushika randa na kukata, kuliko inavyofanyika sasa akifika *VETA* anaanza kufundishwa hesabu, anaanza kufundishwa tena Kiingereza mwaka mzima wa kwanza kwa sababu sisi huku tulipoteza muda kutofundisha *sufficient English and sufficient Mathematic.* Kwa hiyo, ndiyo marekebisho tunayoyafanya ya sura hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila somo litatazamwa kubebeshwa *skills* hata *Physics* badala ya kumfundisha *engine* ya ndege ambayo hatakutana nayo, mnaanza kumfundisha *engine* ya mashine ya kusaga, kama ni gurudumu ajue gurudumu la baiskeli. Mimi nilipokuwa *Tabora School* na wengi tuliosoma, tulijifunza ua linaloitwa *hibiscus flower,* lakini ukimfundisha kuchora ua la mahindi au la maharage au la kunde mazao ambayo analima unakuta mtu hajui na ana elimu ya sekondari. Hayo ndiyo marekebisho tutayafanya kuingiza vitu vilivyo *relevant* kwa maisha yake, anatoka pale ana *biology* ya kumfanya aelewe *basic science* ya *agricultural.* Kwa hiyo, waliotaka tufafanue hilo, nawashukuru sana kwamba tumelipa nafasi ya kufafanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine wameuliza suala la lugha. Nawashukuru sana walioileleza vizuri sana jambo hili. Mimi nakubaliana sana

na Mheshimiwa Aggrey Mwanri na wengine waliosema pamoja na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kwamba, lazima tuendelee kufundisha somo la Kiingereza na tulipe uzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini waliotaka tufafanue ni Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, hawakuwa wanapinga wametaka tufafanue nini msimamo. Sasa mimi napenda niseme sera. Sera ambayo naisimamia ya Elimu na Mafunzo iliyopitishwa na Bunge hili mwaka 1995. Inatamka *clearly* tufanye nini, inasema tufundishe elimu ya msingi na mafunzo ya Ualimu wa *Grade A,* kwa lugha ya Kiswahili na tufundishe Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu kwa lugha ya Kiingereza, pamoja na Ualimu wa Walimu wa Stashahada na wale watakaochukua *degree* za Chuo Kikuu hao tufundishe kwa lugha ya Kiingereza.

Sasa mimi sheria ya elimu kwa sababu nasema hiyo ndiyo sera inavyosema na sisemi sera haiwezi kufanyiwa mabadiliko lakini sheria ya Elimu inasema Waziri wa Elimu pamoja na madaraka yote unayopewa kwenye Sheria lazima kila wakati u-*take into consideration* lugha iliyotumika *you must at all times take into consideration the interest of the people of Tanzania.* Lakini napenda nirudie na mimi mwenyewe kama miongoni wa Jumuiya ya wasomi katika nchi hii nakubaliana na sera ilivyo sasa. Nimeombwa nirudie yale niliyosema *take interest,* sheria inasema: "Waziri wa Elimu lazima kila wakati kwa madaraka uliyonayo, uzingatie maslahi ya Watanzania." Kwa hiyo, huamui tu kwa sababu kuna watu wachache wanadhani inatakiwa iwe vipi unaangalia Watanzania wanavyotaka, ndiyo maana nilivyoombwa na Chuo Kikuu niwape Sekondari mbili za Serikali waziendeshe kwa Kiswahili, niliwakatalia kwa sababu mimi nilijua wazazi wanaweza kunijia juu kwa nini nimewapa watoto wao wakafundishwe kwa lugha ya Kiswahili. Kwa sababu wanavyojua mtoto anakwenda sekondari anajifunza kwa lugha ya Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mimi nasema sioni sababu ya kubadili. Ukichukua kwa sera ilivyo sasa, tukimchukua kijana anayesoma mpaka Chuo Kikuu safari yake yote ya elimu ina miaka 18. Miaka tisa ya kwanza iko kwa lugha ya Kiswahili, kwa hiyo, mtu anayesema nchi yetu hatutoi elimu kwa lugha ya Kiswahili nadhani haielewi hii *fact* kwamba, elimu ya awali miaka miwili, mtoto wa miaka mitano na miaka sita anafundishwa kwa Kiswahili. Miaka saba ya *Primary Education* anafundishwa kwa Kiswahili jumla ni tisa. Akienda sekondari miaka minne *form one* mpaka *form four* na miaka miwili kidato cha tano na cha sita hiyo ni miaka mingapi si miaka sita hiyo, akienda Chuo Kikuu *degree* ya miaka mitatu si inakuwa tisa, kwa hiyo, tisa kwa tisa kule tunafundisha Kiingereza na hapa Kiswahili. Lakini tangu akiwa mwanzo hapa somo la Kiswahili linafundishwa kama somo, somo la Kiingereza na somo la Kiswahili yote yanaendelea kama masomo mpaka anapofika kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiri mgawanyo huu ni mzuri na unaendana na hali ya leo ya dunia ya utandawazi ambayo kama alivyosema Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Kiingereza ndiyo Kiswahili cha dunia hiyo ya utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na jani lake la kichaga, amezungumzia shule iliyo kijijini yenye eka 40, lile jani linalenga zimegwe eka 10 kutoka kwenye shule ile. Tumechunguza sisi shule ile wale wanaoiendesha wanaiendesha katika eneo la Serikali kwani ilikuwa shule ya Serikali wakakabidhiwa waendeshe nadhani KKKT wanaoiendesha ile shule. Hilo eneo lenye eka 40. Lakini ni *Public Land* iliyo mali ya Serikali. Sasa utaratibu kama umekabidhi ardhi na shule inaendeshwa na chombo fulani na pana Bodi ya shule pale tungemshauri Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwamba, maombi yake ya ardhi ile ayaelekeze pale kwa wale waliopo kwanza ndipo yatafika kwetu kupitia kwa wale ambao tuliwakabidhi kuendesha pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa juhudi aliyotueleza sisi wote hapa juhudi yake ya kufungua shule za sekondari, hongera sana. Napenda nimwambie tu anatekeleza vizuri sera ya CCM katika kufungua shule na atakapoamua milango iko wazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Grace Kiwelu alitutaka tufafanue suala la usajili wa shule. Usajili wa shule una hatua muhimu tatu. Kwanza, anayetaka kuanzisha shule lazima aombe kusajiliwa kama Mwenye shule anajaza fomu Namba 6 na anayemsajili ni Waziri wa Elimu. Pili, aombe yeye mwenyewe au anayemteua kuwa Meneja wa Shule kwa kujaza fomu Namba 7 na anasajiliwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa sababu yeye anajihusisha na kuangalia uwezo wako wa kusimamia ile shule, kumeneji ile shule. Hatua ya tatu, baada ya kuwa umesajiliwa kama mwenye shule na meneja wa shule yuko tayari unaomba kusajili shule upate *Registration* ya shule ile. Hizo ndizo hatua tatu muhimu za usajili wa shule. Wapo watu wanaovunja hizo hatua akishapata usajili wa mwenye shule na meneja wa shule anafungua shule anaendelea hiyo siyo sahihi. Nimetoa maagizo kwamba, shule haitakiwi ifunguliwe mpaka shule ile iwe imesajiliwa na mtu anayeanzisha shule akachukua wanafunzi kabla ya shule haijasajiliwa anafanya kosa na asitegemee Baraza la Mitihani kumpa mitihani hata Wakaguzi wa Kanda katika ile mitihani ya *form two* hawatatoa mitihani hiyo. Kwa hiyo, nashauri kwamba, utaratibu huu ufuatwe ipasavyo.

Mheshimiwa Margareth Mkanga, ameshauri kwamba, inafaa walimu wetu wote katika Vyuo vya Ualimu tuwe tunawapa mafunzo ya kuweza kumudu elimu kwa wenye ulemavu. Wizara tunalikubali kwamba, wazo hili ni zuri, tutajaribu kuliingiza katika mfumo wetu wa mafunzo ili angalau wawe wanaweza kumudu kwa kiwango fulani. Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa wazo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limehojiwa suala la masomo nadhani hili kuingiza masomo ya *information communication* au *information technology* katika mitaala, pale nilipoeleza masomo ambayo tunayafundisha kuna shule maalum ambazo tutaziteua kufundisha *options,* yaani katika yale masomo manane niliyoyaeleza zipo shule ambazo zitateuliwa kufundisha *options* katika shule teule. Hapo tutafundisha masomo kama *Information Science, Home Economics, Religious Studies* katika baadhi ya shule hayatakuwa katika shule zote. Kwa hiyo, mtu anayechagua ile *option* akienda shule anaweza aka-*drop* masomo mengine lakini si hisabati, si kiswahili, si Kiingereza, anaweza aka-*drop* yale mengi akaingiza moja ya masomo haya ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuna moja alilolisema hapa likanishtua kweli kweli kwamba, vitabu havipitishwi viwe vya kutumika shuleni mpaka wakubwa pale Wizarani walipwe asilimia 10. Mimi nikasema huyu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, anaweza akazua makubwa kweli kweli. Malipo yanayolipwa yametamkwa kabisa katika taratibu zetu, mtu akipeleka kitabu chake anaomba kipitishwe na Kamati yetu inaitwa *EMARK,* analipa shilingi 250,000/= kwa *title* moja na Kamati ile ina watu wafuatao wanaokaa katika Kamati:-

Mwenyekiti ni Afisa Elimu Kiongozi na Wajumbe ni Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari, Mkurugenzi wa Elimu ya Ualimu, Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi, Mkaguzi Mkuu wa Shule, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Mwanasheria wa Wizara, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu, Katibu Mtendaji wa BAKITA, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania, Mkuu wa Kitivo cha Elimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mkurugenzi Mafunzo *VETA,* ndiyo Kamati ambayo inapitisha kwamba, kitabu hiki kinafaa kitumike katika shule za sekondari ama msingi na kiutaratibu Kamati hiyo huteua Timu ndogo yenye utaalamu wa ndani wa ngazi ile ya Elimu kinapotaka kutumika kitabu na hawa, hutumia muda wao na fedha hizo zinazolipwa hutumika kuwalipa ili waweze kuchambua kwa undani kama kinafaa kwa *Primary Education, Secondary Education,* kwa somo lipi, huu ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuliko kutuhukumu tu ningekushauri kama unajua kuna mtu aliwahi kulipwa *ten percent* au kudai *ten perent* kitabu chake kipitishwe yeye kama Mbunge mwenzangu tafadhali uninong'onezee na ukisikia sikia dalili hizo uniambie. Maana yake tusije tukawazulia mambo hawa watu niliowataja ni watu wakubwa sana, wote niliowataja hawa wanashikilia madaraka hayo kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Niende kwenye masuala yaliyoelekezwa kwenye Idara yetu ya Ualimu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamehoji kwamba tunafungua shule lakini Walimu hawatoshi. Mimi nakubali kwamba, *currently* tukitazama hali ya sasa na tulikotoka, hii ni kweli hatukuoanisha vizuri uandaaji wetu Walimu na ufunguaji wa shule. Lakini napenda kuwahakikishia kwamba, katika mpango wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari ambao nimeuwasilisha katika Bunge hili, jambo hili limetazamwa kwa makini sana na ndiyo maana tunachukua hatua kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatua kubwa, ni *bold measure,* kuamua vyuo viwili vibadilishwe kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kile chuo cha Chang'ombe tumekichagua kwa sababu muhimu. Katika kuviangalia vyuo vyetu vyote tumekuta waliotengeneza michoro kile chuo kilijengwa kwa msaada wa Waamerika. Waliotengeneza majengo yale yamejengwa kuweza kubeba ghorofa nyingine kadhaa na kilitengewa eneo la kutosha. Kwa hiyo, kina *capacity*. Tunachofanya pale ni kuongeza majengo na kuanza kutoa digrii za elimu bila kupunguza

stashahada za elimu. *Infact* pale Chang'ombe tutaongeza wanaopata *diploma* za ualimu pamoja na kuleta wanaopata digrii.

Halafu imechaguliwa Sekondari ya Mkwawa. Sekondari ya Mkwawa wanaojua historia, mimi pia naijua kwa sababu nimesoma pale. Ilikuwa inaitwa *St. Michaels and St. Georges.* Kumbe iliyojengwa ni *St. Michael, St. Georges* haikujengwa, lakini ardhi kwa ajili ya kujenga *St. Georges* ilitengwa. Ndiyo maana ukifika pale pana eneo kubwa sana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa ametuambia anapata *pressure* kwamba, lile eneo halitumiki wananchi wanataka kujenga nyumba iwe sehemu ya mji akasema kama hamtumii nataka tuwarudishie wananchi. Ndio tumekuja na wazo kwamba, kile kiwe ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa sababu pana nafasi. Lengo letu ni kwenda walikokwenda wenzetu kuwa na *University of Education.* Tunalenga pale tuwe na *University of Education* kama walivyofanya wenzetu Kenya, *Kenyatta College* kazi yake ni kutoa Walimu. Ni Chuo Kikuu cha kutoa Walimu na sisi ndicho tulicholenga. *(Makofi)*

Halafu hatua nyingine kubwa ambayo tumeichukua kwa ushauriano na wenzetu wa Elimu ya Juu, tumekubaliana kwamba, digrii ya miaka minne kwa ajili ya elimu sio *necessary.* Nawashukuru nimeona Walimu wengi wameanza kupiga makofi hapa na wasomi wengi, inarekebishwa iwe ya miaka mitatu. Lakini pia tumesema tufanye kama walivyofanya wenzetu wa Makerere zamani. Kule Makerere zamani ulikuwa unaweza ukaenda ukachukua *diploma* ukaondoka, ukarudi baadaye ile *diploma* ikahesabiwa kwenye digrii ukasoma miaka miwili ukapata digrii au ukaenda chuo kingine ukasoma miaka miwili. Kwa hiyo, hii digrii ya miaka mitatu itatengenezwa kwa namna ambayo mwaka wa kwanza ni *Diploma in Education* na huyu mwenye *diploma* akienda kufundisha akirudi anasoma miaka miwili anapata digrii. Kwa hiyo, ni suala la kuleta *efficiency* katika *training* ya ualimu. *(Makofi)*

Lakini pia vyuo vingine 12 vya Ualimu kwa hatua, sio kwa mara moja, vitafanywa kuwa *associate college* za Chuo Kikuu, sasa napata tabu kidogo kupata *translation* ya *associate.*

**WABUNGE FULANI:** Shirikishi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** *Associate college* kwa maana ya kutoa ile *diploma* ya Chuo Kikuu kwamba na wenyewe *diploma* yao inafanana na ile inayopatikana kwenye Chuo Kikuu. Lakini wenzetu wa *University* wanasema haiwezi ikaanza holela lazima tufanye marekebisho fulani fulani. Kwa hiyo, tumeamua tutafanya marekebisho hayo lakini namba moja tumeamua kitakuwa ni Chuo cha Mtwara kitaingia katika utaratibu huu. Ile *TTC* ya Mtwara kwa sababu inazo sifa nyingi hasa za upande wa majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka nifafanue hayo kuhusu *measures* tunazochukua kuhusu Walimu. Imeulizwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wengi, nakwenda kwenye Idara ya Sekondari, wengi wameuliza hii mipango inasemwa tutajenga

madarasa, tutajenga nyumba tunaanzia wapi. Najua ni hali ya kila Mbunge kujua je shule zake za eneo zake zinaingiaje.

Mheshimiwa Philip Marmo, alitoa *challenge* anasema kabla hatujaondoka hapa tutoe orodha kabisa. Sasa napenda niseme pale tuliposema tutajenga madarasa katika shule zilizopo za mikondo miwili kwenda mikondo minne ili zikamilike. Hii tunaifanya kama umefanya hesabu ya shule tulizozitaja na yale madarasa tunafanya shule zote zilizo na mikondo miwili na mitatu kwenda mikondo minne. Shule zote kama unayo katika eneo lako inaingia katika mpango wa mwaka wa kwanza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Philip Marmo, hatuna haja ya kutoa orodha hapa. Orodha ni hesabu shule ulizonazo za mikondo miwili na mikondo mitatu kwenda mikondo minne. Kila mmoja maana yake inaweza kupangiwa kama ni ya mikondo miwili inapangiwa madarasa mawili ya mikondo mitatu inapangiwa darasa moja, lakini na kila moja itakwenda na nyumba moja ya Mwalimu. Kwa sababu tumeamua kwamba, kuanzia sasa kuwe na uwiano wa kujenga madarasa na nyumba za Walimu. Madarasa mawili nyumba moja ya Mwalimu, madarasa mawili nyumba moja ya Mwalimu. Tunataka kwenda kwa *speed* hiyo. *(Makofi)*

Sasa liko suala la shule mpya. Katika bajeti tumesema kuna madarasa yaliyopangiwa kwenye shule mpya. Shule mpya zitakuwa wapi. Tumesema shule mpya zitakwenda kwenye maeneo ambako shule haziko. Haziko kwa kiwango gani? Ndani ya mpango tumeweka *target* ya kila mwaka. *Target* ya mwaka kesho ni kupeleka Sekondari asilimia 35 ya watahiniwa wa darasa la saba. Kwa hiyo, kinachotazamwa ni Wilaya hii inapeleka *percent* gani. Mle ndani ya Wilaya tunaelekeza wataalamu wetu waangalie Tarafa hii inapeleka sekondari *percent* gani. Ile ambayo iko chini ya *35 percent target* ndiko huko tunakotakiwa tupeleke shule ili nao waweze kwenda kwenye *35 percent. (Makofi)*

Kwa hiyo, tumepanga *target* ya kila mwaka mpaka tutakapofika 2010 kila Wilaya ya Tanzania na kila Tarafa ya Tanzania iwe na *capacity* hiyo ya kupeleka *50 percent* ya watahiniwa wa darasa la saba. Ninachoomba ni kwamba, wataalamu wetu watumie kigezo hiki kwa makini, kisitumike kwa kupendeleana na kujenga *access capacity* katika eneo moja ndani ya Wilaya. Kwa mfano, nilikuwa naambiwa Ludewa kuna eneo wanakokaa ndugu zetu wanaitwa Wakisi, karibu ya Ziwa Nyasa, kufika ni kwa *problem*. Sasa ni juu ya Wilaya ya Ludewa ijue Wakisi nao ni Watanzania, Wamanda nao ni Watanzania. Wabunge wa Wilaya ya Mbulu mjue na Wahadzabe nao ni Watanzania na Wanguu nao ni Watanzania. Huko wanakotoka lazima tuweke shule kujenga *capacity* hiyo tunayohitaji. Tukienda kwa mwelekeo huu, nina hakika tunaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeulizwa madai ya Walimu kwamba, Wizara yangu haijaunda Kamati. Naona hili jambo nilitolee maelezo. Wizara yangu kwa madai ya Walimu tuliyokuwa nayo ni ya shilingi 2,590,571,285. Hizi ziko katika mafungu mawili. Fungu la kwanza ni posho ya uhamisho, likizo na matibabu, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, ndicho ninachozungumzia hapa maana yake ndiyo *Vote 46,* ni shilingi

1,246,394,879. Malimbikizo ya mishahara na malimbikizo haya yanatokana na kusitishwa kulipa kulikofanyika mwezi Februari, 2003 mpaka Mei, 2004 kwa sababu ulikuwa unaandaliwa utaratibu mpya. Kwa hiyo, malimbikizo ya mishahara yalikuwa ni shilingi 1,344,176,406, jumla 2,590,571,285. Sasa kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 Juni, 2004, tukiwa hapa Bungeni Wizara yangu imepokea kutoka Hazina fedha za kulipa malimbikizo, fedha za kulipa posho ya uhamisho, likizo na matibabu. Fungu hili la kwanza la Sh. 1,246,394,879 tukapokea fedha tarehe 18 Juni, 2004 na maagizo ya Hazina waliyopewa wataalamu wangu ni kwamba, fedha hizi lazima zilipwe kabla ya mwisho wa fedha. Pale pale wakaanza kufanya kazi na mpaka tarehe ya 30 wakawa wamemaliza kulipa fedha hizo zote.

Kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatamka hapa Bungeni kwamba, tuchukue hatua ya kufanya malipo, kikundi cha wataalamu wa Idara ya Fedha kule Wizarani kwangu walikuwa tayari wanatekeleza jambo hilo na kufanya malipo. Kwa hiyo, ilikuwa ni kazi inayoendelea na wakalipa malipo yote zimebakia shilingi 36,000,000, ambazo ni *improperly vouched,* yaani vocha zake za madai sio sahihi, zimerudishwa huko wanadaiwa wanaofanya madai yale walete ushahidi wa kuthibitisha zaidi. Kwa hiyo, hiki ndicho kilichofanyika. Katika mazingira hayo, kama tunaamua hapa Bungeni iundwe Kamati katika kila Wilaya, kule kwangu fedha zimefika zinalipwa, sikuona sababu ya kuingilia zile hatua zinazoendelea, napenda kulitaarifu Bunge kwamba, kwa masuala ya uhamisho, likizo na matibabu, malipo yamefanywa kwa kiwango hicho. Kwa Walimu wa Sekondari na Walimu wa Vyuo vya Ualimu na Walimu walio katika Idara yetu ya Ukaguzi, kama kuna madai mengine ya kipengele hicho yakija tutayashughulikiwa kwa utaratibu wa kawaida. Lakini kilichokuwa malimbikizo hakipo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye malimbikizo ya mishahara. Malimbikizo ya mishahara baada ya kuwa yamesitishwa, Hazina wametoa Waraka wa Hazina Na. 12. Waraka huo umeleta fomu mpya inayotakiwa ijazwe na wale wanaodai. Utaratibu wa zamani ilikuwa mtu akipata barua ya kupandishwa cheo, wanasubiri ajibu kwamba, amekubali halafu *arrears* na malipo yake ya ziada yanaandaliwa na Idara ya Uhasibu. Imeonekana utaratibu huu wa maandalizi ya malipo haya una mianya. Kwa hiyo, ndiyo maana Hazina wametoa *salary arrears claim form* ambayo tumeambiwa ijazwe upya. Waraka huo umefika tarehe 30 Juni, 2004, hata ningeunda Kamati sasa kwa kweli haina kazi kwa sababu nyaraka hizi wanapelekewa wale Walimu wahusika na kuna mahali wanajaza majina na madai na kuthibitisha ni ya haki na mkubwa wake kama ni *Headmaster* ama Mkuu wa Chuo, kuna mahali anasaini kuthibitisha kwamba, madai haya ni ya haki na madai hayo yakifika fedha zipo katika bajeti ya kuweza kufanyia malipo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, zimetengwa shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, ningependa jambo hili lieleweke kwamba ndipo tulipofikia.

Lipo suala nimeona limehojiwa hapa kuhusu Shule za Sekondari zilizositishwa mitihani ya mwaka huu. Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa

Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, walitaka kufahamu maamuzi kuhusu matokeo ya shule zilizofutiwa matokeo ya mtihani. Ninachoweza kulitaarifu Bunge ni kwamba, tunavyo jumla ya vituo 1,279 vikiwemo vya *Private Candidates* 345 na *School Candidates* 934, vilivyosajiliwa kwa ajili ya mitihani ya Novemba, 2003. Waliofanya mtihani walikuwa 109,523 na watahiniwa 553 ndio walionekana kufanya udanganyifu. Baadhi yao udanganyifu wao ulithibitika moja kwa moja kwa sababu taarifa ilitoka kwa msimamiaji mmoja anasema kwamba, wameonyeshana mitihani hao wafutiwe moja kwa moja. Lakini kwa watahiniwa karibu 401 ilihitajika kufanya uchunguzi kwa sababu udanganyifu ule ulionekana katika usahihishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, iliundwa Kamati ikafanya uchunguzi, walipangiwa wafanye uchunguzi kwa siku 90, walimaliza ndani ya siku 90 ila uchunguzi wenyewe ni jambo kubwa si jambo dogo kwa sababu wanapitia *scripts* zote zilizofanywa, masomo yote kwa watoto 400 ni kazi ya muda mrefu. Lakini nafurahi kulitaarifu Bunge kwamba, juzi tu walinitaarifu wamemaliza kazi hiyo na Mtendaji Mkuu wa Baraza la Mitihani yuko hapa amekuja kunipa *briefing* na nimempangia atupatie *briefing* Wizarani kesho na mara baada ya *briefing* hiyo matokeo ya hatua hiyo yatatangazwa. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira, zimebaki siku mbili, tatu, tu matokeo yatatangazwa. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kusema kwamba, hilo suala inabidi tuwe waangalifu sana katika masuala haya yanayohusu mitihani kwa sababu tunataka tutoe elimu lakini pia tupime mambo haya tuweze kutoa haki kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru Wabunge wengine waliochangia ambao walikosekana kwenye *list* yangu, Mheshimiwa Raphael Mlolwa kutoka Kahama, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir kutoka Mchinga, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, wote hao nawajumlisha katika wale ninaowashukuru. Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', nadhani nimekwishamtaja, nadhani nimewataja wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mambo ya kufafanua ni mengi sana, naomba tu nieleweke kwamba, yale ambayo sikuyagusia katika muda huu nilioutumia hapa ni yale ambayo naona tutakwenda kuyafanyia kazi ipasavyo. Naomba Waheshimiwa Wabunge, mtuamini kwamba, mmetukabidhi kazi ya kwenda kufanya, ninachoomba tuendelee kushirikiana na napenda kuahidi kwamba, kuhusu mpango huu wa MMES, miongozo ya namna ya kuandaa mipango ya Wilaya na mipango ya mkoa inaandaliwa na Wizara yangu na italetwa huko Wilayani ili tuweze kuelekeza uwekezaji huu kule kunakotakiwa ili ifikapo mwaka 2010 kweli tuweze kupeleka asilimia 50 ya watoto wetu wapate Elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni**

Kif. 1001 - *Administration and General* ............. Sh. 5,786,483,200/=

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu kidogo hicho cha 1001 - Uendeshaji, Waziri amesema Wilayani tutaletewa mwongozo wa utekelezaji wa Mradi huu wa MMES. Sasa ufafanuzi ambao ninaomba kutoka kwake pengine utasaidia kuboresha mwongozo huo. Ufafanuzi ninaouomba ni kama ifuatavyo: Fedha hizi ni nyingi kama ilivyokuwa kwenye MMEM. Katika MMEM tumetumia miundombinu iliyoko pale Wilayani katika Ofisi ya Elimu, Ofisi ya Mkurugenzi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na miundombinu hiyo sasa ni kama imechoka kwa sababu Wilaya zingine zinaweza kuwa na *TASAF* inatumia miundombinu hiyo, *DSPCE, DRDP* na kadhalika.

Katika mwongozo anaotarajia kutoa atatumia miundombinu gani, fedha zitatumwa moja kwa moja kwenye shule ambapo nimesema Mwenyekiti wa Kamati ya Bodi baadhi ya Wenyeviti bado ni wale viongozi wa kimila? Idara ya Sekondari haina Ofisi Wilayani. Najaribu kupata picha mwongozo huo utakuwaje. Tuna ajira mpya tutafungua Ofisi mpya katika Wilaya. Wilaya ambayo kama ya kwangu shule ambazo natarajia zitafaidika na mradi huu ni 16. Najaribu kufikiria miundombinu gani tutaiunda pale Wilayani. Atueleze ili katika kuboresha miundombinu hii tuhusishwe. Naomba ufafanuzi huo Ndugu Mwenyekiti.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mheshimiwa Philip Marmo, kwa kuuliza swali hilo ambalo linanipa fursa ya kufafanua. Fedha hii kama mnavyoona imepangwa kwenye *Vote 46. Vote* hii ina *vote holders*. Kwa hiyo, pale ambapo tunaongeza madarasa kwenye shule, tuna *Headmaster* kama vote holder. Tunaongeza madarasa pale shuleni tuna Headmaster kama *vote holder.* Tuna Bodi ya Shule ya kumsaidia katika maamuzi lakini pia katika maelekezo tutakayotoa ni kwamba, Wilaya isijitenge katika mpango wa Wilaya wa Elimu ya Sekondari itaonyeshwa. Lakini *flow* ya fedha itapita kwenye *line* hiyo. Itakwenda kwenye *vote holder* kama zinavyokwenda fedha nyingine za kuendeshea shule na matumizi yake yatapitishwa, *Headmaster* hatafanya peke yake atatumia Bodi ya Shule.

Nimesikia nilichoambiwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Bodi zetu nyingine za shule hazina Wajumbe ambao wana uwezo wa kutosha. Kwa hiyo, natarajia kuitazama upya kanuni hiyo. Kwenye Elimu ya Msingi tulipoanza tulisema angalau Mwenyekiti awe ana Elimu ya Sekondari. Halafu kwenye Sekondari hatujasema hapa. Kwa hiyo, kwa kweli kuna kasoro. Ndiyo maana Mheshimiwa Semindu Pawa, alituambia siku moja kwamba, mganga wa kienyeji ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule mojawapo katika jimbo lake. Sasa hiyo ilikuwa ni sifa labda alichangia sana katika ujenzi wa sekondari lakini hafai katika usimamiaji. Napenda kuahidi kwamba, tutaitazama upya *regulation* hiyo na ku-*specify* sifa za Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Bodi ili wateuliwe kwa kufuata sifa hizo. *(Makofi)*

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimemwomba Waziri azungumzie kidogo kuhusu ajali za moto zinatokea shuleni hasa Mkoa wa Kilimanjaro. Lakini suala hili nilihusisha kwamba, Wizara ina mkakati gani katika *prevention measures.* Kwa mfano, kuanza sasa kuhakikisha shule hizi zinajengewa *fence* hata kama ni kwenda kwa awamu. Kwa sababu shule hizi hazina uzio wowote, kwa hiyo, mtu yeyote anaweza akaingia na kutoka saa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate maelezo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifafanue kwamba, sehemu ya mafungu ya *SEDEP* ni ukarabati wa shule tulizonazo na utakuta tumeeleza kwamba, tutaangalia na marekebisho ya miundombinu ya shule. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba, hilo analolisema tutalizingatia tutakapofanya ukarabati wa shule. Katika mwaka huo wa kwanza utaona tumepanga shule 40 kuzifanyia ukarabati, shule tulizonazo. Kwa hiyo, tutazingatia masuala haya.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri, wakati akijibu hoja za Wabunge kuhusu michepuo katika kufundisha Elimu ya Sekondari kama vile michepuo ya Kilimo, Useremala na Ufundi, alisema kwamba, kutokana na lengo la kupunguza masomo na vile vile kutilia mkazo masomo yale muhimu, basi ndiyo maana amepunguza masomo hayo. Nilitaka kusema kwamba, vile ile mkazo utakuwa ni kufundisha *self reliance* bila *self reliance* kwa vitendo. Kusomea Udaktari bila kutibu wagonjwa mpaka unamaliza udaktari. Nilikuwa na-*quote* kitabu chake cha hotuba hiki ukurasa wa 11 ambapo Waziri ame-*quote* vizuri sana Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya ufundi wa kisasa ni kwamba, unatakiwa uwe na *Engineer* mmoja kwa *Technicians* watano na Mafundi Mchundo 35 mpaka 40, *one to five, five to thirty five, fourty.* Sasa kwa uamuzi huu wa Wizara ni kwamba, uhusiano wa *Engineer* mmoja na *Technician* na Mafundi Mchundo utapungua. Ili kukidhi nia hii napongeza na kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Huenda katika nchi yetu tangu tupate uhuru tuna shule tatu tu ile ya Arusha ya Ufundi, pale Dar es Salaam na ile ya Mbeya. Ile ya Mbeya inatakiwa kiwe Chuo Kikuu na kile Chuo cha Dar es Salaam, nadhani kimepandishwa hadhi ya Chuo Kikuu, kwa hiyo, kuna shule moja tu ya ufundi. Kwa hiyo, kwa uwiano huu wa *one to five to thirty five* kwa nchi yetu hapa hatuna *Technicians.* Katika kutoa mafunzo kila ngazi ina mkazo wake na lengo lake.

Kwa hiyo, hoja yangu hapa ni kwamba, Waziri ametoa maelezo ya kufuta masomo haya, mimi naelewa. Lakini hakusema atafidiaje tatizo hilo ambalo linazidi kupungua katika nchi yetu, vyuo vyote vinataka kuwa Vyuo Vikuu. Kwa mfano, Shule ya Mazengo ilikuwa na vifaa. Shule ya Ufundi Tanga, Moshi na kulikuwa na Walimu katika shule hizo. Kuna ukimya hapa, je, vifaa vya Mazengo, Tanga Ufundi, Moshi na mahali pengine penye vifaa kama hivyo vya ufundi, kwa kuwa sasa tunaamua kuondoa michepuo hiyo, isingekuwa vizuri vifaa hivyo wakaamua kwamba tubakize walau shule chache na walau huu mkakati wa kudumisha *formula* hii tukawa na vifaa hivi vinatumika vizuri kuliko tukinyamaza kimya. Naomba ufafanuzi.

Pili, anafanya vizuri hakuna mhisani anayetusaidia Shule za Ufundi. Hizi Shule za Sekondari zinajenga *awareness* tu na mwamko. Hata kama Watanzania wote wangekuwa na digrii kama ni za *grammar* au Kiswahili bila kuwa na uwezo wa kuumba vitu kwa Elimu ya Ufundi, tutabaki maskini hivi hivi. Nilikuwa naomba kama Serikali si tungekuwa na mpango huo huo kama wa MMES au wa Msingi katika Elimu ya Ufundi, huu wa katikati wa *Technicians* kama tulivyokuwa na *VETA* hapa nchini kusudi kukidhi lengo hili la *self reliance,* ambayo tunaihubiri katika *philosophy* yetu. Naomba ufafanuzi kwa maana ya vifaa vile ambavyo vimebaki kwenye Shule za Ufundi ambazo sasa zitakuwa hazitilii mkazo maeneo hayo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukubaliana naye kwamba, anavyosema ni sahihi kwamba, unahitaji kuwa na uwiano fulani kati ya *Engineers* na Mafundi Mchundo. Kweli lazima uwe na uwiano huo. Lakini ninachosema katika bajeti hii si kazi ya Shule ya Sekondari kufundisha Fundi Mchundo, ndiyo ninachosema. Si kazi ya Sekondari kufundisha Fundi Mchundo kwa gharama ya kukosa kufundisha vizuri Elimu ya Sekondari.

Sasa nije kwenye lile analosema tulikwishakuwa na vifaa vya ufundi kwenye shule alizozitaja Mazengo, Tanga, Moshi. Ni kweli tulikuwa na chuo. Ukitaka kujua namna mambo haya tulivyokuwa tunayafanya visivyo, tulikuwa na Chuo cha Ualimu Kleruu kazi yake kufundisha Walimu kwa ajili ya Shule za Mchepuo. Tulikuwa na Chuo cha Ualimu Monduli kazi yake kufundisha Walimu wa *Agriculture.* Badala ya kufundisha Walimu wa masomo ya sekondari hufundisha Walimu wa *Agriculture.* Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Jackson Makwetta kuwa, kabla sijafikia uamuzi huu, nilitembelea shule na nikaona mambo ya ajabu. Ukienda hizi Shule za Ufundi utakuta vile vifaa vya ufundi ni vile vile ulivyoviweka ulipokuwa wewe Waziri wa Elimu. Vimechakaa kabisa, havifanyi kazi. Yaani ni kufundisha ufundi kwa ubabaishaji kwa sababu *financing* inatushinda. Vifaa hakuna, unakuta mashine ile wanaita sijui *liaise machine* imekwisha, *no tools,* kwa hiyo, tunapoteza muda. Sasa Serikali tunafikiria nini kuhusu jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na *Education Sector Development Program (ESDP),* tulitazama ngazi zote za elimu mpaka *University* tukasema tunahitaji kuziongeza na tunahitaji kuboresha, lakini uanzie wapi? Tukasema uanze na *primary,* unakwenda *secondary*. Katika *next phase* sasa itakuja *Vocational Education Development Plan,* halafu *Higher Development Plan.*

*Actually, initial team* ya *World Bank* iko hapa kuzungumza na sisi juu ya ku-*finance* ngazi hizo mbili, *Vocational* na *University* ili *pyramid* ile ninayoizungumzia iliyoko hapa chini iweze kufanyika, ni lazima upanue hapo juu. Lakini hata *World Bank,* hata nani ukimwambia unapanua, kwa maana ya kupanua, mimi nazungumzia hapa, unapanua huku juu. Ukisema unapanua hapa na hujapanua huku chini haiwezekani! Huwezi uka-*expand Higher Education* wakati huja-*expand primary* na *secondary,* haiwezekani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually,* napenda niseme kwamba, haya tunayofanya kwenye *secondary* sasa yatawezesha hayo ya ngazi za juu. Tutapiga hodi kwenye *Wampesa* tukope. Wako wanaosema tuogope kukopa, tutakosea. Hii fedha ya *World Bank* miaka 40, miaka 10, *grace period and interest free.* Miaka ya kwanza 10, *one percent interest,* miaka inayobakia 20 unapolipa t*wo percent interest,* wakati huo wewe unatoa vijana laki tano wenye Elimu ya Sekondari wanaingia katika ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wako wanaosema tuta-*sustain* vipi? Uta-*sustain because this time around,* uchumi wetu unakua kwa mara mbili ya *gross rate* ya watu na tunataka kuongeza zaidi ya hapo. Kwa hiyo, tusiwe waoga, haya ndiyo yatakayofuata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ndiyo msimamizi wa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, 'kupanua' ni haki aseme hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1001, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Namshukuru sana kwa maelezo yake ya ufafanuzi kwamba, sasa katika bajeti kwa mwaka ujao hakutakuwa na masomo ya mchepuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yake katika ukurasa wa 12 ametuonyesha kwamba, shule zimeongezeka kutoka 649 hadi 828. Kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengi ni ukosefu wa Walimu na Walimu hawa wamekosekana katika *basic subjects* na katika shule zetu za sekondari masomo aliyoyataja, Kiswahili, *English, Mathematics, Geography, History* na *Biology,* yalikuwa *compulsory* mpaka *form IV,* ila unapofika *form III, Physics, Chemistry* na masomo ya biashara ndiyo unachepua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, hawa vijana ambao upeo wao ni masomo ya *arts* na hapa wanalazimishwa wachukue *Physics* na *Chemistry* na Walimu kwa hakika hawapo wa kutosha mpaka hiyo programu ikamilike. Je, wataweza kufanikiwa kufaulu vizuri? Naomba ufafanuzi.

La pili katika hilo hilo, amesema kutakuwa na baadhi ya shule zitakuwa na *option* kwa kuongeza masomo ya *IT* na *Religious Studies.* *Religion* inafundishwa kila shule, je, anataka kufuta *religion* katika shule zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuliza sana suala la mishahara, tunashukuru amelifafanua, lakini anatuhakikishia vipi kwamba sasa Walimu wapya watakaoajiriwa, maana wanapoajiriwa bajeti yao inakuwa imeishaandaliwa, hawatacheleweshewa mishahara tena kwa muda wa mwaka mmoja au zaidi kama ilivyo sasa? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mambo haya unapoyaweka kwenye mabadiliko si suala la kuzima kama unavyozima taa. Siyo kwamba kuanzia mwaka kesho basi hakuna mchepuo, hapana. Tunachofanya una-

*phase-out intake* inayokuja huchukui kwenye masomo hayo, lakini wale ulionao na wamekwishaanza, unakwenda nao mpaka wanamaliza, ndiyo *process* tunayoichukua. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba, hawataathirika wale tulionao.

Wakati huo huo tumesema tuna-*expand capacity* ya Chang'ombe na Mkwawa. Mambo haya tunayaanza mara moja, hatuwezi kutangaza hapa halafu tukawa ni watu wa kuchelewa chelewa. Tangu tumetangaza hapa, *it means* mwaka 2005, shule kama ya Mkwawa hatuchukui *intake* ya *form five* kwa sababu tunaanza hii kazi nyingine. Kwa hiyo, una-*phase-out* moja unaingiza nyingine *and therefore* wale wa *diploma* wanaanza kutoka baada ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, tunaanza kuwapata Walimu wa *Diploma* baada ya mwaka mmoja tukianza nao mwaka kesho katika hii *syllabus* mpya. Kwa hiyo, mambo haya yameandaliwa kwa sura hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maria Watondoha, ameuliza swali la pili kwamba, tunapozungumzia kufundisha *religion* kama *option* katika shule maalum maana yake tunafuta kipindi cha dini katika shule nyingine, siyo. Kipindi cha dini kitaendelea kufundishwa kama kawaida. Hapa nazungumzia somo la *religion* kwa maana ya kutahiniwa. Tuna somo linaitwa *Islamic Studies* na *Bible Knowledge.* Nazungumzia masuala haya kwa maana ya masomo yatakayotahiniwa yatafanywa katika *Special Schools,* lakini kile kipindi cha dini ambacho huwa kinakuwepo katika shule ambapo anakuja mwalimu wa dini fulani kufundisha watu wa dini ile, utaratibu huu utaendelea kama kawaida lakini bila kutahini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mishahara ni kwamba, mimi kama Waziri wa Elimu, nakuwa na masikitiko Walimu wangu wasipolipwa. Isije ikafikiriwa naona raha, mimi nasikitika Walimu wangu wasipolipwa. Wawe Walimu wa Shule za Msingi au wawe Walimu wa Sekondari, mwalimu asipolipwa *I am very touched,* kwa sababu najua ita-*affect performance* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, nitafanya kila aina ya jitihada pamoja na wenzangu ndani ya Serikali, kuhakikisha kwamba, Walimu wanalipwa *more efficiently* na sasa hivi zipo *system* zinatengenezwa kuondoa taratibu zilizokuwa zinatukwamisha.

Kwa hiyo, naomba mtupe muda, kila tunapopata *pressure* hii hatukai, tunakwenda kuangalia tu-*improve* namna gani na nina hakika tutapata *improvement* inayohitajika. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pengine kabla Katibu hajaendelea, nataka tu kutoa ufafanuzi kwa jambo dogo tu. Katika hao wanne ambao wamechangia kipindi hiki, nimepata ki-*note* kutoka kwa mmojawapo kwamba, alikuwa anataka kuendelea kupata *clarification*. Sasa maelezo ni kwamba, ukiona Mheshimiwa Waziri amejibu na bado ungependa kupata *clarification,* basi endelea kusimama hata kama

nimemtaja mwingine, yule nitamkalisha utaendelea kupata nafasi. Nilitaka kuweka hiyo sawa ili msipate kukereka wakati nafasi ipo. *(Makofi)*
Kif. 1002 *Finance and Accounts* ........................... Sh.219,951,000/=

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu hiki 1002 nitaomba tu maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu napenda Wizara hii ipate pesa nyingi na hapa kuna sifuri sifuri nyingi ambazo sikuelewa sifuri zote hizi hawatafanikiwa au vipi, kwa sababu *Personnel* hii ya kwanza kifungu 250100 utakuta kwamba, kuna pesa zake hapa ni nyingi tu, hata hizi za *Employment Allowance* ni nyingi tu. Sasa, unapokuja kwenye kifungu cha 260800 - *Training Expenses,* katika hii *section* ya *Finance and Accounts* hamna *training* kwa mwaka mzima kuna sifuri. Hapo naomba *clarification* kidogo anipe matumaini kwa hawa ndugu walioajiriwa wanapata mshahara au hawapati?

Pia, bila kupoteza wakati, tuangalie hiki kifungu 270300 - *Vehicle and Mobile Equipments,* hali kadhalika ni sifuri sifuri mwaka mzima wa Bajeti. Hapa kidogo hawa watu sijui wanafanya fanyaje kazi zao?

**MWENYEKITI:** Endelea hapa kwenye kifungu hiki hiki. Maelezo yako nadhani yameeleweka kwamba, ungependa maelezo mle sehemu ya sifuri sifuri kwa nini wasitengewe pesa, nadhani ndiyo hoja yako?

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kwa sababu suala la elimu nalitilia mkazo sana.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa, kama ni sahihi basi tumpe nafasi ajibu.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu unipe nafasi tu kidogo ya kwamba, ninapoona sifuri hata kwingine kutanitia wasiwasi na mimi katika suala la elimu hata katika Jimbo langu la Vunjo liko katika mstari wa mbele sana. Kwa hiyo, akiweza ku-*clarify* hii moja itanisaidia na huku kwingine niweze kuendelea bila wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweza kuamua kwamba hazitoshi inabidi uchukue kwenye Idara zote ujumlishe *Training Expenses,* ndicho alichokuwa anakihoji. Ukitazama Idara moja tu hutapata picha kamili. Hii ukienda Idara ya Uhasibu utakuta kuna pesa zake, *Policy and Planning* zipo, *Administration and General,* utakuta zimepangwa fedha nyingi tu. Kwa hiyo, ukijumlisha zote napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mipango ya *Training* kwa mwaka huu fedha za *training* tumewekewa za kutosha. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 *Policy and Planning* ............................ Sh.816,454,500/=

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sikusudii kufanya lolote lile la ajabu hapa, ila tu niishukuru Serikali imekubaliana nami kwa wazo la kuingiza angalau *Special Education Dose* kwa kila mwalimu. Sasa lengo katika utaratibu huu niulize tu kwamba, wamefikiria utaratibu huu utaanza rasmi lini?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatua ya kwanza nzuri ni kwamba, wazo tumelikubali na katika hatua itakayofuata ni Idara yetu ya Elimu ya Ualimu, watakapoitazama Mitaala ya Mafunzo ya Ualimu wataliingiza hili jambo na wataangalia utaratibu wake. Kwa hiyo, siyo rahisi niwe *very specific* tutaanza lini, lakini ni jambo ambalo tunalikubali kwamba ni wazo zuri katika *process* ya ku-*review* mitaala, tuta-*take into consideration* na tutaendelea kutaarifiana na Mheshimiwa Mbunge hapa kwa kadri mwaka unavyosonga mbele. Nakushukuru sana.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi ya kwangu ni kwamba, katika *VVote* hii kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004, tulizungumzia kuhusu *Umbwe Day Secondary.* Shule hiyo ilibidi ihame katika sehemu ambayo Wananchi tulijenga yale majengo na Waziri aliahidi kwamba, Serikali itafidia yale majengo. Sasa tumemaliza mwaka nafikiri nikirudi Jimboni wataniuliza Waziri safari hii amesemaje? Sasa sijajua ni vipi kuhusu fidia hiyo, ningetaka ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anaelewa vizuri sana kwamba jambo hili tulikwama wapi kwa sababu ilikuwa kwanza wao waanze kujenga Shule ya Kutwa, isajiriwe rasmi ili tupate utaratibu wa fedha kuweza kutiririka kutoka Serikalini kwenda kufanya ile kazi. Sasa hivi ameweka jitihada shule ile imekwishasajiliwa, kwa hiyo, sasa inaingia katika shue zilizopo za kuongeza mikondo ili ifikie kuwa na mikondo minne. Kwa hiyo, ukiniuliza tunaanza lini, nasema inaingia katika awamu hii ya kwanza ya madarasa tunayojenga katika shule zilizopo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini wakati tunaanza kujitolea kuhusu ujenzi wa hiyo Shule ya Sekondari ni Tarafa nzima ilichangia pale. Sasa wanachouliza ni kwamba, yale majengo yamebaki pale, je, hakuna namna ya kufidia? *Of course* hii tunayoendelea nayo ya kawaida ni watu wote, lakini kuna michango ya watu. Sasa tukawajibu kwamba hii haitafidiwa tena?

**MBUNGE FULANI:** Mchaga kwa hela!

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Kuna mtu mmoja huku amesema Mchaga kwa hela! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwamba, hizi shule si kwamba Serikali inakuja inajenga na watu wamekaa hivi hivi. Mtakuta kila mahali nimesema ni ruzuku ya kusaidia. Kwa hiyo, napenda

kumhakikishia kwamba, hiyo shule wanayoijenga inastahili na itapewa ruzuku ya maendeleo kwa kila darasa shilingi milioni saba na kila nyumba ya mwalimu shilingi milioni tisa. Tukishaelewana hivi sasa pana kasi gani ya ujenzi pale, naomba Mheshimiwa Thomas Ngawaiya tuwasiliane tu. Kama hizi tunazopanga mwaka huu hazitoshi aje, lakini kwamba tunafidia kwa kusema yale madarasa yako pale, hapana. Watoto wanaosoma kwenye yale madarasa pia ni Watanzania na wanaosoma kwenye yale madarasa ya *border* yanayotumika pale ni Watanzania hao hao. Kwa hiyo, nguvu ya kifedha ya Kitanzania itaingia kusaidia kwenye zile mnazojenga za kutwa pale na mimi nafikiri hiyo inamtosha kabisa.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu 1003, kwenye mchango wangu wa maandishi, nilimkumbusha Waziri ahadi ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa alipotembelea Wilaya za Wafugaji za Ngorongoro, Monduli, Simanjiro na Kiteto. Alisema kwamba, Serikali itajenga sekondari moja katika Wilaya hizo mwaka 1998. Ikawa tukiuliza hilo tunaelezwa kwamba hakuna fedha. Kuanzia mwaka 2003, tukaahidiwa na Serikali kwamba, tungoje mpango huu wa MMES. Sasa MMES imekuja, imetukuta na Waziri alieleza utaratibu wa kupata sekondari hizo za kujengwa na Serikali. Je, hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais itakuwa katika utaratibu huu alioeleza kwamba tutaomba kufikia *percent* ya watoto wanaokwenda *form one* ama hiyo itashughulikiwa kipekee?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa anavyosema Mheshimiwa Parseko Kone, nilimwambia kwamba, ahadi ile ya Mheshimiwa Rais tutaitekeleza katika mpango huu. Kama angeangalia takwimu za Wilaya zake za sekondari walizonazo na zile zinazohitajika kupeleka sekondari, asilimia 50 ya watahiniwa wa darasa la saba na watahiniwa hao tunaowafanyia hesabu ni wale walioingia mwaka 2002 tulipofuta ada. Ataona dhahiri kabisa kwamba, alichoahidi Mheshimiwa Rais sasa tutafanya mara kadhaa zaidi. Haitakuwa hiyo moja, tutafanya mara kadhaa zaidi na Wizara tumelenga kwamba, kila Makao Makuu ya Wilaya pawe pana sekondari inayokwenda mpaka kidato cha sita. Nadhani tukijenga pale Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto sekondari inayokwenda mpaka kidato cha sita, pamoja na hizo nyingine zitakuwa zinaahirisha hapo, Mheshimiwa Parseko Kone ataridhika kabisa kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais imetekelezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Alikuwa anasema ni Simanjiro.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Samahani, ni Wilaya ya Simanjiro.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kifungu 1003 swali langu katika *Policy and Planning* ni juu ya Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa nne anasema Shule za Awali zimeongezeka kwa asilimia 39.6, lakini katika utaratibu wake hajaonyesha chuo chochote ambacho kinafundisha Walimu wa Shule za Awali, hakuna *Scheme of Service* yao ya Shule za Awali. Kwa hiyo, hizi Shule za Awali

anazosema zimeongezeka ni za binafsi? Maana lengo la Serikali ni kuhakikisha katika kila Shule ya Msingi hata vijijini wana Shule za Awali ambako watoto wanaandaliwa.

Je, Serikali imeandaa utaratibu gani kwa ajili ya kuhakikisha tunapata Walimu wenye sifa wa Shule za Awali?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifafanue kama ifuatavyo: Hatuwezi tukafanya kila kitu kwa pamoja. Kama Mheshimiwa Mwalimu Mary Watondoha ameangalia, tangu mwaka 2000 tumeongeza Wanafunzi wa Shule za Msingi kutoka milioni 4.3 mpaka leo tuna milioni 7.08. Ili tuweze ku-*cope* na ongezeko hilo kwa wanafunzi, tulihitaji Walimu wa Shule za Msingi 45,000. Kwa hiyo, kwenye vyuo vyetu tumetoa umuhimu wa kwanza kuwafundisha hao Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Shule za Awali tumeachia Halmashauri za Wilaya na Wananchi kuzijenga na Walimu sehemu kubwa wanatumika wale wale, ndiyo maana tumesema iwekwe kwenye Shule ya Msingi. Nakubali kwamba, hatufanyi suala hili kwa ufanisi sana, *we are limping along,* lakini katika hatua ambapo tutafika tumekamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, tutaanza sasa kuziangalia hizo *refinements* za kufanya *specialisation* tuwe na Walimu watakao-*focus* kufundisha katika Shule za Awali. *Concern* yake naielewa, nakiri hatujaanza kufanya kwa ufanisi mzuri katika hatua hii, lakini naahidi kwamba, katika hatua inayokuja tutajitahidi kuboresha kazi hiyo.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa tunao upungufu sana wa Walimu, je, anapotuambia kwamba tutatumia Walimu wale wale wa Shule ya Msingi hasa vijijini, kweli tunawatendea haki kwamba kweli wana Shule za Awali hizi? Lakini kwa kuwa vipo vyuo binafsi ambavyo vinatoa Walimu wa kada za Shule za Awali, je, Serikali iko tayari kuandaa *Scheme of Service* kwa ajili ya Walimu hawa ili wakipatikana waweze kuajiriwa kwa urahisi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hilo ni zuri, tunaweza kulifanyia kazi. Wizara imevisajiri hivyo vyuo kwa sababu tuliona wanaziba pengo ambalo lipo. Kama ni suala la kusema sasa hivi wamefanya kwa *initiative* yao, Chuo cha Ualimu kama cha *Saint Mary's* kinafundisha Walimu wanao-*focus* kwa ajili ya kazi hiyo na tumekisajili.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Chuo kingine naambiwa na wenzangu hapa wananikumbusha kiko Tanga. Kwa hiyo, tutaliangalia hilo. Nalikubali kabisa kwamba ni wazo zuri.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho 1003, *Policy and Planning.* Leo asubuhi tulipokuwa tukichangia hapa nilizungumzia suala la *syllabus* moja pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii walizungumzia suala hilo la kuwa na *syllabus* tofauti baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

wakati huo huo tukawa na mtihani mmoja katika kidato cha nne. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aseme lolote kuhusu suala hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, kwa kukumbushia suala hili, lakini si jambo ambalo naweza nikalijibu moja kwa moja kwa sababu dhamana ya masuala ya elimu kwa Zanzibar yana Waziri wake. Ninachopenda kumhakikishia ni kwamba, tunashirikiana vizuri sana na Waziri mwenzangu na masuala haya tunayajadili kwamba, kama mtihani ni mmoja katika ngazi ya kidato cha nne na cha sita, kuna haja ya kuangalia *syllabus* ya Elimu ya Msingi nayo iwe na sura moja. Lakini ninachoweza kusema, haya ni mashauriano tu ambayo tunayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, tumekwishazungumza, tumekwishakubaliana na Benki ya Dunia, wamekwishakubali kwamba, zikikamilika *studies* zinazohitajika kwa upande wa Zanzibar nao wataingizwa katika *SEDEP* na itakuwa ni Serikali hii moja ya Muungano ndiyo itaweka sahihi mikataba kwamba tunakopa hizo fedha kwa sababu soko letu la ajira ni moja. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuulizia au kumwomba Mheshimiwa Waziri kifungu cha 4001...

**MWENYEKITI:** Bado, hatujafika huko.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Sasa sielewi kwa nini nimening'inia hapo! *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Chief Education Officer* .................... Sh.3,934,678,900/=

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina jambo dogo, nilikuwa nimechangia kwa maandishi ingawa jina sikulisikia sijui kama alilitaja. Kwanza, namshukuru Waziri mwaka huu wa 2004, amefanya ziara Wilayani Chunya na katika ziara yake akaturuhusu tufungue Shule moja ya Sekondari ya Kiwanja. Pamoja na hiyo ya Kiwanja, ipo na Shule ya Sekondari ya Lupa ambayo ilikuwa ya Wananchi tukaikabidhi kwa Serikali mwaka 2002 na shule hiyo ilipokuwa inakabidhiwa tuliambiwa analetwa tu mwalimu wa kuja kuipokea, *Headmaster* atatafutwa baadaye, lakini mpaka sasa *Headmaster* bado hajaletwa.

Shule ya Kiwanja tulipoifungua napo wakasema apatikane mwalimu yeyote hata kutoka Shule ya Msingi ili aianzishe na ndiyo *Headmaster* wa sasa pale amepatikana kutoka Shule ya Msingi. Yuko pale na ana wanafunzi 80, yaani mikondo miwili na ni mwalimu peke yake na ile shule ya Lupa tangu ilipochukuliwa bado hawajaongeza idadi ya kutosha ya Walimu. Kwa maana hiyo ni kwamba, Walimu waliokuwepo wakati

ikiwa Shule ya Wananchi, baadhi yao ndiyo wapo pale mpaka leo. Nataka tu kujua msimamo au hatua za Wizara ni lini *Headmasters* wa shule hizo, wenye sifa za kuwa *Headmasters,* wataletwa kwa ajili ya Shule ya Sekondari Lupa na Shule ya Sekondari Kiwanja?

Lakini la pili katika hilo hilo, kuna shule nyingine ya Serikali, Shule ya Kanga ndani Wilaya, nayo *Headmaster* wake kwa taarifa zilizopo hana zile sifa za kuwa *Headmaster* kama wanavyoelewa Wizara ya Elimu sasa na kuna utaratibu wa kwamba, angepatikana *Headmaster* mwingine. Sisi katika Wilaya ya Chunya inaonekana Shule zote za Serikali hazina *Headmasters* ambao kwa maana ya tafsiri yenu kwenye Wizara, wenye sifa zinazostahili, hawapo. Kwa hiyo, tunaomba sasa Waziri atuhakikishie kwamba, moja ya hatua atakazozichukua ni kuwapata *Headmasters* kwa shule hizi na kuongeza idadi ya Walimu ili wanafunzi hawa wapate elimu ile wanayostahili kuipata. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu hapa nimelitaarifu Bunge kwamba, mwaka huu tumefungua shule mpya 208. Sasa nikasema ni ongezeko ambalo halijawahi kutokea ukichukua ile namba ya wanafunzi katika sekondari. Wizara ilifanya hivyo kwa kujua kuna mpango huu unakuja.

Kwa hiyo, tulilegeza masharti, tulifungua shule za sekondari sehemu nyingine tulikuwa hatujaandaa vizuri *Headmasters,* sehemu nyingine hata majengo mengine ukiondoa madarasa ya kukaa wanafunzi na vyoo, mengine yalikuwa bado.

Lakini tulikuwa tunajua jibu lake liko kwenye *SEDP,* kwa hiyo, katika *SEDP* kuna fedha za *in service training* na utakuta nimesema mafunzo, *ADEM* nimetaja namba ya watakaokwenda, watendaji watakaokwenda mafunzo *ADEM* hawa tutakaowa-*train* ndiyo watakuja kuwa-*replace* wale walioshikilia ambao hawajawa na sifa zinazohitajika. Kwa hiyo, naomba uvumilivu kwa muda kidogo tutaona mambo yameanza kutengemaa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Inspectorate* ................................ Sh. 2,875,565,300/=
Kif. 2003 - *Mantep Institute*............................... Sh. 166,423,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Basic Education* ................................ Sh. 426,885,700/=

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kifungu hicho hicho 3001 - *Primary Education,* Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hotuba yake na mimi katika mchango wangu niliandika juu ya pesa, posho au mishahara ya wale wanaofundisha, ambao wamepitwa na elimu, kwa kifupi MEMKWA. Katika

kujumuisha hakusema chochote, katika hotuba hakusema chochote, sasa wale watu tuliowachukua wanatusaidia kuwafundisha watoto ambao wamepitwa elimu wanafanya kazi nzuri, lakini kama tutawasahau hao tukazungumzia walimu peke yao bila hawa, lengo la MEMKWA linaweza likaisha bila manufaa yoyote. Sasa mimi ningependa Mheshimiwa Waziri, aseme anafanya nini juu ya kuwapa mishahara au posho au pesa za hawa watu wanaofundisha MEMKWA? Hilo moja. *(Makofi)*

Lakini sambamba na hilo hilo, tumewachukua hawa watusaidie kwa kipindi cha miaka mitatu, baada ya hapo tunafanya nini nao, itakuwa ndiyo basi, itakuwa ndiyo mwisho au tunafanyaje juu ya watu hao wanaotusaidia? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge, aliuliza jambo hili ni katika yale mambo ambayo sikupata muda wa kuweza kuyatolea maelezo. Wizara kupitia Idara yake ya Elimu ya Msingi, bado tunatafuta fedha hatujafanikiwa, kama ambavyo tulikuwa tunataka tuweze kuwalipa mishahara. Mpango Maalum umeandaliwa na Idara yetu ya Elimu ya Msingi kwenda kwenye *Basic Education Development Committee (BEDC),* tunauombea fedha kutoka kwa wahisani tuweze kuwa tunawalipa walimu hao. Kwa sasa hivi kila Wilaya, walimu hawa wanalipwa na Halmashauri. Napenda kukiri nafahamu zipo Halmashauri ambazo zinashindwa kufanya hivyo kwa ufanisi unaohitajika. Lakini pale pale zipo Halmashauri ambazo zinafanya kazi hiyo vizuri. Kwa hiyo, tunaomba waendelee wakati Wizara bado inajitahidi kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa walimu hawa wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa. Pia ameuliza tutafanya nini na walimu ambao tumewaajiri baada ya miaka mitatu, mpango huu ukiisha? Jibu la ukweli na uwazi ni kwamba, kazi yao itakuwa imekwisha kwa sababu wameajiriwa kwa kazi hiyo maalum ya kufundisha wale walioikosa elimu ya msingi. Tutakapokuwa tumemaliza hiyo *assignment,* kazi yao itakuwa imekwisha.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa maana hiyo Waziri anataka kutangaza kwamba, MEMKWA isimame kwa sababu hawezi mtu akafanya kazi kwa matumaini kwamba atakuja kulipwa. Sasa hivi wana mwaka mmoja hawajalipwa na anavyosema ina maana hiyo MEMKWA isiendelee. Mimi nadhani hata ukisema Halmashauri zichukue hilo jukumu Halmashauri zitatoa wapi pesa, wakati mwenye pesa ni Serikali Kuu na Serikali Kuu, ndiyo aliyetangaza mpango huu wa elimu sasa kama ulikuwa huna maandalizi kwa nini usiache? Aache angoje pale atakapopata nguvu ndiyo aje aanze kuendesha mpango wa elimu kwa walioikosa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipendi kukata tamaa na kusema tuache. Mimi ninachopenda kusema ni kwamba, Halmashauri ziendelee kuweka jitihada zao kuwalipa hawa walimu wakati Wizara inatafuta chanzo cha fedha cha kuaminika kuweza kuwalipa hawa walimu. Tutajitahidi kufanya hivyo mapema iwezekanavyo. Lakini tusiseme tuache hiyo itakuwa ni kukata tamaa. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nina swali dogo lakini limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge na pia katika kitabu cha hotuba limezungumzwa sana. Kazi nzuri hii inayofanywa ya shule za msingi na sekondari kuna tatizo ambalo Mheshimiwa Waziri, alilizungumza pale *section* ya ukaguzi ambayo ni tatizo na kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, walipokuwa wanachangia kuna baadhi ya shule za msingi zaidi ya miaka mitatu, minne mpaka mitano, hazijakaguliwa kwa sababu ya ukosefu wa wakaguzi na idara hii tumesema ina matatizo makubwa na katika kitabu kuna upungufu wa wakaguzi 224 kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza. Lakini katika ku-*wind up* pale hajaelezea mkakati gani Wizara hii itazalisha wakaguzi wengi sana ili kukidhi haja ya kukuza elimu. Naomba maelezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatujatosheleza namba ya wakaguzi tunaowahitaji. Lakini tuna wakaguzi kila Wilaya na kila mwaka tunawafundisha. Katika miaka iliyopita tulikuwa tunatoa magari mawili au matatu, kwa ajili ya wakaguzi, bajeti ya mwaka huu tunatoa magari 13, kwa hiyo, tumeongeza juhudi ya kuwapatia nyenzo wakaguzi wetu waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi. Sasa nita-*review* hii namba tunayofundisha kila mwaka, tuangalie uwezekano wa kuongeza kasi ya kuwafundisha wakaguzi wetu. Lakini huduma hii ni muhimu na inahitajika, ni lazima tuiboreshe na namshukuru Mheshimiwa Joel Bendera kwa *concern* yake. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 3001, nina kero mbili ambazo ningependa Waziri azifafanue na kuzieleza. Ametueleza katika majumuisho yake jioni hii kwamba, shilingi 2.5 bilioni zimetengwa kwa ajili ya mishahara na malimbikizo ya walimu wa shule za sekondari na kwamba shilingi bilioni 1.5 tayari zilishatolewa tarehe 18 Juni, 2004 na kupelekwa kunakohusika. Mpaka nilipozungumza na baadhi ya walimu jana, wengine walikuwa hawajapokea chochote. Nilitaka tu kumwomba Mheshimiwa Waziri, kama anakubaliana na ushauri wangu kwamba, kwa kuwa Wizara ya Ujenzi na hasa Mheshimiwa Mwenegoha yupo hapa ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bernard Membe, unazungumzia kifungu 3001, hiyo ni elimu ya msingi, kwa hiyo, alichosema Waziri yeye anahusika zaidi na elimu ya sekondari. Unaweza kuvumilia ukasubiri kwenye sekondari?

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Sawa tu.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 3001 elimu ya msingi, pamoja na kazi nzuri ya Serikali ya kutujengea madarasa, nilisema kwenye hotuba yangu kwamba, pamoja na madarasa tunahitaji nyumba kwa ajili ya walimu. Nyumba nzuri inakuwa *incentive* kwa walimu kwenda vijijini kuliko kwenda kuishi kwenye nyumba za mbavu za mbwa. Sasa katika ukurasa wa nane anasema ruzuku ya maendeleo itatolewa hiyo shilingi bilioni 1,185 kwa Halmashauri. Je, Serikali itakubaliana na mimi kuhakikisha kwamba, wanajenga nyumba sasa za walimu ili kuhakikisha walimu wanaishi vizuri?

La pili, walimu ambao wanaishi katika mazingira magumu ambako hakuna nyumba za walimu wa shule za msingi hata shule za sekondari hapa naweza kuwachanganya, Serikali itakuwa radhi kuwalipa *hardship allowance* ili iwe *incentive* waweze kufanya kazi vizuri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mwalimu Maria Watondoha, kwa *concern* yake. Mimi nakubaliana naye kwamba, tunahitaji kujenga nyumba za walimu zilizo nzuri na mwishoni mwa hotuba yangu, nimetoa maagizo kwamba, ujenzi wa nyumba za walimu ufuate maelekezo yaliyotolewa na Wizara katika kitabu maalum ili tujenge nyumba zenye *standard* iliyo nzuri.

Lakini napenda niseme kwamba, kwa shule za msingi usimamiaji na uamuzi wa tujenge nyumba ngapi za walimu na madarasa mangapi, upo pale kwenye ngazi ya Wilaya. Afisa Elimu Kiongozi, amelazimika kutoa Waraka Maalum, unaotoa *formula* ya nyumba za walimu na madarasa kwa sababu imeonekana Halmashauri wanapopanga mipango yao wanaomba fedha za kujenga madarasa tu bila kujenga nyumba za walimu. Tusikwepe huu ni uamuzi katika utaratibu wa *Local Government Reform,* huu ni uamuzi unaofanywa ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, naomba tusaidie Wilaya zetu sisi Waheshimiwa Wabunge, kusimamia kuhakikisha kwamba, tunajenga nyumba za walimu za kutosha na *standard* iliyo nzuri. *(Makofi)*

Kwa ngazi ya sekondari napenda niseme kwamba, katika bajeti ya mwaka huu, hazijawahi kupangwa fedha za nyumba za walimu kwa kiwango hiki kwa miaka mingine yote iliyopita. Kwa hiyo, inaonyesha kabisa Serikali iko *very concerned* na nyumba za walimu. Sasa swali la kwamba walimu wanaokaa katika maeneo magumu walipwe *hardship allowance* maalum, jambo hili ndani ya Serikali lina mjadala kwamba mwalimu ni miongoni mwa wafanyakazi pale kijijini. Pale kijijini kuna mtu wa afya, kuna mtu wa kilimo, sasa ukim-*treat* mwalimu peke yake, wale wengine nao watahoji, kwa hiyo, ndani ya Serikali limetupa ugumu jambo hili. Kwa hiyo, ndiyo maana tumebaki hivi hivi kwamba, njia nzuri ya kum-*attract* mwalimu tuweke mazingira mazuri pale shuleni, shule nzuri, nyumba nzuri za walimu, yawepo maji pale mpaka kwenye nyumba ya mwalimu. Tukifanya hivyo mimi nina hakika walimu watakubali kwenda kufundisha. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nina swali dogo tu. Kwa kuwa katika fedha za MMEM zilizotolewa awali katika baadhi ya Halmashauri, wananchi walilazimishwa kujenga kwa matofali ya kulaza ili majengo yawe imara ambayo yanachukua *cement* nyingi na gharama kubwa. Je, hili ni agizo la Serikali au ni utaratibu tu katika haja ya kuweza kukidhi mahitaji ya kujenga madarasa ya kutosha na nyumba za kutosha?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwamba, haya ni mambo wanayoamua huko Wilayani na sisi hatuwezi kuyaingilia. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Secondary Education* ........................ Sh. 32,067,586,600/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, endeleeni kusimama hivyo hivyo mpaka tupate majina yote. Mheshimiwa Bernard Membe, tulishakuandika unaweza kukaa chini. Mheshimiwa Lekule Laizer kaa chini, Mheshimiwa Mohamed Missanga kaa. Kwa sababu wengine wanasimama sina uhakika ni kutoka au kuchangia? Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Leonard Shango, mnaweza kukaa chini. Mheshimiwa Anatory Choya, wewe wa kwanza kuandikwa kaa tu. *(Kicheko)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4001 kama nilivyokuwa nimeanza kusema kwamba, shilingi bilioni 2.5 pamoja na shilingi bilioni 1.5 zilizotolewa ni fedha nyingi na nikasema kwamba, Wizara ya Ujenzi, imetufanyia jambo moja Wabunge zuri sana na kila tunapoondoka kwenda kwenye majimbo yetu hutupatia muhtasari wa mgao wa fedha zilivyokwenda katika kila Wilaya ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge, kuweza kufuatilia. Kwa kuwa suala hili la elimu ni kubwa na fedha zinazopelekwa ni nyingi na sisi ndiyo wafuatiliaji wakubwa, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, nadhani huu ni wakati muafaka wa Wizara kuandaa utaratibu ule ule kama unavyofanywa na Wizara ya Ujenzi kwa kutupatia mgawanyo wa fedha tujue kiasi gani kinachokwenda ili tuweze kufuatilia kwa sababu jambo hili ni kubwa zaidi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo ni zuri lakini napenda ijulikane kwamba, kama nilivyosema wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunachotoa sisi kuhusu ujenzi wa shule hasa shule mpya, tunatoa hiyo *guidance* kwamba ziende kwa kufikia kupeleka sekondari asilimia 35. Kwa hiyo, uamuzi wa mpango wa kujenga shule utaanzia kule Wilayani. Sasa tutakapofika kwamba sasa tumekwisha kubaliana kwamba tunajenga shule kadhaa katika Wilaya hii na tunapeleka fedha kwa ajili ya madarasa kwenye shule zilizopo kiasi hiki, nitaangalia uwezekano wa kutekeleza utaratibu anaopendekeza Mheshimiwa Bernard Membe, kwa sababu hiyo ni nguvu mpya ya usimamiaji na ufuatiliaji, inatusaidia sana Wizara. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye kifungu 27300 cha mwisho, *vehicles and mobile equipment*, nilitaka tu kufahamu kwa kuwa sekondari zilizoko katika maeneo magumu hasa Sekondari ya Longido na baada ya shule kuwa na *A-Level* kwa hiyo wanafunzi wameongezeka, kulikuwa na wanafunzi 360 sasa wameongezeka wamekuwa 460. Je, isingekuwa vizuri wapatiwe gari la kuihudumia shule hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba, Shule ya Longido imepanuliwa na nafahamu kwamba, kunahitajika huduma ya gari pale shuleni. Lakini napenda ifahamike kwamba, tatizo hili ni kubwa. Ninachoweza kusema tu nalipokea ombi lake, tutaangalia uwezekano huo kadri mafungu ya fedha yatakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wa maandishi ambao niliuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri, nilieleza tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi katika shule za sekondari zilizoko katika jimbo langu hasa Sekondari ya Sepuka, Sekondari ya Puma kiasi kwamba masomo ya sayansi hayafundishwi na kwa sababu inafifiisha na kudhoofisha kufaulu kwa wanafunzi wa sekondari kwa *level* ya *form four.* Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuangalia uwezekano wa kutuletea walimu wa sayansi katika shule ambazo nimezitaja mapema iwezekanavyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika maelezo ambayo sikuyatoa. Tukiwa hapa Bungeni kulikuwa na hatua muhimu ambayo tuliichukua kutokana na fedha nilizopewa na Bunge hili katika *supplementary budget,* kwa hiyo, tukiwa hapa wamepangwa walimu zaidi ya 2,000 kwenda kwenye shule za sekondari. Kwa hiyo, nina hakika karibu kila Mheshimiwa Mbunge, atakuta hali ya kuwa na walimu shuleni atakaporudi kwenye jimbo lake, atakakuta imebadilika kidogo. *(Makofi)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kweli kwa programu hii nzuri kabisa hasa ya kuchukua asilimia 50 ya watahiniwa sasa hii itatusaidia katika Wilaya ambazo wanafunzi wengi wanamaliza elimu ya msingi lakini sekondari ni chache. Sasa nilikuwa nataka kupata ufafanuzi, sikuona mahali anaeleza labda tutajenga mabweni, mojawapo ya matatizo yetu ni mabweni. Shule inajengwa lakini watoto wanashindwa kusafiri. Kwa hiyo, unaweza kukuta shule iko *under utilized* kwa maana ya wanafunzi wanashindwa kujaza. Sasa programu hii inaweza kutusaidia kujenga mabweni?

Lakini lingine ni shule hizi mpya zinazojengwa, anasema tunajenga mikondo miwili kuongeza ili mikondo iwe minne. Je hizi shule mpya zinazojengwa, tunajenga mikondo minne kwa mkupuo na nyumba mbili za walimu? Lakini bado na mambo ya utawala sasa *program package* nzima inasemaje? *(Makofi)*

Halafu lingine la mwisho labda hili la magari aliloongelea Mheshimiwa Lekule Laizer, mimi ningependa badala ya kutoa gari kwa shule moja basi tupate hata Wilaya moja ipate gari la kuhudumia hizi sekondari mbalimbali katika Wilaya. Ziko Wilaya, shule hazina hata pikipiki na sekondari ziko tano. Sasa badala ya kuipa sekondari moja lori kwa nini usitoe hata kwa Wilaya basi ili likahudumie sekondari mbalimbali katika mahitaji yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufafanua alilouliza Mheshimiwa Danhi Makanga kwamba, suala la mabweni liko katika mpango huu, hatuiti mabweni tunaita hosteli. Katika hotuba yangu ya Bunge nimesema kwamba, zitajengwa pale hosteli zinapohitajika. Kwa hiyo, *financing* ya hosteli itafanyika pale hosteli inapohitajika na kuhitajika kwenyewe ni kuangalia *catchment area* ya ile shule ili kupeleka asilimia 35. Kama kuna watoto wanaotoka mbali hiyo ndiyo hoja

ya kujengwa hosteli, Serikali iweze kusaidia ujenzi wa hosteli. Lakini nayo ni kusaidia kwa kutoa ruzuku ya maendeleo itakayotosheleza vifaa vinavyotengenezwa viwandani.

Suala la kwamba shule inayoanza itakuwa ya mikondo minne au mikondo miwili, kigezo ni ile ile asilimia yetu 35 na kuwepo kwa watoto ku-*feed* ile shule. Tunataka tufanye kazi hii *efficiently,* siyo ujenge mikondo minne, halafu miwili ikae tupu. Kwa hiyo, unaangalia *catchment area* watoto wanaofaulu unaweza ukaanza na mikondo miwili mwaka wa kwanza, mwaka wa pili tukaongeza miwili. Kwa hiyo, tunaangalia kulingana na hali halisi ya eneo. Ninachoweza kusema, *financing* itakuwepo kwa mwaka huo unaokuja kufikisha asilimia 35. Mwaka unaofuata mtaangalia katika ile programu inaonyesha kufikisha asilimia 40 mpaka tutakapofikisha 50%. Suala la magari napenda kuthibitisha kwamba, ni utaratibu wa sasa kwamba, tunapopanga magari tunaangalia kwanza angalau katika kila Wilaya liwepo gari kwa sekondari kadhaa. Tunachofanya tutaliweka katika sekondari moja kwa maagizo kwamba, litatumika na sekondari zilizo katika Wilaya ile. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kifungu hicho 401, *secondary education.* Kwanza, nashukuru na kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeweza kusaidia kupunguza ada ya shule mpaka kufikia shilingi 20,000. Vile vile kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inasaidia kusomesha watoto wasiokuwa na uwezo. Sasa nilikuwa na swali dogo tu katika watoto ambao hawana uwezo, ambao Serikali inawasomesha kwa kuwalipia ada, Serikali haioni isingemalizia jukumu la kuwasomesha wakati wa kufanya mitihani ikawalipia ada ya mtihani kama ambavyo imewalipia ada ya *secondary school?* Haioni kuwa ni vizuri imalizie tu kuwalipia ada ya mtihani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia kabisa Mheshimiwa Lucas Selelii kwamba, zile shilingi 180,000 zilizopangwa za kumsaidia kijana huyu kwa mwaka katika mahesabu zimejumuisha na hiyo ada kwa ajili ya mitihani. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, niliongelea matatizo makubwa ambayo yapo katika shule mbili za Sekondari ya Wilaya ya Iramba. Moja ilikuwa ni Sekondari ya Ndago, nilizungumzia kuwa shule hii ina walimu watatu tu mmojawapo ni Mwalimu Mkuu na nilipokwenda kuitembelea niliambiwa kuwa walimu wanaopangwa kwenda kule wanakataa kwenda. Walimu wamepangwa mara mbili lakini hawakuripoti kwenye shule ile. Nilikwenda mpaka Wizarani kuulizia nikaambiwa tutawapeleka walimu kwenye shule ile. Sasa wakati nikichangia nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kuwa, anihakikishie kuwa hili tatizo litakwisha na kuhakikisha kuwa walimu wamepelekwa kwenye shule. Sasa kama tunaongelea kuboresha elimu ya sekondari, ubora utakuja kama hakuna walimu? Sasa mimi nauliza kama kuna ubora pasipo kufundishwa anieleze?

Pili, nilikuwa nimeongelea Shule ya Sekondari ya Kinampanda, *Tumaini Secondary School,* kwa miaka kumi haina mwalimu wa *Domestic Science* na wasichana wako pale wanapofundishwa wakifanya mitihani lazima wafeli hawawezi kufaulu. Sasa kama kweli tunategemea kuwa shule kama hizi na zenyewe zitatoa mchango wake katika

ubora wa elimu, itakuwaje kama hawapelekewi walimu? Niliomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa matatizo haya yaishe na walimu waende Sekondari ya Kinampanda, *Domestic Science Teacher* na Sekondari ya Ndago waende walimu wa kutosha kusudi wanafunzi wanapofanya mtihani wa kidato cha nne nao waweze kufanya vizuri. Sasa katika kuchangia kwangu pia niliongelea kama kuna matatizo kwa nini walimu hawaripoti kwenye vituo wanavyopangiwa? Wizara inachukua hatua gani? *(Makofi)*

Sasa kama Walimu hawaendi kwenye vituo vile, tutegemee nini katika mashule yale, watafanya mitihani halafu wafaulu au wafeli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leonard Shango umeeleweka kwa sababu hii sio nafasi ya hotuba ni kutaka ufafanuzi. Umeshaeleza Walimu unaowataka kwenye Shule zako na Mheshimiwa Waziri ameelewa, tungoje majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema wakati wa *winding-up* kwamba, nimeandaliwa lundo kubwa sana. Naomba nisome tu ili Mheshimiwa Leonard Shango awe na uhakika. Nasoma kwenye maelezo.

Mtoa hoja ni Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi. Anaomba Shule za Tumaini, Ndago, Kizago na Lulumba zipewe Walimu wa kutosha na wa masomo yasiyokuwa na Walimu. Wizara imetuma Walimu wanane wa Sayansi na watano wa *arts* katika Wilaya ya Iramba katika kipindi cha Januari mpaka Machi, 2004.

Aidha, Wizara imewapanga Walimu wengine saba kwenda Wilaya hiyo ya Iramba mwishoni mwa Juni, 2004 tukiwa hapa Bungeni. Kwa hiyo, nina hakika Mheshimiwa Mbunge atakaporudi atakuta hali imebadilika kama nilivyosema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa *trend* ambayo naiona inaendelea, naomba niwakumbushe, ninajua wote mnafahamu kanuni hizi, lakini ni vizuri nikawakumbusha kwamba, kila mmoja anayetaka kuchangia anayo nafasi ya dakika tano. Wakiwa watu kumi ni dakika 50. Sasa katika kanuni zetu, kanuni ya 81(6), kwa kuwa ni kifungu kirefu sana sitasoma chote. Lakini kinatoa mamlaka kwa Mwenyekiti ya kusimamisha mjadala inapobakia dakika kumi na kuhoji vifungu vyote kwa mara moja. Kwa hiyo, tukichukua nafasi ya hotuba tutajichelewesha kupata ufafanuzi kwenye vifungu vingine kwa sababu Mwenyekiti atahoji vyote kwa ujumla. Nilitaka kulisisitiza hili ili twende vizuri. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waziri alipokuwa akitoa hotuba yake kwa mlolongo unaeleza jinsi gani ya kuboresha elimu katika nchi yetu. Sasa unapoboresha ni pamoja na watoto wa kike. Watoto wa kike ni hawa ambao wanapata matatizo ya kukatisha masomo kwa ajili ya kupata mimba na Wizara inasema kwamba hao watu wanaowaweka mimba watoto wa kike watashtakiwa. Sasa wanashtakiwa na hatua zipi sasa hivi ambazo zinaendelea na ni wangapi wamechukuliwa hatua? Je, Wizara hii ina kitengo? Kwa sababu mimi sielewi, naomba nifafanuliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unaweza kufafanua lakini kwa wangapi, tuwe *realistic*. Hawezi kuwa na takwimu hapa kwa ghafla hivi hivi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimtaarifu Mheshimiwa Lydia Boma kwamba, tumetunga kanuni yenye adhabu kali sana juu ya jambo hili kwamba mtu yeyote anayempa mimba mtoto wa Shule adhabu yake ni kifungo cha kuanzia miaka mitatu mpaka miaka sita na kwa kosa hilo la kumpa mimba mtoto wa Shule hakuna *option* ya faini. Sasa kinachojitokeza mara nyingi imekuwa ni tabia ya watu kukwepa. Sasa hivi tuna mawasiliano na mwenzangu Waziri wa Afya, kusambaza mashine zinazoitwa *DNA*. *DNA* itakuwa inaweza kupima mate ya huyo mtuhumiwa na mate ya mtoto, damu ya huyo mtuhumiwa na damu ya mtoto. Ikithibitika ni *proof* unakwenda Gerezani miaka mitano. Tukisimamia kwa ukamilifu hii itakomesha hawa waroho. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majumuisho mazuri sana aliyoyafanya Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwamba tatizo langu limeshatatuliwa nusu yake kwa sababu ameshaelezea idadi ya Walimu ambao wameshagawiwa katika Shule mbalimbali. Sasa ili na mimi nifahamu kwamba ni Walimu wangapi ambao wamepelekwa katika Shule zangu ambazo wakati wa kuchangia nilichangia katika kuzungumza Bungeni, vile vile nikaandika kwenye Shule hizi tatu, yaani Shule ya Nyakahura, Biharamulo Sekondari pamoja na Kagango, ambazo kwa ujumla zina upungufu wa Walimu karibu 30. Sasa naomba anisomee ama anielezee humu humu Bungeni nijue orodha ya Walimu ambao wamepelekwa kwenye Wilaya yangu.

Halafu la pili linahusu uzoefu ambao nimeupata baada ya kutembelea kwenye Shule nyingi kwamba, nimeona Walimu Wakuu wengi wa Shule za Sekondari, kama alivyotoa mchango wake Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Walimu wengi wa Shule za Sekondari wamekuwa ni wakusanyaji wa *school fees* pamoja na michango mbalimbali na kusahau majukumu yao ya kimsingi. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko lenye Mamlaka maana yake unapotamka humu Bungeni mara kwa mara huko mitaani wanasema haya ni maneno ya kisiasa. Sasa namwomba atoe tamko lenye mamlaka linalopiga marufuku kwamba, Walimu Wakuu wasimamie taaluma tu badala ya kukusanya karo ya Shule pamoja na michango mbalimbali. Wasiwe wanafukuza watoto bila utaratibu wowote na kuwaharibia taaluma yao wanafunzi. Kwa hiyo, naomba atamke rasmi hapa ili ieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nitaanza kueleza kwa kila Mheshimiwa Mbunge, Walimu waliokwenda kwenye Sekondari za kwenye Majimbo yao tutachukua muda mrefu sana. Nilitoa ile kama mfano kwamba, jamani kuna kazi kweli ambayo inafanyika, naomba mniamini kabisa. Lakini kama atataka *specifically* ya kwake na mwingine yeyote akitaka tunaweza tukapeana hizi orodha wakati bado tuko hapa hapa Bungeni. Lakini nina hakika tumeongeza namba ya

Walimu katika Shule za Sekondari, sijasema sasa wanatosha lakini nasema hali imeboreka kidogo na tutaendelea kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakuu wa Shule wasisimamie ukusanyaji wa ada, hilo ni jambo la hatari kabisa kwa sababu *Headmaster* ndio Meneja wa Shule, ndio anayesimamia mambo yote pale na nimesema hapa ada inabakia pale Shuleni. Kwa hiyo, ni sehemu ya *school income. Headmaster* lazima asimamie ukusanyaji wa ada zile Sh.20,000/= zinazokwenda pale na pia ni mfuatiliaji wa zile ambazo nimeahidi hapa kwa niaba ya Serikali zitakwenda kufidia ile tuliyopunguza. Mfuatiliaji wao wa kuzi-*claim* kutoka Wizarani ni huyo huyo *Headmaster.* Kwa hiyo, tuwaamini kwamba watasimamia vizuri. Lakini kutokana na fedha zilizopangwa katika bajeti hii, kitu ambacho nimekisema hapa na sina haja ya kukirudia kwa sababu kiko kwenye hotuba ya bajeti, waache kuzua michango mingine isipokuwa ile michango na shughuli za ujenzi wa shule. Nimesema kabisa tena nimetumia maneno ya Rais Mstaafu kwamba, kuna michango rukhsa nimeitamka mle kwenye hotuba na kuna michango ambayo ni marufuku ile ya kuchangisha wazazi wa wanafunzi peke yao. Tukifuata *procedure* hii kutakuwa hakuna matatizo. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, mimi nimeelewa kabisa. Ninaomba tu kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, nitakuja kuchukua orodha ya hao Walimu ambao wamepelekwa kwenye Wilaya yangu kabla sijaondoka hapa ili nijihakikishie kwamba, kweli kuna Walimu waliotumwa huko pamoja na kwamba namwamini vizuri sana. Halafu vile vile nilivyosema kwamba, *Headmaster* lazima asimamie michango ni kweli, lakini asisimamie pamoja na kufukuzwa kwa wanafunzi bila kusimamia taaluma maana wanafunzi wanafukuzwa ovyo ovyo, ndicho kitu ambacho mimi nakisikitikia kabisa. Wanafunzi wanafukuzwa na Mwalimu anafukuzwa, asipoona hela wanafukuzwa kiasi kwamba wanakuwa wanaharibiwa taaluma yao, wanakuwa kama Maafisa Watendaji wa Kata, wanakusanya ushuru tu. Kwa hiyo, naomba wasifukuzwe, waendelee na masomo yao. Kama ni kusimamia hizo fedha asimamie kweli.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuamini kwamba, katika Bunge hili, Serikali tunaleta maelezo, Waheshimiwa Wabunge mnapitisha bajeti. Kwa hatua tuliyochukua kwamba sasa mtoto wa Shule kwenda Shuleni *term* moja ni Sh.10,000/=, hili suala la kufukuzana Shule mimi nina hakika litapungua kwa sababu wazazi wengi walioingia kwenye *bracket* ya kuweza kulipa Sh.10,000/= kwa muhula ni wengi sana na bado wasio na uwezo tumeongeza. Tumechukua hatua mbili, turudi kwenye Majimbo yetu tukijua Waheshimiwa Wabunge, tumeshirikiana na Serikali, kupunguza mzigo wa ada kwa mzazi na ni lengo watoto wetu wasome. Kwa hiyo na *goodwill* hii iende na kwa *Headmasters* wetu wajue kwamba lengo ni hilo. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nishukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo ya kutosha karibu kuhusiana na maswali yangu. Lakini kuhusu Ualimu, niombe tu kwamba, ikiwezekana basi wale wote ambao tumekuwa tukilalamika tunapotoka hapa, tupate orodha ya Walimu wanaokwenda

katika Wilaya zetu. Lakini la pili ni suala la usafiri. Nafikiri hili ni suala nyeti kwamba linaweza kutumika gari moja katika Wilaya, ni dhahiri kulingana na mapato ya nchi. Lakini hizi Shule zimejengwa mbalimbali, hakuna mawasiliano huko. Tatizo linapotokea katika Shule moja iliyoko kilometa 30, 40, 50, hii Shule ambayo imepata matatizo itapelekaje taarifa kuweza kupata msaada wa kuokolewa? Je, ni kwamba Mheshimiwa Waziri anatamka kutakuwa na *communication equipment* katika kila Sekondari ili kufanya kazi hii iwe nyepesi?

Tatu ni mabweni. Naomba Wizara ifikirie kwamba mabweni kwa wakati tuliofikia ni muhimu. Watoto wetu wa kike wengi wameharibika, wameumia. Wanalala vibaya wanachoka, hawasomi. Sasa ukifirikia kwamba leo karibu Tarafa mbili, tatu, zinakuwa zina Sekondari moja kama vile ilivyo kwa Murusagamba na Rurenge kama nilivyoeleza leo, kama Nyamiaga, Mtobeye, Kirusha na Mgoma, kama nilivyoeleza kwa Wilaya ya Ngara, mimi nafikiri tufikirie kwamba ni budi tuwe na mabweni kwa sababu hasa hasa ya watoto wa kike tuweze kuokoa sehemu hii ya watoto wetu kwenda Shule. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu masuala haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gwassa Sebabili ameomba ufafanuzi wa mambo mawili. Moja, tutafanyaje gari likiwa moja? Kwanza, napenda tusije tukatoka hapa ikaeleweka kwamba, mimi nimesema sasa hatutaki kuwa na magari katika Shule zetu. Gari ni *standard equipment* katika Shule ya Sekondari. Lakini tunazungumza kipindi ambacho hatujawa na magari ya kutosha, tumekubaliana na tena ushauri ulipendekezwa hapa hapa Bungeni kwamba jamani angalau kwa nini lisiwe linawekwa gari moja katika kila Wilaya kuliko kupeleka upande mmoja? Kwa hiyo, sasa tumeanza *allocation*, tukipata uwezo wa kutoa gari tunaangalia Wilaya ile ambako Sekondari zetu zote hakuna gari, tunaweka gari moja na wale *Headmasters* tunawaelekeza utaratibu kwamba, gari hiyo moja itatumika na Shule hizo kwa kufuata ratiba. Kwa hiyo, kama ratiba ikifuatwa na wale wakapanga kazi, hakuna shida tena ya kupigiana simu, nina shida huku. Kila mmoja anajua tarehe fulani mpaka tarehe fulani gari liko kwangu au mwezi fulani gari liko kwangu. Hili ni jambo ambalo wao kama Mameneja wa Shule, wanajua namna ya kulifanya.

Kuhusu suala la hosteli, narudia tena kusema katika *SEDEP,* pale inapohitajika hosteli kwa vigezo kwamba *catchment area* ya kujaza shule ile iwe ya mikondo minne, inahitajika hosteli, mpango huu utasaidia ujenzi wa hosteli. Wanaojenga hosteli bado ni wananchi wenye Shule ile. Isije ikadhaniwa kwamba, ni Serikali sasa inakwenda kujenga hosteli. Wananchi wanaanza kujenga hosteli, Serikali itasaidia vifaa vya kutoka viwandani. Ndicho nilichosema. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake. Ninachotaka kusema ni kuhusu matumizi ya magari. Shule hazina simu wala *radio calls.* Nazungumzia Shule zangu ambazo kwa bahati nzuri nimesema viongozi wakuu wawili wa Wizara ya Elimu wamefika na wameziona. Si vyepesi hata siku moja inapojitokeza kwamba ni dharura, ni tatizo kama kule kwangu kama mnavyojua kuna wakimbizi, nilikuwa namwandikia hapa

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, jana tu wameuawa majambazi pale nyumbani kwangu kwa kuvamia na wakaua watu.

Kuna Paroko wangu mmoja nafikiri hivi ninavyozungumza atakuwa amekufa. Sasa sio vyepesi kwa njia hiyo kutegemea kwamba gari litakuwa liko Shule fulani halafu lije liokoe maisha katika nafasi nyingine kwa misingi hiyo. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri, afikirie kama anavyosema penye matatizo aweke magari, penye matatizo kidogo aweke gari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nadhani ametoa ushauri tu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mimi nimekuwa wa mwisho. Ni programu 40, *Subvote 4001* kifungu kidogo zaidi 270100, *maintenance of physical infrastructure.* Ukiangalia katika kitabu hiki katika fungu hilo mwaka 2002/2003 zilitumika Shilingi bilioni moja. Mwaka 2003/2004 zikatengwa Shilingi milioni 140, mwaka 20004/2005 zimetengwa Shilingi milioni 150. Sasa ninataka kuwa *specific.* Wakati ninachangia nilizungumza kuhusu Shule ya Magamba Sekondari.

Ninaamini *maintenance* ya *physical infrastructure* ni pamoja na majengo katika *Secondary Schools*. Shule hii ya Magamba iliunguliwa na bweni na ile shule kwa mtu aliyesoma pale, ilijengwa na Kanisa la KKKT na ilikuwa ni mojawapo ya Shule nzuri katika nchi hii kabla ya kutaifishwa. Shule ile leo ni gofu. Matatizo yameikabili ile shule na inaonekana katika programu ya MMES hakuna utaratibu wa kukarabati hizi shule tulizokuwa nazo. Sasa Waziri ananiambia nini hasa kwa ajili ya Magamba Sekondari ili nipate kauli ya kuwaambia wananchi kule?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema ni kwamba, katika bajeti hii zimewekwa kabisa, ukisoma katika kielelezo Na.18 ukurasa wa 27, *item four,* matengenezo Shule za zamani, Shule 40 ni Sh.2,734,000,000/=. Sasa kusema Waziri aji-*commit* hapa jamani mambo mengine ni wataalam wanakaa kuangalia *needs,* kuzidiana mahitaji, wanakwenda wanapanga. Turidhike kwamba, katika bajeti hii tumeweka fedha kwa ajili ya tatizo analotuambia mwenzetu, tuwaachie wataalamu watapanga kulingana na kuzidiana kwa mahitaji ya mwaka hadi mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Henry Shekiffu, nilikushukuru sana ulipochangia ulikuwa *very specific* na jibu umelikuta liko kwenye Kitabu cha Mipango ya Maendeleo.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Haitoshi. Mimi shule yangu ina tatizo *peculiar,* imeunguliwa majengo (bweni). Sasa tunapowaachia wataalam, mimi nikawaambie nini hawa? Wanihakikishie hapa kwamba katika *priority* ni pamoja na Magamba Sekondari. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa Mheshimiwa Mbunge kwamba, anafanya kazi ya Kibunge, lakini naamini

kama Waziri ambaye nasimamia Shule za nchi nzima na ninaangalia Wilaya na Mikoa yote, kweli sio sahihi kuji-*commit* bila kuruhusu *process.* Tumemwelewa, tumemsikia, wataalam wamemsikia, tuache *process* ifanye kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Henry Shekiffu, kaa chini hajamaliza. Oh, ameshamaliza. Sasa una hatua gani ya kufanya maana amejieleza, shule ziko nyingi nchi hii zimeungua moto. Amesema kuna fedha zimetengwa wataziangalia, sasa hiyo huridhiki kwamba imetosha, *you have registered your concern*! Haya endelea.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, sio kwamba nikubali yaishe. Mimi ndio nimetoa ombi langu. Kama wengine hawajaomba, nina haki na mimi ya kuomba kwa heshima ya Waziri kwa ajili ya *presentation* yake nzuri, ningependa nishike Shilingi, lakini basi na-*withdraw* kwa heshima yake kwamba, ataona umuhimu wa Magamba Sekondari. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa nadhani ameelewa. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Teachers' Training* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 5,653,294,700/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, narudia tena, tuna dakika kumi tu na itakapofikia mwisho mimi nitahoji yote kwa ujumla. *(Kicheko)*

**MHE. MUTTAMWETA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nipongeze hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Sasa nina jambo moja zito kidogo la kuongeza Shilingi. Kuna kifungu katika *Subvote* 5001, kifungu kidogo 260800. Kama Mheshimiwa Waziri anakumbuka wakati tunaunganisha masomo katika Shule za Msingi tuliahidi kwamba, tutapeleka fedha kwenye Vyuo vya Ualimu ili kutoa *training* kwa ajili ya yale masomo ambayo tumeunganisha. Kwa kweli imekuwa bado ni tatizo kubwa sana katika Shule zetu za Msingi. Walimu wanafundisha hawajui jinsi ya kuyafundisha yale masomo na Mheshimiwa Waziri aliwahi kuahidi kwamba atapeleka kipindi cha nyuma. Sasa ukiangalia katika hii 260800 kwenye *Training Expenses,* nilitegemea kwamba, safari hii hili fungu lingeongezeka. Lakini limeendelea kupungua kutoka shilingi milioni mia na kitu mpaka imebaki shilingi milioni 80.

Sasa hapa hoja yangu ni kwamba, ninaomba tuangalie uwezekano wa kupeleka fedha kwenye Vyuo ili tuwaimarishe wale Walimu ambao wanafundisha masomo ya uraia ambayo tuliyaunganisha na masomo mengine. Wana shida ya kuyafundisha yale masomo na hawana msaada wowote. Kwa hiyo, ninaomba kuongeza Shilingi, maana yangu, sio kupunguza Shilingi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri asipate wasiwasi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nadhani umeelewa, umekaa humu ndani muda mrefu. Sisi kazi yetu ni kupunguza kama tunataka kupunguza au kuidhinisha. Hatuna Mamlaka ya kuongeza maana utatoa wapi? Mwingine.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tu ufafanuzi kidogo. Mheshimiwa Rais alipokuja Shinyanga mwezi Februari, 2004, aliahidi kutupa Chuo cha Ualimu katika Mkoa wa Shinyanga. Mkoa huu una Shule nyingi za Msingi na una wanafunzi wengi na ndio Mkoa pekee ambao una upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi katika nchi hii.

Sasa nilikuwa nimeshachangia kwa maandishi na ninafikiri ninaomba ufafanuzi kwamba mpangilio huo uko wapi mbona hata hajanijibu katika maelezo ya jumla?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie, kama Mheshimiwa Rais aliahidi tutalifuatilia. Lakini isije ikajengeka hoja kwamba, kuna Chuo cha Kimkoa, hatuna Vyuo vya Kimkoa. Tuna Vyuo 34 vinafundisha walimu kwa ajili ya Tanzania nzima. Ila tunapokuwa tuna Chuo kingine kinajengwa kwa sababu ya kusambaza maendeleo, tunajaribu kuangalia iangukie kule ambako hakipo. Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi Wizara iko katika mazungumzo ya hatua ya juu sana na Baba Askofu Balina, ambaye anataka kuanzisha Chuo pale na tuko tayari kum-*support* katika jambo hilo. Kwa hiyo, inavyoelekea kwa mipango iliyopo, Chuo kitakachopatikana Shinyanga ninachokifahamu mimi kwa haraka ni cha *route* hiyo kuliko cha kutoka upande wa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa *agenda* muhimu sana ambazo zimezungumzwa na Mheshimiwa Waziri ni kuhakikisha kwamba, Walimu ambao elimu yao bado haiendani na wakati huu wa sasa, wanaendelea kuelimishwa na kwa mfumo mwingine ambao umeelezwa ni ule wa *CASTA.* Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, miongoni mwa matatizo yanayoukumba mfumo huo usiende ipasikanavyyo, ni tatizo la Watendaji kutokupeleka taarifa maalum za matumizi ya fedha Wizarani na kusababisha kutokuendelea vizuri kwa vituo hivyo vya Walimu vya kujiendeleza. Sambamba na hilo, Walimu kwa ujumla wamekuwa na matatizo mengi ambayo yanatokana na Watendaji kutokuwafanyia haki za kiutekelezaji katika majukumu yao ya kila siku, kwa mfano, mambo ya mirathi na mambo mengine. Sasa Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani leo katika Bunge hili la kushughulikia wale wote wanaokwamisha maendeleo ya haki za Walimu kielimu, kwa kuwaendeleza kielimu, kwa kuwaendeleza au kuwapatia haki zao za mishahara na mambo mengine yote ili kupunguza mlundikano wa matatizo ya Walimu ya kiutendaji na haki zao kwa ujumla? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndio ninayesimamia majukumu hayo ya kuendeleza walimu, sera pamoja na kuja hapa Bungeni kuomba fedha na ndio maana katika *SEDEP* kuna *component* kubwa sana ya *in-service training* ya Walimu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mwalimu Jenista Mhagama, atuunge mkono kwamba, matatizo anayoyazungumzia ambayo yapo lakini kwa kupitisha bajeti hii yenye kiwango kikubwa cha fedha namna hii katika Sekta ya Elimu, tunazidi kupunguza matatizo ya Walimu. Sasa kama kuna mahali ana mawazo tu-*focus* zaidi, mimi niko tayari kusikiliza mawazo aliyonayo kwa sababu naye ni

*professionally trained* Mwalimu atanisaidia. Kwa hiyo, naomba aelewe kwamba nia nzuri ipo, atuunge mkono.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uongezekaji wa bajeti unaonesha mwelekeo wa kutatua matatizo, lakini tatizo ni usimamizi na kuwawajibisha wale ambao wanapuuza usimamiaji wa utekelezaji wa bajeti iliyoongezeka kwa manufaa ya Walimu. Ningeomba kupewa mikakati katika hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unataka kupewa mkakati. Itakuwa ngumu sana. Sijui kama anaweza kutoa mkakati leo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijua palipo na uzembe anaouzungumzia, tuko tayari kuchukua hatua. Hata Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa masikitiko makubwa juu ya malipo ya Walimu yanayochelewa, Mheshimiwa Waziri Mkuu amechukua hatua kubwa sana, ametuambia hapa Bungeni na ameji-*commit* na kuleta taarifa. Kwa hiyo, Serikali wakati huo wote tukijua mambo yanayokwamisha masuala ya walimu tuko tayari kuchukua hatua. Kwa hiyo, tunachohitaji ni kuambiwa *specifically,* tuweze kuchukua hatua, kuliko nikae hapa nipige mkakati wa kiujumla, halafu mkakati utazaa mkakati, tuambiwe *specifically problem* iko wapi, tuko tayari kuchukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nachangia kwa maelezo na kwa maandishi nilieleza matatizo yanayosababisha Wilaya za Geita, Bukombe, Sengerema, Biharamulo, Kibondo pamoja na Ngara kukosa walimu na kutopenda kwenda kule ni kwa sababu katika maeneo hayo hakuna Chuo cha Ualimu na mimi nikaahidi kwamba, nitatoa ardhi ya kutosha kwa ajili ya kujenga Chuo cha Ualimu na kutoa kila linalowezekana kujenga Chuo cha Ualimu. Mheshimiwa Waziri, nguvu hizo mbona amekaa kimya kuna nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni yale yale kwamba, walimu tunawafundisha nchi nzima katika vyuo vyetu. Tunapokuwa na mpango wa kujenga chuo kipya tutazingatia maeneo haya ambako hatujajenga vyuo. Sasa Serikali ukishasema hivyo, utasema nini zaidi. Siwezi nikaahidi kwamba, tutajenga kesho. Nimeelewa Shinyanga, Mwanza, wamejenga hoja mara nyingi katika Bunge hili, nimesikia tukiwa na mpango wa kujenga chuo cha Ualimu kingine tutaangalia maeneo hayo kwa kufuata mahitaji. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 6001 - *Culture and National Languages* ... Sh. 864,324,400/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama mna dakika mbili tu, kwa hiyo, ukiamua kuzitumia zote zitumie, dakika mbili tu.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumza jinsi jamii ya Tanzania inavyoharibiwa na matangazo mbalimbali kwenye runinga na vyombo mbalimbali na nikatoa mfano hapa tangazo la mwanamume mmoja anachagua fimbo ana zaidi ya fimbo tatu na anapiga mluzi, baadaye akapata gongo ambalo anastahili kumpiga mwanamke. Mwanamke yule akawa anastuka, anababaika. Nikasema matangazo haya, Wizara ifanye utaratibu wa kuyafuta. Yanatuletea matatizo kwenye jamii, je, Wizara inasemaje kuhusu matangazo ya namna hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusije tukafikiri kila kitu kiko Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuna Tume zimeundwa za kusimamia masuala haya ya kutangaza vitu kwenye vyombo vya habari, mengine inabidi wasimamie huko. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, kama amesema hapa Serikali tumesikia na Watendaji wetu wamesikia, tutajitahidi. Anayestahili kuchukua hatua hiyo ataliangalia kupitia wataalam, maana yake sasa hivi hata alivyolieleza pamoja na ufundi wake wote wa kueleza, wala sijaelewa na wala siikumbuki. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tunazo dakika 10 sasa tutahoji kwa ujumla, kwa hiyo, hakuna mjadala tena.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni**

| | | |
|---|---|---|
| Kif. 1001 | - *Administration and General* .... ..... ..... | Sh. 310,000,000/= |
| Kif. 1003 | - *Policy and Planning* ... ..... ..... .... ...... | Sh. 1,699,977,000/= |
| Kif. 2001 | - *Chief Education Officer* ... ..... ..... ....... | Sh. 1,499,380,000/= |
| Kif. 2002 | - *Inspectorate* .... ..... .... ...... .. .... . ...... | Sh. 100,000,000/= |
| Kif. 3001 | - *Basic Education* .... .... .... .... ..... ....... | Sh. 41,359,345,000/= |
| Kif. 4001 | - *Secondary Education* ... ... .... ... ....... | Sh. 59,413,581,900/= |
| Kif. 6001 | - *Culture and National Languages* .. .... | Sh. 1,218,000,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha kwa uelewa mkubwa kabisa bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ya mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.37 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 12 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*